Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 25 Julai, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA HAIDI MKULO):** Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mwaka 2004/2005 *[The Annual Report and Accounts of Tanzania Revenue Authority for the year 2004/2005]*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (MHE. BERNARD KAMILLIUS MEMBE:** Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA: (MHE. WILLIAM J. KUSILA):** Maoni ya Kamati ya Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI: (MHE. MUHONGA S. RUHWANYA):** Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kabla ya maswali, kwa kuwa leo ni hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kwa kweli kwa heshima tutatumbue wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi,

Mheshimiwa Kapten Chiligati, lakini wageni hao wamekuja pia kwa niaba ya Mheshimiwa John Lwanji, hao wote ni Wabunge wanaotoka kwenye Halmashauri moja.

Kwa hiyo, Madiwani hao ni wageni wa Wabunge hao wote wawili. Wageni hao ni Madiwani 15, nafikiri wako hapa ndani na wanaongozwa na Mwenyekiti wa Halmshauri hiyo, Ndugu Mheshimwa Diwani Moses Matonya. Vilevile naomba tutambue wageni wa Wizara hiyo ambao ni Askari wa Jeshi la Magereza 50, nafikiri nao wako humu ndani, ama watakuwepo pamoja nasi baadaye, kama wapo naomba wasimame. Ahsante sana, lakini wameambatana na maafisa uhamiaji 15. Lakini naomba pia nimtambue mke wa Mheshimiwa Chiligati, Mwalimu Glena Chiligati, ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 270

**Posho ya Walimu**

**MHE. OMAR S. KWAANGW'** aliuliza:-

Kwa kuwa, wapo Walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu kutokana na jiografia ya nchi yetu; na kwa kuwa, walimu wanafanya kazi kwa muda mrefu na nyakati zingine hufanya kazi kwa kujitolea:-

Je, Serikali ina mpango wa kuwapa walimu posho mbalimbali ya kufanya kazi kwenye mazingira magumu, kufundisha kwa muda wa ziada, kufundisha kwa awamu mbili, ili kufanya kazi yao kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Walimu ndilo kundi kubwa la Watumishi wa Umma lililosambaa na kufanya kazi katika kila kona ya Nchi na baadhi yao katika mazingira magumu kutokana na jiografia ya Nchi na Miundombinu iliyopo. Aidha, walimu pia wamekuwa wakijitolea kufundisha kwa muda wa ziada na katika baadhi ya shule kufundisha kwa awamu mbili *double shift.* Ni kwa kuzingatia umuhimu wa taaluma ya kazi hiyo, Serikali katika kipindi cha nyuma iliongeza posho ya ufundishaji katika mishahara ya walimu wote Nchini ili iwe motisha kwa kazi ngumu wanayoifanya. Katika mabadiliko ya mishahara yaliyofanywa baadaye na Serikali, posho ya ufundishaji kwa walimu na posho nyingine za Watumishi ziliunganishwa katika mishahara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha mishahara ya walimu na Watumishi wengine pamoja na kutoa motisha ya posho

mbalimbali. Ni imani yangu kwamba maboresho ya maslahi ya walimu na watumishi wengine yatazingatiwa katika Tume ya Rais ya kuboresha mishahara iliyoundwa mwezi Mei, mwaka 2006. Hivyo, namshauri Mbunge na watumishi wote wakiwemo walimu kuwa na subira wakati Kamati inatekeleza jukumu walilokabidhiwa

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa watumishi wengine wanalipwa masaa ya ziada wakati wanafanya kazi ya ziada. Je, ni kwanini jambo hilo haliwezekani kwa walimu, ambao wanafundisha *double session* kwenye maeneo mbalimbli?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua hilo ndio maana sasa hivi liko katika mchakato wa kutengeneza mazingira mazuri kwa wafanyakazi wote, na sio walimu peke yao.

Natambua wazi kwamba wafanyakazi wengine wanalipwa *extra duty allowance*, na sio *overtime* kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, lakini kwa walimu mpaka sasa hivi hawajalipwa hiyo *extra duty allowance,* kwa kutambua hilo ndio maana Serikali sasa hivi inafanya kila jitihada na imeunda kikundi kuangalia posho ya walimu na watumishi wengine ambao wako katika mazingira magumu.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningeomba kuuliza swali moja la nyongeza. Amesema kwamba walimu wasubiri ripoti ya Tume iliyoundwa na Mheshimia Rais inayoongozwa na Mheshimiwa Ntukamazima ya kuboresha maslahi ya walimu na wafanyakazi wengine nchini.

Mtakumbuka kwamba hapo nyuma, majibu ya Serikali yalikuwa ni kwamba walimu wasubiri matokeo ya Tume ya Omar Kwaangw' ambayo na wewe Mheshimiwa Mwenyekiti ulikuwa mjumbe wa Tume hiyo, na ripoti tayari, sasa swali langu ni kwamba walimu watasubiri matokeo ya Tume hadi lini? Wakati tume nyingine ya Omar Kwangw' ripoti yake iko mezani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kabisa kulikuwa na Tume ambayo iliongozwa na Mheshimiwa Omar Kwaangw, lakini Tume hiyo ilikuwa inaangalia zaidi malimbikizo ya misharaha.

Sasa Serikali imeshaiangalia hiyo taarifa na malimbikizo ya mishahara kama mlivyoona kwa miaka kadhaa, imelipwa kwa walimu na mingine bado inalipwa. Kuhusu shombo mbalimbali ilikuwa haikuzingatiwa zaidi, zaidi zaidi ilikuwa inaangaliwa zaidi malimbikizo ya mishahara ambayo yalikuwa yamekaa kwa muda mrefu. (*Makofi*)

Na. 271

**Mpango wa Kuboresha Barabara Jijini Dar es Salaam**

**MHE. CHARLES N. KEENJA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwepo mipango ya kuboresha mtandao wa barabara jijini Dar es Salaam kwa muda mrefu sasa; na kwa kuwa, mipango hiyo haijatekelezwa:-

(a) Je, mpango wa kujenga *ring road* utaanza lini, na barabara hiyo itapita wapi?

(b) Je, Serikali ina mpango kuhusu ujenzi wa barabara za lami kutoka *Wazo Hill* – Mbezi Luisi na *Mbezi Beach* – Mbezi Luis kupitia Goba?

(c) Kama hakuna mpango wa kujenga barabara hizo siku za karibuni, Je, Serikali haioni kuwa ni vyema kupima barabara hizo mapema kabla wananchi hawajajenga kwenye maeneo zitakapopita barabara hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mbunge wa Ubungo, lenye sehemu (a), (b) na ( c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kumekuwepo na mipango ya kuboresha mtandao wa barabara Jijini Dar es Salaam ambalo linaendelea kukua kwa kasi kubwa kiasi cha kusababisha sekta ya Miundombinu kama barabara kushindwa kukidhi mahitaji ya watumiaji. Serikali kwa kulitambua tatizo hili ilianzisha mikakati mbalimbali itakayopelekea kuboresha mtandao wa barabara katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mikakati hiyo kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007 Serikali itakarabati na kuimarisha barabara mbadala zikiwemo pia barabara za pembezoni mwa Jiji zinazounganisha barabara Kuu (*Ring road*). Barabara zitakazoimarishwa katika mkakati huu ni pamoja na barabara ya Mbezi Goba – Tangi Bovu, Mbezi Kifulu – Kinyerezi Banana, *Jet Conner* – Vituka – Mtongani

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007 Serikali itafanya upembuzi yakinifu pamoja na usanifu katika barabara ya Tangi Bovu *(Mbezi Beach)* – Goba – Mbezi Luis – Kifulu – Kinyerezi – Majumba sita, yenye urefu wa kilomita 34 itayounganisha barabara kuu za Bagamoyo eneo la kati ya Tangi Bovu na Bunju, Morogoro eneo la Mbezi na Nyerere eneo la Banana ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Gharama ya itakayotumika ni shilingi milioni 160.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kwamba wnanchi hawajengi katika maeneo zitakapopita barabara hizo Serikali hivi sasa inakamilisha mpango wa kumiliki kisheria hifadhi ya barabara zote zitakazoingia kwenye mpango huu ili ziweze kupimwa.

Kwa kuwa maeneo hayo yatawekwa alama haitakuwa rahisi wananchi kujenga katika maeneo husika kwa sababu wataelimishwa.

Na. 272

**Kituo cha Kulelea Watoto Yatima Msimbazi - Dar es Salaam**

**MHE. MOHAMED ALI SAID** aliuliza:-

Kwa kuwa, kituo cha kulelea watoto yatima na waliotekelezwa na wazazi wao kilichoko Msimbazi – Dar es Slaam kina uwezo wa kuchukua watoto 45 tu; na kwa kuwa idadi hiyo ni ndogo sana ikilinganishwa na idadi kubwa ya watoto wa aina hiyo; na kwa kuwa, Serikali haikupanga kasma yoyote kuhusu kituo hicho:

(a) Je, isingekuwa vyema sasa Serikali ikakitengea fedha ili kukiboresha kituo hicho ili kiweze kuchukua watoto wengi zaidi kuliko ilivyo sasa?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza vituo vingine Dar es Salaam na katika Mikoa yote ya Tanzania ili kukidhi haja hiyo.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mbunge wa Mgogoni, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu ya Wizara yangu ni kusajili na kutoa leseni za kuendeshea vituo hivyo ambavyo kwa mujibu wa Sheria ya Makao Na. 4 ya 1968, vituo hivyo vinaitwa Makao ya Watoto. Hata hivyo usajili huu ni pamoja na kuhakikisha kuwa wanaotoa huduma katika vituo hivyo wanazingatia viwango na masharti yaliyowekwa.

Moja ya masharti ya kutoa leseni ya kuendeshea Makao ya watoto yatima na wenye shida ni kuthibitisha kuwa mwendeshaji wa makao anao uwezo endelevu wa kutoa huduma kikamilifu bila kutegemea Serikali. Kwa msingi huo Wizara yangu haiwajibiki kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha makao ya kulelea watoto yatima na wenye shida ambayo yanaendeshwa na wadau binafsi kikiweko kituo cha Msimbazi. Hata hivyo pale Bajeti ya Serikali inaporuhusu Wizara yangu hutoa ruzuku kwa vituo vya aina hiyo tunayo jumla ya makao ya watoto 63 ambayo yamesajiliwa Tanzania Bara. Kati ya idadi hiyo jumla ya makao 9 yako katika mkoa wa Dar es Salaam peke yake.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Makao Na. 4 ya 1964 kuwapelekea watoto makaoni ni hatua ya mwisho baada ya kuthibitisha kuwa hakuna ndugu mwingine au mwana jamii aliye tayari kutoa malezi kwa watoto hao sheria hii inatambua umuhimu wa watoto hawa kulelewa ndani ya familia au jamii kama moja ya haki za msingi za kila mtoto na hii ndiyo Sera ya Wizara.

Kuongeza idadi ya makao hakuwezi kukidhi haja hiyo ndiyo maana Wizara yangu chini ya Idara ya Ustawi wa Jamii inatekeleza mpango wa utambuzi wa watoto yatima na walio katika mazingira magumu zaidi nchini, kwa lengo la kuihamasisha na kuiwezesha jamii kujiwekea mipango mahsusi yenye kuwashirikisha wananchi katika kuwaptaia huduma watoto hawa wakiendelea kupata malezi na kuwa sehemu ya jamii walimozaliwa.

Aidha, Wizara yangu inapenda kutoa taarifa kwa umma kwamba malezi ya watoto hawa ni jukumu la kila mmoja wetu na pia kwamba sheria inaruhusu watoto hao kuhudumiwa nje ya mkoa. Sheria ya Malezi ya Kambo na Kuasili (*Adoption Ordinance Cap*. 335 ya mwaka 1950) inaruhusu malezi ya watoto wa kambo na kuasili (*adoption*) kwa watoto wasio na ndugu kabisa.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa masuala mengi ya watoto wa aina hii yanaelekea zaidi katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Je, Serikali haioni kwamba sasa kuna umuhimu idara ya afya kuhamia katika maendeleo ya jamii? Ili malezi haya yaelekee katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii ya Watoto yatima na wengineo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anayepanga Wizara na Idara, ni Mheshimiwa Rais, sasa labda nitampelekea salamu zake, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, kwa kuwa *phrase* aliyoitumia mama Salma Kikwete wakati anafungua *NGO* yake inayohusu watoto yatima isemayo mtoto wa mwenzio ni wako. Sisi wananchi wote na viongozi tunaiunga mkono. Mtoto wa mwenzio ni wako, sisi viongozi na wananchi wote wa Tanzania, tunakubali hili na tunaunga mkono. Na kwa kuwa watoto hawa yatima ni watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, si kwamba ni watoto ambao hawana mwenyewe.

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu ikafanya mkakati maalum kabisa ya kuweka mpangilio mzuri wa kuwahusisha viongozi wote wa nchi hii wakachangia kwa njia moja au nyingine katika kutoa malezi ya watoto hawa pamoja na masomo yao?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mama Salma Kikwete alizindua kampeni yake kwa kauli mbiu ya mtoto wa mwenzio ni mwanao na hili tunajaribu kulisambaza kila mmoja alione hilo na Serikali kupitia Wizara yangu hivi sasa inafanya utambuzi wa watoto hao lazima tujue idadi halafu na mikakati ndio inafanyika kwa sababu sera ya watoto inawatambua hivyo na kama alivyosema ndugu Msomi, ni suala mtambuka ambalo Wizara yangu na Wizara ya Maendeleo ya Jamii tunashirikiana kwa karibu. Nakubaliana na wazo lako na naomba wiki ijayo tarehe 31 nitakapotoa hotuba yangu utaona mikakati tunayofanya ili wote tulione ni suala letu hawa watoto ni jukumu la nchi nzima na viongozi wote.

Na. 273

### Fungu la Chakula cha Wagonjwa

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imekuwa ikitenga fungu la chakula cha bure kwa wagonjwa wasio na ndugu wa karibu, wasio na uwezo, na wanaohitaji *special diet* katika hospitali za Wilaya na vituo vya afya; na kwa kuwa, huduma hii ya chakula imekuwa haiwafikii walengwa jinsi inavyokusudiwa. Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha huduma hiyo inawafikia walengwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel, Mbunge Viti maalum, kama ifuatavyo:-

Chakula bora ni sehemu muhimu ya matibabu ya mgonjwa, na inamsaidia mgonjwa kupona haraka. Hali ya ugonjwa ikiambatana na matumizi ya dawa yanapelekea kuongezeka kwa mahitaji ya chakula bora na cha kutosha. Hivyo mgonjwa anahitaji chakula bora zaidi kuliko katika hali ya kawaida ya afya.waganga wakuu wa wilaya na mkoa pamoja na wakurugenzi wa hospitali za rufaa nchini wanatambua umuhimu wa chakula katika mchakato mzima wa kutoa tiba kamili kwa wagonjwa. Hivyo wanapaswa kuweka kwenye Bajeti zao za fedha za kutosha kugharamia chakula cha wagonjwa.

Hospitali zote za Serikali pamoja na vituo vya afya zina kifungu cha matumizi mengineyo *(OC)* katika bajeti zao. Katika kupanga matumizi ya pesa hizo ununuzi wa dawa na chakula unapaswa kupewa kipaumbele. Ni wajibu wa mganga mfawidhi wa Hospitali na Mganga Mkuu wa Wilaya akishirikiana na Mkurugenzi Mtendaji kutenga pesa ya chakula kwa wagonjwa wanaotokana mbali na hospitali, wasio na ndugu au jamaa na kuwaletea chakula, watoto na wagonjwa na akili na wale walioandikiwa chakula maalum *specia diet* wauguzi wanapita wodini kila asubuhi ili kupata orodha ya wagonjwa watakaohitaji kupatiwa chakula cha hospitali, hatua hii inapunguza kutupwa kwa chakula kisichohitajiwa. Pale ambapo pesa kwa ajili ya chakula na dawa inakuwa haitoshi au inachelewa kufika kutoka Serikali Kuu, basi waganga wakuu hao, kwa kutumia Kamati zao, wanaruhusiwa kutumia fedha kutoka mifuko ya afya kama *cost sharing*, bima ya afya na mfuko wa jamii wa afya kwa ajili ya chakula. Ndugu na jamaa wa baadhi za wagonjwa huwakupelekea chakula wagonjwa wao waliolazwa kwenye vituo vya afya na hospitali. Tunawashukuru wananchi hao na tunatambua kuwa desturi hii ni nzuri na tunahimiza kwamba iendelezwe. Kwa wagonjwa wengine wote ambao hawapatiwi chakula na ndugu na jamaa zao, ni wajibu wa kituo husika cha huduma kuhakikisha kwamba wanapatiwa chakula.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri ningependa kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wagonjwa hawa wanapata

chakula kidogo, na chakula chenyewe hakipikwi katika ubora unaotakiwa. Sasa je, Serikali inasemaje juu ya kuboresha huduma? La pili kwa kuwa huduma imekuwa ikitolewa kwa muda mrefu sana, na bado haiwafikii walengwa kama jinsi Serikali inavyokusudia. Je, Serikali haioni kwamba sasa ipo ya kuweka ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha wagonjwa wao wanapata huduma hii?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza linazungumzia ubora na uchache wa chakula, mimi nadhani hilo linategemeana na tumbo. Chakula ambacho pamoja kinaweza kikawa kingi mwingine anaona ni kidogo. Lakini tutaliangalia hilo na vilevile kwa usimamizi wa karibu tunazo Kamati za Afya, bodi za afya kwa kila Halmashauri na moja ya kazi yake ni kuangalia huduma katika hospitali, ikiwa ni pamoja na kupatikana kwa chakula na ubora wa chakula. Kwa sababu katika Kamati hizo kuna wataalam wa aina mbalimbali na malalamiko kama hayo yanawafikia wao, na inatatuliwa katika ngazi ya Halmashauri. Sisi kama Wizara tunaotoa maelekezo tu ya jumla.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba niulize swali moja la nyongeza. Nadhani sisi wote tumeshawatembelea wagonjwa mahospitalini, na tutakubaliana kwamba hali ya chakula sio nzuri kama muuliza swali la kwanza alivyobainisha, lakini pia ukiangalia huduma yenyewe inavyotolewa na vyombo vinavyotumika kwa ajili ya kutoa chakula hiki, pamoja na wahudumu ambao wanagawa chakula kwa wagonjwa kwa kweli haviridhishi.

Je, Waziri anaweza akatuambia nini kuhusu hasa vyombo vinavyotumika kuwapa wagonjwa chakula kwamba havirizishi, unaweza ukafikiri wale watu wanapewa chakula ni kama ni mbwa sio binadamu, vyombo vinavyotumika si vizuri. Je, Waziri analijua hili na wanamkakati gani wa kuboresha jambo hali?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Godfrey Zambi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshtushwa kidogo kuambiwa kwamba vyombo vinavyotumika ni kama vya mbwa lakini ameniuliza kama ninalijua hili. Kusema kweli silijui hilo lakini tutaliangalia.

Lakini kama nilivyosema tumetoa madaraka makubwa sana kwa Halmashauri na katika kufanya hivyo kuna Bodi ambazo zina nguvu ndiyo zinasimamia mambo mengi ya huduma zetu katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vyombo ni vichakavu katika mifuko yetu hii ya uchangiaji upo uwezekano wa kubadilisha vyombo hivyo kwa kutumia mifuko hiyo iliyopo katika kila hospitali au kituo cha Afya. Tumewahi kusimama hapa, Wabunge

wamekuwa wakiomba *Ambulance* tukapendekeza kwamba Halmashauri kwa kutumia hii mifuko waweze kutenga pesa kwa ajili ya kazi hiyo. *(Makofi)*

Nina imani kwamba kama Bodi zinafanya kazi vizuri uwezekano wa kubadilisha vyombo vya chakula hata ubora wa chakula upo ningeomba Halmashauri zisimamie suala hili na sisi kama Wizara tutatembelea na tutaangalia pale tunapokuta kuna mapungufu tutayarekebisha na kutoa maelekezo. *(Makofi)*

Lakini Halmashauri ni nyingi ziko 114 tusingetegemea kwamba Waziri atakuwa kila hospitali wakati wote.

Na. 274

**Nafasi ya Kulaza Wagonjwa Hospitali Amana**

**MHE. JANETH M. MASSABURI** aliuliza:

Kwa kuwa, Hospitali ya Amana inapokea wagonjwa wengi zaidi ya uwezo wake, hali inayopelekea kulaza wagonjwa wawili au zaidi wenye maradhi tofauti katika kitanda kimoja, na kwa kuwa hali hiyo huweza kusababisha kuambukizana magonjwa:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa utaratibu huo unawatesa hasa watoto na akina Mama?

(b) Je, Serikali Kuu haioni umuhimu wa kupanua hospitali za Amana, Mwananyamala na Temeke ili kupunguza tatizo hilo sugu?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Massaburi Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa Serikali imekuwa ikipanua miundombinu ya Huduma za Afya, kadri uwezo unapopatikana bado mahitaji ya huduma za afya yamekuwa makubwa kutokana na mfumuko wa idadi ya wakazi, na miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujaribu kupunguza tatizo la huduma za Afya Jijini Dar es Salaam Serikali kwa kutumia fedha za mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika yaani *ADB,* inafanya ukarabati wa Hospitali ya Muhimbili, Hospitali tatu za Manispaa yaani Ilala, Kinondoni na Temeke pamoja na Zahanati 32, na kujenga hospitali iliyopo Kigamboni yenye vitanda 50. Mpango huu umeongeza jumla ya vitanda 82 kutoka vitanda 120 hapo awali hadi vitanda 202 katika manispaa hizi tatu katika kipindi cha mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo napenda kumjibu Mheshimiwa Janeth Massaburi Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

(a) Si nia ya Serikali kuwalaza wagonjwa wawili katika kitanda kimoja. Ili kupunguza tatizo hili, Serikali hivi karibuni itakaa na Manispaa zote tatu. Matatizo ya Amana ni sawasawa na ya Mwanamyamala na ya Temeke. Kwa hiyo, tutakaa nao na ili kuweza kuhamasisha wananchi kwa kutumia nguvu zao, michango ya wadau mbalimbali makusanyo ya Halmashauri pamoja na fedha zinazotokana

Serikali Kuu tuweze kuwa na Miradi ya Maendeleo iweke mikakati ya kujenga vituo vya afya kufuatana na idadi ya mahitaji ya watu. Serikali itanunua vifaa tiba na wataalam wanapohitajika. Vituo hivi vya afya vitatoa huduma karibu zaidi na wananchi na pia kupunguza msongamano katika hospitali ya Amana na hospitali nyingine katika Manispaa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na ongezeko la watu maradhi, magonjwa na majeruhi na pia kukua kwa kasi kwa teknolojia ikiwa ni pamoja na vifaa tiba, Serikali inaendelea na mpango wake wa upanuzi wa hospitali hizi na imeanzia kwa kutumia fedha za ndani na mkopo toka Benki ya Maendeleo ya Afrika. Mpango huu ni endelevu kwa nia ya kuboresha huduma zitolewazo katika hospitali hizi.

Pia, Serikali itafanya juhudi za pamoja na Manispaa husika kwa nia ya kuongeza na kuboresha mazingira na huduma zitolewazo katika Zahanati na vituo vya Afya pamoja na kuongeza vingine kufuatana na mahitaji. (*Makofi*)

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa, hospitali ya Amana ina upungufu mkubwa wa madaktari ambapo hivi sasa ni daktari bingwa mmoja tu pamoja na upungufu wa vifaa.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza madaktari bingwa angalau wafike watano?

Je, Serikali iko tayari kuipatia hospitali ya Amana vya *Ex-ray, Ultra sound* na mashinde ile ya kuondoa usingizi.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Massaburi kama ifuatavyo:-

Nakubaliana naye kwamba kuna upungufu mkubwa wa madaktari pale Amana lakini hii kauli inaweza ikarudiwa kwa Hospitali zote hapa nchini, nimewahi kusimama hapa na kuelezea kwamba kuna mpango maalum wa kuweza kuongeza vituo vya afya pamoja na wafanyakazi.

Nimewahi kueleza hapa kwamba hii itabidi ifanyike kama mradi tulivyofanya MMEM kwa sababu kila unapokwenda wafanyakazi si madaktari tu wafanyakazi wote wa afya ni pungufu sasa hivi kwa wastani tunao 50% ya ikama inayohitajika.

Kwa hiyo, namna ya kupata madaktari na kuongeza madaktari katika hospitali ya Amana itakwenda sambamba na jinsi tutakavyokuwa tunapata madaktari wa kutosha na kuwasambaza nchi nzima.

Swali la pili lilikuwa linahusu vifaa ni kweli vifaa ni haba lakini Mheshimiwa Massaburi anajua nilitembelea ile hospitali na kuna mengi niliyoelekeza ambayo tayari yameanza kufanyiwa kazi. Ni kweli *Ex-ray* ni ya muda mrefu lakini inafanya kazi. Lakini tutajitahidi kwa kadri tunavyoweza kwamba vifaa vinavyopatikana tunavisambaza kufuatana na mahitaji. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge bado Wizara ya Afya haijawasilisha hotuba tuna nafasi nzuri ya kutoa hoja zetu. Naomba tuendelee kwa ajili ya muda na swali linalofuata, Mheshimiwa Serukamba Mbunge wa Kigoma Mjini.

Mheshimiwa Kaboyonga kwa niaba yake tafadhali.

Na. 275

**Mradi wa Upembuzi Yakinifu – Kigoma**

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA (K.n.y. MHE. PETER J. SERUKAMBA)** aliuliza:

Kwa kuwa, Manispaa ya Kigoma ni kati ya Manispaa zenye miundombinu duni ya maji safi isiyo na miundombinu ya uondoaji maji taka hali inayochangia milipuko ya magonjwa; na kwa kuwa, Serikali iliafiki hatua ya utekelezaji wa mradi wa upembuzi yakinifu (*Feasibility Study for Kigoma Water Supply and Environmental Sanitation Project*) ambapo hatua zote za mradi huo zilikamilika hususan mkopo kusainiwa kati ya Serikali na *NDF* pamoja na tenda za utekelezaji.

(a) Je, inachochelewesa kuanza kwa mradi huo ni nini?

(b) Je, Serikali inafanya jitihada gani ili kuharakisha kuanza kwa mradi huo?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi wa kutumia pesa za ndani kutatua tatizo la maji safi na maji taka kabla ya msaada wa nje ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Peter Serukamba, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Manispaa ya Kigoma – Ujiji ina wakazi wapatao 175,000 kulingana na *census* ya mwaka 2002 na watu wanaoongezeka kwa 7.5%. Inakadiriwa watu kufikia 797,000 ifikapo mwaka 2020. Ongezeko kubwa la watu linatokana na wakimbizi wengi kutoka nchi jirani zinazopakana na Mkoa huo.

Chanzo kikuu cha maji cha Manispaa hii ni Ziwa Tanganyika, na mahitaji ya maji ni mita za ujazo 16,600 kwa siku, ikilinganishwa na mita za ujazo 10,000 ambazo zinaweza kuzalishwa kwa sasa. Mfumo wa majisafi uliopo ni wa siku nyingi na umechakaa hivyo kutokidhi mahitaji ya maji hasa ikizingatiwa kuwa ongezeko la watu haliendi sambamba na upanuzi wa miundombinu. Aidha, katika manispaa hii hakuna mfumo wa majitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Mfuko wa maendeleo wa nchi za *Nordic – Nordic Development Fund (NDF)* itatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwenye manispaa ya Kigoma sambamba na miradi ya kuzuia uchafuzi wa Ziwa Tanganyika, (*Pollution Control*), uondoaji wa maji ya mvua (*Storm Water Drainage*) na ukusanyaji a taka ngumu (*Solid Waster Management*) kwa gharama ya shilingi bilioni 4.

Mradi huu utatekelezwa chini ya mpango wa mrai Mkuu unaojulikana *Lake Tanganyika Integrated Regional Development Programme* na unaratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Idara ya Mazingira na unafadhiliwa kwa pamoja na Benki ya maendeleo ya *Afrika, Nordic Development Fund, Food and Agriculture Organisation, United Nations Development Programme na International Union for Conservation of nature* na utahusisha nchi za Tanzania, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Congo na Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mradi huu kama nilivyoeleza hapo juu unahusu wadau mbalimbali wakiwemo nchi nne na mashirika ya kimataifa matano, hivyo nyaraka kama mikataba na *Protocol* mbalimbali inahitajika baada ya kuanza utekelezaji wa mradi. Kutokana na ukubwa *complexity* wa mradi, kuanza kwake kumechelewa.

(b)Ili kuharakisha kuanza kwa mradi Wizara yangu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Kigoma – Ujiji (KUWASA) tayari imeandaa rasimu ya nyaraka za zabuni kwa kuzingatia muongozo wa Benki ya Dunia na kuziwasilisha kwa wadau husika kwa majadiliano. Rasimu hiyo itakamilishwa na Idara ya Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais baada ya kupata maoni yanayohitajika. Mradi unatarajiwa kuanza mwaka 2006/2007.

(c) Katika mpango wa muda mfupi wa kutumia fedha za ndani, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa Miundombinu iliyopo. Katika mwaka 2005/2006 Serikali ilitenga shilingi milioni 15 kwa ajili ya ununuzi wa mabomba na waka 2006/2007 Serikali imetenga milioni 50 kwa ajili ya ununuzi wa mabomba na viungio vyake. Aidha, Wizara imeendelea kusimamia kwa karibu kuhakikisha kuwa fedha zinazopatikana kutokana na maduhuli ya maji zinatumika kuendesha na kukarabati miundombinu iliyopo.

Na. 276

**Ujenzi wa Mabwawa.**

**MHE. DAMAS P. NAKEI** aliuliza:

Kwa kuwa, inajulikana kuwa Maji ni Uhai na kwa kuwa, mvua ni chanzo mojawapo cha Maji kama Maji hayo ya Mvua yatavunwa.

(a) Je, Serikali inatambua kuwa kuna umuhimu wa kujenga mabwawa katika kila kijiji nchini kwa matumizi ya binadamu na wanyama?

(b) Je, ni lini Serikali itajenga amabwawa katika vijiji vyote vya Kata ya Mbugwe, Nkaiti, Ufana na Dabil?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Damas Nakei, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa maji ni uhai na maji ya mvua yakivunwa ni mojawapo ya vyanzo vya maji. Aidha, Serikali inatambua umuhimu wa kujenga mabwawa nchini, hususan katika maeneo kame yasiyo na vyanzo vingine vya maji. Hivi sasa, kuna takriban mabwawa 705 nchini. Katika vijiji ambavyo vimebahatika kuwa na vyanzo vingine vya maji, vyanzo hivyo vinaendelezwa ili viweze kutoa huduma ya maji kwa binadamu na mifugo.

Kwa kutambua umuhimu huo Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 6.5 katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa katika mikoa kame. Serikali itaendelea kugharamia ujenzi wa mabwawa kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina nia ya kujenga mabwawa katika maeneo ambayo yataonekana kuwa teknoloji hiyo ndiyo muafaka. Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Babati inatekeleza mpango wa ujenzi wa mabwawa kwa lengo la kutimiza nia hiyo. Katika mwaka 2004/2005 Halmashauri ya Wilaya ya Babati ilianza ujenzi wa mabwawa matatu katika Tarafa ya Mbugwe, mabwawa hayo yapo katika Vjiji vya

Sarame, Saangaiwe na Vilima Vitatu. Ujenzi wa mabwawa hayo upo kwenye hatua mbalimbali na unatekelezwa chini ya Programu ya Hifadhi ya Ardhi na Mazingira yaani (*Land Management Programme – LAMP*) inayofadhiliwa na *SIDA – Sweden*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Miradi Shirikishi ya Maendeleo ya Kilimo (*Participatory Agricultural Development and Empowerment Project – PADEP*) Wilaya imeandaa mpango wa kujenga mabwawa katika vijiji vya Olasiti na Ofana. Mpango huu umeshaanza kutekelezwa ujenzi wa bwawa katika kijiji cha Olasiti na ujenzi wa bwawa katika kijiji cha Ufana utaanza mwaka wa fedha 2006/2007. Aidha, kijiji cha Maganjwa, Kata ya Dabil, Tarafa ya Dareda kilipangwa kujengewa bwawa chini ya mpango wa *Participatory Agricultural Development and Empowerment Project – PADEP* lakini katika kuweka vipaumbele wanakijiji waliamua kujenga ghala badala ya bwawa. Hata hivyo, wameomba kujenga mradi wa maji kupitia *TASAF* na utekelezaji utaanza mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya kwa kutumia fedha kutoka Serikali Kuu imepanga kujenga bwawa katika Kijiji cha Mwada Kata ya Mwada Tarafa ya Mbugwe na kijiji cha Matufa kata ya Magugu Tarafa ya Mbugwe katika mwaka wa fedha 2006/2007. Aidha, Halmashauri ya Wilaya inaendelea kupokea mahitaji ya mabwawa kutoka kwa wnanchi ilikuyaweka katika mipango ya Wilaya.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, Kwa kuwa, mabwawa anayoyazungumzia Mheshimiwa Naibu Waziri ni mabwawa madogomadogo na hayakufanyiwa usanifu wa kihandisi yaani Engineering Design je Waziri atakubaliana nami kwamba angalau katika kila Kata Serikali ikubali kujenga angalau bwawa moja lililosanifiwa kihandisi katika Kata za Mbugwe, Mkaiti, Ufana na Dabil.

La pili, katika Kata ya Ufana kulikuwa na mpango wa muda mrefu wa kukarabati bwawa la Secheda, je mpango huo umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza, napenda kumuarifu ya kwamba katika mabwawa haya ambayo sasa hivi yatajengwa na *PADEP* ni maswali ambayo yatatumiwa usanifu lakini hata hivyo kama jinsi alivyoomba kwamba kila Kata kujengwa bwawa ambalo lifanyiwe usanifu swali hilo tumelipokea na tunamsihi yeye kwanza ashirikiane na Halmashauri kuwaomba hilo ili liweze kufanyiwa utaratibu na pia liweze kuwekewa wakati wake lini lifanyiwe usanifu na pia liweze kuja kwenye Wizara kwa ajili ya kufikiriwa katika bajeti za baadaye zijazo.

Swali lake la pili la kuhusu bwawa ambalo anasema kwamba limesahauliwa na liweze kufanyiwa ukarabati napenda kumwarifu ya kwamba bwawa hilo tunalifahamu lakini pia tutawasiliana na Halmashauri na sisi wenyewe Wizara kwa sababu tulikuwa tuna mpango wa kwenda huko na bado ziara yetu iko palepale na sisi pia tutafika kuona hali halisi ilivyo.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, Wizara ya Maji imeanza vizuri sana kwa kuainisha kila Wilaya na kuamua kwa makusudi mazima kutoa maji kwenye vijiji 10 kwenye kila Wilaya na kwa kuwa zoezi la uvunaji maji tumekuwa tukilizungumzia kwa muda mrefu.

Je haioni sasa ni wakati muafaka tena kupita kuainisha kwenye kila Wilaya ambazo zina matatizo ya maji kusudi huu mradi wa uvumanaji wa maji uweze kutekelezwa kwenye kila Wilaya angalau mabwawa mawili kwenye kila Wilaya angalau mabwawa mawili kwenye kila Wilaya hasa kwenye zile Wilaya ambazo ni kema kama Wilaya ya Mbarali?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Estherina Kilasi Mbunge wa Mbarali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika program hii ya maji ya vijijini ambayo kila Wilaya inapata miradi yake 10 kwamba kuna wawezeshaji maalum na wahamasishaji ambao watakwenda huko kuweza kwanza kuwahamasisha vizuri wananchi na baada ya hapo kuna washauri ambao watakwenda kwa ajili ya kuongea na kijiji husika ili waweze kukubaliana nao ni aina gani ya mradi wanaoutaka. Katika kutachagua mradi uhuru wanao wanakijiji aidha wachague kisima au wachague bwawa au wachague miundombinu kama wana chemchem au vyanzo vilivyopo. Kwa hiyo ni wananchi wenyewe wanachochagua kufuatana na matakwa yao na mahitaji yao ndiyo hapo sisi tunatekeleza kufuatana na hilo.

Na. 277

**Vijana Kuangalia Picha za Ngono.**

**MHE. ALI KHAMIS SEIF – (k.n.y MHE. SALIM HEMED KHAMIS)** aliuliza:

Kwa kuwa, vijana wengi nchini wamejiingiza katika janga la kuangalia vipindi vichafu vya ngono kupitia mitandao ya *Internet*.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti wamiliki wa mitandao hivyo ili kuwaepusha vijana wa Kitanzania kuangalia vipindi hivyo vichafu vinavyoangamiza maadili mazuri ya Mtanzania, lakini pia vinaathiri vijana wetu kitabia?

(b) Je, ni hatua gani za kisheria zinatakiwa kuchukuliwa kwa wale watakaovunja agizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis Mbunge wa Chambani lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, kwa kushirikiana na Taasisi za Kimataifa na watoa huduma, wanafanya juhudi mbalimbali kuelimisha jamii na kudhibiti picha za ngono kwa kuzingatia Sheria zilizopo na kutumia utaalamu wowote uliopo kwa sasa, ingawa bado suala hilo ni gumu kwa kuwa si rahisi kudhibiti picha hizo zinazosambazwa kutoka nchi nyingine. Vilevile Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kushirikiana na Makampuni yatoayo huduma za *Internet* (*Internet Service Providers – ISPS*) yanaangalia uwezekano wa kutumia *software* kujaribu kuchuja picha chafu zisiwafikie watumiaji wa huduma hizo. *Software* hizo ni kama zikikubalika zinafikiriwa kuwekwa kwenye *gateways* na *Internet Exchange Point.* Suala hili pia linatakiwa kuridhiwa na watoaji wakubwa wa nchi za nje wanatoa huduma kwa makampuni yaliyopo hapa nchini.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kosa la jinai chini ya Kifungu cha 175 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu (Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania) kwa mtu yeyote kusambaza, kutengeneza au kukutwa (*to have in possession*) picha za ngono au maandishi yenye lugha chafu. Adhabu yake ni kifungo cha miaka 2 au kulipa faini ya shilingi elfu mbili.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Je, namuuliza wako wangapi wamekamatwa kutokana na kosa hilo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: Katika kipindi chote toka uhuru kwa sasa hatuna *record* za watu waliokamatwa kwa sababu mtandao huu umeanza karibuni na wanaoangalia vitu hivyo wanaangalia kwa usiri mkubwa sana ila Serikali inaendelea kujiandaa kikamilifu kukabiliana na teknolojia hii mpya.

**MWENYEKITI:** Kwa kuwa wengi mnaonyesha na swali hili na hotuba ya Waziri bado haijawasilishwa hapa mezani naomba tuendelee.

Na. 278

**Mpango wa Kuanzisha Diploma ya Uhandisi – Vyuo vya Ufundi.**

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, sasa hivi tunavyo Vyuo vitano (5) vinavyotoa mafunzo ya Ufundi sanifu katika ngazi ya *FTC* vilivyopo katika Mikoa ya Mbeya, Arusha, Rwegalulila, Karume – Zanzibar na Taasis ya Sayansi na Teknolojia kilichopo Dar es Salaam, na kwa kuwa Serikali ina mpango wa kuanzisha kozi ya Diploma ya kawaida ya Uhandisi (*Ordinary Diploma in Engineering*) karika badala ya *FTC.*

(a) Je, kozi hiyo ni kwa ajili ya *DIT* pekee au ni pamoja na vyuo vingine?

(b) Kama jibu katika sehemu ni ndiyo. Je, kuna sababu zipi za msingi zilizosababisha kubadili mfumo wa mafunzo ya *FTC?*

(c) Je, Wizara imejiandaa vipi kwenye Vyuo ambavyo vina uhaba wa walimu, *workshops* n.k

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:

Kwa niaba ya Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu lenye sehemu a, b, na c kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa vyuo vitano alivyovitaja Mheshimiwa Cosmas Masolwa, vingali vinatoa mafunzo ya ufundi sanifu wa ngazi ya *FTC*. Hata hivyo kufuatia Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya mwaka 1996 na baadaye Sheria Na. 9 iliyoanzisha Baraza la Taifa la Ufundi *NACTE*, ngazi hiyo ya mafunzo iko katika hatua za kuondolewa *(phased out*). Badala yake umeanzishwa mfumo mpya wa utoaji mafunzo na Tuzo za ufundi uitwao *NTA* yaani (*National Technical Awards*) kwa vyuo vyote vya ufundi nchini, na siyo Taasis ya Teknolojia Dar es Salaam tu. Tuzo zinazotolewa katika mfumo huu zinaanzia ngazi ya Diploma ya Kawaida yaani (*Ordinary Diploma*).

(b) Kwa kuwa, jibu lasehemu (a) ni Siyo, sehemu (b) haina ulazima wa kujibiwa. Lakini hata hivyo ni vema kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako tukufu kuwa mfumo huu wa Tuzo za *NTA* mitaala yake iko katika mafungu (*Modules*) na inazingatia umahiri yaani (*Competence*).

Lengo lake ni kumwezesha mhitimu kuwa na uwezo mkubwa wa utendaji wa kazi na ushindai kwenye soko huria la kazi. Hii ni moja ya sababu za kubadilika mitaala na mfumo wa Tuzo za zamani za *FTC.*

(c) Maandalizi ya Wizara ni katika kuboresha miundombinu, kununua vifaa vya kufundishia na kuajiri walimu katika vyuo husika ili kuviwezesha kutoa mafunzo na kupata wahitimu walio bora zaidi. Chuo cha Ufundi Karume kinamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya Wizara ya Elimu na Amali.

Hata hivyo, kuanzia mwaka 2003, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi limeendesha warsha na semina mbalimbali kwa Walimu wa Taasisi na Vyuo vya Ufundi kuhusu usimamizi wa mafunzo na uendeshaji wa mfumo mpya na mafunzo, uandaaji wa mitaala na utungaji wa mitihani n.k Chuo cha Ufundi Karume kimeshirikishwa kikamilifu katika warsha na semina hizo.

Na. 279

**Umeme Jimbo la Karagwe**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais alipotembelea Karagwe katika kampeni zake alisikia kilio cha wananchi wa Karagwe kuhusu kutokuwa na umeme na aliahidi kuwapatia umeme hasa miji midogo ya Ihembe, Nyaishozi, Kyanyamisa, Rugu *World Vision*, Nyakaiga na Rwambaizi:-

(a) Je, ni lini Serikali itawapatia umeme wananchi wa sehemu hizo Jimboni Karagwe?

(b) Je, ni lini maeneo yapi yatakayopewa umeme Jimboni Karagwe?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Umeme *TANESCO* na mtaalam mshauri (*consultant*), *SWECO* inafanya upembuzi yakinifu wa kusambaza umeme maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Karagwe, yakiwemo maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Mtaalamu Mshauri alizungukia maeneo hayo kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu mwezi Februari na Machi 2006 na utayarishaji wa ripoti unaendelea. Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo, *SIDA* ambalo ndilo limetoa fedha za kufanyia upembuzi yakinifu, imeonyesha nia ya kufadhili mradi huu. Upembuzi yakinifu ulifanyika katika maeneo yafuatayo:-

(i)Kayanga kuelekea Bisheshe, Nyakayanja, Nyaishozi, na Ihembe.
(ii)Kayanga kuelekea Lukaka, Kakiro, Nyabwengira, Lunyaga na Rwambaizi.
(iii)Kayanga kuelekea Rwebwera, Nkwenda, Kyerwa, Isingiro hadi Murongo.
(iv)Rwebwera kuelekea Kamagambo, Nyakagoyegoye na Nyakaiga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya mtaalam mshauri ikikamilika Wizara yangu kupitia Wizara ya Fedha itawasilisha kwa Serikali ya Sweeden maoni ya fedha za miradi hii. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana. Waheshimiwa Wajumbe naona muuliza swali la msingi ameridhika na kwa kuwa muda wa maswali umekwisha na maswali yote tumemaliza naomba nitoe matangazo yafuatayo:-

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii anaomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuwa kutakuwepo na Kikao cha Kamati leo tarehe 25 katika Ukumbi uleule wa kila siku saa 5:30 Asubuhi hii na kikao hicho kitaongozwa na Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara Mheshimiwa William Shellukindo, anaomba kuwatangazia wajumbe wote wa Kamati hiyo ya Uwekezaji na Biashara kwamba kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo leo tarehe 25 Julai, 2006 saa 5.00 asubuhi katika ukumbi namba 432 ghorofa ya nne. Wajumbe wote wanaombwa kuhudhuria.

Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee Kaimu Mwenyekiti wa Wabunge wa Mjini Magharibi, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka Mkoa Mjini Magharibi wa CCM na CUF kwamba wanatakiwa kuhudhuria katika Mkutano huo muhimu leo tarehe 25 Julai, 2006 katika chumba namba 228 ghorofa ya nne jengo la Utawala. Lakini mkutano huo utafanyika baada ya kuahirisha Bunge saa 7.00.

Naomba nitangaze tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Michezo ya Waheshimiwa Wabunge, Naibu Waziri, Mheshimiwa Joel Bendera anaomba kuwatangazia wale wachezaji wote maarufu wa timu *football* ya Bunge na timu ya netiboli ya Waheshimiwa Wabunge kwamba mazoezi yaendelee kupamba moto zaidi. Kwa kuwa ile mechi yetu na ma-*veterinary* wa Mpwapwa kwa mwaliko rasmi wa Mheshimiwa George Lubeleje itafanyika siku ile ile iliyopangwa ya Jumamosi na hivyo safari imeshaanza kufanyiwa maandalizi. Kwa hiyo, timu hizo zinatakiwa ziendelee kujinoa zaidi ili zikachukue ushindi huko Mpwapwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwatambue wageni wetu wanafunzi 43 na walimu 10 wa shule ya msingi Mbwanga ya Mjini Dodoma. Tafadhali naomba wanafunzi na walimu wasimame. Ahsante. Karibuni sana wanafunzi na walimu kwenye Shughuli zetu za Bunge. (*Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitambue uwepo wa vijana saba 7 wa Kundi la Hamasa kutoka Jimbo la Mbarali wageni wa Mheshimiwa Estherina Kilasi. Ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitambue uwepo wa viongozi wawili wageni wa Mheshimiwa Bernadeta Mushashu ni bibi Emelda Nyaishozi na Consolata Protaz. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru hayo ndiyo matangazo yaliyofika mezani kwangu. Naomba Katibu tuendelee.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007
### Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa mapema leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwa ushindi mkubwa kilichoupata kwenye Uchaguzi wa Desemba, 2005 na kukiwezesha Kuunda Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, pia Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Rais Amani Karume kwa ushindi mkubwa walioupata kwenye uchaguzi uliopita.

Aidha, nachukua fursa hii kumpongeza Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM kwa kura asilimia 99.99 kuwa mwenyekiti mpya wa Chama tawala Chama Cha Mapinduzi, pia nampongeza Katibu Mkuu mpya wa CCM, Mheshimiwa Yusufu Makamba pamoja na Sekretarieti yake.

Nawapongeza kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wabunge wa vyama vyote waliorejea tena Bungeni pamoja na wale wapya. Nampongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Mbunge wa Monduli kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu.

Vilevile nampongeza Mheshimiwa Spika kwanza kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mbunge wa Jimbo la Urambo Mashariki, na pili kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge hili Tukufu. Nampongeza pia Mhshimiwa. Anna Makinda kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Aidha nampongeza Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge letu kama Wenyeviti wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawapongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wa Fedha, na Mipango na Uchumi na Uwezeshaji kwa hotuba zao walizozitoa mapema katika Mkutano huu wa Bunge ambazo pamoja na mambo mengine zimetoa mwelekeo wa Bajeti ya Serikali na hali ya uchumi wetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa William Kusila, Mbunge wa Bahi, kwa kuyapitia na kuyachambua Makadirio ya Mapato na

Matumizi pamoja na ushauri wao katika masuala mbalimbali ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Usalama Nchini. Kwa ujumla katika vyombo vya Ulinzi na Usalama vinavyosimamiwa na Wizara yangu, yaani Jeshi la Magereza, Uhamiaji, Idara ya Wakimbizi, na Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji, vimetoa mchango mkubwa katika kudumisha amani na utulivu katika kipindi chote cha mwaka uliopita. Nachukua nafasi hii kuvishukuru vyombo mbalimbali vya Ulinzi na Usalama hapa nchini kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kudumisha hali ya amani na utulivu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2005/2006 na Matarajio ya Mwaka 2006/2007. Sasa naomba kutoa tathmini ya utekelezaji wa malengo yaliyopangiwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika kipindi cha mwaka uliopita wa 2005/2006, na kuelezea matarajio yetu kwa mwaka huu wa (2006/2007). Napenda kusisitiza kwamba katika shughuli zote za Wizara, Ilani ya Uchaguzi ndiyo imekuwa dira na mwongozo katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapato, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilipangiwa kukusanya mapato ya Serikali ya jumla ya Shilingi bilioni 12.95 kwa mwaka 2005/2006. Hadi kufikia Juni, 2006, makusanyo halisi ni Shilingi bilioni 15.84, ikiwa tumevuka lengo la mwaka mzima kwa shilingi bilioni 2.89 sawa na asilimia 22.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** matumizi, mwaka uliopita Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iliidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni 66.23 kwa matumizi ya kawaida *(Reccurent*) na Shilingi bilioni 4.26 kwa matumizi ya miradi ya maendeleo *(Development).* Hadi kufikia Juni, 2006, jumla ya shilingi bilioni 65.83 ya fedha za matumizi ya kawaida *(Reccurent)* zilitumika ikiwa ni asilimia 99.4 ya malengo. Aidha kwa fedha za miradi ya maendeleo, hadi Juni, 2006 zilikuwa zimetumika shilingi bilioni 3.15 sawa na asilimia 73.9 ya lengo la mwaka. Asilimia hii ipo chini kidogo kutokana na sehemu ya fedha za udhibiti wa UKIMWI kuchelewa kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo ya ujumla, naomba sasa nipitie maeneo kwa kila Idara.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Jeshi la Magereza, jukumu la Jeshi la Magereza ni kuhifadhi wahalifu wa aina zote pamoja na kurekebisha tabia za wafungwa ili wamalizapo vifungo vyao wawe raia wema katika jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2005 hadi Aprili, 2006 hali ya Ulinzi na Usalama wa Magereza yote 122 nchini imeendelea kuwa shwari na hakuna matukio yaliyojitokeza ambayo yameathiri hali ya Ulinzi na Usalama wa vituo. Matatizo makubwa yanayolikabili Jeshi la Magereza Mheshimiwa Mwenyekiti, ni pamoja na msongamano wa wafungwa na mahabusu ambao unasababishwa na sababu mbalimbali ikiwemo nafasi finyu ya magereza; matatizo mengine ni uhaba wa vyombo vya usafiri, uhaba wa vitendea kazi, uhaba wa nyumba za makazi ya askari, pamoja na uchakavu wa majengo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Magereza yote nchini yanaruhusiwa kisheria kuhifadhi wahalifu 22,669 lakini hivi sasa yanahifadhi wastani wa wahalifu 45,000. Takriban nusu ya hao ni mahabusu ambao kesi zao hazijaamuliwa na Mahakama. Idadi hii ni zaidi ya mara mbili ya uwezo wa Magereza yenyewe. Serikali inatafuta dawa ya kudumu ya kuliondoa tatizo la msongamano; na tunaliomba Bunge hili Tukufu liisaidie Serikali kupata ufumbuzi wa tatizo hili pale Serikali itakapoleta mapendekezo ya kubadili baadhi ya sheria zinazosababisha msongamano magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi natoa shukrani za dhati kwa uamuzi wa kihistoria wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alioufanya wa kutembelea magereza ya Mkoa wa Dar es Salaam tarehe 04/05/2006 ili kupata picha ya maendeleo na matatizo ya Magereza ikiwa ni pamoja na kujionea hali halisi ya maisha ya Askari na Maafisa. Ziara hii imeleta msisimko mkubwa wa utendaji kazi katika Jeshi la Magereza na pia imeleta faraja kubwa kwa wafungwa na mahabusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ziara hii inaashiria dhamira kubwa na nzuri aliyonayo Mheshimiwa Rais na Serikali ya Awamu ya Nne katika kuboresha hali ya maisha na huduma zitolewazo na Jeshi la Magereza na kutatua matatizo yanayolikabili Jeshi la Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Magereza mengi makubwa yamejengwa zamani wakati wa ukoloni na ni machakavu. Lakini kutokana na ufinyu wa bajeti, Serikali haijaweza kujenga magereza ya kutosha mengine makubwa mapya. Aidha kuna jumla ya Wilaya 36 bado hazina magereza. Jitihada zimeanza za kukarabati magereza ya zamani na kujenga magereza mapya hasa katika Wilaya ambazo hazina magereza. Kazi hii inafanyika kwa awamu kutegemea hali ya bajeti ya Wizara yetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utaratibu wa Msamaha wa Parole, Sheria ya msamaha wa Parole ilipitishwa na Bunge hili kwa lengo la kuwasamehe wafungwa wanaoonyesha kujirekebisha kitabia na kimwenendo baada ya kutumikia theluthi moja ya vifungo vyao na vile vile kutoa motisha kwa wahalifu hao kujirekebisha kitabia. Na vilevile kupunguza msongamano magerezani. Sheria hii ilifanyiwa marekebisho mwaka 2004 kwa kupanua wigo wake. Tangu marekebisho ya sheria hii hadi sasa jumla ya wafungwa 1,314 wamenufaika.

Hata hivyo sheria hii bado haijakidhi matarajio kwa kuwa wigo wake bado ni mfinyu. Hivi sasa wapo wafungwa wengi magerezani ambao wamejirekebisha kitabia lakini hawanufaiki na sheria hii kwa vile aina ya makosa yao sheria hairuhusu wapewe msamaha. Hivi sasa Wizara yangu ikishirikiana na Wizara ya Sheria na Katiba na Wizara Usalama wa Raia, tunaandaa Muswada wenye mapendekezo ya marekebisho ya sheria hii kwa lengo la kupanua wigo ili wafungwa wengi zaidi waliojirekebisha kitabia wanufaike. Muswada huu utakamilika muda si mrefu ujao na utawasilishwa katika Bunge hili Tukufu ili kupata ridhaa ya Waheshimiwa Wabunge. Ni mategemeo yetu kwamba Waheshimiwa Wabunge mtatuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuimarisha Programu za Urekebishaji wa Wafungwa. Katika Programu za urekebishaji wa wafungwa magerezani, Jeshi la Magereza limeanza kutekeleza mpango wa uendeshaji wa shughuli za wafungwa nchini kote kwa kutumia mtandao wa kompyuta *(offender management information system)* kwa kuanzia na vituo vya magereza ya Mkoa wa Dar es Salaam. Utekelezaji katika Mikoa mingine utafanyika kwa awamu kadri fedha zitakavyokuwa zikipatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu za urekebishaji wafungwa zimeendelea kutekelezwa kama ilivyoelezwa katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka jana (2005/2006). Katika hotuba hiyo ilielezwa kuwa, Jeshi la Magereza linahitaji vitendea kazi vya kutosha ili shughuli za urekebishaji mienendo ya wafungwa zitekelezwe, hasa kwa kuwapa stadi za kazi. Serikali imeendelea kuchukua hatua za makusudi katika kuboresha mashamba ya magereza kwa kununua matrekta kumi na tano (15) pamoja na zana zake; na kukarabati matrekta ya zamani. Ununuzi wa matrekta utaendelezwa mwaka huu wa fedha. Hizi ni jitihada za kufufua kilimo katika mashamba ya magereza ili Jeshi la Magereza lijitegemee kwa chakula na kuuza ziada katika ghala la akiba ya Taifa *(SGR)*. Vile vile ili kuwafundisha wafungwa stadi za kilimo bora ili wamalizapo vifungo vyao stadi hizo ziwasaidie kuboresha kilimo chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali, Magereza imeweza kuboresha mazingira kwa kupanda miti katika maeneo mbalimbali nchini. Miradi ya kupigiwa mfano ipo katika magereza ya Bariadi na Maswa, chini ya ufadhili wa UNDP. Kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji, kazi ya ukarabati wa bwawa la kumwagilia mpunga gereza la Bagamoyo imekamilika.

Kwa upande wa mifugo, uchimbaji wa mabwawa manne ya kunywesha maji mifugo unaendelea katika gereza Ubena. Pia limeanzishwa shamba la nyasi za mifugo huko Gereza Kimbiji (Kigamboni) Sambamba na ununuzi wa zana za kuvunia nyasi hizo. Miradi ya upandaji miti itaenezwa katika magereza yote nchini ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha viwanda vidogo vidogo, mashine na vipuri vya Viwanda vya Uhunzi (Ukonga) na Kiwanda cha viatu - Karanga – (Moshi) zimenunuliwa. Sambamba na hilo, mafunzo ya ufundi kwa wafungwa na askari, yanayohusu uashi, useremala, ufundi bomba, umeme na ufundi rangi yameendelea kutolewa katika Chuo cha Ufundi cha Magereza Mbeya. Lengo la mafunzo hayo ni kuongeza kujitegemea katika uendeshaji wa miradi ya magereza na pia kutoa ujuzi kwa wafungwa ambao utawawezesha wajiajiri wenyewe baada ya kumaliza vifungo vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma kwa Wafungwa Magerezani, pamoja na tatizo la msongamano mkubwa wa wafungwa na mahabusu magerezani, Wizara yangu imeanzisha programu ya kuboresha huduma za wafungwa magerezani kwa kuzingatia haki za binadamu.

Katika kutekeleza programu hiyo tayari tumeboresha sare za wafungwa kutoka kwenye kaptura, sasa wanavaa kaunda suit, pia tunatoa sweta na mablanketi katika maeneo ya baridi, aidha sasa wafungwa wanalalia magodoro badala ya mikeka ya katani (virago). Huduma za elimu, lishe na matibabu pia zimeanza kuboreshwa.

Mwaka huu wa fedha tutaendelea kutekeleza programu hii, hasa kwa kusambaza *Radio* katika kila Gereza nchini, na televisheni kwa magereza makubwa yaani *Central Prisons.* Lengo la programu hii ni kuwawezesha wafungwa waishi maisha kama binadamu wengine. Ikumbukwe kwamba adhabu pekee ya mfungwa ni kule kutengwa na jamii, lakini utu na utanzania wake anabaki navyo, hivyo anayo haki ya kuhudumiwa vizuri anapokuwa kwenye adhabu ya utenganisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Mafunzo kwa Askari**,** Jeshi la Magereza limeendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya ndani na nje ya nchi kwa ajili ya askari wake. Mwaka uliopita askari wapya *(recruits)* 595 walihitimu mafunzo ya awali na kuajiriwa rasmi kama askari. Aidha, askari 50 wanachukua mafunzo ya uongozi wa ju *(gazetted officers course)*, 132 wako kwenye kozi ya mafunzo ya kati *(advance course),* na wanafunzi wengine 37 wanaendelea na mafunzo ya cheti cha sheria Chuoni Ukonga. Jeshi la Magereza limeanza mafunzo mengine ya awali kwa wanafunzi wengine 690 mwishoni mwa mwezi Mei, 2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya watumishi 564 wako katika Vyuo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi katika taaluma mbalimbali za kiwango cha Stashahada, Stashahada ya juu na Shahada ya Uzamili katika fani zinazohitajika na magereza kama, Uboharia, Utunzaji wa Mahesabu, Utawala, Sheria, Uchumi, Madawa, Mifugo na Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Utekelezaji wa Miradi kwa Mwaka 2005/2006, katika mwaka uliopita (2005/2006), Jeshi la Magereza lilitekeleza miradi ifuatayo:-

(i) Ukarabati wa jengo la Ofisi mpya ya Makao Makuu, Dar es Salaam.

(ii) Ukarabati wa magereza makongwe yenye ulinzi mkali *(Central prisons)* ya Maweni – (Tanga), Uyui – (Tabora), Gereza maalum Isanga – (Dodoma), Bohari Kuu ya Magereza Keko na Lilungu – Mtwara.

(iii)Ujenzi na ukarabati wa mabweni ya wafungwa na mahabusu Mbinga, (Ruvuma) na Igunga – Tabora . Aidha, ujenzi wa mabweni mawili yenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya wafungwa 150 katika gereza Mbarali umekamilika. Kazi ya ujenzi wa mabweni ya wafungwa zinaendelea katika gereza la Wanawake Morogoro, Kahama, Mkuza, Liwale, Mahabusu Tabora, Ileje, Ngudu, Lushoto, Kayanga, Bwangwe, Kigongoni, Kambi Kimbiji na Kambi Mvuti.

(iv) Ukarabati na ujenzi wa nyumba za askari ulianza katika vituo vya Chuo Kiwira, Chuo Ruanda, Chuo Ukonga, Gereza Iringa, Kibiti, Kayanga, Bunda, Ubena, Magereza (Mkoa) Manyara, Ileje, Mbarali, Mbinga, Keko na Kimbiji.

(v) Umefanyika ukarabati na uimarishaji wa mifumo ya maji safi katika magereza ya Newala – Mtwara, Kimbiji – Dar es Salaam na Kwamgumi – Tanga na ukarabati wa mifumo ya maji taka katika magereza ya Pangani na Chumbageni – Tanga, Kitai – Ruvuma, Ubena – Pwani na Bukoba – Kagera.

(vi) Upimaji wa ardhi ulifanyika na fidia imelipwa katika maeneo yaliyotwaliwa na Jeshi la Magereza katika magereza ya Nkasi – Rukwa, Shamba la Mallya (Mallya stock Farm) –Segerea – Dar es Salaam na Kilindi – Tanga.

(vii) Hatua zimechukuliwa za kuimarisha mashamba na viwanda vidogo vidogo. Katika magereza mbalimbali kwa kuwapatia matrekta, pembejeo; pia mashine za viwandani.

(viii) Yamenunuliwa magari 40 ya aina mbalimbali pamoja na Pikipiki 13 na kusambazwa katika magereza mbalimbali.

(ix) Kazi ilianza ya ukarabati na upanuzi wa Gereza la Mahabusu - Iringa pamoja na ujenzi wa nyumba za askari.

(x) Ujenzi ulianza wa Magereza mapya katika Wilaya za Igunga, Mbarali, Mbinga, na ukamilishaji wa Gereza jipya la Mbozi.

(xi) Utoaji wa Elimu juu ya janga la UKIMWI.

Jeshi la Magereza limeendelea vita dhidi ya rushwa ndani na nje ya Jeshi. Mpango mkakati wa kupambana na rushwa ndani ya Jeshi umeandaliwa na kusambazwa kwenye vituo vyote kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya Jeshi la Magereza katika Mwaka wa Fedha wa 2006/2007. Katika mwaka huu wa fedha wa 2006/2007 Jeshi la Magereza limejiandaa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuajiri askari wapya 903 na kuwapatia mafunzo ya awali *(Recruit training)*.

(ii) Kukamilisha ukarabati wa Jengo litakalotumika kama Makao Makuu ya Jeshi la Magereza.

(iii) Kukarabati Jengo litakalotumiwa kama Ofisi ya Mkuu wa Magereza Mkoa wa Dodoma.

(iv) Kuendelea na ukarabati wa majengo na miundombinu ya Magereza yenye ulinzi mkali likiwemo Gereza Maweni, Uyui, Ukonga, Lilungu na Gereza Maalum Isanga.

(v) Kuendelea kukamilisha baadhi ya viporo vya miradi ya mabweni ya wafungwa na mahabusu na kuendelea na ujenzi wa magereza ya Mbarali, Mbinga, Igunga, Meatu, Kahama, Kasulu, na Bangwe (Kigoma).

(vi) Kukamilisha ujenzi wa nyumba za askari zilizoanza mwaka 2005/2006 katika magereza ya Loliondo - Arusha, Mbulu, Manyara, Mpwapwa, Dodoma Mwanga, Kilimanjaro, Iringa, Sumbawanga, Kibiti, Namajani – (Mtwara) na Wami Vijana – Morogoro.

(vii) Ujenzi wa nyumba mpya za askari utaanza katika magereza ya:- Igunga, Mkuza na Kigongoni – (Pwani), Lindi, King'ang'a – (Dodoma), Rombo, Rusumo, Mbinga, Mbarali, na Mbozi na Kikosi maalum Ukonga – Dar es Salaam.

(viii) Kuendelea kujenga nyumba mpya za askari na Maafisa wa Mkoa mpya wa Manyara (Babati).

(ix) Kuendelea kuimarisha mifumo ya maji safi na maji taka katika magereza mbalimbali ili kuachana kabisa na utaratibu uliopitwa na wakati wa wafungwa kujisaidia kwenye mitondoo.

(x) Kupima maeneo ya Magereza ya King'ang'a, Mpwapwa, Kibondo, Mugumu, Chuo Kiwira, Tandahimba – Mtwara, Ubena, Mkuza, Meatu, Uyui, (Kambi Kakola na kambi Kazima), Nzega na Kambi Kizitwe – Rukwa.

(xi) Kuanza ujenzi wa Magereza mapya ya Wilaya za Karatu, Hanang, Nkasi, Luangwa na Bukombe.

(xii) Kununua magari 82 na matrekta matano kwa ajili ya shughuli za Magereza kama ifuatavyo:-

    (i) Kununua magari maalum kumi na moja (11) kwa ajili ya kusafirisha mahabusu kwenda na kurudi Mahakamani.

    (ii) Kununua malori matatu (3) na tani 7 (7 *Ton Long Wheel Base*).

    (iii) Kununua *Tipper* mbili (2) za tani 7 (*7tons dump trucks*)

    (iv) Kununua magari madogo ya mizigo 64 *(4WD STD station Wagon P/ups)* kwa ajili ya vituo vya Magereza ya Wilaya sitini na nne (64)

(v) Kununua magari madogo mawili (2) (2 *saloon cars*)

(xiii) Kutoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi wa Magereza 120.

(xiv) Kuendeleza uzalishaji katika mashamba ya kilimo na mifugo kwa kuyapatia zana za pembejeo zinazotakiwa.

(xv) Kuendelea kununua mashine na vipuri mbalimbali za kuendeshea viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya kushona viatu, useremala na uhunzi.

(xvi) Kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii chini ya Mpango wa Menejimenti ya Misitu ya Asili na Kilimo Mseto *(Natural Forestry Resources Management and Agro Forestry Centre)* kuanzisha mradi wa kupanda ekari 3,000 za miti aina mbalimbali katika Magereza ya Idete – Morogoro, *Isupilo* – Iringa na Msalato hapa Dodoma.

(xvii) Kufanya utafiti wa nishati mbadala kwa ajili ya matumizi ya kupikia chakula cha wafungwa magerezani na kuondokana kabisa na matumizi ya kuni ili kuokoa mazingira ya nchi yetu.

(xviii) Kulipa madeni yote ya nyuma ya Askari wote wenye madai na kuondoa kabisa kero hii iliyodumu kwa mrefu.

(xix) Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa vyuo vya Ukonga na Kiwira, Mbeya.

(xx) Kuimarisha matumizi ya Kompyuta ikiwa ni pamoja na kueneza mtandao wa *Offenders Management Information System* katika Mikoa 12 ya Tanzania Bara.

(xxi) Kuendeleza vita dhidi ya rushwa.

(xxii) Utoaji wa Elimu kwa Umma juu ya shughuli za Magereza.

(xxiii) Kuendelea kutoa Elimu juu ya athari na namna ya kujikinga na UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Jeshi la Magereza, kuanzia mwaka huu (2006/2007), litaanza kwa awamu kutekeleza jukumu lake la kisheria la kusafirisha mahabusu kutoka magerezani kwenda Mahakamani na kwa wale ambao hukumu zao zitakuwa bado, kuwarejesha magerezani. Jukumu hili kwa sasa linafanywa na Jeshi la Polisi. Nia ni kulipunguzia Jeshi la Polisi mzigo wa kuwasafirisha Mahabusu kila siku ili wafanye kazi zao za msingi za kupambana na Wahalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma za Zimamoto na Uokoaji, Utekelezaji 2005/2006. Majukumu ya msingi ya Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji ni kuokoa maisha na mali kwenye majanga ya moto au ajali mbalimbali na kuzima moto. Kazi nyingine zinazofanywa na askari wa Zimamoto ni kutoa mafunzo ya tahadhari na kinga ya moto kwa Umma na watendaji wake pamoja na kufanya ukaguzi kwenye maeneo mbalimbali ili kuhakikisha usalama wa wananchi na mali zao dhidi ya hatari ya majanga ya moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka uliopita wa 2005/2006 yalitokea matukio ya moto 426 katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Jitihada zilifanyika kuzima mioto hiyo na kuokoa maisha ya watu na mali. Hata hivyo Vikosi vya Zimamoto katika mwaka uliopita vilikabiliwa na matatizo mbalimbali, yakiwemo; uhaba wa vitendea kazi, hasa magari ya Zimamoto, uchache wa askari wa Zimamoto, mafunzo, baadhi ya Manispaa kutokuwa na vikosi vya Zimamoto (Bukoba, Singida na Kibaha) na kadhalika. Serikali imekuwa inachukua hatua za kutatua matatizo hayo kwa awamu. Katika kipindi cha 2005/2006 mambo yafuatayo yamefanyika:-

(i) Ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto na kutoa elimu wakati wa ukaguzi *(Fire Prevention and Protection).* Maeneo yaliyofanyiwa ukaguzi ni 8,492, ikiwa ni pamoja na: matenki ya kuhifadhi mafuta *(tank farms),* vituo vya mafuta, magari, majengo mbalimbali, Hoteli, Viwanda, Maghala, Maduka ya Madawa na Maduka ya kawaida, Maduka ya Fedha, Shule na Hospitali na kadhalika..

Napenda kutoa wito kwa wananchi kwamba wanapojenga nyumba bora na kununua magari lazima wahakikishe wanaweka vifaa vidogo vidogo vya kuzima moto na wajifunze namna ya kuvitumia. Kila mwananchi awe askari wa Zimamoto katika eneo lake.

(ii) Mwaka uliopita (2005/2006) Serikali Kuu ilitoa fedha kwa ajili ya kununua magari ya Zimamoto kwa Manispaa saba za:- Dodoma, Lindi, Moshi, Kibaha, Singida**,** Bukoba na Morogoro. Aidha katika mwaka huu wa fedha (2006/2007), Serikali Kuu imetenga fedha za kununua magari ya Zimamoto kwa ajili ya Manispaa za Arusha, Shinyanga, Sumbawanga, Musoma**,** na Halmashauri za miji ya Babati, Korogwe, Arumeru na Kahama. Halmashauri hizi zinashauriwa zianze kuunda vikosi vya Zimamoto na kuajiri askari wa Zimamoto ili kujenga uwezo wa kupambana na majanga ya moto katika maeneo hayo. Wizara yangu itakuwa tayari kushirikiana na Halmashauri husika katika kuimarisha vikosi vyao vya Zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** matarajio 2006/2007. Hivi sasa usimamiaji wa utekelezaji wa shughuli za Zimamoto na Uokoaji nchini upo katika mamlaka za Halmashauri za Miji, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Bandari. Vile vile kuna vikosi vitatu vya Zimamoto vya Makampuni binafsi. Shughuli kubwa ya Wizara yangu ni kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera, na kuratibu shughuli za kuzima moto yanapotokea matukio makubwa ya moto. Lakini uratibu unaofanywa hivi sasa hauna nguvu za kisheria. Muswada wa sheria unaandaliwa ili kuongeza nguvu za usimamizi na utendaji wa Jeshi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Wizara yangu katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 ni kuangalia upya sera , sheria, na muundo wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji nchini kwa nia ya kuliimarisha Jeshi hili ili lifanye kazi kwa ufanisi zaidi na kukidhi matarajio ya wananchi. Katika shughuli hizo, mafunzo yatatiliwa mkazo na Chuo cha Zimamoto na Uokoaji pia kitaimarishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Huduma za Uhamiaji, shughuli kuu ya Idara ya Uhamiaji ni kudhibiti uingiaji na utokaji wa watu nchini. Udhibiti huu unachangia katika kuimarisha ulinzi na usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** katika kipindi cha Julai, 2005 hadi Aprili, 2006, jumla ya wageni 404,899 waliingia nchini, ikilinganishwa na wageni 409,525 walioingia nchini katika kipindi kama hiki cha 2004/2005. Aidha wageni 380,758 walitoka ikilinganishwa na wageni 348,977 waliotoka katika kipindi hiki kwa mwaka uliopita. Kwa jumla wageni walioingia na kutoka nchini ni wengi, hii inatokana na hali ya amani, utulivu na usalama iliyopo nchini, mazingira bora ya uwekezaji, kupungua kwa hofu ya ugaidi miongoni mwa wageni, pamoja na kuongezeka kwa matangazo ya vivutio vya Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwa wageni wanaoingia na kuishi nchini ni wale wenye vibali halali kulingana na kazi wanazofanya, Idara ya Uhamiaji ilitoa jumla ya hati mpya za ukaazi 5,475 ikilinganishwa na vibali 4,641 vilivyotolewa mwaka uliopita wa 2004/2005. Aidha, hati 1, 663 ziliongezwa muda ikilinganishwa na hati 1, 402 zilizoongezewa muda katika kipindi kama hiki cha mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki jumla ya Pasipoti mpya za kusafiria 142,707 zilitolewa, kati ya hizo 736 ni za Utumishi, 2,075 za Kidiplomasia na 139,089 za kawaida. Katika kipindi hiki hakuna Pasipoti zilizoongezwa muda kwani Pasipoti zote za zamani zilibadilishwa na kutolewa mpya. Pasipoti mpya zinasomeka kwa Kompyuta na ni za kiwango cha Kimataifa, na haziwezi kughushiwa kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** katika kipindi cha Julai, 2005 na Aprili, 2006. Serikali iliwapa Uraia wa Tanzania wageni 104 ikilinganishwa na wageni 47 waliopewa Uraia katika kipindi kama hiki mwaka uliopita. Takribani 75% ya wageni waliopewa Uraia ni wanawake walioolewa na Watanzania.

Waliopewa uraia katika kipindi hiki kutokana Mataifa mbalimbali ni kama ifuatavyo:- Uingereza 7, India 32, Jamhuri ya Kidemokrasia Kongo 5, Yemen 7, Msumbiji 3, Rwanda 4, Kenya 15, Shelisheli 1, Lebanon 1, Switzerland 3, Irani 3, Somalia 7, Italia 1, China 1, Pakistan 6, Burundi 4, Ukraine 3, na Ufilipino. Aidha katika kipindi hiki (2005/2006) Watanzania 55 waliukana Uraia wa Tanzania na kupata Uraia wa Mataifa mengine kama ifuatavyo:- Zambia 6, Norway 7, Ujerumani 8, Czech 2, Denmark 7, Canada 5, na Australia 1. Ukanaji huu ulikuwa na sababu mbalimbali zikiwemo dhana ya kutafuta maisha mazuri na kuolewa na kuoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, doria na misako ya wahamiaji haramu yenye lengo la kudhibiti ukaaji wa wageni haramu nchini ilifanyika katika sehemu mbalimbali nchini

kama vile Mahotelini, Migodini, Vijijini, Mijini na sehemu nyingine za maficho. Kutokana na zoezi hili walikamatwa wageni 1,016 ikilinganishwa na wageni haramu 2,275 waliokamatwa wakati kama huu mwaka 2004/2005. Katika Kipindi wageni waliokamatwa walichukuliwa hatua mbalimballi kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| Waliofukuzwa nchini | 910 |
| Waliostahitakiwa | 118 |
| Waliolipa faini | 23 |
| Waliofungwa | 16 |
| Kesi zinazoendelea | 25 |
| Walioachiwa huru | 41 |

Aidha katika kipindi hiki Vijana wa Kitanzania watoro (stowaways) 472 walirudishwa nchini. Wengi wa vijana hao wamekuwa wakiondoka nchini kinyume cha sheria, kanuni na taratibu kwa mawazo kwamba huko ughaibuni kuna maisha bora kuliko hapa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vitambulisho vya Kitaifa, sasa nieleze hatua tuliyofikia katika mradi wa kutoa vitambulisho vya Uraia. Tumemaliza hatua ya upembuzi yakinifu na tumeandaa mchakato *(Action Plan)* wa kuanza maandalizi ya utekelezaji wa mradi huu katika mwaka huu wa fedha (2006/2007). Mara baada ya kupata baraka za Serikali, itaitishwa tenda ili kupata Kampuni yenye ujuzi na uwezo wa kuisaidia Serikali katika utekelezaji wa mradi huu. Maandalizi mengine kwa mfano ya kupata jengo la mradi, na watumishi wa mradi yameanza kufanyika. Vile vile zoezi la kuwatambua wageni wanaoishi huko vijijini na mijini, na kuwaorodhesha limeanza katika Mikoa ya mipakani na baadaye litaendeshwa katika Mikoa yote Bara na Visiwani ikiwa ni mkakati wa kuzuia wageni wasipate vitambulisho vya Uraia hapo zoezi la kutoa vitambulisho hivyo litakapoanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka jana, Wizara yangu ilitoa ahadi ya kuweka mtandao wa Kompyuta *(Local Area Network)* kwa baadhi ya vituo vya Uhamiaji vya mipakani na Ofisi za Mikoa. Napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa mradi wa kuweka mtandao umeshaanza kutekelezwa kwa awamu. Hivi sasa mtandano umewekwa katika Ofisi za Makao Makuu ya Uhamiaji Dar es Salaam, Zanzibar, Arusha. Vile vile katika Vituo vya Viwanja vya Ndege vya Kimataifa vya Mwalimu J. K. Nyerere, Kilimanjaro, na Zanzibar; vile vile vituo vya Namanga na Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Mjini Magharibi (Mwanakwerekwe).

Lengo ni kuviunganisha vituo vyote vya mipakani katika mtandao wa Kompyuta ili kufuatilia nyendo za wageni waingiao na waondokao nchini kwa njia za kisayansi zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti iliyopita ilitolewa ahadi ya kuanza ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji ya Mkoa wa Kusini Unguja katika eneo la Tunguu na Kituo cha kuingilia wageni mpakani mwa Tanzania na Msumbiji eneo la Kilambo (Mtwara). Ujenzi wa Ofisi ya Mkoa wa Kusini Unguja umekamilika na Ofisi hiyo ya kisasa kabisa

sasa imeanza kutumika. Ujenzi wa Kituo cha Kalambo (Mtwara) pia umekamilika. Hali kadhalika, ilitolewa ahadi ya kuanza ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji za Mikoa ya Manyara (Babati) na Dar es Salaam. Napenda kulijulisha Bunge kuwa hatua ya kwanza ya kupata michoro imekamilika, na sasa tunaanza mchakato wa kumpata wakandarasi watakaojenga majengo ya Ofisi za Mkoa wa Dar es Salaam na Mkoa wa Manyara (Babati) katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchakato mzima wa kujenga Ofisi mpya, pia katika bajeti ya 2005/2006 Wizara yangu imefanya ukarabati wa majengo ya Ofisi na nyumba za makazi ya watumishi katika vituo vya KIA, Namanga na Sirari na ukarabati wa paa la Ofisi ya Mkoa wa Kigoma umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ilitoa ahadi kuwa tungeajiri Maafisa Uhamiaji wapya 322 na kusomesha wengine 137 ili kuongeza idadi ya Maafisa Uhamiaji wenye ujuzi kazini. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba pamoja na nyongeza ya ajira mpya tuliyopata, Wizara yangu mwaka uliopita, iliajiri Maafisa Uhamiaji wapya 330. Aidha, watumishi 137 wako katika vituo mbalimbali vya hapa nchini na nje ya nchi wakihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali katika kipindi cha 2005/2006, Idara ya Uhamiaji imekabiliwa na matatizo mbalimbali yakiwemo ufinyu wa bajeti, uchakavu na ukosefu wa vyombo vya usafiri kwenye baadhi ya Mikoa, Wilaya na Vituo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupunguza tatizo hilo, Wizara imenunua magari 30, Pikipiki 10 na kuyasambaza katika Mikoa mbalimbali, pia na mitumbwi mitatu yenye injini imenunuliwa kwa ajili ya doria kwenye mwambao wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapambano dhidi ya rushwa ndani ya Idara ya Uhamiaji yanaendelea. Katika mwaka 2005/2006, Idara ya Uhamiaji iliendesha Semina iliyohudhuriwa na Maafisa Uhamiaji wapya 330 waliokuwa kwenye mafunzo ya awali katika Vyuo vya *CCP – Moshi* na Magereza Kiwira juu ya athari za mianya ya rushwa katika utoaji wa huduma za Uhamiaji. Idara pia inaendelea kuuelimisha ummaa juu ya utaratibu wa utoaji wa huduma za Uhamiaji ili kuweka uwazi kwa kila mteja anayhudumiwa. Suala la wananchi wetu kutumia watu wa kati (wakala) kupata huduma zetu linaendelea kupigwa vita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki tumeanzisha utaratibu wa kutoa Visa stickers katika vituo vya *J. K. Nyerere International Airport, ZIA, KIA* na Namanga; pia Balozi zetu za London, The Hegue, Roma, Washington na Paris. Hii ni awamu ya kwanza ya zoezi hili ambalo litaendelea mwaka huu wa fedha (2006/2007) ambapo litahusisha Ofisi zetu zote za Balozi na vituo vyote vya mipakani. Hatua hii itadhibiti mapato yatokanayo na utoaji wa Visa kwa wageni wanaoingia nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matarajio ya mwaka 2006/2007. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Idara ya Uhamiaji inakusudia kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kufanya ukarabati wa majengo katika vituo vya Manyovu, Mabamba, Rusumo, Mkoa wa Pwani, Sirari na Kilimanjaro.

(ii) Ununuzi wa magari 20, Pikipiki 30, Boti 4 na Jenereta 15.

(iii) Kuanza ujenzi wa Ofisi za Mikoa ya Dar es Salaam, Manyara, Mtwara na Kituo cha Kagunga Mkoani Kigoma na kukarabati Jengo la Ofisi ya Mkoa wa Dodoma.

(iv) Kuanza utekelezaji wa mradi wa vitambulisho vya Uraia, ikiwa ni pamoja na kupata watumishi wenye ujuzi, kuanza ujenzi wa Jengo la Mradi huo, na kupata mzabuni atakayetengeneza vitambulisho hivyo.

(v) Kuajiri Maafisa wapya 143 na kuwapeleka watumishi 140 kwenye kozi mbalimbali za kujiendeleza za muda mrefu na mfupi.

(vi) Kuendeleza zoezi la kutoa Visa stickers kwenye vituo vingine 17 vya kuingilia nchini pamoja na kuzihusisha Ofisi za Balozi zetu zote.

(vii) Kuanzisha Chuo cha Taifa cha Uhamiaji, *(National Immigration Training Institute)* huko Moshi. Hiki kitakuwa Chuo cha kwanza cha aina hii hapa nchini tangu tupate Uhuru. Chuo kitatoa mafunzo ya fani ya Uhamiaji kwa Maafisa wa ngazi za kati na ngazi za juu. Mafunzo ya awali (recruit) yataendelea kutolewa katika Chuo cha Polisi Moshi na Chuo cha Magereza – Kiwira.

Mheshimiwa Spika, Huduma kwa Wakimbizi. Katika mwaka 2005/2006 nchi yetu imeendelea kuhifadhi maelfu ya mamia ya wakimbizi toka nchi za Burundi, *DRC,* Somalia na kwingineko. Wakimbizi hao wako katika Mikoa ya Kagera, Kigoma, Rukwa, Tabora na Tanga. Hadi kufikia tarehe 30 Mei, 2006 jumla ya wakimbizi wote wanaohifadhiwa nchini katika makambi 11 na maeneo ya makazi (4) walikuwa ni 554,973. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuimarika kwa hali ya amani na utulivu katika nchi za Burundi na *DRC,* idadi ya waomba hifadhi wapya wanaopokelewa toka nchi hizo imepungua sana hadi kufikia chini ya elfu moja katika kipindi cha kuanzia Julai, 2005.

Hata hivyo, Serikali yetu ilikataa kuwapa hifadhi ya ukimbizi wananchi wa Burundi wapatao 10,500 walioingia nchini mwezi Machi na Aprili, 2006 ambao baada ya kuwahoji ilionekana dhahiri walikuwa wanakimbia njaa sio mapigano. Hata hivyo kwa sasa wote hao wamesharejea nchini kwao baada ya chakula cha msaada kuanza kutolewa na Umoja wa Mataifa katika maeneo waliyoyakimbia nchini mwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2005/2006 utekelezaji wa zoezi la kuwarejesha wakimbizi wa Burundi na *DRC* kwenye nchi zao za asili uliendelea. Aidha, mpaka tarehe 30 Aprili, 2006 jumla ya wakimbizi 215,000 wa Burundi na 17,382 wa *DRC* walikuwa wamesharejea. Hata hivyo, urejeaji wa wakimbizi wa Burundi uliathiriwa na hali ya ukame na njaa katika nchi hiyo.

Kwa upande wa *DRC,* kasi ndogo ya urejeaji imesababishwa na hofu ya hatma ya uchaguzi mkuu utakaofanyika mwisho mwa mwezi huu, pia kutumiwa kwa meli moja tu ya *Mv. Mwongozo* ya *TRC* katika Ziwa Tanganyika yenye uwezo wa kusafirisha wakimbizi 500 kwa safari moja. Ili kasi ya zoezi hilo iweze kuongezeka, tunaangalia uwezekano wa kupata meli za ziada za kubeba wakimbizi; pia ni mategemeo yetu kuwa iwapo uchaguzi wao mkuu utafanyika kwa amani, hali hii itawavutia wakimbizi wengi kurudi makwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yanayodumaza utekelezaji wa zoezi la urejeaji wa wakimbizi yamekuwa yakijadiliwa na Kamisheni mbili za kuratibu zeozi la urejeaji kati ya Tanzania, Burundi na *DRC* ambazo zimekuwa zikikutana kujadili utekelezaji.

Mwezi Mei, 2006, tulikuwa na Kutano wa Tume ya Pamoja *(Tripartite Commission)* kati ya *DRC,* Tanzania na *UNHCR*. Mkutano ambao tulikubaliana pamoja na mambo mengine, kurekebisha gati ya Kigoma ili meli zisogee karibu zaidi kwenye ukingo wa Ziwa, kuzidisha juhudi za kuhamasisha Wakimbizi ili warudi *DRC* na kwamba *UNHCR* waongeze vituo vya mapokezi ya wale watakaorejea makwao ikiwa ni pamoja na misaada mingine ya kuanzia maisha, kama vile chakula. Tunatazamia utekelezaji wa kasi utaanza kuonekana mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa nchi yao utakaofanyika Mwezi Huu wa Julai, na hasa iwapo utafanyika kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea na jitihada za kuihuisha Sheria ya Wakimbizi ya mwaka 1998 *(Refugee Act No.9 of 1998)* ili iweze kulingana na Sera ya Taifa ya Wakimbizi pamoja na mabadiliko mengine. Zoezi hilo halikukamilika katika mwaka 2005/2006 kwa sababu ya kutoa nafasi ya kuwahusisha kikamilifu wadau mbalimbali katika mchakato huo. Matarajio yetu sawsa ni kukamilisha zoezi hilo katika mwaka huu wa 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetoa Uraia kwa Wakimbizi wa Somalia 281 ambao ni Wabantu wenye asili ya Kizigua na ambao wako katika makazi ya Chogo, Handeni, Mkoani Tanga. Aidha, bado tunashughulikia maombi mengine ya Uraia ya wakimbizi hao. Hapa nchini hatuna sera ya kutoa Uraia kwa wakimbizi. Hata hivyo uamuzi wa kuwapa Uraia wakimbizi wa Somalia, ni wa kipekee; na unatokana na ukweli kuwa Wakimbizi hawa pamoja na kuishi Somalia kwa zaidi ya miaka 200, asili

yao ni Tanzania (ni Wazigua) na wameonesha nia thabiti ya kuendelea kuishi hapa nchini hata kama hali ya amani na utulivu itarejea nchini Somalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza ya mradi wa kukabiliana na athari za wakimbizi katika Mkoa wa Kigoma na Wilaya ya Ngara, (Mkoani Kagera), ambao unafadhiliwa na Serikali ya Denmark, Serikali hiyo imekubali kufadhili awamu ya pili ya mradi huo ambao utagharimu Shilingi za Tanzania bilioni 10.9 *(Danish Kronor M.60).* Uamuzi wa kuendelea na mradi huo umechukuliwa baada ya tathmini ya awamu ya kwanza kuonesha mafanikio na Serikali ya Denmark kuridhika nayo. Aidha, Wizara itaendelea kuiomba Jumuiya ya Kimataifa kuendelea kusaidia maeneo yaliyoathiriwa na wakimbizi hususan katika nyanja za hifadhi ya mazingira, ukarabati wa miundombinu, ujenzi na ukarabati wa Zahanati, Maji, Shule na Sekta nyingine za kupunguza umasikini. Haya yakifanyika kwa kiwango kikubwa, itakuwa ni aina ya fidia au kifuta machozi kwa mzigo mkubwa wa kuhifadhi Wakimbizi walioubeba wananchi wa maeneo hayo kwa miaka mingi kwa niaba ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu hivi karibuni imeridhia ombi la Serikali ya Marekani kuwahamishia nchini mwao (Ressettlement) Wakimbizi 15,000 wa Burundi waishio katika Mikoa ya Kigoma na Kagera. Wakimbizi hao ni wale waliokimbilia nchini katika miaka ya 1970; Serikali imekubali ombi hili kwa kuwa hatua hii inatupunguzia mzigo wa kuhudumia wakimbizi hapa nchini. Utekelezaji wa zoezi hili utakaoanza mwaka huu utahusisha *UNHCR* pamoja na Shirika la *International Organization for Migration (IOM).* Serikali itahakikisha kuwa utekelezaji wa zoezi hilo unafanywa kwa umakini ili kutoathiri zoezi la urejeaji wa wakimbizi wengine wa Burundi linaloendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza msongamano magerezani, Wizara yangu itaendeleza utekelezaji wa programu ya Huduma ya Jamii *(Community Service)* ambayo malengo yake ni kuwezesha wafungwa wenye makosa madogo madogo na wanaofungwa kifungo kisichozidi miaka mitatu, kutumikia adhabu zao katika jamii wakifanya kazi za jamii bila malipo. Katika kipindi hiki programu hii imeanza kutekelezwa katika Mikoa sita ya majaribio (Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Mtwara na Kilimanjaro), jumla ya Wafungwa 273 wanatumikia vifungo vyao nje ya Magereza wakitumikia jamii. Mwaka huu wa fedha tunapanua programu hii ili vile vile itumike katika Mikoa ya Kagera, Shinyanga, Mara, Tanga, Arusha na Iringa.bila malipo. Lengo la programu hii Mheshimiwa Spika, ni kwamba wafungwa watakaokuwa wakihukumiwa chini ya sheria hii wasiingie Magerezani bali waende moja kwa moja Vijijini au mitaani kwao na kupewa kazi za kutumikia jamii na hivyo kupunguza msongamano magerezani na pia kuishirikisha jamii katika kurekebisha tabia za wahalifu.

Mwaka wa fedha 2006/2007 utaratibu huu utapanuliwa ili utumike katika Mikoa mingine sita ya:- Kagera, Shinyanga, Mara, Tanga, Arusha na Iringa. Azma ya kuipeleka programu hii mara moja katika mikoa yote nchini bado inashindikana kutokana na ufinyu wa bajeti unaoikabili programu yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ngazi ya Mikoa na Wilaya, utekelezaji wa programu ya Huduma kwa Jamii una matatizo makubwa kutokana na watekelezaji wakuu, yaani Watumishi wa Kada ya Ustawi wa Jamii *(Probation Officers)* ni waajiriwa wa Wizara ya Afya naUstawi wa Jamii hivyo katika mazingira haya ya utendaji. Sekretarieti ya Huduma kwa Jamii na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ujumla, hatuna mamlaka ya moja kwa moja katika kuwasimamia watumishi hao. Tatizo hili linatafutiwa ufumbuzi na Serikali kwa kuzishirikisha Wizara za Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mambo ya Ndani, Afya na ustawi wa Jamii, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Msajili wa Vyama vya kijamii inaendelea na kazi ya kuchambua na kuandikisha Vyama vya hiari vya kijamii *(Associations)* pamoja na madhehebu ya dini. Idadi ya Asasi hizo imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka na kwa sasa kuna jumla ya Vyama vya hiari 13,325 vilivyosajiliwa. Wizara yangu inafanya uchambuzi wa vyama hivyo ili kubaini uhai wao. Vyama 1,230 tayari vimebainika kutokuwa hai. Zoezi la kuchambua uhai wa vyama hivyo ni la msingi na bado linaendelea hasa ikizingatiwa kuwa vyama vingine vimeandikishwa muda mrefu uliopita tangu 1954.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu naomba nitoe shukrani za pekee kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe, Mbunge wa Mtama, ambaye amenisaidia vizuri sana kuendesha kazi za Wizara na kila mara amekuwa hachoki kunipa ushauri na ushirikiano wenye manufaa makubwa kwa Wizara.

Aidha naomba kutoa pia shukrani zangu kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ndugu Solomon Odunga, Kamishna Mkuu wa Magereza, Mkurugenzi wa Uhamiaji, Mkurugenzi wa Idara ya Wakimbizi, Kamishna wa Zimamoto, na wafanyakazi wote wa Wizara ambao kwa ushirikiano wao wamewezesha Bajeti hii kuandaliwa. Aidha natoa shukrani kwa Ndugu Bakari Mahiza aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii ambaye hivi karibuni amehamia Wizara ya Usalama wa Raia kwa wadhifa huo huo, kwa juhudi zake wakati wote alipokuwa nasi na kwa ushirikiano anaouendeleza mpaka sasa.

Namshukuru kwa namna ya pekee Waziri aliyenitangulia Mhe. Balozi Omar Ramadhan Mapuri kwa kunilea nilipokuwa Naibu Waziri chini yake katika Wizara hii, na hatimaye kunikabidhi Wizara hii ikiwa na misingi imara ya utendaji kazi.

Napenda pia kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Manyoni Mashariki kwa kunipa ridhaa ya kuwawakilisha Bungeni kwa kipindi cha pili, nikiwa Mbunge wa kwanza kupewa kipindi cha pili katika Jimbo letu tangu tupate Uhuru. Nawashukuru sana kwa imani hii nami naahidi sitawaangusha.

Namshukuru pia Mhe. Rais kwa kuniteua kuongoza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, haijapata kutokea Waziri kurudia katika Wizara hii, lakini safari hii imetokea.

Nashukuru sana. Naahidi kwamba nitatimiza wajibu wangu kwa bidii, haki na uadilifu wa kiwango cha juu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wahisani wote ambao misaada yao imeiongezea nguvu Wizara yangu katika kutekeleza majukumu yake. Wahisani hao ni pamoja na *USA,* Netherlands na Dernmark. Napenda pia niyashukuru Mashirika ya Kimataifa ya *UNHCR, UNAFRI, WFP, IOM,* na *UNDP* pamoja na wote ambao kwa njia moja au nyingine wanaendelea kuisaidia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lituwezeshe kutekeleza hayo yote niliyoyaeleza kwa kupitisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya jumla ya Shilingi 96,181,748,000/= kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007 kama ifuatavyo:-

**Fungu 29 - Magereza.**

| | | |
|---|---|---|
| Mishahara *(PE)* | Sh. | 23,292,008,000/= |
| Matumizimengineyo *(OC)* | Sh. | 42,322,000,000/= |
| Matumizi ya Maendeleo | Sh. | 5,260,001,000/= |
| **JUMLA............................** | **Sh.** | **70,874,009,000/=** |

**Fungu 51 - Utawala.**

| | | |
|---|---|---|
| Mishahara *(PE)* | Sh. | 1,633,520,000/= |
| Matumizi mengineyo *(OC)* | Sh. | 2,817,800,000/= |
| Matumizi ya Maendeleo | Sh. | 2,266,000,000/= |
| **JUMLA ..................** | **Sh.** | **6,717,320,000/=** |

**Fungu 93 - Uhamiaji**

| | | |
|---|---|---|
| Mishahara *(PE)* | Sh. | 4,425,621,000/= |
| Matumizi mengineyo *(OC)* | Sh. | 8,801,800,000/= |
| Matumizi ya Maendeleo | Sh. | 5,362,998,000/= |
| **JUMLA .................** | **Sh.** | **18,590,419,000/=** |

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. WILLIAM J. KUSILA – MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni Na.

81(1), Kanuni ya Bunge, Toleo la 2004, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika Mwaka wa Fedha 2005/2006 pamoja na Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2006/2007 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii ni taarifa ya kwanza ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama katika Serikali ya Awamu ya Nne, kwa niaba ya Kamati nzima napenda kwanza kabisa kumpongeza Mheshimwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa ushindi mkubwa alioupata katika Uchaguzi Mkuu wa Rais na Wabunge. Napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kuwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Amani Karume, Rais wa Zanzibar kwa ushindi mkubwa alioupata katika Uchaguzi Mkuu uliopita. Nampongeza pia Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa Mb. kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu uteuzi ambao ulithibitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nakupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa na Bunge hili kwa kura nyingi. Aidha, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimwa Anne S. Makinda Mb. kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Vile vile pongezi mahsusi ni kwa Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama Mb. ambaye sasa amekalia kiti cha Mheshimiwa Spika, na Mheshimiwa Job Yustino Ndugai Mb. Kwa kuchaguliwa kwao katika nyadhifa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama inampongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa CCM Taifa.

Aidha, naungana na wasemaji waliotangulia kuwapongeza wale wote walioteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa Luteni Mstaafu, Yusuf Rajab Makamba, kwa kuteuliwa kwake kuwa Katibu Mkuu wa CCM. Mheshimiwa Kapteni Jaka Mwambi, kuwa Naibu Katibu Mkuu Tanzania Bara.

Wengine ninaowapongeza ni pamnoja na Mheshimiwa Rostam Aziz, kwa kuwa Katibu wa Uchumi na Fedha, Mheshimiwa Aggrey D. Mwanri, kuwa Katibu wa Itikadi na Uenezi, Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro, kuwa Katibu wa Siasa na Uhusiano wa Kimataifa na Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, kuwa Katibu wa Oganaizesheni wa CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza tena Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa jinsi anavyoshughulikia matatizo yanayolikabili Taifa letu kama vile wimbi la ujambazi, mfumuko wa bei ya mafuta, baa la njaa, tatizo la umeme na mengi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo maalumu, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Maoni na Ushauri wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama yanatokana na Taarifa iliyowasilishwa na Mheshimiwa Kaptein John Zephania Chilligati,

Mb. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, mbele ya Kamati, tarehe 31 Mei, 2006. Jijini Dar es Salaam. Katika kuijadili na kuichambua taarifa ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka 2006/2007 Kamati ilipitia mafungu yafuatayo:-

1. Fungu 29 – Magereza;
2. Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; na
3. Fungu 93 – Uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa maoni na ushauri wa Kamati, naomba kuwapongeza, Mheshimiwa Kapteni John Zephania Chilligati, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Ndugu Solomon Odunga, Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wataalamu wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya licha ya matatizo kadhaa wanayokabiliana nayo. Nawapongeza pia Maafisa wa Jeshi la Magereza na askari wote kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na utiifu wao kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Ahadi za Serikali katika Bunge la bajeti la mwaka 2005/2006 na Taarifa ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama katika Bunge la Bajeti la 2005/2006. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imetekeleza ahadi zake kwa sehemu kubwa. Aidha, kuhusu utekelezaji wa Ushauri na Maoni ya Kamati ya Bunge na ulinzi na Usalama kwa Mwaka 2005/2006, Kamati imeelezwa kuwa ushauri ulizingatiwa na unaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii, Kamati ilielezwa kuwa ili kutekeleza kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa Fedha 2006/2007, Wizara inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe matumizi jumla ya shs. 96,181,748,000/= kwa mafungu yote matatu ya Wizara hii kama alivyochanganua mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza kuhusu taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya ndani ya nchi kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006; na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007, sasa naomba kutoa Maoni na Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Ili kupunguza msongamano wa wafungwa Magerezani, Kamati inashauri kuwa mpango wa Serikali wa kujenga Magereza mapya uendelee kama ilivyokuwa imeshauriwa na Kamati hii mwaka 2005/2006. Pamoja na ushauri huu, ni maoni ya Kamati hii kuwa kuna haja ya kuangalia uwezekano wa kutenganisha Wafungwa na Mahabusu ili kuongeza ufanisi katika Jeshi la Magereza. Sambamba na ushauri huu, wafungwa wenye umri mkubwa watenganishwe na wale wenye umri mdogo.

Kuhusu masharti magumu ya dhamana kwa mahabusu, Kamati inashauri kuwa tatizo la Mahakimu kuweka masharti magumu ya dhamana litafutiwe ufumbuzi wa haraka kutokana na hali yenyewe Magerezani kuwa mbaya. Sambamba na ushauri huo,

pale ambapo sheria imetaja adhabu za kifungo na adhabu zisizokuwa za kifungo tu. Mahakama itoe adhabu zisizokuwa za kifungo pale inapowezekana badala ya kutoa adhabu ya kifungo tu.

Kwa kuwa Jeshi la Magereza lina jukumu zito la kuwahifadhi na kuwalinda wafungwa na mahabusu wasitoroke, na kwa kuwa hata katika Wilaya mpya hupatikana wahalifu waliohukumiwa kifungo, Kamati inashauri kuwa Wilaya mpya zipatiwe Magereza yao. Aidha, kwa Mkoa wa Dar es Salaam, ni maoni ya Kamati kuwa Serikali iangalie uwezekano wa kujenga Mahakama karibu na Gereza Kuu la Ukonga. Kwa kufanya hivyo:-

- Kwanza, tatizo la msongamano wa wafungwa litakuwa limepatiwa ufumbuzi

- Pili, itapunguza gharama ya mafuta na matengenezo ya magari ambayo hutumika kuwasafirisha mahabusu kwenda Mahakama zilizopo hivi sasa.
- Tatu, itapunguza uwezekano wa wafungwa kutoroka wakati wanaposafirishwa kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

4. Kamati hii ilipojadili taarifa ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, iliona kuna haja ya kupunguza ugumu wa masharti ya dhamana kwa njia ya Sheria. Kamati inashauri kuwa kwa kuzingatia aina ya kosa lenyewe, masharti ya dhamana yalegezwe kwa mtuhumiwa.

5. Kwa vile hutokea baadhi ya watuhumiwa huwekwa mahabusu kwa kubambikiziwa makosa kwa makusudi, Kamati inashauri kuwa askari wenye tabia hiyo mbaya ya kubambikizia makosa wachukuliwe hatua kali mara watakapobainika kufanya hivyo.

6. Kwa kuwa Mpango wa Parole mpaka sasa umewasaidia watu wachache kinyume na ilivyotarajiwa, Kamati inashauri kuwa Muswada wa Sheria inayolenga kupanua wigo wa Mpango wa Parole kama ilivyoelezwa na mtoa hoja uharakishwe ili kupunguza tatizo la msongamano Magerezani.

7. Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Huduma kwa Jamii (Community Service) kama njia ya kupunguza msongamano Magerezani, Kamati inashauri kuwa uandaliwe utaratibu wa wataalamu wa Huduma za Jamii na Maendeleo ya Jamii walioajiriwa katika Utumishi wa Umma kuwatumia wafungwa wanaofungwa kifungo kisichozidi miaka mitatu, katika Miradi ya Maendeleo ya Jamii. Vile vile Kamati inashauri kuwa mpango wa kutekeleza Sheria ya Huduma kwa Jamii ambao umeanza kutumika katika mikoa sita:- Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Mtwara na Kilimanjaro uharakishwe katika mikoa mingine.

8. Kamati imebaini kuwa kutokutana kwa Kamati za Wilaya na Mikoa za kusukuma kesi, ni miongoni mwa sababu za msongamano mkubwa Magerezani. Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama inashauri kuwa Serikali itoe maelekezo na kuhakikisha kuwa Kamati hizi zinakutana kwa wakati na kutekeleza jukumu hili muhimu.

9. Hivi karibuni Kamati ilipata fursa ya kutembelea vyombo vya Ulinzi likiwemo Jeshi la Magereza. Katika ziara hiyo Kamati ilibaini tatizo la upungufu mkubwa wa nyumba za askari Magereza jambo ambalo athari yake ni kubwa kiutendaji.

Ili kutatua taizo kubwa la nyumba na makazi ya askari, na kwa kuzingatia haja ya kutumia vizuri ardhi, pamoja na udhibiti mzuri katika utendaji wa ki-askari, Kamati inashauri kuwa uandaliwe Mpango wa Ujenzi wa Maghorofa kwa ajili ya makazi ya askari. Katika kutatua tatizo hili Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama vile *NSSF, LAPF* na mengineyo ihamasishwe kujenga makazi hayo na kuwapangisha askari kama inavyofanya kwa taasisi nyingine za umma.

10. Aidha, Kamati iligundua kuongezeka kwa wafungwa waliohukumiwa kutokana na makosa ya kujamiiana jambo ambalo linachangia kuwepo kwa msongamano Magerezani. Ni maoni ya Kamati hii kuwa; kwa kuwa idadi ya wafungwa wanaohukumiwa kwa makosa ya kujamiiana inaongezeka, Sheria ya Makosa ya Kujamiana inapaswa kuboreshwa. Vile vile elimu kuhusu sheria hii itolewe kwa wananchi.

11. Taarifa iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mbele ya Kamati ilieleza hatua za kuboresha huduma za wafungwa Magerezani. Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi zake katika hatua hizo. Pamoja na hivyo Kamati inashauri kuwa kasi ya kuboresha malazi ya wafungwa ikiwa ni pamoja na kutumia vitanda vya *"double deka"* iongezeke zaidi kwa kuzingatia haki za binadamu.

12. Kwa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2006/2007 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linatarajia kukamilisha sheria mpya ya Jeshi hilo ikiwa ni pamoja na kuanzisha "Commanding Post" katika kila Mkoa, Kamati inashauri kuwa utekelezaji wa malengo hayo ufanyike haraka sambamba na ununuzi wa magari ya kutosha kwa ajili ya Zima Moto na Uokoaji. Kuhusu Utumishi katika Jeshi hili, Kamati inashauri kuwa Muundo wa Utumishi (Scheme of Services) katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji uwekwe wazi ili kubainisha taratibu za kutoka cheo kimoja kwenda kingine.*(Makofi)*

13. Kuhusu idara ya Uhamiaji ni maoni ya Kamati kuwa chumba kinachotumika kutayarishia Hati za Kusafiria hakina nafasi ya kutosha kwa ajili ya kazi inayofanyika. Sambamba na maoni hayo Kamati inashauri kuwa samani na vitendea kazi viongezwe kwa ajili ya kuongeza ufanisi. Vile vile Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi zake za kudhibiti ukaaji wa wageni haramu nchini. Hata hivyo ni maoni ya Kamati kuwa operesheni za kijeshi za pamoja zitumike kudhibiti tatizo hili la ukaaji wa wageni haramu.

14. Kwa kuwa ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la Wakimbizi ni Wakimbizi kurejea makwao Kamati inashauri kuwa juhudi za kuwarejesha Wakimbizi makwao ziendelezwe.

15. Kwa vile kuna taarifa kuwa Upembuzi yakinifu uliolenga kujua namna nzuri ya utoaji vitambulisho umekamilika. Kamati inashauri kuwa kasi ya kutekeleza zoezi hili iongezeke ili vitambulisho vya Watanzania viweze kupatikana kwa haraka.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, haya ndiyo maelezo ya uchambuzi wa Kamati yangu kwa muhtasari. Kama yapo maeneo mengine ambayo sikuweza kuyasugia, natumaini Wajumbe wa Kamati hii pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine watayazungumzia pale watakapopata fursa ya kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii kuwasilisha maoni ya Kamati katika kipindi hiki cha bajeti ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Nne. Napenda pia kukupongeza kwa mwanzo mzuri wa uongozi wako katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, napenda nimpongeze Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mb. Naibu Spika kwa mwanzo mzuri wa uongozi wake wakati wote unapomwachia madaraka kuendesha Shughuli za Bunge. Naomba pia kuwapongeza Wenyeviti, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama na Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mb. kwa kuanza uongozi wao vizuri mara zote ulipokasimu madaraka kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukuwa fursa ya pekee kabisa kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa michango yao mizuri sana na ya kina wakati wa kuichambua bajeti ya Wizara hii na naomba niwatambue kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika, Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Kanal Saleh A. Farrah, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Dr. John S. Malecela, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Kanali Feteh S. Mgeni, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Muhammad I. Sanya na Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda.*(Makofi)*

Mwisho kabisa, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Bwana Damian S. L. Foka na Makatibu wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Ndugu Elisa Mbise na Ndugu Athuman Hussein kwa kuihudumia vema Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA – MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi 2006/07 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(c) na 81(1) Toleo la mwaka 2004. Naomba Taarifa hii kwa vile imewasilishwa mezani inukuliwe Hansard kama ilivyo hata kama sitakuwa nimemaliza kuisoma.

Aidha, napenda kutoa pongezi za dhati kwako wewe Mheshimwa Spika, na Naibu Spika, Mhe. Anna Makinda kwa kuchaguliwa kushika nyadhifa hizo. Vile vile kwa Mheshimiwa Job Yustino Ndugai Mb. na Mheshimiwa Jenista J. Mhagama Mb. kwa kuwa Wenyeviti wa Bunge letu. Tuna imani kubwa na nyinyi na tunaamini kuwa mtaitumia imani hiyo kujenga Bunge lililo huru, la haki na lenye uwezo wa kweli wa kusimamia Serikali katika utendaji wa kazi za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kwa kuwashukuru tena wazazi wangu kwa malezi bora na elimu walionipa ambayo imeongeza mwangaza katika maisha yangu. Vile vile familia yangu yote kwa upendo, usapoti, ushirikiano na ushauri katika kila siku ya maisha yangu. Bila ya kuusahau uongozi wa chama changu Taifa na Mkoa vile vile wanachama wenzangu na Wabunge wenzangu kwa ushirikiano wanaonipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti napenda kuchukua nafasi hii kwa mara nyingine tena. Kukishukuru chama changu CHADEMA kwa kunichagua kuwa Mbunge Viti Maalum. Ninaamini hii ni changamoto kubwa kwangu nitahakikisha kuwa naitukuza heshima hii kubwa waliyonipa kwa kukitumikia Chama changu na Watanzania wote kwa uadilifu mkubwa tena bila woga. Nachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa uongozi wa Kambi ya Upinzani kuniteua kuwa Msemaji Mkuu wa Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Naahidi nitatekeleza wajibu wangu kwa uwezo wangu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapongeza kwa dhati kabisa Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Chilligati na Naibu wake Mheshimiwa Bernard Membe, kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi naomba sasa nijadili hoja ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama ilivyowasilishwa kwako muda mchache uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Magereza ni mojawapo ya Idara muhimu katika Serikali yetu ya Tanzania, kutokana na umuhimu wake kwa maendeleo ya jamii yetu. Baada ya wazee wetu kulikomboa Taifa letu na nchi yetu kuwa huru, dira ya Idara hii ilibadilika na kuwa mfumo wa kurekebisha raia waliopatikana na hatia ya kuvunja sheria za nchi ili watokapo gerezani wawe raia wema katika jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Inasikitisha sana kuwa hadi kufikia sasa, karibia miaka arobaini na tano tangia tupate uhuru wetu, mfumo wa uendeshaji wa Magereza yetu bado haujaweza kutofautiana na ule wa wakati wa kikoloni. Kuanzia majengo, mazingira ya

kuishi wafungwa na wasimamiza wao, mazingira ya kazi, chakula, fikra za watendaji wa Idara hii na hata baadhi ya sheria, bado hazitofautiani sana na hali ya wakati wa ukoloni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha zaidi ni kuwa katika masuala mengine hali imekuwa mbaya zaidi kuliko wakati ule. Kwa kweli hali ya Idara ya Magereza ni mbovu kiasi cha kugeuka kuwa hatari kwa wafungwa na hata askari wetu tuliowapa jukumu la kuisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa ripoti mbalimbali zinazotolewa na asasi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa, Magereza yetu yamekuwa yakilalamikiwa kwamba yanaongoza kwa uvunjaji wa misingi ya haki za kibidamu wakati umefika wa kutambua kwamba walio ndani ya kuta zile za magereza ni binadamu kama sisi na wanastahili haki kama binadamu wengine kupatikana na hatia ya kuvunja sheria za nchi hakumfanyi mtu kuondolewa utu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msongamano wa kutisha wa wafungwa katika Magereza yetu ni tatizo kubwa ambalo kila siku tunaambiwa kuwa linatafutiwa dawa. Wakati akiwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara hii ya 2005/2006, Mheshimiwa Waziri alikiri kuwa hadi kufikia tarehe 1 Aprili, 2005, Magereza ya nchi yetu yalikuwa na wafungwa na mahabusu 44,985, huku uwezo wake ni wafungwa 22,699. Taarifa zingine zinaonyesha kwamba Magereza ya Maswa, Babati na Kahama kwa pamoja yaliripotiwa mnamo tarehe 01/08/2005 kuwa na msongamano wa zaidi ya asilimia 100. Hii inatisha Mheshimiwa Mwenyekiti.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mahabusu nalo ni tatizo kubwa. Wengi wa mahabusu wanarundikwa kama mizigo katika vyumba vidogo vyenye hewa finyu ambavyo kwa kweli havina hadhi ya kutumiwa na binadamu. Na mbaya zaidi, mahabusu wengi wamekuwa wakiswekwa pamoja na wafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni maana siku hizi hatujui tofauti ya mtuhumiwa na mhalifu? Kumchanganya mtuhumiwa katika gereza ambalo anapaswa kuwepo mhalifu kama sheria za nchi zisemavyo, ni kinyume cha sheria na ukiukwaji mkubwa wa haki za kibinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tatizo hili sio tu linanyanyasa Watanzania, lakini pia linajenga chuki miongoni mwa jamii dhidi ya vyombo vya dola na Seikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ni lazima ichukue maamuzi mazito katika sekta ya Mahakama zetu ili kushughulikia matatizo ya kisheria yanayowakumba ndugu zetu waliopo katika Magereza yetu. Kesi nyingi hazisikilizwe kwa madai kwamba upelelezi bado unaendelea. Watu wanakaa mahabusu zaidi ya miaka sita kwa kisingizio cha upelelezi kutokamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano halisi ni kuhusu mwanamama mmoja mwenye jina la Illuminata, wa Songea ambaye tangia mwaka 2001 hadi hivi sasa amekuwa akisote mahabusu bila ya kesi yake kushughulikiwa ipasavyo. Taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu iliyotembelea zaidi ya Magereza 40 nchi nzima mwaka 2004, inaonyesha dhahiri kesi za aina hii. Ndugu huyo amepelekwa Mahakamani kwa mara ya mwisho mnamo mwezi Desemba 2004 na hadi sasa bado anateseka mahabusu. Mbaya zaidi ni kuwa kama mtu huyo akikutwa hana hatia Serikali itakwepa kumlipa fidia kwa kumuweka mahabusu muda wote huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine sugu katika Magereza yetu ni lile la chakula ambacho Serikali yetu inatoa. Chakula kinachotolewa Magerezani hakina hadhi ya kuitwa chakula cha binadamu. Ni dhambi kwetu sote hapa kukaa na kuangalia binadamu mwenzetu anapewa lishe duni na hatari kwa afya yake kama vile yeye sio binadamu kama sisi. Watanzania wanapaswa kujua nini haswa tatizo. Hivi kuna ugumu gani kwa ndugu zetu hawa kupatiwa chakula chenye thamani ya kupewa binadamu. Hata kukipika kikaiva inakuwa tatizo ukiachilia mbali dozi ya ugali na maharage wanayopambana nayo kila kukicha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kuchanganya watoto walio chini ya miaka 18 na wahalifu wakubwa waliokubuhu kwa kweli si kitendo cha busara kwa maslahi ya Taifa letu. Kuwachanganya watoto hawa katika gereza moja na wafungwa watu wazima ni kuhatarisha usalama wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto hawa watokapo mle Magerezani wengi huishia kuwa wahalifu sugu na hatari kuliko hata walimu wao wanaowakuta katika Magereza hayo. Watoto hawa kwa kweli ni lazima waondolewe kule bila ya kuchelewa. Tukiendelea na makosa haya hapo baadae vijana hawa watatukumbusha tuliyowatendea sasa na sijui tutawajibu nini kama watatupa hata hiyo nafasi ya kuwajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watoto wetu hawa wamekuwa wakitoka katika Magereza haya wakiwa na hadithi za kusikitisha mno. Wengi wao wamekuwa wakikumbwa na matatizo yanayowafanya kutothamini tena utu wao. Wapo wanaotoka na magonjwa ya zinaa, wapo wanaochanganyikiwa kiakili na wapo wanaotoka huko wakiwa vilema wa kijinsia. Ingawa Serikali yetu inadai kuwa hakuna udhalilishaji wa kijinsia wanaofanyiwa wafungwa wetu hasa watoto na vijana hawa, lakini ukweli hauwezi kufutika kwani ushuhuda wao upo. Watanzania walio wengi wanaishangaa Serikali yetu inavyojaribu kukanusha kuwepo kwa tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa kuwarekebisha watoto wetu ni lazima uchukuliwe kwa umakini wa hali ya juu. Ni aibu kuwa wakati idadi ya watoto wanaojikuta katika matatizo na Sheria ya *Children in Conflict with Law* kama sheria ya nchi yetu inavyowatambua, Idara ya Jela za Watoto imekuwa ikitelekezwa katika kila Bajeti ya nchi hii. Kwa kadri ya taarifa zilizopo, nchi yetu ina Gereza moja tu la vijana ambalo liko Wami na manne ya watoto yaliyopo katika Mikoa ya Arusha, Mbeya, Dar es Salaam na Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itueleze ina mkakati gani wa makusudi katika kupanua Magereza kwa ajili ya vijana na watoto na kutoa fedha za kutosha ili vijana na watoto hao ambao kwa bahati mbaya wanaingia kwenye uhalifu wapate malezi na huduma zinazostahili pindi wawapo Magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine linalowakabili wafungwa ni lile la magonjwa ya kuambukizwa. Watanzania wenzetu walio Magerezani wanasumbuliwa mno na magonjwa ya ngozi, ugonjwa wa Kifua Kikuu na mengine mengi ya kuambikizwa. Haya yote yanasababishwa na hali mbaya iliyokuwepo huko, lakini zaidi ni taratibu mbovu za matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na malalamiko kuwa utoaji wa matibabu kwa wafungwa sio mzuri kwani wafungwa hukosa dawa mpaka wengine wenye ndugu karibu hulazimika kununua dawa ingawa hilo ni jukumu la Serikali. Kinachosikitisha zaidi ni kuwa katika Bajeti ya Serikali hakuna mpango wowote unaoonesha nia ya Serikali yetu kuboresha huduma za afya kwa wafungwa wakati ni hivi karibuni tu pamoja na matatizo mengine Rais wetu aliahidi kulishughulikia tatizo hilo. Katika malengo ya Serikali mwaka huu, kiasi cha Shilingi bilioni mbili, msaada kutoka Benki ya Dunia, zimetengwa kwa ajili ya Mradi wa Kuzuia Ukimwi (*Tanzania Multi-Sectorial Aids Project)*. Ni vizuri Serikali ikatueleza ni jinsi gani fedha hizi zitakavyotumika na zitasaidiaje kuboresha mfumo mzima wa utoaji huduma na kupiga vita dhidi ya Ukimwi Magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipitisha sheria ambayo inatoa adhabu mbadala kwa mtuhumiwa yaani *Community Service Act 2002*. Sheria ambayo inamwezesha mtuhumiwa aliyehukumiwa kifungo cha chini ya miaka mitatu kutumikia kifungo chake kwa kufanya kazi za jamii. Inasikitisha kuona kuwa tangu kupitishwa hadi hivi sasa, bado mamlaka zinazohusika hazijaweza kutekeleza wajibu wake ipasavyo. Tunaishauri Serikali iboreshe sheria hii mara moja ili kuondoa urasimu wa utekelezaji wake.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ifanye mabadiliko makubwa katika sheria hiyo au iunde mfumo mwingine utakaokuwa huru na ambao hautaruhusu urasimu wa aina yoyote katika utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya *Parole Act* (1997), ni sheria nyingine ambayo kama ingetumiwa kwa ufanisi, ingepunguza sana msongamano uliopo Magerezani. Sheria hii ambayo inamruhusu mtuhumiwa mwenye hukumu ya zaidi ya kifungo cha miaka mitatu (3) kutumikia theluthi ya hukumu yake Gerezani na miaka inayobakia kutumikia kifungo cha nje kwa kufanya kazi za jamii, tunaitaka Serikali kuwaeleza watanzania ni sababu zipi zinazopelekea sheria hizi kutotumiwa ipasavyo hadi hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha programu hii, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni lazima ishirikiane kwa karibu na Idara ya Mahakama katika kubuni

mbinu mahiri zinazolenga kuondokana na kudorora kwa zoezi hilo. Lakini vilevile matumizi ya sheria hii yasiwe mlango mwingine wa rushwa na upendeleo kama ambavyo Watanzania wengi walivyoonyesha wasiwasi wao wakati ule tulipokuwa tunaianzisha. Ni lazima Bodi inayohusika na utekelezaji wa sheria hii ilazimike kufanya kazi zake kwa uwazi na ukweli. Wahusika wake lazima wapimwe kwa vigezo vya uadilifu kimatendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine linalohusiana na Idara hii ya Magereza ni kuhusu shughuli na miradi ya vitega uchumi na uzalishaji mali Magerezani. Wafungwa wetu wamekuwa wakifanya shughuli mbambali kama vile kilimo, useremala, ujenzi, ufugaji na kadhalika. Shughuli hizi zimekuwa chanzo kikubwa cha mapato Magerezani. Katika Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya mwaka wa fedha 2005/2006, kiasi cha Shilingi milioni 500 kilitolewa kwa ajili ya kuboresha viwanda vya Magereza na kiasi kama hicho kimeombwa kwa ajili ya mwaka wa fedha 2006/2007. Vilevile, jumla ya Shilingi milioni 400/= zilipitishwa mwaka 2005/2006 na Shilingi milioni 500 zimeombwa kwa mwaka 2006/2007 kwa ajili ya uboreshaji wa mashamba ya Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hatujapitisha mamilioni hayo kwa mwaka huu, Watanzania wanapaswa kujua yafuatayo:-

(i) Fedha zilizotengwa mwaka 2005 zimetumikaje na kama kuna fedha zozote kati ya hizo zimetumika tofauti na zilivyokusudiwa?

(ii) Hadi hivi sasa ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya wale wanaotuhumiwa kutumia vibaya fedha hizo kama taarifa mbalimbali zisemavyo na kama ni kweli hayo yametokea?

(iii) Miradi yote ya Magereza inayohusisha wafungwa imeingiza kiasi gani cha fedha kwa kipindi cha miaka mitano na fedha hizi zimetumikaje? Wafungwa wanaoshiriki katika miradi hiyo wanafaidikaje?

(iv) Mbona mapato hayo yasitumike katika kuboresha angalau chakula chao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa ni ukosefu wa shukurani kama hatutatambua jitihada za Serikali za kuboresha Idara ya Uhamiaji, ambayo ni Idara nyeti nchini kwa kuajiri vijana wengi wenye elimu ya juu na kuboresha vitendea kazi. Idara ya Uhamiaji bado ni kero kubwa kwa Watanzania. Mianya ya rushwa, uzembe na usumbufu usio wa lazima bado havijapatiwa dawa inayofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji vibali vya kazi *(work permits)* kwa wageni wasio na sifa ambao huchukua nafasi finyu za vijana wetu wa kitanzania katika soko la ajira ni moja ya matatizo ambayo bado kabisa hayajapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama tuna mpango wa kuwa na Shirikisho la Afrika Mashariki, hatuwezi kuendelea kuacha baadhi ya wakorofi wachache kuvunja

sheria zilizopo hivi sasa. Vitendo vyao hivi sio tu ni uhalifu, lakini pia vinajenga chuki kati ya vijana wa nchi zetu hizi ambao ndio wahusika na walengwa wakuu wa mchakato huu wa Shirikisho la Afrika Mashariki

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu kwa sasa iko chini ya Wizara ya Sheria. Lakini Ofisi hii inashughulika na kazi nyeti sana kwa usalama wa Watanzania na Taifa kwa ujumla. Utaratibu wa sasa katika Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu hauwezeshi Idara ya Uhamiaji kudhibiti watu wanaojiandikisha katika Kitengo cha Uzazi kama raia na hatimaye kupata *Passport* za Tanzania kwa njia ya udanganyifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vizazi na vifo linahusu uraia wa mtu na watu ambao wamebobea katika shughuli hiyo ni Idara ya Uhamiaji. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Kukihamisha kitengo hiki kutoka kwa Kabidhi Wasii Mkuu na kuwa chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ili kurahizisha utendaji kazi, udhibiti na kuondoa urasimu;

(ii) Kukifanya kitengo hiki kuwa Wakala anayejitegemea wenye kuwajibika kwa Wizara ya Mambo ya Ndani; na

(iii) Ku-*computerize* na ku-*link* shughuli zote zihusuzo kurekodi vizazi na vifo kwenye Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu, mahospitali ya Mikoa na Wilaya moja kwa moja na Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, zoezi la kuandikisha Vizazi na Vifo ni muhimu kwa uhai mzima wa Taifa. Ndiyo inayomtambulisha mtu kama raia na hivyo awe na haki ya *Passport* au aweze kushiriki kwenye shughuli ndani ya nchi kama vile uchaguzi wa ngazi mbalimbali na hata haki ya kupata ajira kama mwananchi katika nchi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya wageni wanakuja nchini kwa shughuli za matembezi, masomo ama utafiti, lakini baadaye wakifika nchini mwetu wanabadilika na kuwa ama Wawekezaji wa biashara ndogondogo ama wafanyakazi katika Maofisi mbalimbali nchini. Tena wamekuwa wakipata mafao makubwa kuzidi Watanzania ambao wana elimu na uzoefu wa kiwango cha juu zaidi. Uzembe, rushwa na kukosa uzalendo miongoni mwa Watendaji wa Idara ya Uhamiaji na/au uandikishaji wa vizazi na vifo usiozingatia uraia wa kweli ni miongoni mwa sababu kubwa za tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa kuchukua nafasi hii kutoa mapendekezo yetu kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kuboresha zaidi Idara hii.

Idara ya uhamiaji iendeleze zoezi la kuajiri vijana wengi wenye elimu ya juu. Zoezi hili liendane na kuongeza uadilifu miongoni mwa Maofisa wanaohusika na zoezi la uajiri na upandishwaji vyeo ambalo limekuwa likilalamikiwa sana hasa upande wa Zanzibar.

Idara ya Uhamiaji iendelee kupatiwa vifaa vipya vya kisasa kuweza kushindana na kasi ya mabadiliko ya kiteknolojia ambayo yanawezesha wahalifu mbalimbali kukwepa mitego inayowekwa na Watendaji wetu kunasa wavunja sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vituo vyetu mipakani ni lazima viunganishwe na Ofisi nyingine Wilayani, Mikoani na Makao Makuu kiteknolojia ili kuondoa usumbufu na kukosekana kwa habari nyeti za wageni wetu waingiapo na watokapo nchini mwetu. Ni muhimu hivi sasa Idara hii ikawezeshwa vilivyo kuweza kuboresha mfumo wa mawasiliano ya *Internet* kati ya vituo vyake vyote na sekta nyingine nyeti nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utoaji wa pasi mpya za kusafiria ni suala lingine muhimu kwa Serikali kulitolea ufafanuzi wa kina. Watanzania wamelipokea zoezi hili kwa shauku kubwa, lakini bahati mbaya kama ilivyo kawaida yetu, uamuzi wa kutekeleza zoezi hili ulichukuliwa wakati bado Taasisi husika hazikuandaliwa ipasavyo. Matokeo yake zoezi hilo limekuwa kero kubwa kwa Watanzania. Vilevile, unatakiwa uangalifu mkubwa katika kusafirisha *passport* kuzuia kupotea kwa *passport* hizo hasa zile zinazosafirishwa kwenda katika Balozi zetu nje ya nchi. Pia kuna Watanzania wanaolazimika kusubiri zaidi ya miezi sita kupata *passport* zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za kuwa baadhi ya wasio Watanzania wamekuwa wakikutwa na *passport* hizi mpya ni za kushitua mno. Tunapenda kupata maelezo ya kina kuhusu suala hili na ni *passport* ngapi ambazo zimegundulika zikitumiwa ama kutolewa kwa wasio Watanzania katika kipindi kati ya mwaka 2004 na 2006? Ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya waliokutwa nazo na waliohusika kuzitoa *passport* hizo kwa wahalifu hao? Serikali inaeleza kauli gani kuhusu *passport* hizi ambazo zilichapishwa kwa gharama kubwa kwa maelezo kuwa haziwezi kugushiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uraia ni suala nyeti na gumu sana katika nchi yetu. Suala hili limekuwa likisababisha matatizo mengi kwa Watanzania. Wote tunajua jinsi gani baadhi ya Watanzania ambao wengi walijitolea kulitumikia Taifa letu kwa uaminifu mkubwa sana, walivyojikuta wakiwa katika usumbufu mkubwa kwao na kwa familia zao. Kwa kweli hii ni aibu na Serikali inapaswa kuchukua hatua za kuwaomba radhi wale wote waliofikwa na tatizo hilo. Wakati umefika kwa Serikali kulichukulia suala hili kwa umakini mkubwa ili suala hili kamwe lisije kutumika tena na maadui wa maslahi ya nchi yetu, wa nje na wa ndani, kutugombanisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umefika wakati baadhi ya Watanzania wa Mikoa ya mipakani kama vile Kigoma, Mtwara, Mbeya na Kagera wamekuwa wakijutia ama wao kuzaliwa au wazazi wao katika maeneo hayo. Wapo wanaoanza kujiuliza kama uraia wa Tanzania siku hizi umekuwa wa madaraja. Wengine wana haki ya kuwa nao bila chokochoko wakati wengine ni lazima wathibitishe tena kwa usumbufu mkubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Moja ya mfumo muhimu wa kulishughulikia suala hili ni uandikishaji wa mtoto punde anapozaliwa. Ni wazi kabisa kuwa ili Taifa litambue idadi ya raia wake, ni pamoja na kuandikisha raia wake mara wanapozaliwa tena bila ya

usumbufu wowote. Mfumo uliokuwepo hivi sasa una matatizo mengi mno. Ukosefu wa elimu ya kutosha inayowezesha Watanzania kutambua umuhimu wa uandikishaji wa watoto wao punde wanapozaliwa ni moja ya sababu hizo. Sababu nyingine ni ukweli kuwa ni Watanzania wachache wanaotumia hospitali zetu kujifungulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona mwananchi anajua umuhimu wa kujiandikisha pale anapotafuta *passport* ya kusafiria au anapotakiwa kujiunga na Elimu ya Juu. Kwa kweli hii ni aibu kwetu, kwani inadhihirisha ni jinsi gani Serikali yetu haichukulii umuhimu wa kuwaelimisha wananchi wake masuala nyeti kama haya.

Ili kuondoa tatizo hili, ni muhimu kwa Serikali kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Kuboresha mfumo wa mawasiliano kati ya Idara husika na uandikishaji wa watoto Mikoani na Makao Makuu. Inapaswa kuwa na mfumo ambao utawezesha taarifa za mtu kuweza kupatikana Mkoa hadi Mkoa bila ya kuambiwa arudi kule alipojiandikisha kufuatilia faili lake;

(ii) Mfumo huu uhusishe pia mipango mingine kama vile utoaji wa *passport* mpya na vitambulisho vya uraia;

(iii) Kuboresha mafao ya Watendaji wake katika Idara hii na nyingine zihusikazo na masuala ya uandikishaji wa watoto ili kuvutia vijana wenye uwezo mkubwa kiutendaji; na

(iv) Kupitia upya sheria zetu zinazo husika na suala la uandikishaji watoto wetu na taarifa za vifo ili kuondoa mianya ya rushwa, uonevu, usumbufu ambapo wakorofi wachache wanatumia kuwanyanyasa Watanzania wenzao kwa sababu ya madai ya kuwa na matatizo ya uraia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika enzi hizi za dunia ya utandawazi na ushindani wa soko huria, suala la uraia wa zaidi ya nchi moja lina umuhimu wa kipekee. Umuhimu huu unatokana na ukweli kuwa Tanzania kama nchi nyingine za Dunia ya Tatu, imekumbwa na tatizo la watu wake wengi kuhamia katika Mataifa mengine ikiwa kama jitihada za kujiendeleza kielimu na kiuchumi.

Tanzania ina watu wake wengi nje ya nchi ambao wangelipenda kuja kusaidia kusukuma gurudumu la maendeleo nchini kwao bila ya kuathiri mafanikio waliyoyapata katika nchi walizopo. Ukienda katika nchi nyingi, utakuta Watanzania wengi, ambao ni wasomi wakubwa, wataalamu wa masuala mbalimbali na Wawekezaji wazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hazina kubwa sana ambayo Serikaliyetu hadi sasa imeshindwa kuja na mbinu thabiti za kuitumia kwa manufaa ya Taifa letu. Hazina hii haihusu wale ambao wana asili ya Tanzania tu, bali hata wengine ambao nao pia wangependa kuja kwetu kushirikiana nasi kupambana na matatizo tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua hili, wenzetu wa Ghana wamekuwa mstari wa mbele kujenga mazingira bora ya kuwezesha watu wao walioondoka nchini humo kurudi nyumbani kuendeleza sekta mbalimbali za maendeleo.

Wenzetu hawa wameanzisha Wizara maalumu inayoshughulikia mahusiano na maslahi ya Waghana waishio nje ya nchi yao *(Ghanaian Diaspora).* Vilevile, wameanzisha sheria inayowawezesha waafrika wengine waliolowea ughaibuni *(African Fiaspora)* kama vile Wamarekani weusi na wengineo kutoka visiwa vya Carribian na Ulaya kuweza kuwa na haki maalum katika kuwawezesha kushiriki katika masuala ya kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitahada hizi zimeweza kuisadia nchi ya Ghana kupata zaidi ya asilimia 37 ya mapato ya Taifa (*GDP)* kutoka kwa wananchi wao waishio nje. Hii ni sawa na Dola za Kimarekani bilioni tatu. Hivi sasa kiasi kikubwa cha uwekezaji kutoka nje, yaani *Foreign Direct Investment (FDI)* kimeongezeka na sehemu kubwa inatoka kwa Wawekezaji wa Kimarekani wenye asili ya Afrika. Sekta ya Utalii ya Ghana imeweza kufaidika kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingine za Afrika zilizoanzisha mipango na sheria kama hizo ni Ethiopia, Afrika Kusini na Rwanda. Hawa wote wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa bila ya kuathiri mfumo wa kisiasa na kijamii katika nchi hizo. Hata sisi hatupaswi kuacha mafanikio makubwa kama wanayopata wenzetu, kwa kisingizio cha hofu ya masuala ya kihistoria kama vile suala la matatizo ya kisiasa Zanzibar.

Vilevile, mtindo wa kutowatambua wananchi wetu walio nje ambao wana uraia wa nchi nyingine unasababisha chuki isiyo ya lazima baina ya wananchi hao na Serikali yetu kutokana na wao kuhisi kuwa mfumo uliopo unawabagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna njia mbalimbali ambazo Serikali yetu inaweza kulishughulikia suala hili. Njia hizi ni kama zifuatazo:-

(i) Kuanzishwa kwa sheria ya *Dual Citizenship* ambayo itatoa haki kwa watu wenye asili ya Kitanzania waishio na wenye uraia wa nchi nyingine kupata haki sawa ya kiraia pindi wajapo nchini;

(ii) Kutoa haki maalum za kiuchumi na kijamii kwa wageni mbalimbali, hasa wale ndugu zetu Waafrika waliolowea ughaibuni *(African Diaspora)* wenye nia ya kuanzisha na kuendeleza miradi na mipango mbalimbali ya kimaslahi yenye kulenga ujenzi wa Taifa letu; na

(iii) Kutoa haki ya kuwa na hati za kusafiria za Kitanzania kwa Watanzania waishio nje bila ya kulazimika kuomba tena uraia hapa nchini.

Pamoja na Mapendekezo hayo, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili, ni lini ahadi ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu aliyoitoa Marekani kuwa kabla ya mwisho wa muda wake atahakikisha Sheria ya *Dual Citizenship* imepitishwa? Ahadi hii ilitolewa mbele ya ulimwengu na Watanzania hao wangependa kujua maandalizi ya Sheria hiyo yamefikia wapi

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanikiwa kufanya hayo, ni wazi hata tatizo la kukosa Walimu na Wataalam wengine litapungua kwa kiasi kikubwa na kuongeza ajira kwa vijana wetu kutokana na uwekezaji watakaofanya. Tunapoweza kuwahakikishia ndugu zetu hawa kuwa hawatapoteza mafanikio ambayo tayari wameshayapata wakiwa huko nje, ni rahisi kwao kujitolea kuja nchini kufanya miradi ya muda mrefu na muda mfupi halafu pengine wakarudi walipotoka kuendelea kujiimarisha na wataitangaza vyema nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vitambulisho vya uraia nalo lina umuhimu wa kipekee kwa Taifa letu. Kitambulisho cha uraia sio tu kitamwezesha Mtanzania kujihakikishia uraia wake katika enzi hizi za kutoaminiana, lakini pia litawezesha Serikali yetu kupambana na wimbi la wahamiaji holela ama haramu kama vile wanavyoitwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa mzaliwa wa Mkoa wa Kigoma, binafsi nimeshuhudia jinsi Watanzania wenzangu wengi wanavyokumbana na manyanyaso na usumbufu wa kutakiwa kuthibitisha uraia wao. Kutokana na mfumo duni wenye mapungufu mengi uliokuwepo, Watanzania wamekuwa wakipimwa uraia wao kwa kuangaliwa sura zao kama vile kuna sura rasmi ya kitanzania na nyingine ni haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha masuala ya usalama wa Taifa letu, suala la vitambulisho vya uraia lina maslahi makubwa kijamii. Kuwa na vitambulisho vya uraia kutarahisisha mambo mengi kwa Taifa kama vile kutambua watu wetu katika matukio mabaya kama ya ajali. Watanzania wengi wamekuwa wakizikwa bila ya ndugu na jamaa zao kuwa na taarifa kutokana na kushindwa kuwa na vitambulisho rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na vitambulisho vya uraia kutawezesha kutekelezwa kwa sheria mbalimbali zinazohusu haki za watoto wetu na vijana. Tukiwa na vitambulisho vya kitaifa, ni wazi tatizo la vijana wetu kujihusisha na mambo kama ulevi uliopindukia wakiwa na umri mdogo litadhibitiwa. Tatizo la watoto na vijana wetu wadogo kukesha usiku kucha katika majumba ya starehe pamoja na wakubwa zao ama hata wengine wenye umri wa wazazi wao, nalo litadhibitiwa ipasavyo. Ni aibu kuona kumbi za starehe za usiku zinajaa watoto wadogo wenye umri hata usiofika miaka 15 wengi wao wakijihusisha na ulevi na matendo yasiyo ya kistaarabu katika umri mdogo sana. Ukiuliza kwa nini hilo linatokea, wahusika wanasingizia kukosekana kwa utambulisho rasmi unaonyesha umri wa vijana wetu hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili ni lazima lifanyike sasa kabla vuguvugu la Shirikisho la Afrika Mashariki halijafika hatua ya mbali. Tukichelewa kutekeleza zoezi hilo sasa, ni wazi tutashindwa kutambua Watanzania halali hapo baadaye. Zoezi hili litaweza kufunga mianya ya vijana wasio Watanzania kujipatia kazi zinasopaswa kufanywa na vijana wetu. Suala hili ni muhimu, kwani lisipodhibitiwa litaendeleza

husuda, chuki na kutokuaminiana kati ya vijana wetu wa Afrika Mashariki, hali ambayo imekuwa ikiongezeka kila siku zinavyozidi kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu vilevile kuhakikisha Makao Makuu ya zoezi la vitambulisho vya uraia kujengwa hapa Dodoma. Hii inatokana na ukweli kuwa sio tu ndio Mji wetu Mkuu, lakini vilevile ni katikati ya nchi yetu. Suala hili la vitambulisho vya uraia ni haki ya Watanzania wote na sio wale waishio Dar es Salaam na Mikoa jirani tu. Hivyo, Watanzania hawana budi kuchangia machungu ya usumbufu utakaowapata wakati wa zoezi hilo kwa hali inayofanana na sio kuwapendelea baadhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile suala la haki za usiri wa taarifa za wananchi ni lazima liangaliwe kwa umakini sana. Sheria lazima itungwe kulinda maslahi na haki za Watanzania kuhusiana na matumizi ya taarifa zao binafsi zitakazokuwemo katika mfumo huu wa vitambulisho vya uraia. Ni lazima sheria itungwe kueleza bayana ni nani na kwa sababu zipi, taarifa za mwenye kitambulisho zinaweza kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitakuwa haki kwa taarifa za Watanzania kuachwa wazi kwa mtu ama Asasi yoyote ya nje ya mipaka yetu. Taarifa za wananchi wetu zisipewe watu ama Asasi zozote za Mataifa ya nje ambayo yanadhani ni haki yao kuingilia siri za nchi yetu na watu wake. Hili ni lazima liwekwe wazi kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapendekeza teknolojia itakayotumika iwe yenye ubora na usalama wa taarifa za Watanzania. Ni bora kutumia fedha nyingi zaidi kutengeneza vitambulisho bora kama vile teknolojia ya *Smart Card* ambayo sio tu inahakikisha usiri wa taarifa za wahusika, lakini pia ni madhubuti kuliko *Two Dimension Bar Code.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msisitizo maalum, tunaomba suala la wananchi wetu wanaotoka Mikoa ya mipakani kuchukuliwa kwa umuhimu wa hali ya juu na sio kuendelea kuwabughudhi eti kwa kuhofia uhalali wa uraia wao. Lisipochukuliwa hivyo, misingi ya umoja wa Taifa letu itaathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hayo, tunapenda Watanzania wataarifiwe rasmi lini sasa vitambulisho hivyo vitatoka? Kwani fedha zilishatengwa miaka mingi iliyopita, tenda zilishatolewa siku nyingi, lakini hakuna taarifa zinazotolewa. Ni kiasi gani cha fedha sasa zitatumika kutekeleza zoezi la kutoa na kusimamia vitambulisho vya uraia nchini? Taarifa hiyo ni lazima ielezee kwa undani kiasi hicho kitatumika kwa masuala gani na kwa muda gani na zoezi hilo litachukua muda gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapaswa kuanza shughuli za kutoa elimu kwa wananchi kuhusu zoezi hilo ikiwa ni pamoja na kuwaeleza umuhimu wake, haki zake, matumizi yake na jinsi ya kushiriki katika kulitekeleza. Sheria na vyombo vitakavyohusika na zoezi hilo, ni lazima ziwe wazi kwa wananchi kabla ya zoezi hilo kuanza rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukarimu wetu kwa wenzetu wanaokumbwa na matatizo mbalimbali katika nchi zao, ni moja ya mambo ambayo yanadhihirisha upekee wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarimu wetu, hasa wa wananchi wa Mikoa ya mipakani kama Kigoma na Kagera, umesababisha usumbufu mkubwa kwa wenyeji wa maeneo hayo. Kusumbuliwa kuthibitisha uraia wao ni moja ya matokeo ya ukarimu wetu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwaka 2005/2006, Bunge lako Tukufu liliarifiwa kuhusu mpango wa kuwasadia wananchi waliothirika kuwepo kwa wakimbizi katika maeneo yao. Tunapenda Bunge lako Tukufu litaarifiwe mpango huo umefikia wapi na umekuwa na mafanikio gani kwa Watanzania husika hadi kufikia sasa. Kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Serikali ya Denmark ilitoa Shilingi bilioni tisa kwa ajili ya miradi ya ufundi stadi, maji, kilimo, hifadhi ya mazingira, ardhi, misitu na maliasili nyingine katika maeneo yaliyo karibu na makambi ya ndugu zetu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa, miradi hiyo ilipaswa kuanza kutekelezwa mwezi Januari, 2004 na ilipaswa kuwa kwa muda wa miaka mitatu. Pamoja na kuhitaji taarifa ya mafanikio yaliyopatikana hadi hivi sasa, ni vyema wananchi wakajua mgawanyo wa fedha hizo ulivyofanywa katika kila senti ya mradi huo.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania ni maeneo mangapi yanayozunguka Makambi ya Wakimbizi yalinufaika na fedha hizo na kwa kiasi gani na kwa shughuli ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani pia ingependa kujua Serikali kama ina mpango wowote wa kurekebisha Sheria ya Wakimbizi *(Refugees Act,1998).* Ikumbukwe kuwa sheria hii ilitungwa bila ya kuanza na sera mahsusi kama ilivyo kawaida kwa sheria zote.

Kwa kuwa hivi sasa tuna sera rasmi, yaani *Refugees National Policy*, ni lazima kuziangalia upya sheria zetu ili ziendane na sera hiyo. Watanzania wana haki ya kujua kama Serikali imeanza jitihada zozote kuhusiana na marekebisho ya sheria hiyo au la na ni vipi Watanzania wa maeneo yanayoathirika na suala hili wanahusishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Zimamoto ni moja ya Idara nyeti nchini mwetu, lakini hadi hivi karibuni imekuwa ikiangaliwa kwa umuhimu usiokidhi matakwa yake. Watanzania wengi wamepoteza maisha na mali zao kutokana na mfumo duni wenye kukatisha tamaa wa Idara ya Zimamoto katika Miji yetu. Inastaajabisha kuona kuwa hata katika enzi hizi za dunia ya soko huria na umuhimu wa Wawekezaji, Idara hii bado haijapewa umuhimu unaostahili katika mipango yetu nchini. Katika Miji mikubwa kama Jiji la Dar es Salaam ambapo mashindano ya kujenga majumba makubwa na

viwanda vyenye thamani ya mabilioni ya fedha bado mfumo wa Zimamoto unafanana na ule wa Dar es Salaam ya mwaka sabini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya kulindwa na majanga ya moto imeyumbishwa sana na wanyonge wa nchi hii wanaendelea kufukarishwa kutokana na majanga ya moto. Ni vigumu sasa kujua nani hasa anawajibika na Zimamoto. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe tamko kuhusu wafanyabiashara na wamiliki wa nyumba au wananchi ambao wanapoteza mali zao kutokana na janga la moto unaotokana na uzembe wa Idara ya Zimamoto, mara gari linafika kwenye ajali bila maji au linachelewa hadi nyumba nzima inateketea. Je, hawastahili kulipwa? Serikali inasemaje kuhusu hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda kuchukua fursa hii kutoa mapendekezo ya jinsi gani mikakati iliyopo wakati huu inaweza kuboreshwa kwa ufanisi zaidi ili kuwanusuru Watanzania kutoka katika adha hii ya moto na ajali mbalimbali.

Serikali inapaswa kubadili mfumo wa Zimamoto katika nchi nzima ili kuendana na matakwa ya hivi sasa. Majukumu ya Zimamoto ni lazima yarudishwe mikononi mwa Serikali kuu. Ni lazima kuhakikisha kuwa kila Wilaya ya nchi hii inapata magari yasiyopungua matatu kwa Wilaya ndogo na sio chini ya matano kwa Wilaya kubwa. Hili liendane na uboreshaji wa vitendea kazi vingine kwa Askari wetu wa Zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miji mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Tanga na Mbeya ,lazima yapewe umuhimu wa kipekee na muundo wake uwe unaendana na mahitaji yake yanayokua kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha hili, Wizara ni lazima iepuke tabia iliyojijengea ya kununua magari ya Zimamoto na vifaa vyake vyenye gharama kubwa kupita kiasi wakati hivi sasa tunaweza kupata vifaa hivyo tena vyenye ubora zaidi kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, kwa taarifa yako ya Kambi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na hatua inayofuata, naomba niwatambulishe wageni walioko hapo mbele yetu. Tunao wageni kutoka *SADC*, Dr. Thomas Agustino Salomao, yeye ni *Executive Secretary* wa *SADC*, amembatana na Mrs. Lefa Martin, yeye ni *Head of Cooperation and Communication* wa *SADC.* Wameambatana na mwenyeji wao Mr. Hurbert Mlangwe, yeye ni *Director of Regional Cooperation* katika Wizara yetu ya Mambo ya Nchi za nje. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupata maelezo toka kwa mtoa hoja ambaye ni Waziri mwenye dhamana ya Wizara hiyo na baada ya kumsikiliza Mwenyekiti wa Kamati na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, sasa tutaanza majadiliano ya pamoja. Hapa Mezani kwangu tayari ninao wasemaji kumi ambao wameshaomba kuchangia na

tutaendelea na mjadala wa kuchangia hoja hii mpaka saa saba na hatimaye tutarejea Bungeni saa 11.00 jioni kuendelea na mjadala wetu kwa muda wa saa moja. Itakapofika saa kumi na mbili jioni tutaanza majumuisho kwa utaratibu ambao tumeuzoea wa kupitisha Bajeti yetu.

Ninaomba nichukue nafasi hii kuwataja Waheshimiwa ambao wameshaomba kuchangia. Tutaanza na Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu. Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Sijapata Nkayamba. Lakini wapo waliochangia mara mbili na kama nafasi itaturuhusu tutaendelea na Mheshimiwa Abdul Marombwa na Mheshimiwa James Lembeli.

Kabla sijamruhusu, nimepokea hapa malalamiko kwamba Waheshimiwa Wabunge wamekuwa *very much concerned* na lile tangazo langu la timu kwenda kucheza Mpwapwa, lakini wanasema wana wasiwasi timu hiyo kweli imejiandaa vizuri. Sasa *Captain* ameniambia kwamba Golikipa, Mheshimiwa *Capt.* John Komba yuko tayari kabisa kwa mapambano na hakuna wasiwasi na atasaidiwa na Golikipa namba mbili, ni Mheshimiwa Maria Hewa, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mwanza. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Josephine Genzabuke ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani. Kabla sijachangia, naomba kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kura nyingi. Vilevile, nampongeza tena Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi mwezi uliopita kwa kura nyingi. *(Makofi)*

Napenda kumpongeza tena Mheshimiwa Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine tena kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Aman Abeid Karume kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.

Napenda kumpongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa na Rais kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupitishwa kwa kura nyingi na Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kura zao nyingi. Napenda niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wote na Manaibu Waziri kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kwa kushika nafasi nyeti katika Serikali yetu. *(Makofi)*

Nimpongeze Spika wetu, Mheshimiwa Samuel Sitta, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kwa na Wabunge wa Bunge hili, bila kumsahau Mheshimiwa Anne Makinda, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikupongeze wewe mwenyewe kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge hili. Wewe kama mwanamke, umekuwa kama ni kioo na mfano kwetu sisi wanawake kuweza kujifunza kwa mambo yako mazuri. Nimpongeze Mheshimiwa Job Ndugai, naye kwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru wanawake wa Mkoa wa Kigoma kwa kuweza kunipatia ridhaa yao ili niweze kuwa Mwakilishi wao katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nawashukuru sana. Nitakuwa ni mchoyo wa fadhila nisipowashukuru wananchi wote kwa kuweza kuichagua CCM kwa kura nyingi na kura zao nyingi zikaweza kuipatia asilimia nyingi CCM, hata wanawake 58 waliotokana na asilimia zao nikiwemo mimi kuweza kupata Wabunge wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nichangie mada hii ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani. Naomba niongelee kuhusu Wakimbizi ambao wako katika Mkoa wa Kigoma. Tangu wakimbizi walipoingia katika nchi yetu, kumekuwa na matatizo mengi ambayo yamekwishajitokeza na ambayo mpaka sasa yanaendelea kujitokeza ambayo yanaletwa na wakimbizi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Watanzania ni watu wenye huruma, wenye imani, tuliwapokea wakimbizi wale kwa moyo mkunjufu. Tukidhani kwamba ni watu wema. Sio kwamba wote sio wema, lakini baadhi yao ni watu ambao sio wazuri. Baada ya Wakimbizi kuingia, kumetokea matatizo mbalimbali ambayo wamekuwa wakiwafanyia wananchi wanaoishi katika Mkoa wa Kigoma hata Mikoa mingine kwa mfano Mkoa wa Kagera. Kumekuwa kukijitokeza ujambazi, wakimbizi wale wanakwenda kuwavamia watu majumbani kwa kutumia silaha hadi kuwapora mali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakimbizi wale wameendelea kusababisha mambo ya wizi katika mashamba ya wanachi wanaoshi Vijijini ambavyo viko karibu na Makambi yao. Utakuta wakati mwingine wananchi wamelima mashamba yao, wakimbizi wale kutokana na roho zao za chuki na mbaya wanakwenda kwenye mashamba ya wananchi wale kama wao ndiyo wenye mashamba wanavuna mazao. Kwa mfano, mtu kalima shamba lake la maharage, wanakusanyika, wanakwenda kuvuna maharage kama ndiyo mashamba yao. Mwenye shamba akienda shambani anakamatwa na kupigwa na wakati mwingine hata kuuawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli vitindo hivi tumevivumilia muda mrefu sana, tumechoka. Tunamwomba Waziri wa Wizara hii atusaidie ili tuweze kuishi kwa amani katika nchi yetu. Sisi tumegeuka kama vile ndiyo Wakimbizi. Unakwenda kwenye shamba lako unakuta mtu anavunamahindi. Badala ya yeye kukimbia, wewe mwenye shamba ndiyo unalazimika kukimbia ili uweze kunusuru maisha yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hali hii inatutisha na inatukatisha tamaa. Unakuta watu wanajipangia mipango yao ya maisha, kwa mfano mtu anapanga anasema kwamba mwaka huu nataka nilime na baada ya kulima, nitakapovuna nipeleke mazao yangu nikauze. Nikishauza, niweze kujinunulia pengine baiskeli ya kuweza kunisaidia kufanya shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kubeba mizigo kutoka shambani,

kubeba familia kupeleka hospitali. Lakini unapokuwa umenunua baiskeli ile, kabla hata hujaifikisha nyumbani, unakuta kundi kubwa la wale Wakimbizi limewasubiri watu waliotoka kununua baiskeli zao, wanawanyang'anya na hata wakati mwingine kuwaua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Wizara ya Mambo ya Ndani, iweze kutusaidia wananchi tunaoishi mipakani kwa kutuwekea ulinzi unaofaa kwa sababu watu wengi wamekuwa wakiuawa na wananyang'anywa baiskeli zao na wananyang'anywa mali zao, lakini wakimbizi wale weanaendelea kutamba kama vile wao ndio wenye haki ya kuishi katika nchi hii. Tunaomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utunzaji wa mazingira, hili limekuwa likizungumziwa sana. Wakimbizi wale tangu walipoingia katika nchi hii, kwa kweli mazingira yetu yameharibika sana. Unakuta wanakata miti hovyo, sio kwa sababu wanapenda, wanalazimika kukata miti kwa sababu ile miti ndiyo inayowawezesha kupata kuni na hata miti ya kujengea nyumba zao. Sasa, pamoja na kwamba ni haki yao kukata miti ile, lakini mazingira yameharibika sana. Tungeomba Serikali vile vile iliangalie hili kwa sababu wale watu wakiendelea kukaa hapa, kwa kweli tutashtukia hasa Mkoa wa Kigoma na Kagera imebaki ni jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo mambo ya mazingira, cha kushangaza, kwa mfano Mkoa wa Kigoma, hususan Wilaya ya Kasulu na Kibondo, wananchi wanaoishi maeneo yale yanayozunguka Makambi ya Wakimbizi, wanashangaa sana kuona wao mpaka sasa hivi ninavyozungumza hapa, wananchi wanaoishi maeneo ambayo yamekaribiana na Wakimbizi wanafukuzwa kwenye mashamba yao kwamba wasilime kwa maana ya kwamba wanaharibu mazingira na wanaharibu Hifadhi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha kuwashangaza, ni pale wanapoona Wakimbizi ambao sio wazawa wa nchi hii, wakiendelea kuharibu mazingiara, lakini Serikali inaendelea kuwafumbia macho, lakini wao ambao ni wazawa wa nchi yetu, wanafukuzwa, wanaambiwa watoke kwenye maeneo ambayo kuna miti, warudi sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watalima wapi? Wao ni wazawa, wanafukuzwa kwamba wasilime kwenye mashamba yao. Lakini Wakimbizi Serikali inawafumbia macho. Ukweli uko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali ijaribu kulitupia macho jambo hili, wasiwepo watu wanaopendelewa eti kwa sababu wao ni Wakimbizi na wengine wanaonewa wakiwa kwenye nchi yao. Usawa uko wapi? Hii ni dhuruma! Ukiwakuta wakimbizi wao wamekaa pale, hawaguswi na mtu yeyote kwa kudai kwamba Umoja wa Mataifa utalalamika. Sasa sisi kwa nini wanatufanyia hivyo? Basi na sisi tunaomba watafute jinsi ya kutusaidia ili tuweze kubaki na haki katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie uraia. Kunaandaliwa vyeti vya uraia, lakini kabla ya kutayarisha vyeti vya uraia, tunaomba watakapokuwa wanaandaa vyeti vile, wawe waangalifu kwa sababu Wakimbizi wengi wanajifanya ni Waha kwa

sababu wana zungumza Kiha na Kiha kinafanana sana na Kirundi. Mtakuja kushtukia Warundi ndiyo wamepewa vitambulisho vingi hata wakaweza tena kutuzidi sisi wazawa wa eneo lile. Mtakapokuja kushtuka, Warundi ndiyo wengi, Waha tumebaki ni wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya Mambo ya Ndani itakapokuwa inashughulikia mambo ya vyeti vile vya uraia, ihakikishe wazawa wanashirikishwa ili kuweza kuwatambua watu ambao ni wazawa na watu ambao ni Wakimbizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mengi zaidi, isipokuwa ninazidi kuwasisitiza watu wa Mambo ya Ndani ikiwemo Serikali kwa kushirikiana na Mashirika ya Umoja wa Mataifa, kuziangalia Kigoma na Kagera, wamebeba mzigo muda mrefu.

Sasa Serikali itawawekea kumbukumbu gani? Kwamba, watu hawa waliwahi kubeba mzigo kwa kuwahifadhi Wakimbizi, kwa sababu miundombinu wameharibu sana. Magari yale yanapokuwa yamepita yamebeba Wakimbizi au chakula cha Wakimbizi, barabara hata kama imetengenezwa leo, ukienda asubuhi, barabara haina kazi kwa sababu magari yanayopita pale, yamebeba uzito mkubwa sana.

Hivyo basi, tungeomba Serikali pamoja na kwamba tumekwishaahidiwa kwamba katika kipindi cha miaka hii mitano, tutatengenezewa barabara. Tunaomba tupewe kipaumble jamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme vile vile tunaomba na wenyewe Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini atupatie kipaumbele haraka sana kwa sababu wakati mwingine wagonjwa wanakuwa wengi katika hospitali zile za Wakimbizi, wanalazimika kupelekwa kwenye Hospitali za Wilaya. Sasa wanapopelekwa pale, unakuta huduma inakuwa haitoshelezi. Kwa wiki unakuta pengine *X-Ray* ni mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine hata wale ambao siyo Wakimbizi, kwa sababu Wakimbizi wameletwa na gari moja kwa moja mpaka pale Hospitali, wanapewa kipaumbele kushughulikiwa, sisi ambao ni wazawa unaweza kushtukia umerudi nyumbani, unaambiwa wewe utarudi siku nyingine. Tunaomba na hilo Serikali ilione.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke kwa mchango wako mzito. Ninaomba sasa nimwite Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, lakini simwoni hapa ndani. Basi naomba nimwite Mheshimiwa Diana M. Chilolo na Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu ajiandae.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba unisamehe kwa sababu nilijua mimi ni mchangiaji wa nne, basi nilikuwa naendelea na utaratibu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, naomba basi nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi, Ndugu yangu, kaka yangu, Mheshimiwa *Capt*. John Z. Chiligati, pamoja na Naibu Waziri, Ndugu yangu, Mheshimiwa Bernard K. Membe, bila kumsahau Katibu Mkuu wa Wizara hiyo na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa Bajeti hii ambayo imeonyesha mwelekeo mzuri wa kuweza kutoa huduma katika sekta zote ambazo ziko ndani ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, naomba nitumie nafasi hii kuongelea suala la Magereza kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Serikali kwa kuandaa mahali pa kuwatunza wahalifu wetu pale wanapohukumiwa kifungo. Tunaishukuru sana Serikali yetu, kwani imeboresha sana mazingira ya Magereza yetu. Lakini, pamoja na hayo yote, mazingira wanayokaa wafungwa kuwa mazuri, lakini bado hatujatoa huduma kwa wafungwa wetu ili waweze kupata elimu, ujuzi, ili wanapotoka huko, waondokane na uhalifu. Kwa sababu wafungwa wengi waliojaa kwenye Magereza wanatokana na wizi, ujambazi, udokozi, inawezekana hawa wanafanya tu hayo kwa sababu ya ukata.

Sasa, endapo tutawapa mafunzo ambayo yatawawezesha kumudu maisha yao, tutakuwa tumewasaidia sana wafungwa hawa wanapotumikia kifungo wakipata elimu, kwa mfano ufundi washi, ufundi seremala, ushonaji na mambo mbali mbali. Wakitoka hapo, wataweza kwenda kuanzisha miradi yao ya kuzalisha mali ili waweze kuondokana na masuala ya kudhulumu, kuiba na hatimaye kufikishwa hapo, kwani, mara nyingi wafungwa wanapotoka Magereza, huwa hawajajifunza lolote, akifika nyumbani anarudia kazi ile ile, siku mbili unamkuta yuko Magereza tena.

Kwa hiyo, nitashukuru sana Serikali ikitoa vifaa vya kutosha katika Magereza yetu ili wafungwa waweze kupata elimu mbalimbali za kuzalisha mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niongelee suala la mahabusu. Ni kweli tuna mahabusu wengi sana katika Magereza yetu, lakini mahabusu hawa kwa nini wanakaa muda mrefu sana katika Magereza yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni wakati muafaka Wizara zitegemeane. Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Usalama wa Raia na Wizara ya Katiba na Sheria, wawe wanawasiliana ili kuona ni mahabusu gani wameshakaa muda mrefu katika Magereza yetu ili kesi zao ziweze kutiliwa maanani, ziendeshwe, hatimaye wapate hukumu zao, kama kutoka watoke, kama kutumikia kifungo, basi watumikie, kuliko ilivyo sasa wanakaa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio wote walioko mahabusu kwamba wana hatia, wako wengine hawana hatia, wamefika tu pale kwa sababu ya kuhisiwa, sheria lazima ichukue nafasi yake popote pale panapojitokeza dosari bila kujali huyu ana hatia ama hana hatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba sana Serikali sasa ifike wakati mahabusu wetu wasikae Magerezani kwa muda mrefu, kwani tunawacheleweshа, wanaachana na familia zao, wakati wengine hawana hatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, naomba niongelee kuhusu haki za binadamu. Ni kweli wafungwa lazima watumikie vifungo na mahabusu lazima wakae huko. Lakini yako mambo ya msingi wanayoyakosa wanapotumikia vifungo vyao, kwa mfano, chakuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafungwa wetu wanakula mlo mmoja kwa siku. Akishapata uji wa asubuhi ambao siyo mlo, atatumikia huko mpaka atapata chakula saa nane, akiishakula saa nane, mpaka kesho yake saa nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chakula hakihusiani na adhabu, pamoja na adhabu wanazotumikia, lakini naiomba Serikali ihakikishe inawahudumia wafungwa wetu kuwapa chakula kama binadamu wengine, kama raia wengine wanavyopata. Binadamu wa kawaida anapata chakula kutwa mara tatu. Anapata chai asubuhi, chakula cha mchana na chakula cha jioni. Hivyo basi, ni wakati muafaka kuwatendea haki wafungwa wetu ili na wenyewe waweze kupata milo kama tunavyopata sisi wengine kwa sababu suala la chakula halihusiani na adhabu walizonazo. Kuwanyima chakula ama kuwapunguzia mlo, ni kutokuwatendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, ndani ya Magereza kuna vijana, wako Magereza miaka 18 na kuendelea. Vijana hawa nao wanalala na watu wazima kwenye *hall*. Mimi naomba sana tujitahidi sasa kuhakikisha tunagawanya *hall* zetu katika vyumba, kila mfungwa awe na chumba chake ili kupunguza mambo mengine, mfano; maambukizo na kuzua matatizo mengine, kama ngono zinafanyika ndani ya Magereza yetu kwa sababu watu wanalala pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali hasa hawa vijana, kama inawezekana, basi lianzishwe Gereza la Vijana, watengwe wenyewe huko, wasichanganywe na watu wazima kwa sabababu vijana tunategemea kwamba anapokwenda kule, apate Shule, akitoka arudi nyumbani amebadilika. Lakini anapokutana na magwiji, yaani majambazi sugu, vijana wetu wanaendelea kupewa mbinu za kukomazwa, hatimaye akitoka hapo, anakaa nyumbani siku mbili, anarudi tena huko huko. Nina hakika tutakuwa hatuwafundishi wala hatuwalei vijana wetu ambao ndiyo Taifa la leo na kesho. Ninaomba sana Serikali iwafikirie vijana kuweza kuwalea katika vifungo, katika malezi ambayo tunahakikisha kwamba wakitoka huko, watakuwa wamebadilika kitabia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la Maaskari kupandishwa vyeo. Maaskari huwa wanastaafu kulingana na vyeo walivyokuwa navyo. Unakuta Askari asiyekuwa na cheo, mwisho wake miaka 45, mwenye cheo anakwenda mpaka miaka 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali iwe na utaratibu mzuri wa kutoa nafasi za Askari kwenda kusoma ili Maaskari wengi waweze kupanda vyeo, kwani Maaskari wanakuja kustaafishwa wakati bado wana umri mzuri wa kutumikia nchi hii na wana uwezo wa kutumikia nchi hii. Nitashukuru sana Serikali kama itakuwa na utaratibu

wa kudumu ulio mzuri, Askari wengi wawe wanakwenda kuchukua mafunzo kwa awamu ili Askari wengi waweze kuwa na vyeo na Askari wengi waweze kustaafu kwa umri wa miaka 60 kama wanavyostaafu Maaskari walio na vyeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kuhusu magari ya Zimamoto ama Vikosi Vya Zimamoto. Tunashukuru sana Serikali sasa hivi inaboresha sana Vikosi vya Zimamoto. Katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri, amegusia kwamba hata Manispaa ya Singida amepeleka vitendea kazi kwenye Kikosi cha Zimamoto na siyo vitendea kazi tu pamoja na gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya mwaka 2005 zilitengwa Shilingi milioni 365 kwa ajili ya kununua gari ya Zimamoto kwa Manispaa ya Singida, lakini, pesa zilizokwenda ni Shilingi milioni 200 tu ambazo mpaka sasa hivi hatujafaulu kununua gari ya Zimamoto. Kupitia Bajeti hii, basi naomba Serikali ikamilishe Shilingi milioni 165 ili Manispaa ya Singida iweze kupata gari la Zimamoto. Kwa kufanya hivi, mtakuwa mmetusaidia sana Wana-Singida kwa sababu matukio ya moto yako kila mahali. Hata Manispaa ya Singida matukio haya yapo, lakini yanatuwia vigumu kuweza kuokoa kwa sababu hatuna gari ya Zimamoto. Mandhari tayari toka mwaka 2005 azma ilikuwepo na juhudi zilionekana, tunaomba basi juhudi hizi zikamilishwe ili Wana-Singida wapate gari ya Zimamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongee kuhusu pia hao hao Maaskari wa Kikosi cha Zimamoto. Pamoja na juhudi zote zinazofanyika za Serikali, bado wachache. Mimi Singida hata siwajui, sijui wako wapi! Mimi naomba Kikosi cha Zimamoto kiimarishwe na siyo kuimarishwa tu, vijana wa Kikosi hiki wawe wengi na wapate mafunzo zaidi. Katika mafunzo yanayotolewa ya Askari Magereza, Kikosi hiki kitiliwe maanani sana kipate Askari wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea hilo, naomba niongelee juu ya vyeti vya kuzaliwa. Tunashukuru sana Serikali inajitahidi kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa vijana, lakini *Speed* ya kutoa vyeti hivi, bado inakwenda pole pole sana. Vijana wengi wanakosa kwenda kuchukua mafunzo mbalimbali kwa sababu ya kukosa vyeti vya kuzaliwa. Pamoja na juhudi zote za Serikali, bado utekelezaji huko Mikoani ni wa kusuasua. Vijana wetu wanakosa ajira kwa sababu ya kutokuwa na vyeti vya kuzaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Serikali ifuatilie utekelezaji huko Mikoani ili vyeti hivi viwe vinatolewa kwa muda mfupi ili vijana wanapopata nafasi za kwenda kusoma, basi waweze kwenda kusoma ili pasiwe na kipingamizi cha kukosa cheti cha kuzaliwa. Siyo cheti cha kuzaliwa tu, pamoja na *passport*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi siku hizi wamestaarabika, wanapenda kusafiri nchi mbalimbali kwa biashara, kwenda kusoma na shughuli mbalimbali, lakini hata *passport* zinatolewa kwa kusuasua huko Mikoani. Hivi kuna tatizo gani? Mimi naomba huduma hii iende kwa asilimia 100 Mikoani. *Passport* zitolewe Mikoani.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mlolongo wa kufuata *Passport* Dar es Salaam ni mzito, unachukua muda mrefu, hatima yake wananchi wanakaraika na mwisho wake azma zao zinakwama na biashara zao zinachelewa. Mwingine anashindwa kwenda kusoma kwa sababu ya kuchelewa kupata *passport*, muda unapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia hilo, sasa nizungumzie kuhusu nyumba za Maaskari. Kweli nyumba za Maaskari zipo, lakini nyumba zile hazitoi maadili yoyote kwa vijana. Askari anapofika muda wa kuoa, anakuwa na mke wake anapata watoto, tena wenye jinsia mbili tofauti, watoto wa kiume na wa kike, ana nyumba yenye chumba kimoja na sebule, hivi mnategemea askari huyo atatoa maadili gani kwa watoto wake? Tunawasaidiaje Maaskari wetu hawa ambao tayari wameshakuwa na familia zao? Wana watoto katika kuelimisha watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani tulikuwa tunaweza tukawadanganya watoto kwamba, mtoto nimenunua hospitali, sasa hivi wanaelewa wanatoka wapi, kwa sababu ya malezi, kwa jinsi tunavyoishi. Askari anakuwa na chumba na sebule, unafikiria kuna siri gani hapo? Mtoto utamweleza nini? Mtoto wa kike na wa kiume kweli walale chumba kimoja! Maadili yako wapi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *speed* ya Serikali ya kutaka kujenga nyumba, naomba kasi iongezwe kwa sababu hata Singida nyumba za Magereza bado ni ndogo mno, zina chumba na sebule. Tunaomba nyumba sasa ziwe na nidhamu ya kulea familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hilo, basi sasa nimalizie kwa kuipongeza Bajeti hii na kuwapongeza Wakuu wa Magereza kwa nchi nzima, kwa kweli wanajitahidi. Mazingira yao ni masafi, wamepanda miti , wamedumisha usafi, hata ukiingia ndani ni kusafi, hata chakula kinachopikwa, mimi nilishawahi kuonja, ni kizuri.

Kwa hiyo, kwa pongezi hizi, naomba wadumishe usafi na wadumishe upandaji wa miti ili mazingira yao yaendelee kuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo, niongee kuhusu suala la ulipwaji wa mishahara. Maaskari wetu kwa kweli wana hela ndogo kwa sababu hawana hata muda wa kuzalisha mali. Mtumishi mwingine anapotoka kazini, anaweza akaenda nyumbani akajilimia bustani yake, akaingia akaendesha shughuli yoyote, lakini Askari ana muda gani wa kuzalisha mali? Akishatoka kazini, amechoka na kazi zenyewe za mchana na usiku, anapata muda saa ngapi wa kuzalisha mali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwahurumie sana hawa vijana. Ndio maana Askari wetu wanajiingiza kwenye masuala ya rushwa kwa sababu ya ukata. Tuhakikishe tunawatengenezea mazingira ya kufanyia kazi, kuwaboreshea mishahara yao na posho zao wapate kwa muda muafaka na vile vile basi, Tume iliyoteuliwa na Mheshimiwa Rais kuona mishahara ya watumishi, iangalie na Magereza. Hao ni wenzetu, ni watumishi wanaotegemewa na Taifa hili katika kuhudumia wananchi wetu wanaopata matatizo mbalimbali na kutumikia vifungo. Ili waweze kufanya kazi zao kwa uhakika, lazima

Askari ahakikishe kwamba nyumbani usalama upo, chakula kipo na hakuna matatizo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine kuchangia mada hii ya Waziri wa Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *Dual-Nationality*, mtu mmoja ana uraia wa nchi hii, halafu ana uraia wa nchi nyingine, una utata mkubwa na sio hapa Tanzania tu, kwa sababu karibu dunia nzima inajadili. Katika majadiliano ambayo yanaendelea duniani, nchi nyingi, Wakenya sasa hivi wanajadili hili suala. Ni suala zima la usalama wa nchi. Unapokuwa na raia wa hapa na raia wa kule, usalama wa nchi unakuwa *compromised* kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamejadili juu ya uwezekano kwamba wageni wengi sana wanaweza wakamiminika kwenye nchi yako, siku utakaporuhusu nchi yako kuwa na *Dual-Nationality*. Kuna masuala mengine ya kijasusi, watu wako hapa, lakini wanakuwa hawana uzalendo wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile, *experience* ambayo nchi hii imepata kwa mfano wageni kutoka nchi mbalimbali, wamekuja wakapata *Passport* za Tanzania na tuna habari kulikuwa na mtu anaweza akalipa kiasi fulani cha fedha, halafu akakuletea *passport* ya Tanzania. Watu wamekaa kwenye *bar* wana-*bet*, mgeni anamwambia mwenyeji, Mtanzania anasema, nchi yenu hii *it has no big deal.* Mimi naweza nikapata *passport* ya Tanzania. Wanaweka mezani pesa, halafu baada ya wiki mbili anamletea *passport* ya Tanzania inayoeleza kwamba yeye amezaliwa Kijiji fulani kule Karagwe. Hili suala limewafanya Watanzania wengi sana wafike mahali wanatia shaka wazo lolote la kuleta *Dual-Nationality*. Nchi yetu itaingiliwa kwa kiasi gani na wageni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la kutunza rekodi za nchi yetu. Hatuna uhakika ni Watanzania wangapi wako nchi hii. Mmoja atasimama atakwambia tuna Watanzania milioni 33, mwingine atakwambia tuna milioni 34, nimesikia rekodi nyingine zinasema tuna milioni 36 na wengine wanasema tuna milioni 40, hatujui. Lakini pia, hatujui ni Watanzania wangapi walioko nchi nyingine. Waliko Kenya ni wangapi? Walioko Malawi ni wangapi? Sudani ni wangapi? Kosovo ni wangapi?

Mheshimia Mwenyekiti, juzi kulizuka vita Mashariki ya Kati na wote tunafahamu, nchi nyingi zilikimbilia kwenda kuwaokoa raia wao. Walituma manowari za kivita. Lakini Watanzania wangapi walikuwa wamekumbwa katika ule msukosuko, kwa sababu lazima wapo! Nchi yetu imeongea na nchi zipi nyingine wawasaidie kuwaondoa? Ni tatizo la kuwa hatuna takwimu za kutosha!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Wakimbizi, limewafanya raia wa kawaida na nazungumzia raia tu ambao wanaona Wakimbizi ndio wanapewa *preferential treatment* kwenye matibabu, alizungumzia Mheshimiwa mwenzangu hapo. Maisha ya Wakimbizi

yanakuwa maisha bora kuliko maisha ya watu wanaowazunguka. Ukivuka tu Kijiji cha wakimbizi, wananchi hawana maji. Ili wachote maji, wanakwenda kwa Wakimbizi ili watibiwe, wanakwenda kwenye *Dispensary* ya Wakimbizi na hali hii imeleta wasiwasi kwamba siku tutakaporuhusu *Dual-Nationality*, nchi yetu itaingiliwa kwa kiasi gani na haya yamekuwa ni mawazo ambayo yako kwa watu wengi. Watu wengi wanafikiri haya mambo yanaweza yakaiathiri vipi Tanzania? *Feelings* za watu zinabadilika kutokana na haya yanayoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba niseme susla la *Dual-Nationality*, linatakiwa li-*serve interest* ya Tanzania na linatakiwa liwe ni kwa ajili ya Watanzania wanaoweza wakafaidika kwa kuwa na uraia wa pili kwa maslahi na manufaa ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa duniani tuna nchi kama Nigeria, ni nchi iliyo na watu wengi takriban kuliko nchi nyingine zote za Afrika. Hakuna nchi yoyote duniani, hakuna Mji wowote mkubwa duniani, *as much as you might think* ambao hauna Mnaigeria. Lakini, Nigeria iliamua kwamba, kwa sababu yoyote ile, Mnigeria hatanyang'anywa uraia wa Nigeria kwa sababu ameweza kupata uraia wa pili au ameweza kupata haki ya kukaa katika nchi fulani kama raia wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi duniani pamoja na Uingereza, popote atakapozaliwa Mwingereza, hata kama amezaliwa na mjukuu na mjukuu na mjukuu, nchi ya Uingereza inasema wewe utaendelea kuwa raia wa Uingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazimbabwe wote ambao wana asili ya Uingereza, mpaka kesho wanahesabiwa ni raia wa Uingereza, kwa sababu gani? Hakuna mtu mwenye akili timamu anayeweza akaikana nchi yake! Hakuna mtu mwenye akili timamu anayeweza akamkana baba na mama, hakuna mtoto wa Kitanzania aliyetoka Songea, aliyetoka Vunjo au Loliondo, anayeweza akaikana Loliondo, anayeweza akaukana Uchaga wake au Umakonde wake au Usukuma wake. Watanzania wataendelea kuwa ni Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu wengi Watanzania wako nchi mbalimbali duniani. Tunao Watanzania walioko Spain, Uingereza, America, Canada na siku moja nilipita Tel Aviv, Israel, nikakuta kuna Watanzania wako Israel, nchi ambayo huwezi hata ukafikiri wapo. Watanzania wako dunia nzima! Lakini *they are proud to be Tanzanians* na wanapopata heshima ya kupata *a Nationality* ya Taifa lingine hawatakiwi waukane uraia wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2005 kwa takwimu za Waziri, Watanzania 55 wamelazimika kufumba macho wakiwa wanatoa machozi wanasema: "Ninaukana uraia wa Tanzania ili niwe Mnorway." Nani alikwambia Mhindi akiwa hapa anaweza akaambiwa aukane uraia wake ili awe Mtanzania? Mtanzania aliyezaliwa hapa hata kama angeenda nchi yoyote duniani, kumfanya aukane uraia wake ni kumwondolea haki yake ya msingi. Mtanzania yeyote bila kujali yeye ana asili gani, ni mweupe au mweusi, kabila gani ametoka, Mkoa gani ametoka, sehemu gani ya nchi ametoka, ni Mtanzania.

Siyo Serikali wala siyo chombo chochote kwa sheria ambazo zinaweza zikatungwa zina haki ya kumwondolea mtu uraia wake. Watu wanatafuta kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi duniani zinasema: "Mtu aliye na uraia wa nchi hii atasoma kwa nusu ya bei." Hata Uingereza, asilimia 50 ya bei ndiyo watalipa *tuition* katika Vyuo Vikuu. Lakini Watanzania wengi sana kwa sababu ya uzalendo tulionao ni ngumu kuukana uraia ukijua kwamba ukirudi hapa inabidi uanze kuambiwa "leta *visa* uliyonayo." Mtoto wa Kinyaturu pale ame-*happen* kwenda India halafu mnamwambia aanze kupatiwa *visa* ya kuja Tanzania! Hicho ni kitendo ambacho ni kinyume na haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaongea hapa kwa niaba ya Watanzania wengi sana walioko duniani.

**MBUNGE FULANI:** Hasa vijana.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Hasa vijana, ahsante sana. Hawa watu hawana mtu wa kuwazungumzia hapa kwa sababu kilichopo ni hofu, ni mashaka, ni wasiwasi, kwamba tukileta *dual nationality* hiki kitatokea, hiki kitatokea na hizi sababu zina ukweli. Lakini ninachotaka kusema *dual nationality* ni ili sisi tupeleke Watanzania wetu wapate wanachoweza kukipata na waendelee kubaki kuwa Watanzania. Nchi hii haitakaa imkane mtu aliyezaliwa hapa. Ndiyo maana tunasema tatizo likitokea Botswana ni lazima Watanzania twende tukawachukue Watanzania wetu. Lakini hutamwuliza wewe ni Mtanzania wa ngapi? Wewe ni mjukuu? Hebu leta hati. Watoto wanaozaliwa uhamishoni ni lazima waandikishwe kama watoto wa Tanzania. Nchi nyingi zinalilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi hapa wameoa wageni na kwa sababu wameoa hao wageni, moja kwa moja mwezi unaofuata ile nchi inakwambia: "Wewe umeoa mtu wa kwetu, tunakupa uraia wa kwetu." Tanzania hapa kama mwanamke akiolewa na mgeni akataka apate uraia wa huko aliko mume wake, wanamwambia: "Na uraia wa nchi hii tunaomba uukane kuanzia sasa hivi." Tunawaonea watu wetu. Hakuna sababu yoyote ya kuwaonea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili ni suala zima la kiuchumi. India ni nchi ambayo wanaipenda sana kwa sababu baada ya miaka michache sana ya India kuwa nchi maskini yenye watu wengi, Wahindi walifanikiwa kupeleka watu wao dunia nzima wakasoma. Kama mnafahamu, kuna wale waliokwenda California, eneo linaloendesha teknolojia ya juu ya kompyuta. Watu walioweza kuiendeleza Marekani walikuwa ni Wahindi na baada ya miaka kadhaa wameanza kuteremka India.

Sasa hivi kila Kampuni ya teknolojia ya juu wanapeleka watu wao India ama wakaanzishe Makampuni au wakafundishwe kazi, kwa sababu watu hawa walikuwa na *flexibility* na walijua. *Knowledge* ambayo wanaipata watu wetu, ungeuliza nchi nzima Maprofesa wangapi Watanzania wako duniani, wakati hapa hatuna walimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunasema tunaomba tulete watu wanaitwa *expatriates* na watu wanaamini mtu akiitwa *expert* ni lazima awe Mzungu, asiwe tu Mtanzania ndio anakuwa *expert*. Tungeweza kuwa na watu wetu ambao ni *expatriates* wako huko waliko, wakalipwa pesa ambazo tunawalipa hawa wengine. Ni Watanzania wangapi wangerudi nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Watanzania wangapi wanalalamika? Anatoka kijana wa watu anasoma Brazil, anafika *airport* ana mizigo yake tu ni mwanafunzi, wanamwambia: "Wewe umetoka Brazil, fungua kwanza hilo begi. Hebu tuone una nini?" Wanawawanyanyasa watu katika nchi yao! *This is wrong!* Nchi nyingine duniani unapokuwa raia, kwanza wameweka kabisa eneo la raia kupita, wanapita bila kuulizwa. Unaonyesha *passport* yako unapita. Hapa Tanzania unamkuta mtu amenuna kweli kweli, kisa yeye ni Afisa wa Uhamiaji. Amenuna kweli kweli utafikiri yeye dunia hii yuko peke yake! Anaanza kukuuliza: "Umetoka wapi?" Unasema: "Nimetoka Norway." "Eeh, ndiyo, hebu fungua, una kitu gani?"

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ni lazima tufanye kila tuwezalo kuwafanya Watanzania walioko duniani wapende nchi yao. Mtu afikirie asipokuja Tanzania mwaka mmoja atamani kuja nyumbani. Mapokezi ya *airport* muda mfupi mtu aambiwe karibu. Wale wanaofanya kazi Uhamiaji waambieni kuna kitu kinaitwa *smile*, *is a good thing, you smile*. Mtu amerudi nyumbani, lakini unakuta mtu kanuna kweli kweli utafikiri hiyo kazi ni ya kwake binafsi. Watabasamu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi tumewapelekea kompyuta, lakini zile kompyuta unakuta mtu anadonoa limoja *pap,* halafu anatazama tena. Mtanzania anakaa robo saa bila kupata huduma! Anarudi nyumbani katika nchi yake, halafu anaporudi kule unategemea aje hapa nchini, unategemea walete pesa zao! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakenya wanaiendeleza nchi yao. *Western Union is thriving* kwa sababu gani? Kwa sababu Waafrika walioko nchi nyingine wanapeleka pesa majumbani kwao. Nchi ya Eritrea na Nigeria zinaongoza Afrika kwa sababu Eritrea wao wameweka sheria, wewe kama ni Mueritrea na unakaa huko nje, ni lazima ulipe kodi ili waendelee kujua wewe ni mwananchi. Uchumi wa nchi hizi umeendelezwa sana kwa sababu watu wanapeleka pesa. Lakini ili vijana wetu walete pesa wawasaidie *school fees* watoto wao, wawasaidie wadogo zao, wawasaidie baba zao na mama zao ni lazima tuwakubali, ni lazima tuwajengee mazingira. Mtanzania anapopiga hodi nyumbani akaribishwe kwa mikono miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe wito kwa Serikali, bila kuchelewa walete Muswada wa Sheria hapa Bungeni utakaopitisha Sheria ya *Dual Nationality.* Niondoe *fear* tu, watu wengi wana mashaka, watu wengi wanafikiri watu wa Rwanda watavamia Tanzania, watu wa Kenya watavamia Tanzania. Sheria hii ni kwa sababu ya Watanzania wenzetu walioko kule, wanapopata haki ya kuwa raia wa kule tusiwanyang'anye uraia wa Tanzania kwa sababu Mwenyezi Mungu alipokufanya wewe Mtanzania, angeweza kukufanya uwe Mbulgalia. Utanzania ni kitu cha kujivunia, kibaki humu ndani. Tanzania *just like other countries,* lazima iwajali watoto wake popote walipo duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kukuomba tena na kwa kuiomba sana Wizara hii isisuesue, isitie shaka, ilete huu Muswada wa Sheria, upite kwa sababu utakuwa na mustakabali na utakuwa na maslahi ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Nyalandu. Naomba nimwite sasa Mheshimiwa Sijapata Nkayamba. Nilisema atafuatiwa na Mheshimiwa Abdul Marombwa, lakini namwona Mheshimiwa Yono amerejea hapa ndani. Kwa hiyo, ataanza Mheshimiwa Yono kwa kuwa amechangia mara moja na Mheshimiwa Abdul Marombwa atafuatia. Mheshimiwa Sijapata, tafadhali karibu.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuzungumza ili nami niweze kuunga mkono hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani. Sitakuwa mzungumzaji mkubwa, ila nitazungumza kidogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelekea moja kwa moja kwa wafungwa wanawake. Kwa kweli ni kitu ambacho kilikuwa kinanisikitisha. Siku za nyuma kabla sijawa Mbunge nilikuwa nikiona wafungwa wanawake wana mimba, nilikuwa najiuliza: Je, hizi mimba wakati wako jela wanazipata vipi? Nikaja kufuatilia. Kuna mwanamke alikuwa amefungwa kwa muda wa miaka miwili, anasubiri kumalizia kifungo chake baada ya miaka miwili na nusu alifungwa akiwa hana mimba.

Wakati huo huo, wanawake wanapokuwa jela huwa wanalindwa na Bibi Jela na wanakaa sehemu ambayo iko mbali kabisa na vyumba vya wanaume ambao na wenyewe wamefungwa jela. Sasa cha ajabu ni kwamba, mwanamke huyo anapofikisha mwaka mmoja au miwili unakuta ana mimba na wakati huo huo huwa hana mawasiliano na mume wake. Wakati mume wake anakuja kumwona huwa yule Askari mwanamke anayewalinda naye yuko hapo hapo na wanapozungumza wanasikia, huwa hawaendi faragha. Sasa nashangaa hiyo mimba huwa imetoka wapi mle jela? Naomba kuuliza, huyo mtoto atakayezaliwa baba yake ataitwa nani? Ataitwa Jela au Magereza? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri baadaye aweze kunipa majibu na huyo mtoto atakayezaliwa atakapokuwa mtu mzima au mtu mkubwa anataka kwenda Shule atasomeshwa na nani? Atasomeshwa na Gereza au atasomeshwa na Bwana Magereza au atasomeshwa na Serikali? Je, huyo mwanamke huko ndani ya jela ametendewa haki ya kupata mimba akiwa ndani ya jela? Au kama labda hiyo mimba ameipata kwa Roho Mtakatifu, leo tutaambiwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielekee kwenye matukio yaliyojitokeza mwaka 2003 katika Kijiji cha Simbo na Kasuku. Kulitokea matukio mbalimbali ya kuchoma moto nyumba za watu. Walichomewa wananchi waliokuwa wanahisiwa kuwa ni wachawi. Hao waliochoma hizo nyumba walikuwa ni wananchi wale wenye hasira kali na wananchi wenye hasira kali huwa siyo wachache, wanakuwa kama 200 hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo nyumba zilichomwa usiku na wananchi hao, lakini Maaskari walivyokuja kuwashika wale wananchi, walikuwa wanamshika mtu yeyote tu aliyehusika na ambaye hakuhusika baadaye wakapelekwa Polisi.

Walivyotoka Polisi wakapelekwa Mahakamani, walivyopelekwa Mahakamani kesi yao ikawa inaendelea, lakini cha ajabu ni kwamba, kila siku baada ya wiki Maaskari wanakuja kuwashika wale wale waliopeleka Mahakamani, lakini wakiwafikisha njiani wanawaachia. Sasa hapo ndiyo nashangaa, walikuwa wanawaachia kwa nini wakati walitumwa waje kuwashika wawapeleke ndani na wakati huo huo kesi yao iko Mahakamani? Kilichokuwa kinawafanya kuja kuwashika mara mbili mbili, mara tatu tatu usiku ni kitu gani? Wakifika njiani wanawaachia, hawawafikishi kule kunakotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri anipe majibu, ni kwa nini walikuwa wanawafikisha njiani na hawawafikishi kule kunakohusika? Kila ikipita wiki wanakuja tena wanawashika, yaani unakuta wale wananchi tena hawana amani. Kwa hiyo, hao wananchi walikuwa wananyanyasika sana. Yaani ilikuwa inabidi sasa wale wananchi wawe wanalala nje, hawalali ndani maana wakilala ndani wanakuja kuvunjiwa milango wanawekwa ndani ya karandinga wanapelekwa. Wakifikishwa njiani, wanashushwa. Sasa walikuwa wanashushwa kwa nini? Naomba Mheshimiwa Waziri leo atupe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona maelezo yangu ni hayo, siwezi nikaendelea zaidi ya hapo, ila ninachoomba ni majibu ya hao wanawake wanaopewa mimba wakiwa mle ndani ya jela. Leo naomba niyapate, wanapata sehemu gani hizo mimba na watakapozaa baba yao atakuwa ni nani na watahudumiwa na nani? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga hoja mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Sijapata kwa hoja hiyo ya wanawake na watoto na majina yao. Naomba nimwite Mheshimiwa Yono Kevela na muda ukiendelea kuwepo, Mheshimiwa Lucy Nkya naye kwa sababu amechangia mara moja tu na ameingia, atachangia, ameniletea taarifa alikuwa kwenye Kamati.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Marombwa naomba unisamehe, tutaendelea mchana kama hivi sasa muda hautatosha. Karibu Mheshimiwa Yono na Mheshimiwa Lucy Nkya ujiandae.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwa kweli kwa sababu nitachangia zaidi kwenye Wizara nyingine, lakini na hii nieleze kidogo kuhusu hali halisi ilivyo huko hasa katika upande wa vibali vya uraia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imejitokeza kwamba uraia ni kitu muhimu sana kwa sababu nchi nyingi duniani wananchi wanapewa vibali vya uraia, lakini nchini kwetu vibali vya uraia naona vinasuasua. Ninazungumza kwa sababu mimi mwenyewe yamenikuta, kwamba unaweza ukaona kuna raia wengine, wananchi wanabambikiziwa kwamba: "Huyu ahamishwe siyo raia." Lakini wakati fulani ni visa tu vya upande wa biashara au upande wa siasa, mtu anaambiwa kwamba huyu sio raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha mwaka 2003 mimi Yono Stanley Kevela, yalinikuta. Tukapitia sehemu zinazohusika, wanasema kwamba wewe siyo raia, uhame nchi hii. Tena anayetaka kunihamisha alikuwa ni mtu wa Bukoba, mfanyakazi wa Uhamiaji. Anasema: "Wewe Yono Stanley Kevela siyo raia wa Tanzania, ni mtu wa Afrika Kusini." Sasa, bahati nzuri niko hapa Bungeni, naelewa hivyo vitendo, watu wengi wanatendewa hasa katika visingizio vya biashara au kwenye siasa, mtu anaweza akabambikiwa kuwa sio raia. Nashauri Wizara ya Mambo ya Ndani iwe na uangalifu sana katika hili suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2003 nimehangaishwa sana mpaka nikaandika barua. Nimshukuru Mkurugenzi wa Uhamiaji Mr. Kiomana ndiyo akanitetea kwamba huyu bwana anabambikiziwa, lakini yule kijana amenisumbua sana. Sasa, naelewa kuna tatizo hilo linawapata Watanzania wengi, wanabambikiziwa. Mtu anashindwa kwenye biashara au kwenye siasa anaamua kumpakazia mwenzake. Vitendo hivyo vingine vinajitokeza, niliviona kwa macho yangu na vimenikuta. Kipindi fulani nilitaka kwenda Marekani, nilizuiwa kwa kuhofu kwamba mimi siyo raia. Nimekwenda Ubalozi wa Marekani pale wanasema: "Aah, wewe uraia wako ni wa wasiwasi." Mimi na mke wangu tukazuiwa kwenda Marekani. Kwa hiyo, vitu kama hivyo vipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza hivyo kwa niaba ya Watanzania wote wanaonisikiliza na wa Jimbo langu la Njombe Magharibi kwamba, kwa kweli hapa Tanzania wakati fulani vitendo vinavyofanyika sio vizuri kabisa. Kujitetea ili nisihamishwe, nikajaza mafomu mengi sana, ili kuthibitisha uraia.

Kwa hiyo, vitu kama hivi nilikuwa nafikiria kwamba tuwe waangalifu sana navyo. Bahati nzuri Serikali inajitahidi kufanya kazi nzuri sana, lakini wakati fulani malalamiko mengine yanayopelekwa ni ya uongo. Halafu mbaya zaidi, kuna watu ambao wako wengi wameingia nchini humu kinyemela, hao hawaguswi, wakitoa chochote tu wanalindwa. Sasa tutafika wapi?

Mtu ambaye ni mnyonge ananyanyaswa kwenye nchi yake, lakini mtu mwenye uwezo, mwenye pesa haguswi! Tunafahamu wako wengi tu wanakaa na ndiyo wanaingiza wahalifu na sisi tulikuwa tunategemea kwamba suala la kufichua Wahamiaji wengi ni suala la kila Mtanzania. Lakini sasa kuna wakati fulani Watanzania wanaweza wakawa na hofu kwamba ukipeleka kwamba fulani kaingia kinyemela, yule mtu anaanza kupata matatizo kwenye biashara na kwenye sehemu mbalimbali. Kwa hiyo, nafikiria Uhamiaji ijitahidi sana isilinde Wahamiaji ambao sio halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishie kwa kushukuru kwamba kwa kweli naunga mkono hoja na Bajeti ni nzuri, ila tu kwa kweli narudia kwamba tuwe waangalifu sana

katika kushughulikia hili suala la uraia na vibali vya uraia vitolewe mapema na wakati tunatoa vibali tunaweza tukatoa vibali kwa watu ambao sio wenyewe kabisa, tuwe tuna *verification*. Naona nisichukue muda mrefu, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. LUCY S. NKYA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Baada ya hapo, nimpongeze Waziri wa Mambo ya Ndani, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na wataalam wake wote kwa kutengeneza hotuba nzuri ambayo imetupa mwanga wa kuelewa zaidi shughuli za Magereza, shughuli za Uhamiaji na shughuli nyingine ambazo zinatendeka chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, ningependa nimpongeze Waziri na Wizara yake kwa kuja na tamko kwamba nchi hii tutaanza kuwa na vitambulisho vya uraia. Ni jambo zuri na litasaidia kuonyesha kwamba Mtanzania ni nani na kupunguza kero na adha ambazo Watanzania wengine wanazipata.

Lakini basi, ningependa nitoe angalizo moja tu kwamba, kama mtindo au mkakati wa kutengeneza hivi vitambulisho hautaangaliwa kwa busara na kwa uangalifu, tutatengeneza *avenue* za kutoa tena rushwa, kutakuwa na mazingira ya rushwa kwa wale ambao watapewa hili jukumu. Bahati mbaya katika hotuba yake, Mheshimiwa Waziri hakutueleza kwamba huo mpango wa kutoa hivi vitambulisho utakuwaje ili kutuondoa wasiwasi kwamba mazingira ya rushwa hayatakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kushauri kwamba, katika zoezi hili, ni vyema Viongozi wa chini, Wenyeviti wa Mitaa pamoja na Madiwani na Uongozi kwenye Kata ushirikishwe kikamilifu ili waweze kutoa taarifa kamili kwamba, raia aliyepo katika eneo lao ni nani na asiyekuwa raia ni nani kwa sababu kuna Wakimbizi wengi ambao wamesambaa, hasa wale ambao wamefanikiwa kuzungumza lugha ya Kiswahili, basi wameamua kujifanya kwamba na wao ni raia wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia nitoe pongezi kwa mikakati yao ya kuboresha kilimo pamoja na mafunzo ya ufundi. Lakini haya Magereza yetu yako kwenye Vijiji vyetu, yako kwenye jamii zetu, sijaona mahali ambako wale wananchi wanaozunguka yale Magereza wanafaidi huu ujuzi *especially* ujuzi wa kilimo ambao uko ndani ya Jeshi letu la Magereza. Naomba sasa basi, Wizara ishauri Magereza ambayo yanafanya shughuli za kilimo yatoe ujuzi na mafunzo kwa vile Vijiji vinavyozunguka.

Nitoe mfano, tuna Gereza la Kiberege. Lile Gereza ni la kilimo, lakini ukiangalia mashamba yao ni mazuri kuliko mashamba ya Vijiji vinavyozunguka Gereza lile. Sasa, sisi wananchi tunaozunguka haya Magereza tunafaidi nini? Naomba basi uwepo mkakati wa ujirani mwema wa kuweza kutoa ule ujuzi na utaalam ambao wenzetu wa Magereza walionao waweze kuwasaidia wananchi wanaowazunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza haya, naomba sasa nizungumze kero kidogo kuhusu Jeshi la Zimamoto. Naomba niseme ukweli kwamba, wananchi wengi hawaridhiki na huduma za Jeshi hili. Nimekuwa najiuliza hivi hawa wanafunzwa wapi? Wanapewa maadili gani ya kazi? Kwa sababu mtu ambaye kweli unaipenda kazi yako *and you are real committed,* kuona kwamba unazuia madhara ya moto katika jamii, basi utakuwa tayari wakati wowote unapoitwa, gari lako liwe na maji. Tunashangazwa kuona kwamba gari la Zimamoto linakwenda kwenye maeneo na ndiyo linaanza kutafuta maji. Tunaanza kujiuliza, kulikoni? Au huko waliko wamefungiwa maji? Kama wanafungiwa maji, basi tunaomba Idara ya Maji iwape maji.

Lakini itakuwa ni vizuri basi wakiwa na ile tunasema kwamba *quick response,* wanapoondoka wahakikishe haya magari kweli yanafanya kazi, haya magari yana ngazi, haya magari yamejaa maji, *otherwise* inakuwa kwamba kuwa na magari yasiyofanya kazi yamepaki na watu wameajiriwa kufanya kazi wanafika kwenye eneo la ajali wanashindwa kufanya kazi, inaonyesha picha ambayo siyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, napenda kuzungumza kuhusu vijana wanaofungwa katika Magereza yetu. Hawa vijana wanapelekwa kule kwa sababu aidha ni vibaka au ni wavuta bangi au wanauza bangi. Lakini kinachosikitisha, hawa vijana wanapoachiwa kurudi katika jamii zetu wanakuwa wamepata ujuzi zaidi wa kuwa wahalifu walio wakubwa zaidi. Inakuwaje mtu anapelekwa Magereza kwenda kufunzwa kuwa raia mwema, akirudi anakuja amepata ujuzi wa kuwa mhalifu wa kupindukia? Anarudi akijua mbinu za kuuza bangi vizuri, anarudi akijua mbinu za kuiba vizuri na wanasema kule kwamba, tunafundishwa na tunaweka vikao vya Mahakama namna ya kujibu na namna ya kwenda kujitetea Mahakamani.

Sasa ningeomba, muundo wa uendeshaji wa shughuli kule Magerezani usiwe ni kuwaita tu asubuhi foleni mkafanye kazi, mkafanye hivi, hapana. Kuwepo basi na *rehabilitation* ya kitabia (ukarabati wa kitabia). Wapate muda wa kuzungumza na kuelezwa ni nini maana ya kuwa raia mwema. Pamoja na kwamba tunawapa mafunzo ya ufundi stadi wa kuja kufanya shughuli, basi tuhakikishe kwamba wakirudi ule ujuzi walioupata wanautumia, siyo kwamba wanarudi kwenye uhalifu tena au kufundisha wengine.

Tunajua kwamba Serikali ina nia njema, lakini inawezekana labda wale wanaofanya hizi kazi hawajajua kabisa wajibu wao, wanafikiri pale ni kumuadhibu mtu tu. Pamoja na kumuadhibu, basi tumpe fursa ya kuwa raia mwema atakaporudi na aweze kuwa mfano kwa wengine katika Kijiji au pale Mjini anapotokea. Hilo naomba liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwa wale wafungwa wanawake. Mwenzangu Mheshimiwa Sijapata amezungumza kwamba wanapata mimba tu. Mimi naomba kuzungumza kama Daktari. Nimekuwa ninawaona wafungwa wanaletwa hospitalini, wana magonjwa ya zinaa. Unamtibu anapona, akishapona *give him another two weeks or one month,* anarudi. Wanapata wapi haya maradhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubaliane kwamba kuna mambo kule Gerezani ambayo yanatendeka ya kutokuwajibika kwa wale wanaowajibika kulinda wale wafungwa na afya zao. Akinamama wanazaa ndiyo, wanapata mimba na hatujawahi kusikia Serikali imezungumza kukemea hili. Sasa nani atakayekemea?

Naomba niseme wazi, hawa akinamama, hawapewi mimba na wafungwa wenzao. Wafungwa wenzao hawawapi hawa akinamama mimba, wafungwa wenzao hawawaambukizi hawa akinamama magonjwa yaambukizwayo kwa njia ya kujamiiana, wanaambukizwa na wale wanaowaangalia.

Naomba hili livaliwe miwani ya ziada kuhakikisha kwamba maadili ya kulinda utu wa mwanamke, maadili ya kulinda utu wa vijana wetu yanalindwa. Vijana wanaingia mle wakiwa hawana UKIMWI. Vijana wanakuja wamepata magonjwa ya zinaa, siyo magonjwa ya zinaa ya kawaida wanayopata wanaume, hapana. Ni kwenye njia ya haja kubwa. Wanakalia mle chooni? Ndiyo! Tuzungumze kabisa! Tuseme ukweli! Ni lazima hawa vijana walindwe, wasitumike tu na hawa wanawake wasitumike tu kama vyombo ambavyo vinatoa burudani kwa wale ambao wanawaangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanamke hata kama ni mhalifu ana heshima yake, atarudi kwa mume wake, wengi wao waliporudi wakaachika kwa sababu walirudi aidha wana maradhi, au wamebeba watoto. Nafikiri hili ni jambo ambalo litaipa hili Taifa letu heshima kama mwanamke atalindwa mle.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni msaada wa kisheria katika Magereza yetu kwa wale wanaohukumiwa. Wengi wa Watanzania hawajui haki yao ya kukata rufaa. Lakini tunaamini kwamba kule Magerezani kuna Wanasheria wamepewa hiyo kazi ya kuhakikisha kwamba mfungwa anapoingia mle anaelezwa na anapewa mikakati ya kuweza kukata rufaa ili aweze kupata haki yake. Kinachosikitisha ni kwamba, siyo wengi wanapata hiyo fursa, hawaelewi na hawapati msaada, ni nani anayetakiwa? Hawana Wanasheria kule Magerezani, wapo kumlinda nani?

Tunaomba hao Wanasheria watumike vizuri kuwasaidia, kuna wengi ambao wanakosa haki zao kwa sababu tunakubali kwamba rushwa ipo kwenye Mahakama yetu. Sasa kama rushwa ipo kwenye Mahakama yetu, kuna Watanzania wanapelekwa Magerezani kwa kukosewa haki kabisa na kwa kuonewa. Tunaomba Wizara na Jeshi la Magereza lihakikishe kwamba kila Mtanzania anapoingia, kunakuwepo na fursa ya yeye kuelezwa kwamba anaweza akakata rufaa na akapata msaada wa kukata rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza kwa sababu nina *experience* moja. Katika Wilaya ya Kilosa imefungwa familia, yaani baba, mama na watoto, kisa, kwa sababu mama amegombana na Mwalimu Mkuu kwa kumtumia mtoto vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kuzungumza amemtumia vibaya kwa namna gani, lakini kuna Mwalimu mmoja wa Shule ya Msingi kule Kilosa miaka miwili iliyopita alimtumia mtoto vibaya kwenye shughuli za ushirikina na shughuli za ngono.

Mama mzazi na baba mzazi wakaenda kugombana kwa sababu alikuwa na uwezo wa kumhonga hakimu, wakaenda kufungwa baba, mama, mtoto na mtoto mchanga. Wamefika kule Gerezani, wanaomba kusaidiwa kupata nakala ya hukumu hawakupata msaada mpaka imebidi mimi niende nikaitafute na kuanza kuomba *review* ya kesi ambayo ilichukua siku tatu wakaachiwa. Sasa kama walikuwa wamefungwa kwa haki, kwa nini *review* ifanyike siku tatu ili familia iachiwe? Naomba Magereza ifanye kazi ya kutetea haki za wale ambao wananyimwa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumza ni kuhusu sakata la nyumba za Kihonda *White House Morogoro*. Ilikuwa ni mwaka 2005 limetokea sakata, sawa Magereza imenunua zile nyumba kutoka *leather goods,* lakini kulikuwa na wafanyakazi wa *leather goods* walikuwa wanaishi kwenye zile nyumba na walikuwa wanaishi mle kwa sababu walikuwa hawajalipwa haki zao. Sasa kwa sababu Magereza walikuwa na nguvu ya kutumia Askari wao, walikwenda wakawapa mkong'oto, kipigo hasa! Tupa vyombo nje! Fanya kila kitu! Wakawatoa nje. Sawa wameondoka, lakini ilibidi hata Serikali kwenye ngazi ya Wilaya na Mkoa iingilie, lakini bahati mbaya hawakutusikiliza.

Walikuwa na haki ya kuchukua nyumba zao. Nafikiri wao kama walinzi wa amani kungekuwepo na fursa ya kuwa na *dialogue* kati ya wao na wale waliokuwa wanaishi kwenye nyumba wapewe muda wa kuondoka, ili wajue hatma yao ni nini kwa sababu hata malipo yao kutoka *PSRC* walikuwa hawajalipwa. Sasa inapofika mahali Serikali inaamua kuwanyima watu haki kwa kuwatupa nje kutokujali ana watoto, ana kabati ana kakitanda, hata kama ana kigoda, lakini apewe muda wa kujitayarisha aondoke nacho.

Mimi nafikiri mpaka sasa hivi sijaridhika, ningeomba Serikali iwaombe radhi wale wananchi kwa sababu bado hawajalipwa haki zao, walitupwa nje, tena unamtumia mfungwa, mfungwa *has nothing to loose* hata akikupiga kipigo cha kufa kwa sababu yumo ndani. Tayari ana *serve a sentence* atakutandika tu. Sasa kulikuwa na sababu gani ya kutumia wafungwa kwenda kupiga wale wananchi wa Kihonda, wengi wao wakiwa wanawake na kuwatupa nje? Naomba hilo Mheshimiwa Waziri anipe jibu la kuridhisha kwamba Serikali imefanyaje kuwasaidia wale watu? Lakini najua wengine mpaka leo pa kuishi hawana, wanaishi kwa watu na mali zao ziliharibika na zilitupwa nje. Pamoja na kwamba wale wananchi wamekuwa waungwana hawataipeleka Serikali yao Mahakamani, lakini Serikali inajua kwamba kila mtu ni mtoto wake, atapenda kuhakikisha kwamba kila mtoto wake anapata chakula na anapata haki aliyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza, ningependa nizungumzie Uhamiaji. Kumekuwa na zoezi la kutoa *passport* mpya. Tunashukuru kwamba wanajitahidi sana kufanya lile zoezi. Lakini ningependa wawe waangalifu kidogo, kuna watu mle ndani ambao nafikiri siyo waajiriwa wa *Immigration* labda ni *middle men,* wanaingilia kuwapa wananchi wetu matatizo ya kupata *passport,* wanakaa mlangoni, wanatoka *I don't know* kama uongozi unajua, lakini wale Watendaji wanafanya kazi yao vizuri, kwa hilo nawapongeza. *(Makofi)*

Lakini kuna watu ambao wanajifanya ni ma-*agent* wa kutafutia watu *passport,* ninaomba Idara iangalie hilo kwa sababu itaweza ikaleta picha mbaya ya kujenga mazingira ya rushwa ambayo naamini kwamba hayapo ila hao mawakala wanajitia kwamba ni wajuaji wanaweza wakamsaidia mtu anayetoka Kijijini kupata *passport,* wanaweza wakachafua kazi yao nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, naomba niunge mkono tena hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ingawa kulikuwa na danadana kidogo huko nyuma, nasogeza mbele, lakini hatimaye nimepata hii nafasi, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja ingawa nitataka maelezo baadaye kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwa haya mambo ambayo mimi binafsi nitakayoelezea katika mchango wangu.

Kwanza nianzie kuhusu malengo ya Jeshi la Magereza. Katika mwaka 2006/2007 katika Jimbo langu mimi nina Gereza la Kibiti. Kabla ya kuja Bungeni mwezi wa Sita mwanzoni nilikwenda kulitembelea lile Gereza la Mng'alu na nilivyokwenda Gereza la pale niliona mambo ya ajabu ambayo binafsi sikuwahi kwenda katika lile Gereza. Ni mara yangu ya kwanza kwenda mwezi huu wa Sita. Lakini hali ya Gereza la Mng'alu ni mbaya sana. Kwanza katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 15 anasema malengo ya mwaka huu ni kuhakikisha kuwa anakamilisha ujenzi wa nyumba za Askari zilizoanza kujengwa mwaka 2005/2006. Niseme ule ukurasa wa 15 na 16 ametaja Gereza la Kibiti lakini lile Gereza ni la Mng'alu siyo Kibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Gereza lile, nyumba iliyofanyiwa marekebisho ni nyumba moja tu ya Mkuu wa Gereza na sio nzuri. Lakini nyumba nyingine za Askari wote walioko pale Kambini nyumba za udongo, nyumba ambazo hazina hadhi ya kuishi Askari Magreza hasa akiwa na cheo chochote kile nyumba zile hazina hadhi. Sasa anaposema kwamba mwaka huu anataka kukamilisha ujenzi wa nyumba hizo pale, sio kukamilisha ujenzi ni kwenda kujenga nyumba. Nilitaka nijue pengine mwishowe anieleze kwamba katika Gereza la Mng'alu ni nyumba ngapi za Askari wa Magereza zitakazoweza kujengwa katika Bajeti ya mwaka huu? Nyumba sio nzuri kabisa, Mheshimiwa Waziri akienda kuziona mwenyewe utaziogopa, ni nyumba za udongo zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa pili, nizungumzie kuhusu hali ya Gereza la Mng'alu. Lile Gereza kwa kweli ni kama nilivyosema mimi sijapata kuliona, limejengwa kwa bati juu na bati chini. Wakati wa mchana mle ndani mnakuwa na joto kali la ajabu, ni *full suit* ya bati. Wakati wa usiku hali ndiyo hiyo hiyo, baridi inakuwa kali sana kwa sababu ni bati tupu. Lakini kibaya zaidi hayo mabati yote hizo paa zake zinavuja. Wakati wa masika mahali pa kulala hakuna, maji yanaingia mpaka ndani. Sasa nilikuwa naangalia: Je, kwenye Gereza la Mng'alu kuna fedha zozote ambazo zimetengwa kwa ujenzi, si kwa ajili ya ukarabati? Pale hakuna ukarabati kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijaziona. Ninaomba sana kabla ya kuanza kujenga Magereza mapya haya yaliyokuwepo yaangaliwe hasa liangaliwe Gereza la Mng'alu, hali yake siyo nzuri. Gereza hili halina uzio, uzio umewekwa wa miti tu. Wale wafungwa pale mimi nadhani wana moyo sana kuendelea kukaa kutokana na hali ilivyo ni rahisi hata mtu kuondoka. Lakini wapo wanaendelea kufanya kazi. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri ajiandae kulijenga upya Gereza lile ili liweze kufanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Katika Gereza hili, vile vile nizungumzie suala la Ofisi. Ofisi ya Mkuu wa Gereza, nayo ni ya udongo. Ofisi ile imewekwa sakafu ya *cement,* lakini sasa ni udongo. Sasa Ofisi ya Gereza kubwa kama lile unajenga Ofisi za Udongo, tunatarajia kitu gani? Afisa wa Jeshi, anakaa kwenye Ofisi ambayo ni ya udongo, kwa karne hii ya sasa ni aibu. Hawa wenzetu wa Magereza wanachotoka wao ni vifaa vya ujenzi peke yake. Ukiwapelekea *cement*, ukiwapelekea misumali, watafanya kazi zile vizuri sana. Bajeti yao ni ndogo kulinganisha na maeneo mengine kwa sababu hawahitaji fedha za fundi, mafundi wako ndani mle mle Gerezani. Kwa nini tunashindwa kuwapatia vifaa ili zitengenezwe Ofisi nzuri? Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, aliangalie hili kwa kupatia kipaumbele hasa hasa Gereza la Mng'alu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Gereza la Mng'alu ni Gereza la kilimo. Lina zaidi ya hekta 30,000 ambazo zimetengwa kwa ajili ya shughuli za kilimo. Cha kusikitisha kwenye Gereza lile, hakuna trekta, hakuna chochote kile. Sasa Gereza la kilimo unawapatia majembe ya ngwamba, majembo ya mkono tunatarajia nini?

Nilipokwenda kuzungumza na wale wafungwa, waliniomba sana walisema: "Kama tunataka kuleta mabadiliko Mheshimiwa Mbunge, iombe Wizara ituletee trekta moja tu. Tunaweza kuzalisha chakula cha kulisha hata kama Wilaya nzima ya Rufiji kwa mwaka mzima. Kwa nini tusiwapatie hivi vifaa kama trekta ili hawa watu waweze kufanya kazi yao vizuri? Tukiwapatia zana Gereza lile, litakuwa na jina kamili kama ni Gereza la kilimo litakuwa kweli ni Gereza la kilimo. Naomba Mheshimiwa Waziri, aangalie pengine kwenye Bajeti yake ya mwaka huu au hata ya mwakani, aweke trekta kwenye Gereza la Mng'alu, hali ya Gereza lile itakuwa nzuri sana na wala hawataomba chakula, watajitosheleza wao wenyewe na watakuwa na *surplus* ya kuwapatia wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Gereza lile vile vile niliona jambo moja la ajabu la mahabusu. Nilikwenda pale Gerezani nikazungumza pia na mahabusu. Nilimwona mahabusu wa miaka 12, watoto wadogo wa miaka kati ya 12 na 17 walikuwa wanne. Sasa nilikuwa naangalia hivi mpaka anawekwa ndani huyu mtoto alikuwa na makosa gani? Nilipowauliza wale watoto wakasema tu kwamba wengine waliiba mahindi ya kuchoma amewekwa ndani, hakimu hayupo anakaa wiki mbili/tatu kwa kosa dogo la kuiba mahindi mtoto wa miaka 12.

Sasa nilikuwa naomba sheria hizi ziangaliwe na wale wanaopeleka ndani watoto kama hawa kuwachanganya watu wakubwa, kwani wao hawajui madhara wanayopata hawa watoto kule ndani na wanakaa kwa muda mrefu sana kabla kesi yao haijaamuliwa.

Nilikuwa naomba Waziri, aliangalie hili suala la mahabusu, hawa watoto wa miaka 12 wakipelekwa Mahakamani kwa kosa lile kama kweli inathibitika pale pale hakuna sababu ya kuchelewesha hii ya kesi. Kama hukumu itakuwa ni ya viboko, sijui kama ni viboko au kitu gani, itolewe hukumu wakati ule ule asiende kuchanganywa na watu wengine wakubwa kule. Mtoto wa miaka 12 unamuweka ndani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kubambikiwa kesi miongoni mwa wa mahabusu waliokuwa mle ndani wana muda mrefu sana kwa sababu tu ya kubambikiwa kesi. Hili suala lipo, tunaomba sana Wizara yako iangalie Askari. Baadhi ya Askari sio waaminifu. Wamekaa kwa muda mrefu katika Vituo wanajenga uhasama na baadhi ya wananchi wanaokaa katika maeneo yale, matokeo yake wanabambika kesi wale ambao pengine ni maadui zao. Sasa hilo ni jambo la msingi sana kuangalia, ukaaji wa muda mrefu wa askari. Askari mwingine ana miaka saba, mwingine ana miaka kumi kwenye kituo kimoja anafanya nini huyu mtu? Hivi hakuna vituo vingine vya Askari kupelekwa maeneo mengine? Kwa nini wasihamishwe hawa watu? Nilikuwa naomba sana uhamisho huu ufanyike ili kupunguza hili suala la watu kubambikiwa kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Shule ya Msingi Wami - Vijana. Katika kujibu swali moja la Mheshimiwa Mbunge wiki iliyopita, Waziri alizungumza kwamba Wami - Vijana, ni Shule ambayo inawaandaa wafungwa ili wapate Elimu ya Msingi. Hilo ni kweli mimi nilikuwa Afisa Elimu Taaluma katika Wilaya hiyo. Lakini pale pana matatizo. Matatizo yaliyokuwepo ni kwamba, ile Shule haifundishi vizuri ingawa watoto wanaosoma kwenye Shule ile wanafaulu vizuri sana. Mahula wao wa mafunzo unaanzia mwezi Juni, baada ya shughuli za kilimo kumalizika kuanzia Januari mpaka Juni ni kilimo tu.

Lakini baada ya kutoka, ndipo kuanzia mwezi Julai wanasoma kwa muda miezi miwili, wanafanya mtihani wa darasa la saba, hiyo ndiyo hali halisi. Wale wanafunzi wanaofaulu kwenye Shule ile wote hawapelekwi Sekondari. Mwaka 2001 mwanafunzi wa kwanza katika Mkoa wa Morogoro alitoka Shule ya msingi Wami Magereza na alipangiwa kwenda Shule ya Sekondari Mzumbe. Lakini tokea mwaka 2001 mpaka leo watoto wanafaulu, labda mwaka 2005 ambapo mimi sikuwepo kwa sababu niliondoka pale mwezi wa Saba wanafunzi wale hawaendi Sekondari. Ile haki yao ya elimu haipo. Wanafaulu tu Elimu ya Msingi, Sekondari hawaendi. Ukiuliza, wanasema *nature* ya kosa lililompelekea mpaka yeye kufungwa haruhusiwi kutoka pale. Sasa nilikuwa naomba Serikali kama kweli inataka kutoa elimu kwa hawa vijana wanaofungwa, basi kama hawana uwezo wa kwenda kwenye Shule za Sekondari za kawaida za Serikali waandaliwe Shule yao ya Sekondari ili waweze kupata elimu yao ya juu ya Sekondari kwani wana akili. Mtoto wa kwanza mwaka 2001 ametoka katika Shule ya Sekondari Wami Magereza, kwa nini tusiwapatie Shule itakayoweza kuendeleza vipaji vyao, wanaweza kuwa raia wazuri sana hapo baadaye vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nilikuwa naomba Shule ya Msingi ya Wami iangaliwe kwa sababu kama nilivyosema, mihula yao ya kufundisha ni siku chache sana. Hivi kwa nini wasiwe na wakati asubuhi wakalima mchana kwa sababu wale wanakaa pale, wakasoma masomo yale ya *Primary* vizuri badala ya kusubiri mpaka Shule zote

zimalizike ndipo hawa watu waanze kusoma masomo yao. Nasema, wale vijana wamefungwa tu kutokana na matatizo mbalimbali. Lakini uwezo wao wa akili ni mkubwa sana na unaweza ukasaidia sana maendeleo ya Taifa letu kama akili yao ikiendelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niseme tu kwamba nilikuwa na ombi mwaka huu wa fedha 2005/2006, kuna suala la umeme unapelekwa pale Kibiti, naiomba sana Wizara ishirikiane na Wizara ya Nishati na Madini ipeleke umeme kwenye Gereza la Mng'alu. Nadhani ukienda umeme pale, kazi kubwa sana itafanywa na wale wafungwa na maendeleo ya Gereza lile yatakuwa makubwa mno. Hilo ndiyo lilikuwa ombi langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, nasema tena kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya muda tulionao kuona kwamba umeshatutupa mkono na wachangiaji wawili niliobaki nao hawa wote wameomba wachangie mchana, kwa hiyo, naomba nitamke kwamba mchana tutaanza na Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir atakuwa mchangiaji wetu wa kwanza, atafuatiwa na Mheshimiwa Paul Kimiti na baadaye Mheshimiwa Naibu Waziri na Mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri, wataendelea na kumalizia kujibu michango ya Wabunge kupitia hoja zao.

Naomba nitambue tangazo hili na kulitangaza, Katibu wa *Amani Forum* Mheshimiwa William Ngeleja anaomba kuwatangazia Wajumbe wa Sekretarieti wa *Amani Forum* wakutane Saa 7.15 mchana Ukumbi Na.321 kwa ajili ya Kikao muhimu sana. Baada ya kutoa matangazo hayo, naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.50 Mchana Bunge liliahirishwa Mpaka Saa 11.00)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na majadiliano yetu ya leo, naomba kwa heshima niwatambue wageni waliokaa kwenye *Gallery* ya Spika, tunaye *IGP*, Said Mwema, tunaomba kumkaribisha sana leo kwenye Ukumbi wetu wa Bunge. Lakini ameambatana na Katibu Mkuu Usalama wa Raia, Bwana Bakari Mahiza, mume wa Naibu Waziri Elimu na Mafunzo ya Ufundi. *(Makofi)*

Pamoja nao, tunaye Kamishna Godwin Mtweve, Kamishna Khalid Lwizan, Kamishna Paul Chagonja, Kamishna Alfred Tibaigana, Kamishna Robert Manumba na *ASP* Otieno Mpambe. Tunawakaribisha sana katika Bunge. Kwa niaba ya Bunge, nasema karibuni sana. *(Makofi)*

Msemaji wetu wa mchana wa kwanza kwa mchana huu wa leo atakuwa Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, atafuatiwa na Mheshimiwa Paul Kimiti na baada ya hapo,

tutaendelea na ule utaratibu wetu wa Naibu Waziri na Mtoa hoja kuendelea na hoja yake. Mheshimiwa Hafidh Ali tafadhali. Hayupo!

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kusema machache katika hoja hii ya Mambo ya Ndani na kwa kweli mimi nitakuwa sina mengi lakini kwanza nichukue nafasi ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake wote katika Wizara kwa kuwasilisha vyema hoja hii katika Bunge letu Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini pili, naipongeza Serikali kwa jumla za awamu zote hadi Awamu hii ya Nne ya Jamhuri ya Muungano kwa kuendeleza vizuri Wizara hii ya Mambo ya Ndani ambayo inagusa Zanzibar ikiwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, mchango utakuwa sio mkubwa, lakini niende moja kwa moja katika Uhamiaji. Uhamiaji pamoja na Wizara yenyewe na Serikali kwanza ningesema hakuna jambo muhimu katika Jamhuri hii kama kuaminiana. Tuna miaka 40 hivi sasa na ushee na shughuli za Uhamiaji kama zilivyoelezwa katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri zimekwenda vizuri. Lakini kuna mambo ambayo yanagusa moja kwa moja upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano ambayo kwa upande wangu ninahisi yangefanyiwa marekebisho kidogo ili kuwapa moyo wale Watendaji wetu wanaoshughulika na shughuli hizi za Uhamiaji zinazogusa mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya 1980 kuja hadi 1990 kule Zanzibar kulikuwa na utaratibu wa mtu anapoomba uraia, basi shughuli zake huwa zinamalizwa Zanzibar. Wizara ya Mambo ya Ndani iliunda Kamati ya watu wanane chini ya Waziri Kiongozi wa Serikali ya Zanzibar, ambao ndio walikuwa wanashughulikia shughuli hizi za kuomba uraia kwa upande wa Zanzibar. Nimesema hakuna jambo kubwa kama kuaminiana na ningemwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, basi aliambie Bunge hili, ilikuwaje hata Kamati ile ambayo iko chini ya Waziri Kiongozi ikaondolewa dhamana ambayo ilipewa ya kutoa uraia ndani ya Zanzibar kwa raia wa Zanzibar au kwa wananchi wa Zanzibar katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na badala yake hivi sasa shughuli hii mwenye kauli ya mwisho ni Waziri wa Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nimezungumza suala la kuaminiana, sioni mantiki ya kwanza, basi tufike mahali Kamati iliyoundwa na kukubaliwa na Wizara ya Mambo ya Ndani katika kipindi kirefu kilichopita ikiwa chini ya Waziri Kiongozi. Kamati ile hivi sasa shughuli zake zote zimerudi katika Wizara ya Mambo ya Ndani na maamuzi ya mwisho anayo Mheshimiwa Waziri. Hii ilitokea wapi? Sheria hii ilibadilishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano au kama nilivyozungumza mwanzo kuna mtu kapenda basi shughuli hizi zichukuliwe na Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi Waziri angetusaidia kwa hili. Kwa sababu katika kuleta mahusiano mazuri katika kuaminiana zaidi na utendaji ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Kamati hii imekuwa haina mengi, wala haina shughuli za kufanya. Shughuli yake ni kupokea aidha maombi kwa wale wanaoomba uraia na baadaye kupendekeza kwa Mheshimiwa Waziri. Sasa mtu mzito kama Waziri Kiongozi kumpa nafasi kama hii, halafu ukasema apendekeze, hili ningemwomba sana Mheshimiwa Waziri baadaye apendekeze kidogo, haiingii katika mantiki. Naomba sana Mheshimiwa Waziri aje anisaidie ilikuwaje hata ukabadilishwa utaratibu ambao ulikuwa unafanywa mwanzo.
Lakini Uhamiaji, dosari hii niliyozungumza, nichukue nafasi ya kuipongeza sana Idara ya Uhamiaji Bara na Visiwani kwa utendaji mzuri wa kazi zao. Juzi kulikuwa na swali hapa liliulizwa na Waziri, akajibu kwamba, kwa sasa hivi kama unataka *passport,* kwa utaratibu iliyojiwekea, haichukui zaidi ya siku nne kwa Zanzibar. Lakini ikatajwa kiasi cha wiki moja kwa Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba kweli hivi sasa ndani ya Uhamiaji Zanzibar katika suala zima la kuchukua *passport book* kama huna matatizo mengine, yako mwenyewe, basi kweli haizidi zaidi ya siku nne, unapata *passport book* na kufanya shughuli zako. Ni hatua kubwa ya kupigiwa mfano ambayo siku za nyuma ilikuwa haijawahi kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niondoke hapo, nielekee Magereza. Kwenye kitabu hiki, wakati Mheshimiwa Waziri alipokuwa anatusomea, kuna baadhi ya mambo mengi ambayo ilikubali kwamba yako kwenye Magereza, matatizo mbalimbali kama msongamano wa mahubusu na wafungwa na mambo mengine kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubali kwamba pia kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri, hali ya Magereza ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, bado haijaboreshwa kiasi ambacho kinachotakiwa na hasa hivi sasa Tanzania ikiwa tumeingia katika hali ya demokrasia na haki za binadamu ndani ya dunia tunayoishi hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niipongeze Magereza kwa ushirikiano mzuri iliyonao baina ya Idara hii ya Magereza Tanzania Bara na Vyuo vya Mafunzo Zanzibar. Hawa ni watu ambao wanashirikiana sana, wanapeana mafunzo sana, wanabadilishana utaalam na kwa kweli kama inavyoitwa, Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa mimi ninavyoona hivi sasa wakati umefika tuna miaka 40, imeshafika haja sasa hivi kuunganisha baina ya Vyuo vya Mafunzo Zanzibar na Magereza Tanzania Bara. *(Makofi)*

Kama kuna Uhamiaji Zanzibar, kuna Uhamiaji Bara, basi sioni kuna taabu gani isiwe kuna Magereza Zanzibar kwa utaratibu maalum na kuna Magereza Bara. Kwa nini nikasema hivyo? Nasema hivyo kwa sababu shughuli za Idara hizi mbili zote zinafanana. Zinafanana kwa maana ya kutekeleza shughuli za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini pia zinafanana kwa sababu ya mafunzo wanayopeana watu hao wawili au Idara hizi mbili. Askari wanapewa mafunzo na wakati wanachukua mafunzo ya Magereza Bara. Lakini wakati mwingine wataalam kutoka Magereza Bara wanakuja Zanzibar. Ningemwomba basi Mheshimiwa Waziri alifikirie suala la kuunganisha Vyuo vya Mafunzo na Magereza Tanzania ili iweze kufanya kazi pamoja. Kule Zanzibar

tumeweka Vyuo vya Mafunzo kwa maana ya kushughulikia wafungwa wanaofungwa kule kwa maana kule tungeita wanafunzi na kwamba wanafunzi wanafundishwa.

Mheshimiwa Waziri kasema kuna Vyuo maalum ambavyo vinatoa mafunzo ili baadaye watakapoondoka wafungwa hawa waweze kujitegemea kwa shughuli mbalimbali. Lakini kwa Bara ningemwomba sana Mheshimiwa Waziri akaliangalia suala la hawa wafungwa sugu. Wafungwa sugu wana madhara mengi kwenye Magereza. Kuna taarifa tunazozipata baada ya kutembelea kule kwamba kuna mambo ambayo sio ya kawaida yanayofanywa na wafungwa hawa sugu na kuna wafungwa wapya wanakwenda kule wanapata taabu sana, kwa sababu wanakuwa hawajui taratibu za kule na yale mambo yaliyomo ndani ya mazingira ya Magereza yenyewe hayazungumziki katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na matatizo yale, mambo yanayofanyika ndani ya Magereza baina ya mtu na mtu lazima yapigwe vita na tuweze kupata hao vijana wanaozungumza kwamba akitoka wawe wanakuja na mafunzo mazuri au wanakuja na taaluma nzuri badala ya vijana kutoka na hali mbaya. Sasa Mheshimiwa Waziri kwa upande wa Magereza ningeomba sana suala hili alisimamie vizuri, kama kuna dawa nyingine ya wafungwa hawa sugu, basi ingetafutwa ili kusaidia vijana wetu wanaoingia kule waweze kujifunza mambo mema na kubadili tabia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo ningependa kulizungumza ni kuhusu uraia zaidi ya nchi moja. Limezungumzwa hapa kwamba kuna ombi au kuna mwelekeo baadhi ya watu kutaka raia wa Tanzania wanaoishi nje, basi wawe na uraia zaidi ya nchi moja. Kwa upande wangu, sioni kama baya, lakini mara nyingi mimi suala linapokuja hapa halafu likagusia Zanzibar kwamba liwe kigezo, huwa linanishtua kidogo na linaniondoa pale mantiki ya mwenzangu ambaye amezungumza na naona kama anataka kutupeleka mahali pengine. Kwa nini utaratibu huu usiwe Zanzibar peke yake? Hii ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar siyo kwamba wenyewe ni wakorofi, hapana. Lakini mimi najua kwamba Zanzibar kwa sababu wanahisi labda Zanzibar wanaweza wakalikataa suala hili, usishangae sasa tukakataa kwa sababu Zanzibar wanaweza wakakataa suala hili. Wale wenye mwelekeo wa suala hili wao hawana, pengine wanaelekea kwenye kupiga kura. Sasa ukitaka kuchanganyisha uraia wa nchi mbili halafu na kupiga kura, ni vitu viwili tofauti. Inategemea umeishi muda gani huko uliko. Una *hold passport* ya aina gani na halafu unataka uraia wa Tanzania. Masuala mawili haya ni tofauti. Sasa waliolizungumza hili kwa kutegemea kwamba labda kuna kupiga kura, ah! Wazanzibar wasifikirie hilo. Unaweza ukawa una uraia wa nchi mbili lakini usipige kura Zanzibar. Sasa kama kuna watu ambao wameleta hoja hii kwa maana kuelekea kupiga kura mwaka 2010 Zanzibar hatutaki na tutaendelea kukataa. *(Makofi)*

Lakini kweli tunataka uraia kwa maana ya kuja uwekeze, ujenge nchi yako, karibu sana. Sasa tutakuwa macho sana kwa hili na tutalizungumza kwa kina kwa sababu nina hakika litakapoletwa pande mbili za Jamhuri ya Muungano watakaa watalizungumza na mwisho wake tutakubaliana. Lakini sisi tutafika mahali tuseme wale wanaotegemea

kupata uraia wa nchi mbili kwa maana waje kupiga kura Zanzibar hawana nafasi tena na hili wasitegemee. *(Makofi)*

Lakini kama tunakwenda kimataifa, imetolewa mifano humu, Msemaji wa Upinzani, akatutajia Ethiopia, Ghana na sehemu nyingine. Tunapotaka kuchukua nafasi ya kuoanisha au kufananisha, basi tuchukue mazingira ya nchi zenyewe. Huwezi kufananisha Tanzania na Ghana. Huwezi ukaifananisha Tanzania na Ethiopia na nchi nyingine. Tanzania tuna maadili yetu, tuna taratibu zetu. Kuna aina ya tulivyojitawala ndani ya Tanzania, sote tunajua. Sasa ukitaka kulinganisha kwa sababu ya kuipa nafasi katika hoja yako, kwa Zanzibar hakuna. Tuko tayari kuwapokea, lakini ni wazi kwamba Tanzania watataka kuwekeza kuendeleza Jamhuri ya Muungnao wa Tanzania na Zanzibar, lakini kama unakuja kwa kupiga kura, nafasi hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na wenzangu kwa kuwashukuru wale wote ambao wameandaa mada hii. Lakini nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya mchana huu kuchangia hoja hii muhimu na nitoe pongezi kwa jinsi ambavyo unaendesha Vikao vyetu vya Bunge na jinsi ulivyokaa na kuenea katika Kiti hicho cha Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Rais kwanza kwa kumteua Mheshimiwa Capt. John Chiligati kuwa Waziri, Mheshimiwa Bernard Membe kuwa Naibu Waziri na Ndugu Solomon Odunga kuwa Katibu Mkuu. Mimi nimeridhika kabisa jinsi walivyoandaa hoja hii na mimi naiunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeamua kusimama kwa sababu kubwa tatu. Kwanza, ni kuelezea shukrani zangu ambazo katika kipindi kilichopita, Mheshimiwa Waziri, ambaye alikuwa Naibu Waziri anakumbuka katika Bunge lililopita nilikuwa nimeahidiwa mambo kadhaa, lakini bahati mbaya sijui ni ukosefu wa fedha, hayakutekelezwa. Leo nashukuru kusema kwa dhati kwamba amenifurahisha Mheshimiwa Waziri baada ya kusema sasa mambo niliyoyaomba yanaanza kutekelezwa. Moja, ni suala la kutupatia fedha kwa ajili ya kununulia gari la Zimamoto Mjini Sumbawanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hiyo ni heshima kubwa kwa sababu kati ya malalamiko ya wananchi ambayo katika Jimbo langu moja ni ukosefu wa gari la Zimamoto. Mwaka 2005 ni kweli ahadi ilitolewa ya kwamba gari litanunuliwa, lakini kutokana na ukosefu wa fedha, labda haikuwezekana. La pili ni suala zima la kuendeleza ukarabati wa nyumba za Askari wa Magereza Mjini Sumbawanga.

Nasema namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kuliona hilo kwa sababu hali ya nyumba hizo ni mbaya. Ni mbaya kwa kweli unasikitika Magereza kwa nini wanaendelea kuishi katika nyumba za aina hiyo. La tatu, ni kukamilisha upimaji wa maeneo ya Magereza eneo la Kizwite pale Mjini Sumbawanga ambayo itatusaidia labda kuhamisha hata Gereza letu la Mahabusu pale Mjini ili sasa liweze kuwa na nafasi kubwa ya kuweza kuchukua mahabusu wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilipomaliza Shule ya Sekondari, kazi ya kwanza niliyokuwa nimechagua na nikaenda kwenye kozi ni ya Afisa Magereza. Lakini sikumaliza hata mwezi mmoja nilitoroka.

Nilitoroka baada ya kuja kugundua kumbe Afisa Magereza amekuwa ni sehemu ya mfungwa kushinda na wafungwa ndani ya Gereza. Nikaona vipi kujipeleka mwenyewe kujifunga, kwa nini? Nalisema hilo kwa sababu kazi ya Afisa Gereza ni kubwa na ni nzito. Wenzetu wanaishi katika mazingira nusu wafungwa. Tangu asubuhi mpaka jioni wamo ndani na wanajifungia usiku pamoja na wafungwa. *(Makofi)*

Athari zake tunazifahamu, ilifikia sehemu fulani kusema wenzetu kwa kweli wanaonyesha utii sana kwa Serikali yetu, kuweza kukaa na wafungwa wakawatuliza na tukaishi kwa amani kwa sababu wako wakorofi mle ndani, wakiamua siku kubomoa nchi itatetemeka. Lakini wameishi nao. Sasa nikasema kama vivutio havipo kwa kuwasaidia Maafisa Magereza waendelee kukaa Magerezani, iko siku moja tutapata watu wa ajabu kuwa Maafisa Magereza mle ndani, wazuri watakimbia na ndiyo maana nataka kuwapongeza kwa kuvumilia kuendelea kuishi katika mazingira hayo. Nasi kama Wabunge, tutaendelea kuwatetea ili wapate vivutio vya kuendelea kufanya kazi yao katika utii na uaminifu katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Magereza yetu sitaki kuirudia. Nataka nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, ametoa taarifa nzuri sana. Lakini pia Kambi ya Upinzani wamejitahidi sana kutoa taarifa nzuri. Mimi nadhani yale ambayo yameandikwa, tutamwomba Mheshimiwa Waziri azingatie endapo yatakuwa ndani ya uwezo wetu ili tuyatekeleze, hali ya Magereza iendelee kuwa mzuri.

Mwanzoni tulikuwa tunaogopa na bahati nzuri *IGP* Mwema yuko hapa. Mwanzoni, wakati Wizara iko moja ambapo Polisi na Magereza walikuwa pamoja mara nyingi Bajeti iliyokuwa ikitolewa inaonekana kwamba Polisi wanapendelewa zaidi kuliko Magereza na ndiyo maana hali ikaanza kujumuika kusema labda Polisi ni muhimu zaidi kuliko Magereza ambayo sio kweli. Kila mmoja ana jukumu lake. Magereza wana jukumu lao, Polisi wana jukumu lao. Sasa kwa sababu wametanganishwa hakuna la kulalamika. Kazi iko kwa Mheshimiwa Waziri, sasa awajengee mazingira mazuri upande wa Magereza wafanye kazi yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ningependa kusema haya matatu yafuatayo:- Kazi mojawapo ya Mbunge ni kutembelea Magereza angalau kwa mwaka mara moja. Nami nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge watembelee Magereza katika maeneo yao. Mbunge kisheria anaruhusiwa kutembelea Magereza yake wakati wowote.

Nalisema hilo kwa sababu mimi mwaka huu nilipopata nafasi ya kutembelea Gereza, nimegundua mambo ya ajabu. Wako wenzetu ambao wamefungwa kwa kuonewa. Wako wengine wametiwa mahabusu kwa kuonewa tu. Wengine kukomoana tu. Hakuna haki inayotendeka. Lakini tunapotembelea, tunajifunza mengi. Mwaka huu peke yake nilipotembelea Gereza la pale Mjini Sumbawanga, nilipata mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitumia nafasi hiyo kama Mbunge kupeleka kwenye Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Mwenyekiti wake akiwa Mkuu wa Wilaya kumwelezea mambo niliyoyapata Magerezani. Kwa taarifa, ilisaidia baadhi ya vijana watano, sita wameondolewa kwenye Magereza. Kwa hiyo, nasema tungetumia njia hiyo, tungewapunguza hata baadhi ya wengine ambao kwa kweli wameingia mle, aidha kwa kuonewa, tusingoje hizi *parole,* hapana. Sisi wenyewe tutumie nafasi yetu kuelezea hali halisi ya humo ndani ya Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ningependa kushauri kuhusiana na Sheria Na. 5 ya mwaka 2002. Sheria hii ilikuwa inazungumzia kuhusiana na Bodi ya *Parole.* Bodi ya *Parole* tumwulize Waziri tatizo lake ni nini? Hivi imekwama wapi? Au ni kwa sababu *Parole* inakutana mpaka fedha zipatikane ndiyo wakutane? Kwa nini *Parole* isifanye kazi ya kuendelea kuwaangalia wale wote ambao wametimiza masharti yanayotakiwa kisheria waondolewe au wafungwe nje ili kupunguza mlundikano wa wafungwa na mahabusu katika maeneo yetu? Tulidhani tuliangalie na Waziri labda ajaribu kutuelezea kwamba *Parole* imeshindwa au kuna matatizo gani, kwa nini haitekelezi majibu ambayo tulitarajia kuyapata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili Sheria Na.6 ya mwaka 2002 nayo inazungumzia juu ya *Community Service* ambayo inazungumzia juu ya huduma za jamii kwa vifungo vidogo vidogo ya kwamba, badala ya kuendelea kuwafunga watu katika Magereza, wafungwe nje. Tatizo liko wapi? Mbona hatua haichukuliwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ni suala la Sheria ya Kunyonga watu. Mimi mwaka 2005 kama nakumbuka, taarifa tuliyokuwa tunapewa ya kwamba zaidi ya wafungwa 500 ambao walishahukumiwa kunyongwa, walikuwa hawajanyongwa. Nini kwa ajili ya Rais lazima aweke sahihi yake au muhuri wake kukubali wanyongwe. Tatizo liko wapi? Rais anaogopa nini kunyonga watu? Kama anaogopa kunyonga watu kwa sababu ya imani tu ya kwamba haoni sababu ya kumaliza maisha ya mtu bila ya maelezo ya kutosha, basi tukubali yafuatayo:-

La kwanza, Sheria yetu ya kunyonga tuifute. Tuifute kabisa, kwa sababu imedhihirisha kwamba hata Rais wetu hataki kunyonga watu. Kama ipo, kwa nini tuzaje watu? Tuifutilie mbali, tuwe kama nchi nyingine ambayo unapewa adhabu miaka 30, miaka 40 yaishe. Nilidhani hilo tuliangalie. Mimi nina imani kabisa kwamba, Rais wetu angependa haki itendeke, hataki watu kuwakatisha maisha yao. Lakini ni vizuri tukaliangalia.

Lingine, naomba Magereza yaendelee kuwa na shughuli za uzalishaji. Kule kwetu kuna Gereza la Moro la kilimo. Tuliomba tuongezewe wafungwa kutoka sehemu nyingine, wafungwa ambao wanakaa katika Magereza mengine hawana kazi yoyote, waje Rukwa wafanye kazi ya kilimo, tuzalishe chakula cha kutosha kuliko kukaa Mjini bila kazi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, punguzeni watu kutoka Butimba, kutoka Keko, waje Rukwa walime. Tunadhani itatusaidia sana kurudisha hadhi ya Magereza yetu na badala

ya kuwa kila wakati tunatafuta fedha kusaidia Magereza, watajitosheleza kwanza kwa chakula na watakuwa na ziada, mradi tuwapatie zana na vifaa za kufanyia kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Waziri atuambie tuliomba mwaka 2005 tuongezewe, lakini wakasema kwamba kuna matatizo hapa na hapa. Hilo nadhani ni vizuri na nina imani kabisa Kamishna wetu Mkuu, Ndugu Banzi, ataliangalia hilo ili aone namna ya kulikamilisha, tulikamilishe hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kutoa pongezi kwa Mkurugenzi wa Uhamiaji Ndugu Kihomanwa, amejitahidi sana pamoja na hali ngumu ya maeneo ambayo anafanyia kazi. Ofisi zake kwa kweli ni ndogo, lakini pia jitihada imeanza kuonekana ukilinganisha na kipindi tulichoanza nacho. Lakini ni vizuri nikaomba kazi ifuatavyo:-

Kwanza, ni kuangalia kabisa kwamba Mikoa ya Kagera, Kigoma na Rukwa wamevamiwa sana na hawa wenzetu ambao wanaitwa Wakimbizi. Lakini Mkoa wa Rukwa kwa kipindi kirefu haijapata msaada wowote kutokana na haya mataifa ya nje ambayo yanatoa fedha kwa ajili ya kutengeneza miundombinu ikiwa ni pamoja na barabara. Tungepata msaada wa barabara kutoka Mpanda mpaka Uvinza tungeweza angalau tukawa na ahadi nzuri ya barabara katika maeneo hayo na ni vizuri mkaliangalia hilo katika misingi ambayo mnaiomba.

Lingine ni vituo vya mipakani. Ni vizuri tukaangalia wenzetu wanafanya nini. Napenda kushukuru kwa sababu katika Mkoa wetu wa Rukwa tuliomba Kituo cha Kasesya mpakani mwa Zambia na tumejengewa Kituo kizuri sana chenye *standard* sawa na wenzetu wa Zambia na hiyo ndiyo inayotakiwa ya kwamba tuwe na vituo ambavyo vinajenga hadhi ya nchi yetu. Lakini nimeona sehemu nyingine hakuna hata Kituo. Nilikuwa nachukua mfano wa eneo moja ambalo nilikuwa naliangalia hapa hasa katika Mkoa wetu wa Ruvuma, kuna Kijiji kimoja kinaitwa Muhukuru. Muhukuru ni Kijiji ambacho kinapakana na Msumbiji ambako ndio watajenga barabara na daraja la kuunganisha Msumbiji pamoja na Tanzania.

Upande wa wenzetu kwa sababu ni wajanja, wamewahi kujenga Ofisi ya Uhamiaji na Polisi mapema. Upande wetu hamna lolote, pako kimya, watu wanavuka kwa kutumia magogo, usiku na mchana. Hivi kwa nini tusifikirie kuanzisha ujenzi wa Kituo cha Uhamiaji katika eneo hilo? Mimi nadhani ni vizuri mkaliangalia kwa sababu sijui kwa nini Mwenyekiti hulisemi hilo, maana yake ni kwako Peramiho kule. Lazima nikusemee, hapa huwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifika kule nikaona kwamba kuna haja ya kuwa na Kituo muhimu kwa kweli vinginevyo, tutachelewa, wenzetu watatuwahi, watakuwa na kituo kizuri. Daraja likishajengwa, hakuna lolote upande huu, watu watajipitia kama wanavyotembea hovyo bila utaratibu wowote. Nilidhani ni vizuri mkaliwekea umuhimu. *(Makofi)*

Halafu la mwisho ni Kitengo cha Asasi zisizo za kiserikali za *NGOs*. Nimetambua jitihada za Asasi hizi, zimekuwa ni nyingi. Waziri hukuzizungumzia kwa undani.

Lakini Asasi zisizo za kiserikali zimekuwa nyingi sana na zimekuwa nyingi. Tusipoangalia tutashindwa hata kuweza kuzidhibiti. Ni vizuri tukaona namna ya kusaidia Kitengo hiki, wana kitengo kadogo sana tena kina watumishi wawili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo hicho tukiangalie kwa undani zaidi, kwa sababu tunataka kipate wataalam wengine, wapate zana za kisasa, lakini la ziada ikiwezekana wapate wataalam ambao watazunguka na kuangalia hizi Asasi ambazo zinafumka kila siku ni za kweli au za Mitaani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka kusema kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia na nina imani Mheshimiwa Waziri ataendelea vizuri. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuhusu haki za binadamu zinavyovunjwa katika Magereza Tanzania. Katika ukurasa wa 10 katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii, Mheshimiwa Waziri, amezungumzia kuboresha huduma za wafungwa kutoka kuvaa kaptura hadi *Kaunda suit*, sweta, blanketi na kadhalika. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hatua hiyo, lakini suala la msingi kwa mwanadamu ni uhai wake kwanza. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, atoe ufafanuzi wa kina, sababu na namna atakavyoboresha haki za binadamu magerezani.

Hivi sasa kuna mauaji yanayotokea katika magereza yetu ya Tanzania, hivyo ni sababu gani mauaji yanatokea katika magereza yetu? Mfano hai ni mauaji yaliyotokea katika Magereza ya Kimbiji na Isanga. Serikali itachukua hatua gani ili mauaji haya ya wafungwa na mahabusu yasitokee tena?

Je Mheshimiwa Waziri, unaweza ukalifafanulia Bunge letu Tukufu, nini kilichotendeka hasa na hatua gani zimechukuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba ufafanuzi wa kina, kuhusiana na suala la kudhalilishwa mahabusu kwa kupekuliwa kupita kiasi wakiwa uchi wa mnyama, je, hii ndiyo kuboresha haki za binadamu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 26, Mheshimiwa Waziri, amezungumzia vitambulisho vya Kitaifa, kuanzia Tanzania Bara hadi Visiwani. Lakini huko Zanzibar, tayari kuna vitambulisho kama hivyo, je, Mheshimiwa Waziri, haoni

kuwa Wazanzibari watakuwa na vitambulisho viwili viwili na je, ni kipi kitakachokuwa na nguvu ukitilia maanani vile vya Zanzibar viko katika mfumo wa Kimataifa.

Mheshimiwa Waziri, haoni kuwa ni vyema hiyo fedha ikatumika kule visiwani kwa wale ambao hawakuwahi kujiandikisha? Je, vitambulisho hivyo vitakuwa vya kudumu na vitaanzia umri gani au kwa kila mtoto wa Tanzania anayezaliwa? Naomba ufafanuzi.

Kwa vile wafungwa wanapata mafunzo maalum ili wawe raia wema wanapomaliza vifungo vyao, je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba, wakati umefika magereza yasiitwe kwa jina hilo na sasa yaitwe Vyuo vya Mafunzo kama vile Zanzibar, kwa kuwa kunatolewa mafunzo ya amali na uraia mwema?

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kuteuliwa kushika nafasi hizo katika Uongozi wa Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nami niungane na wenzangu katika kuwapongeza kwenye utendaji kazi wao na pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hatuba yake nzuri. Ninapenda kuwasilisha hoja zangu ili nipatiwe majibu, ambayo yataweza kuleta changamoto katika kusukuma mbele maendeleo ya Wizara hii. Wizara hii ni muhimu sana kwa nchi yetu na ili umuhimu huo uweze kuwa bora, ni vyema iangalie maslahi ya watendaji kazi wake. Iweje wafanyakazi wa Idara zote zilizo chini ya Wizara hii, mpaka sasa wanapewa mishahara midogo, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba, hii ni mojawapo ya sababu za mianya ya rushwa na ufanisi mdogo? Ni lini Serikali italitatua tatizo hili? Naomba nipatiwe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Uhamiaji ni Idara kubwa sana katika masuala yote ya Uhamiaji na Uraia nchini. Inasikitisha hadi sasa Serikali haijaweza kuona kwamba, baadhi ya wafanyakazi wa Idara hiyo wana elimu ya chini hatimaye wanashindwa kutekeleza kwa ufanisi kazi zao.

Suala la kukamata wahamiaji haramu, limekuwa likitekelezwa bila mpangilio mzuri, kwani wahamiaji haramu wanapokamatwa ni muhimu wasafirishwe au kuchukuliwa hatua zinazosatahili, lakini inaelekea Serikali hili halitiliwi mkazo, kwani haikutenga fedha za kuweza kusafirisha/kurudisha makwao hao wahamiaji haramu, Je, naweza kupewa maelezo ni kwa nini Serikali haikutenga fedha hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la huduma ya zimamoto na uokoaji, bado haitoshi na ni duni mno, kwani matatizo yanapotokea/majanga hayo, tumeshuhudia mali na maisha ya watu, yakiteketea aidha, kwa kukosa magari (mengi mambovu/hayapo kabisa) na hakuna vifaa vya kisasa. Ni lini Serikali inataunda *Central Command Post,* ambayo itakuwa inawajibika moja kwa moja na huduma hizo. Naomba nipatiwe majibu ya hoja zangu. Ahsante.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Ndani ni muhimu sana na ni nyeti kwa usalama wa nchi, pamoja na kuwa Wizara hii

imegawanywa kwa Wizara ya Usalama wa Raia, bado Wizara hii ina majukumu mengi ikiwa ni pamoja na wakimbizi. Tanzania ni nchi yenye wakimbizi wengi sana, ambao kwa kiasi kikubwa, wamekuwa wakichangia uingizwaji wa silaha haramu. Naipongeza Wizara kwa jitihada zake za kuwadhibiti wakimbizi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahabusu na magereza yetu, hayaridhishi pamoja na kwamba, mahabusu hawapaswi kukaa *cell* kwa zaidi ya saa 24, lakini kutokana na ukosefu wa watendaji, wamekuwa wakichukua muda mrefu sana mahabusu.

Magereza yetu nayo hayafai, mtaalamu mmoja wa masuala ya jamii *(sociologist),* alisema kipimo cha kujua ustaarabu wa nchi yoyote ni magereza yake. Magereza yetu yamefurika wafungwa mfano, gereza la watu 70 linakuwa na watu zaidi ya 300. Huu ni uvunjaji wa haki za binadamu. Bado tuna kumbukumbu ya mahabusu waliofia katika *cell* ya kule Mbeya, mpaka leo hatujaelezwa hatua zilizochukuliwa dhidi ya wahusika. Huu ulikuwa ni uzembe wa hali ya juu, kwani wahusika waliamini ili mradi chumba kipo, basi lazima nafasi ipo bila kujali athari zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *passport*, limejadiliwa kwa kirefu kuwa ni haki ya kila mwananchi, mwenye umri wa miaka 18 na zaidi. Kwa mfano, kutokana na kutokuwa na *passport*, wasafiri wengi wamekuwa wakikwama kusafiri, kwani mara nyingine safari huwa ni za kushtukiza. Hali ya uharaka wa kupata *passport,* imefanya wasafiri wataabike sana na mara nyingi kutoa mlungula (rushwa), ili afanikiwe. Katika suala la *passport*, inashangaza sana kuona hata Wabunge wametakiwa kulipa tena kwa ajili ya *diplomatic passports* wakati zile za awali zilikuwa bado mpya. Ni kwa nini Wizara, isingewapa Waheshimiwa Wabunge waliokuwa na *passport* mpya, *non-diplomatic passport* ya bure?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Kitengo cha Zimamoto kutokuwa na *facilities* ni nyeti na linahitaji liangaliwe kwa jicho la huruma. Inasikitisha kuona magari haya yakifika sehemu ya tukio, yanakuwa hayana maji hivyo, kufanya moto uzidi kuteketeza mali za watu. Lakini pia inasikitisha zaidi, kuona wananchi wanaathirika wakitozwa fedha kwa ajili ya kuzimiwa moto wakati hii ni mali ya Serikali na wananchi wanalipa kodi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nashauri kuwa wafungwa walioko magerezani, wasitiriwe kimavazi na maeneo wanayoishi yawe safi. Lakini pia watoto wa chini ya miaka 18, watengewe sehemu zao ili kupunguza tatizo la ukahaba. Pia kina mama wapewe *special attention* na *care* ili wasipate mimba zisizotarajiwa kama ambavyo imekuwa ikitokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni budi nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu wa Wizara na wataalamu wote, kwa kuandaa hotuba nzuri, yenye mwelekeo. Mimi binafsi, naunga mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namwelewa vizuri Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, utendaji wake wakati alipokuwa Naibu Waziri, hakuwa na maringo wala makeke. Anawasikiliza Wabunge pale wanapokuwa na matatizo yao na kuyatatua kwa mfano, mimi binafsi nilipomwendea kuhusu tatizo la Ofisi ya Uhamiaji Mkoa Kusini Unguja alinipokea na kunisikiliza, hatimaye ofisi hio ikajengwa mororo kabisa na hivi sasa imeshafunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ofisi nzuri ipo tayari hapo Tunguu, sasa nawaombea wafanyakazi wake, angalau wachache, wapatiwe nafasi za masomo ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, kama desturi yake asiniangushe, linalowezekana litekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti ningependa kutoa mchango wangu juu ya watoto wanaowekwa mahabusu, kuchanganywa na watu na watu wazima. Ningeomba Wizara ifuatilie kwa ukaribu swala hili, kwani watoto hawatendewi haki wanapochanganywa na watu wazima. Pia msongamano wa wafungwa gerezani unakuwa ni mkubwa sana, hivyo kusababisha wafungwa hawa kuishi kwa shida sana gerezani. Naiomba Serikali au nashauri kuwa, wale wafungwa wa miezi sita au mwaka, wawekwe kifungo cha nje ili kupunguza msongamano kama inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti kumekuwepo na kutojali wagonjwa ndani ya magereza wanapokuwa wanaumwa, mpaka hapo anapozidiwa mfungwa ndipo wanaanza kumuhudumia. Naomba Wizara ifuatilie suala hili kwa ukaribu ili kuhakikisha wanapata huduma kwa wakati, kwani nao wanayo haki ya kupata matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba ya Waziri, yenye matumaini kuwa watajenga Gereza Meatu, bado naweka msisitizo kuwa, suala hilo lipewe kipaumbele kwani Gereza la Maswa linakuwa na msongamano mkubwa wakiwemo mahabusu na wafungwa toka Meatu.

Mhesimiwa Mwenyekiti, tabia ya kuwepeleka maahusu wa kiume wakiwa wamevua mashati ni kitendo cha kuwadhalilisha hivyo, naomba Wizara iangalie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Kwenye Jimbo la Songwe lipo Gereza la Ngwala, liko umbali wa km. 206 hadi Makao Makuu ya Wilaya – Chunya. Pia liko umbali wa km. 235 hadi Makao Makuu ya Mkoa – Mbeya. Gereza hilo lina magari aina ya *Canter* na *Landrover,* ambayo yote hivi

sasa ni mabovu. Naishauri Serikali itoe gari hasa aina ya Lori kati ya magari 82, ambayo Wizara itayanunua katika kipindi hiki cha fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ndiyo shughuli inayofanyika katika Gereza hilo la Ngwala. Miaka ya 1980 - 1990 gereza hili lilikuwa linalisha Gereeza kuu la Mkoa Mbeya na Wilaya ya Chunya kwa ujumla. Pia Gereza lilikuwa linajitosheleza kwa chakula, hivi sasa linapelekewa chakula na Wizara, sababu ni kutokuwa na vitendea kazi. Nashauri wilaya itoe trekta moja, kwa ajili ya kuendeleza kilimo endelevu

Miaka mitatu iliyopita, Gereza la Ngwala lilianzisha kilimo cha Kahawa kwa majaribio. Zao hili limestawi vizuri sana na linaendelea vizuri. Nashauri Wizara iliwezeshe Gereza la Ngwala ili waendeze kilimo hicho kwa manufaa ya gereza na taifa kwa ujumla.

Kwenye Mji Mdogo wa Mkwajuni katika jimbo la Songwe, ipo Kambi kwa ajili ya kuwahifadhi wafungwa wagonjwa, ambao hupelekwa huko kwa ajili ya matibabu kwenye Hospitali ya Mwambani. Kambi hiyo haina jengo la kuwahifadhi wafungwa hao, wamejengewa kibanda ambacho hata ukakisukuma kinaporomoka. Jengo lililokuwepo liliezuliwa mwezi Desemba, 2005, hadi sasa halijaezekwa.

Naishauri Wizara, ijenge jengo imara la kuwahifadhi wafungwa. Pia naiomba Wizara itoe gari aina ya *Canter* kwa ajili ya matumizi ya Kambi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakupongeza wewe na Wizara yako kwa ujumla, kwa kazi nzuri katika mazingira magumu. Wizara hii ina matatizo mengi kama ulivyobainisha katika hotuba yako, lakini chimbuko la matatizo hayo ni matokeo ya kuahirisha matatizo kwa muda mrefu. Si kosa la Wizara, ni la Serikali kwa ujumla na kwa maana hiyo, hayawezi kutatuliwa katika muda mfupi. Tunaomba Serikali ilione hilo na *progessively* itafute ufumbuzi.

Pili, katika jimbo langu tatizo kubwa ni utaratibu mbaya ambao siyo wa kisheria wa kuweka washukiwa uhalifu katika maeneo (kawaida ni makao ya kata), yaliyo mbali na sehemu za uhalifu. Kwa kuwa hakuna utaratibu wa chakula kwa mahabusu hao, washtakiwa hulazimika kuleta chakula au fedha ya kuwalisha mahabusu wakati wakingoja hakimu ambaye mara zote hakai pale, huja tu baada ya muda mrefu. Mara nyingi washtakiwa hukata tamaa na kufuta mashtaka yao au kuyatelekeza. Haki hupotea. Nashauri kuwa suala hilo zima litazamwe kwa lengo la kulitafutia ufumbuzi.

Tatu, naunga mkono hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Naomba Mheshimiwa Mwenyekiti, unifikishie salamu za shukrani kwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Viongozi wa Magereza, hususan Kamishna wa Magereza, aliyesaidia sana ukoo wangu kumzika Hayati Francis Galinoma, alipoaga dunia mwezi Januari, 2006. Japokuwa

alikuwa amestaafu, baada ya kutumikia Magereza kama *Assistant Commissioner of Prisons* kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nawatakia kila la kheri.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini nina yafuatayo:-

Kwanza, ujenzi wa Gereza jipya la Igunga, unakwenda polepole na kufanya mrundikano wa wafungwa na mahabusu kwenye Gereza dogo la Nzega. Kwa ushauri, naomba mahabusu wa Igunga wapelekwe Gereza la Uyui.

Pili, kwa kuwa mahabusu ni sehemu ya Jeshi la Polisi na Mahakama, kwa nini Serikali isijenge mabweni ya mahabusu hukohuko Polisi na Mahakamani?

Tatu, naomba malalamiko ya malipo ya Mzabuni wa Gereza la Nzega yatafutwe ufumbuzi wa kudumu.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa John Z. Chiligati, Waziri wa Mambo ya Ndani na Mheshimiwa Bernard K. Membe, Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu, Ndugu Solomon Odunga, kwa hotuba nzuri, yenye mwelekeo wa shughuli zao katika Wizara hii iliyoundwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nataka kuelekeza maoni yangu katika mgogoro wa siku nyingi katika Jimbo langu la Masasi, kati ya Gereza la Namajani na Kijiji cha Ngalole katika Kata hiyo ya Namajani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya 90, wananchi wa Namajani walitoa ardhi kwa Magereza ili waanzishe Gereza la Kilimo, walioneshwa mipaka ambapo baadaye palipimwa. Kadri miaka ilivyopita, Magereza walijitanua na kuingilia zaidi katika Kijiji cha Ngalole. Huu ni mfano wa Mwarabu na ngamia jangawani, wakati alipomkarimu ngamia katika hema lake na hatimaye kumtimua kabisa. Magereza imetumia ubabe kuchukua ardhi zaidi toka kwa wananchi wa Namajani, ambao ndio waliwakaribisha hapo mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumezuka mgogoro mkubwa baina ya watumishi na wananchi, kiasi kwamba, mwaka 2003 kulikuwa na *confrontation* iliyopelekea Magereza kutumia nguvu na kuwapeleka wanakijiji 87 Mahakamani, ambako walitozwa faini ya Sh.425,000 ama kifungo. Faini ililipwa na wananchi hao kuachiwa. Toka wakati huo mpaka leo, hakuna utulivu na kuna matukio mengi tu ya uvunjaji wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati, Wizara ya Mambo ya Ndani, inafahamu sana juu ya mgogoro huu, lakini ufumbuzi wa kudumu mpaka sasa haujapatikana. Kwa kuwa suala lenyewe linamhusu Mkuu wa Gereza la Namajani, pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Masasi, ambao wamelichochea tatizo hili kutokana na maslahi yao binafsi, namwomba Waziri, pamaja na Serikali, kutatua matatizo yaliyojitokeza ya mpaka baina

ya Magereza na Kijiji cha Ngalole. Wizara ikubali kurudi katika mipaka ya awali ili kuruhusu upanuzi wa kawaida wa Kijiji cha Ngalole, ambacho kina wakazi wengi sana. Ili kuwepo na ushirikiano mzuri uliokuwepo hapo awali, Magereza imwondoe Mkuu wa Gereza la Namajani, ambaye amechangia sana kuwepo na uhusiano mbaya kati ya Gereza na wanakijiji wa Namajani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri aunde Tume ya kuchunguza mgogoro huu au akubali mpaka wa awali utumike na kuwakataza magereza waache kujitanua kwa mabavu katika maeneo ambayo sio yao. Zaidi ya hapo, wananchi wanalalamika kuwa, wao wananyang'anywa ardhi ambapo Maafisa Magereza wote wa pale Wilayani na Mkoani Mtwara, wanakuja kulima mashamba makubwa, ambapo wananchi hawaruhusiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala hili ni la kiutawala zaidi, namwomba Waziri wa Mambo ya Ndani, alitolee kauli ili wanakijiji watulie na kuendesha shughuli za maendeleo bila bughudha ya Dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja lakini naomba maelezo ya kuridhisha kutokana na mgogoro huo kati ya Gereza la Namajani na wananchi wa Ngalole katika Wilaya ya Masasi.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyenzi Mungu, kwa kunipa uzima na uwezo wa kuchangia walau kidogo, kuhusiana na Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msongamano wa wafungwa katika magereza yetu nchini ni wa kutisha sana. Suala hili linaonekana kuwa sugu sana, maana kila mwaka Serikali husema kwamba, italishughulikia suala hili, lakini bado tatizo lipo pale pale. Pamoja na wafungwa, mahabusu nao wanachangia kuleta msongamano ndani ya magereza. Kesi zinazowakabili mahabusu hazisikilizwi kwa muda mrefu, hivyo husababisha kuongezeka kwa msongamano magerezani. Ni vyema sana Serikali ichukue juhudi ya makusudi ili kuondokana na msongamano magerezani. Hivyo, tunashauri kuwa, Wizara ishirikiane na vyombo husika ili kuhakikisha kwamba, kesi zinazowakabili mahabusu waliopo magerezani, zinasikilizwa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wakimbizi nchini limekuwa likilalamikiwa sana na wananchi wengi hapa nchini, hasa wale wanaoishi mipakani mwa nchi yetu na hasa hasa Mikoa ya Kagera na Kigoma. Wakimbizi kutoka nchi jirani kama vile Burundi, wamekuwa wanalalamikiwa sana kwamba, wanahatarisha usalama wa raia na mali zao. Kwa hiyo, tunaishauri Serikali, pamoja na juhudi nyingine, ipange mikakati maalum ya kuwadhibiti wakimbizi ili wasisambae ovyo mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhitimisha mchango wangu kwa kutoa angalizo maalum kama ifuatavyo: Ili kuondokana na msaongamano, lazima Serikali iongeze kasi ya ujenzi wa magereza nchini; iwekwe mikakati maalum ya kuwateganisha

mahabusu na wafungwa; na Serikali itafute njia ambayo itaweza kupunguza mahabusu katika magereza yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kama suala la kulegeza masharti ya dhamana kwa mahabusu litatiliwa maanani, tutapunguza kwa kiasi fulani msongamano ndani ya magereza yetu

**MHE. DR. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Morogoro ni miongoni mwa Mikoa yenye magereza mengi sana, lakini pia kuna wafungwa wengi mno, hasa mahabusu na wafungwa wenye vifungo vidovidogo visivyozidi miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielezee zaidi magereza yaliyoko katika Wilaya ya Morogoro na hasa Jimbo langu la Morogoro mjini. Manispaa ya Morogoro inayo Gereza la Mahabusu na Gereza la Kihonda. Magereza haya yanatoa huduma kwa wakazi wanaokadiriwa laki tatu, ukiondoa idadi hii ya wakazi wa Morogoro Manispaa. Pia kuna mkusanyiko mkubwa mno wa watu wengine kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania, hasa ukizingatia kuwa Morogoro ni njia panda karibu robo tatu ya Mikoa yote ya Tanzania. Hivyo, kunakuwa na mchanganyiko wa Tabia na ndio maana kunakuwa na kesi nyingi zaidi. Hata hivyo, yapo Magereza mengine, ambayo yanategemea sana huduma zote muhimu kutoka Manispaa hii ya Morogoro, kama Gereza la Mkono wa Mara na Gereza la Mtego wa Simba, yaliyoko Morogoro Vijijini; Gereza la Mbuguni; Gereza la Wami Mkuu na Gereza la Wami Vijana, yaliyoko Mvomero na Gereza la Ubena Bwawani, lililoko Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani katika hotuba yake ukurasa wa 36 kuhusu huduma za jamii *(Community Services),* ambayo malengo yake ni kuwezesha wafungwa wenye makosa madogo madogo na wanaofungwa kifungo kisichozidi miaka mitatu, kutumikia adhabu zao katika jamii, wakifanya kazi za jamii bila malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Mtwara na Kilimanjaro tu. Swali langu ni kuwa ni vigezo gani vilivyotumika katika kuihusisha Mikoa iliyotajwa hapo juu peke yake?

Kwa nini Mkoa wa Morogoro haupo katika mpango huu, hasa ukizingatia kwamba, Morogoro ni miongoni mwa mikoa yenye msongamano mkubwa sana, lakini pamoja na tatizo hilo, bado Morogoro ipo karibu na Dar es Salaam lakini ikaachwa katika mpango huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nahitaji maelezo ya kina zaidi au vinginevyo Mkoa wa Morogoro uingizwe katika mpango huu kabla ya kuunga mkono hoja. Nitaunga mkono hoja endapo tu nitapata maelezo ya kutosha na ya kufaa kwa niaba ya wananchi wa Morogoro.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kitendo chake cha busara cha kutembelea baadhi ya Magereza hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa ujumla, kwa kuandaa Hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, sasa naomba kuchangia hoja iliyoko mbele yetu kama ifuatavyo: Mkakati wa namna ya kuipunguzia mzigo Serikali kulisha wafungwa katika Magereza hapa nchini, kwa kuwa nchi yetu inayo Magereza makubwa 12 yenye mchepuo wa Kilimo ambayo ni Gereza la Mollo (Sumbawanga); Gereza la Kitengule (Kagera); Gereza la Kiberege (Kilombero); Gereza la Kitai (Mbinga); Gereza la Mang'ola (Karatu); Gereza la Mbigiri (Morogoro); Gereza Isupilo (Iringa); Gereza Idete (Kilombero); Gereza la Mkwaya (Mbinga); Gereza la Songwe (Mbeya); Gereza Ludewa (Iringa); na Gereza la Bagamoyo (Pwani). Naishauri Serikali kupitia Idara ya Magereza, ijikite katika kuimarisha Kilimo katika magereza hayo, kwa kuwatumia wafungwa hao, kwani kwa kufanya hivyo, kutaipunguzia Serikali mzigo wa kuwalisha wafungwa hao, lakini pia itakuwa ndio njia ya kuwapatia elimu wafungwa hao ili baada ya kumaliza kutumikia kifungo chao, waitumie Elimu hiyo kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Takwimu ni kwamba jumla ya wafungwa na mahabusu katika magereza yote hapa nchini ni 45,000. Hivyo, wafungwa 45,000 kwa mwaka watakula kilogramu 12,150,000 ambazo ni sawa magunia 121,500. Iwapo Serikali itanunua unga (sembe) kwa bei ya shilingi 60,000 kwa gunia la kilo 100, kwa hiyo magunia 121,500 x 100 itagharim shilingi 7,290,000,000, ambayo ni sawa na asilimia 80 ya fedha zilizotengwa na Serikali, kwa ajili ya chakula cha wafungwa kwa mwaka.

Kutokana Serikali kutumia asilimia 80 kwa kununua unga, umefika wakati muafaka, magereza yote yenye mchepuo wa kilimo, yaweke mpango kabambe wa kulima mahindi na maharage kwa lengo la kujitegemea. Kila Gereza lilime eka 600, liwe na Wataalam wa kutosha wa Kilimo na Maofisa Magereza, wawe wabunifu katika kuipunguzia mzigo Serikali na kadhalika. Kwa kufanya hivyo, ziada ya fedha itasaidia kuboresha miundombinu katika magereza na kadhalika. Naomba ufafanuzi zaidi katika suala la magereza kujitegemea kwa kulima chakula chao wafungwa kwa nchi nzima (Mpango Mkakati).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nachukua nafasi hii kumpongeza MheshimiwaWaziri, kwa kukabidhiwa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu ni kuwa kwa sababu katika kipindi kirefu, Magereza Bara na Chuo cha Mafunzo Zanzibar, wamekuwa wakishirikiana kwa karibu sana na kwa sababu kazi zao zinalingana, wakati sasa umefika wa kuviunganisha vyombo hivi na kuwa ni vya Muungano katika utaratibu maalum wa kiutendaji. Hii

itasaidia sana kutoa uzoefu kwa askari na pia kujifunza mbinu na tabia za wahalifu mbalimbali, ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini pia utaratibu huo utatoa nafasi ya wahalifu sugu kudhibitiwa ndani ya magereza yetu inapotokea haja ya kuhamishwa kutoka upande mmoja wa Jamhuri. Vile vile utaratibu huo utatoa nafasi kwa askari wa vyombo hivi, kujifunza mbinu na taratibu za kazi, pale watakapopewa nafasi za muda mfupi na mrefu za mafunzo ndani ya magereza yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ni jambo la kusikitisha, kuona hali ya huduma za wafungwa na mahabusu zilivyo ndani ya magereza yetu. Wizara imesema kuwa imenunua magodoro kwa ajili ya kulalia wafungwa, lakini inaonekana magodoro hayo hayakuwafikia walengwa au yalikuwa kidogo, kwani hadi sasa bado wafungwa wanalalia majamvi yasiyoridhisha. Bado Wizara inatakiwa ichukue hatua madhubuti ya kuhakikisha kuwa, eneo la magereza sio eneo la kuzaliwa UKIMWI, kwani vitendo vya kujamiiana ndani ya magereza yetu vimepamba kasi na vinahatarisha maisha ya wafungwa na hatimaye kueneza ugonjwa huo wanapomaliza adhabu yao. Lazima kuwe na mkakati maalum wa ama kuwahasi wale wafungwa wanaojidai kuwa ni wababe kwenye magereza au adhabu za vitendo hivi ziongezwe marudufu ili wafungwa wapya wasiiingie kwenye mtego wa maisha ya magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kuwapongeza Wajumbe wa Kamati hii, kwa kufanya uchambuzi wa kina na kubaini matatizo yaliyopo ndani ya majeshi yetu, hasa Jeshi la Magereza na kuyatolea maoni ili yaweze kupata baraka katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuungana na wajumbe hawa katika vipengele viwili:

Kwanza, Jeshi la Mageeza na ukaaji wa wageni haramu. Kwa kweli wakati umefika wa kutoa kipumbele katika Jeshi la Magereza, ukizingatia kazi nzito, kubwa, mazingira magumu waliyonayo katika utendaji wao wa kazi na maisha yao katika kazi. Ikumbukwe askari hawa wanawajibika kuwatunza watu, ambao wamevunja maadili na wakahukumiwa kifungo hivyo, wanawatunza wafungwa wenye tabia mbalimbali kama ujambazi, wizi, ubakaji, ulevi wa madawa ya kulevya na kadhalika. Hivyo, askari hawa wanakuwa na jukumu zito la kuwarekebisha wafungwa hawa ili warudi katika maadili ya kawaida. Askari hawa huwa wana kazi kubwa, kwani nao wanalazimika kuishi maisha ya jela, jua, mvua, kutembea kwa miguu, kufanya kazi usiku na mchana, wakilinda wafungwa hawa, lakini bado askari hawa wanaishi katika mazingira mabovu, mishahara midogo, marupurupu madogo, ambayo pia hupatikana na kwa shida kutokana na urasimu mkubwa uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nasisitiza suala la ujenzi wa nyumba bora za askari, maslahi bora, pamoja na kupewa vitendea kazi hasa usafiri, wilaya nyingi nchini zina gari moja tu la magereza aina ya kenta, ambayo hufanya kazi ya utawala za kila siku na mkuu wa Gereza kutumia pia kwa safari za kikazi. Gari ambalo halina hadhi kwa

Afisa wa Magereza, hivyo nashauri Wizara iboreshe zaidi suala usafiri kwa kuwapatia magari Maafisa hawa na pikipiki kwa askari wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandaji vyeo kwa askari wa Jeshi la Magereza pia umekuwa na matatizo, naomba Wizara iwe na mango maalum, ulioboreshwa na unaotekelezeka wa kuwapatia kozi mbalimbali ili waweze kukuza uwezo na kuwawezesha kupanda vyeo kama ilivyo kwenye Jeshi la Ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaaji wa wageni haramu katika nchi yetu ni tatizo kubwa katika nchi yetu na ni jambo linalotakiwa kupangiwa utaratibu mzuri, kwani uingiaji wa wageni katika nchi hii, imekuwa ni holela mno ikilinganishwa na nchi za jirani. Kwa kutokua na utaratibu, nchi inakumbwa na ujambazi, kuletewa mila potofu, magonjwa, kumiliki ardhi yetu na mambo mengi ambayo si maadili ya Taifa hili. Hivyo, mpango maalum ya kuwasaka na kuzia uingiaji holela, udhibitiwe ili matatizo yanayojitokeza katika tatizo hili yaweze kumalizika .

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yangu matatizo haya yatafanyiwa kazi ili kuleta ufanisi katika Jeshi hili la Magereza.

Mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara kadhaa nimelifuatilia suala la *Dual Citizenship* ndani ya Bunge, Serikali imewahi kutoa ahadi kuwa, inakusanya maoni ya Watanzania kupitia *Law Reform Commission.* Hata *Website* kwa lengo hilo ilianzishwa na baadaye kufungwa bila maelezo yoyote. Mwaka 2004, Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, katika *interview* ya *TV*, akiwa Marekani alikaririwa akitoa ahadi kushguhulikia suala hilo kabla ya kumaliza kipindi chake. Kwa hatua ya awali, aliahidi kuanza na utaratibu unaotumika Ethiopia. Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani aliyepita pia alikiri ndani ya Bunge kuwa, utaratibu wa sasa ni wa kibaguzi kwa wanawake, licha ya sababu za kiuchumi.

Sasa naomba maelezo ya kina, utaratibu wa kuanzisha *Dual Citizenship* umefikia hatua gani, ili nchi yetu isiendelee kukosa manufaa ya *Dual Citizenship.* Iwapo bado, ni sababu gani za msingi, zinazochelewesha uanzishaji wa jambo hili? Ni kwa nini Serikali inapata kigugumizi hata baada ya Ahadi ya Rais wa Awamu ya Tatu. kwa Watanzania walioko Marekani na Canada? Ni lini Serikali italeta Bungeni marekebisho ya Sheria zinazowabagua wanawake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni muda mrefu tangu suala la vitambulisho vya Taifa lianze kujadiliwa na hata fedha nyingi kutengwa. Nataka Serikali ilieleze Bunge hili ni kitu gani kimecheleweshwa utekelezaji wa jambo hili? Pia kama uchambuzi umemalizika, je, *tenderer* aliyeshinda *(contractor)* ni nani na anatoka kampuni gani na nchi gani?

Iwapo *tender* imeshatolewa, bila shaka siyo siri tena, kazi hiyo sasa itagharimu kiasi gani na itachukua muda gain, kutengeneza vitambulisho? Nadhani Serikali ituambie wazi kama mtengenezaji ndiye pia atakayetoa au vitatolewa na Idara ya Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania sasa wana haki ya kupewa taarifa kamili kuhusu jambo hili. Ni vema pia Bunge likaarifiwa maandalizi haya yamegharimu kiasi gani hadi sasa. Nategemea kushika shilingi iwapo sitapata majibu ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani za dhati

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inagalie jinsi Ubalozi wa Uingereza unavyo wanyanyasa Watanzania wanaokwenda kuomba *visa.* Hivi sasa Watanzania inawalazimu kulala nje ya jengo lao, eti kwa kuwahi nafasi yaku-*present* maombi yao. Serikali iongee nao. Nchi nyingine wanatoa *appointments* kwa njia ya kutoa Namba na Tarehe zake, hawa Waingereza wanafanya dharau, hawataki *appointments* ila mistari tu. Huu si ustaarabu.

Tuangalie suala la Tanzania kuwa na *Dual Citizenship*, wapo Watanzania wengi wanofanya kazi nje ya nchi, wanalazimika kukosa haki mbalimbali za kujiendeleza katika nchi hizo, kwani wanataka kuendelea na uraia wao. Jambo hili sasa wakati umefika, hii *globalization* imefanya jamii mbalimbali kwenda nchi mbalimbali kufanya kazi. Ni vyema, wananchi wa Kitanzania nao wanufaike na huo utandawazi kwa kuwa na *Dual Citizenship.*

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliowasilishwa Bungeni au Hotuba Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na hotuba na Taarifa Kamati ya Ulinzi na Usalama, wote nawapongeza kwa kuwasilisha mapema na ufafanuzi mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza lina jukumu kubwa ya kuhifadhi wahalifu wa aina zote, pamoja na kurekebisha tabia za wafungwa ili wamalizapo vifungo vyao, wawe raia wema. Kwa hiyo, naiomba Serikali iiwezeshe vizuri Wizara ili iweze kusimamia vyema na Jeshi hili liwe la kileo, kwa uwezo vifaa, usafiri, mashamba, chakula, afya, mafunzo mazuri na hali zote.

Uhamiaji ni Jeshi la Ulinzi na lenye kupewa majukumu ya kuhamia na kuhama, kwa kusafirisha, kuingiza na kuwatoa ndani na nje ya nchi. Kwa nchi yetu Idara ya Uhamiaji ni muhimu. Naiomba Serikali, iajiri vijana wengi ili kukidhi haja na wapewe elimu na nyenzo zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zimamoto ni Jeshi letu lenye kazi nzuri na jukumu kubwa, tunawashukuru sana na wazidi kuendelea na majukumu yao. Serikali kwa sasa

iwe tayari kuipa fedha Wizara, ili Zimamoto waweze kutekeleza majukumu yao na wawe na uwezo wa kuhimili hali ya hatari ikitokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Wakimbizi, nao wapewe uwezo wa kusimamia vizuri na kupunguza au kumaliza, wakimbizi waingiao kiholela ili nchi ikae kwa amani, utulivu na umoja, kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Idara ya Uhamiaji, iwe inajitegemea kwa sababu ni Idara nyeti, inayohusiana na inashabihiana na Magereza na Zimamoto, bora iondolewe Utumishi iwe inajitegemea.

Napenda kupata maelezo yakinifu, kuhusu watumishi watano wanaofanya kazi Idara ya Uhamiaji Zanzibar, ambao walikuwa na vyeo, baada ya kuja Sheria wameondolewa kwenye vyeo vile na kuteremshwa. Wakaelezwa wawe na sifa, wamejiendeleza na kuwa na sifa; hadi leo kwa nini hawajarejeshewa vyeo hivyo? Naomba maelezo yakinifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata maelezo yakinifu kwa nini watumishi wa Uhamiaji wakati wanahamishwa, hawapatiwi haki zao za usafiri, yaani fedha za usafiri. Mfano hai ni wa Ndugu Thatib Kombo, amehamishwa kutoka Pemba kwenda Makao Makuu ya Uhamiaji Zanzibar, hadi hivi sasa marejesheo ya fedha za usafiri hajarejeshewa na si peke yake, wapo na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Naibu Waziri, Mheshimiwa Bernard K. Membe, pamoja na Wwatendaji wote wa Wizara hii, kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia katika sehemu tofauti, nitaanza na Idara ya Uhamiaji. Idara hii inatakiwa kuimarishwa katika ngazi za Wilaya mpaka kufungua ofisi katika ngazi za Kata. Hii itasaidia Wizara kupambana na wahamiaji haramu, ambao muda mwingine wanaweza kuwa ni majambazi, wanaoingia katika nchi yetu kwa njia zisizokuwa za halali. Nashauri Wizara iendeshe esmina au kutoa elimu, kwa wananchi na Viongozi wa Serikali za Vijiji, kuhusu kutambua wahamiaji haramu, pia waimarishe ujirani mwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu wageni wanapoingia nchini, kwa kupitia *airpot* au mipakani. Kuna zile karatasi za *arrival*, nyuma yake katika vielelezo vya sababu ya kuingia nchini, kuna kile kinachosema *seeking employment*; hivi hiki kipengele ni cha nini wakati kuna mtu anakuja kufanya kazi, atakuwa tayari ameshapata *visa* ya kazi kutoka huko huko kwenye Balozi zetu?

Ushauri wangu, wageni waingiapo nchini, kama wamekuja kwa ajili ya utalii lazima *passport* zao zigongwe muhuri, hawaruhusiwi kufanya kazi. Pia Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Kazi, wakati wanapo-*extend visa,* waangalie ni kwa nini wana-*renew visa* zao, wageni wejue. Unakuta wanafanya kazi halafu wanalipa Dola za Kimarekani 50 tu. Hii itasaidia kulinda kazi zinazoweza kufanywa na wananchi wa Tanzania badala ya wageni. Naomba jibu kama hicho kipengele cha *seeking employment* kitafutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwa na msongamano kwenye Magereza/Mahabusu hapa nchini na hii inapelekea uwezekano wa wafungwa kupata magonjwa ya kuambukiza kama vile Kifua Kikuu; kwa nini Wizara isiwapime wafungwa kabla hawajaingia jela, wawe na kadi kama za *clinic* ili ijulikane kama mfungwa anaingia na ugonjwa atibiwe asichanganywe na wale wazima, pia kama mfungwa alitoka magereza na ugonjwa, ijulikane amepata jela au alikuja nao ili aweze kutibiwa ipasavyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jibu, Wizara ina mikakati gani kwa hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kila binadamu anastahili haki zake za msingi za kuishi, kwa kweli ni jambo la kusikitisha jinsi wafungwa wanavyosafirishwa wakiwa wamesimama kama ng'ombe kwenye lori na ilishakatazwa watu wasisafiri wakiwa wamesimama kwenye malori. Kwa nini yale malori ya magereza yasiwekewe viti? Hawa ni binadamu lazima wawe *handled* kama watu. Jukumu hili lichukuliwe na magereza wahakikishe wafungwa wanaketi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo ningependa kuchangia ni kuhusu vitambulisho vya uraia *(ID).* Kwa kuwa watu bado wanaongezeka kuzaliwa na watu wanazidi kuwa wengi, nafikiri Serikali ichukue uamuzi wa kuanza kutoa *ID* kwa watoto, ambao wanazaliwa wakati huu. Hii itawasaidia kuweka *record* mfano, kuanzia Januari, 2007 watoe *ID* kwa watoto wote waliozaliwa. Kwa hiyo, Serikali inabaki kutoa vitambulisho kwa waliobaki. Naomba Serikali itujibu ni lini vitambulisho vya uraia vitaanza sababu mpaka sasa hivi umekuwa ni wimbo, lazima Serikali ina mikakati wamepanga wataanza lini?

Kuhusu Kiwanda cha Viatu cha Magereza Moshi, kwanza napenda kuwapongeza kwa *quality* nzuri ya viatu vya ngozi vinavyotengenezwa. Watengeneze *stock* ya kutosha kwa sababu walipeleka viatu vyao kwenye Maonesho ya Saba Saba, lakini hawakuwa na *stock* ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu, naomba kuwasilisha.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kwanza kabisa, kumshukuru Waziri na Naibu Waziri, kwa kufanya kazi nzuri sana katika Wizara hii. Ubora wa kazi yao, unadhihirishwa na bajeti nzuri ya mwaka 2006/2007. Nimesoma bajati ni nzuri. Aidha, nawapongeza pia Watendaji wote wa Wizara na Maofisa wote, kwa kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri na bajeti nzuri, ningependa kuchangia katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna msongamano mkubwa sana katika magereza yetu hapa nchini, ambao unachanganya wafungwa bila kujali umri kuanzia miaka 18 na kuendelea. Hali hii si kwamba inadharirisha utu wa mtu, lakini pia inakiuka msingi ya haki za binadamu. Naishauri Serikali kupitia Wizara hii, iwatenge wafungwa kwa kuzingatia umri wao, pia hata majukumu yao ndani ya magereza yazingatie umri wao. Pili, katika jitihada za kupunguza msongamano magerezani, Bodi ya *Parole*, ambayo ipo kwa mujibu wa Sheria, iendelee na jitihada za kuwaondoa magerezani, wafungwa ambao wanaonesha tabia njema na wenye makosa madogo madogo wasamehewe.

Tatu, nashauri pia yaanzishwe magereza maalum ya wafungwa wanawake na askari watakaohusika wawe pia wanawake. Hii itaepusha wanawake wafungwa kupewa mimba na kupata watoto wasio na baba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za kuishi askari magereza ni chache sana na hazikidhi haja kwa maaskari wote. Pamoja na uchache wa nyumba hizo, lakini pia nyingi ziko katika hali mbaya sana, hii inaonesha kwamba, hakuna ukarabati wa kutosha wa nyumba hizo. Mimi nimebahatika kutembelea Gereza la Ukonga mara kadhaa, kwa kweli hali ya nyumba za kuishi askari ni mbaya, kwa maana zote, yaani ni ndogo na chakavu. Leo wakati tupo Karne ya 21, inashangaza kuona askari wetu wanaishi kwenye nyumba zilizojengwa kwa bati, kuanzia chini hadi juu maarufu kama *full suit!* Nashauri Wizara iendelee na juhudi za kurekebisha hali hii, ili tuboreshe makazi ya askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Serikali ione umuhimu wa Idara hii, kwani ni muhimu sana katika kudhibiti uhamiaji holela na watu kutoka nchi nyingine, hasa ukizingatia kwamba, Tanzania ndiyo nchi pekee yenye amani na utulivu katika ukanda wa Maziwa Makuu. Hivi karibuni kumekuwa na wimbi la wahamiaji haramu kutoka Somalia, Ethiopia, Sudani, Rwanda, Burundi, *DRC* na kadhalika, ambao wengi wao wamekuwa wanakamatwa nchini, wakiwa hawana nyaraka za kusafiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inatia wasiwasi na inaacha maswali mengi juu ya utendaji kazi wa Idara hii, hasa ukizingatia kwamba, wengi wa watu hawa hukamatwa ndani ya nchi kama vile Singida, Dar es Salaam, Iringa Mbeya na kadhalika. Usalama wa mipaka yetu inaonesha kuwa hauko salama sana. Nashauri Wizara na Serikali kwa ujumla, iongeze mikakati ya kukabiliana na hali hii, kwa kuwa na udhibiti wa njia zisizo rasmi. Lakini pia Maafisa wanaoweza kupitisha watu hao kwa kupewa rushwa, waangaliwe mienendo yao mipakani na wasikae muda mrefu mipakani ili kuondoa hali ya mazoea ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuishukuru Serikali kwa kuwa na mpango wa kutoa vitambulisho vya uraia kwa Watanzania wote. Hata hivyo, napenda kuishauri Wizara kwamba, muda wa kuanza kutoa vitambulisho hivyo kwa wananchi wetu wanaoishi mipakani, isipokuwa makini inaweza kukuta inawapa vitambulisho vya uraia, watu wasiokuwa Watanzania na baadhi ya Watanzania kuvikosa. Hapa suala ni

uangalifu na uaminifu, kwa Maafisa watakaohusika katika zoezi hilo. Pili, Watanzania wanaoishi pembezoni ya nchi ni vizuri pia wakapewa umuhimu wa kupewa vitambulisho vya uraia, kwani hawa ndiyo wamekuwa wakisahauliwa katika mambo mengi sana. Ni vizuri pia Wizara ikajiandaa vizuri ili maeneo yote ya nchi yaweze kufikiwa kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Serikali yetu inakabiliwa na tatizo kubwa la vifaa vya zimamoto, hasa magari ya zimamoto. Pia magari yaliyopo mengi ni ya zamani na kwa msingi huo, yana teknolojia ya zamani sana hivyo, hayafanyi kazi kwa ufanisi unaotegemewa. Zaidi ya hayo, askari wengi wa zimamoto waliopo, wamekuwa watu wazima sana, wengi wanakaribia kustaafu. Hali hii ilionekana pale Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Miundombinu, ilipotembelea Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na kutembelea Kikosi cha Zimamoto. Nashauri Serikali kupitia Wizara hii, iendelee kuiimarisha Idara hii muhimu, ikiwa ni pamoja na kununua magari mapya ya kisasa na kuajiri askari wenye elimu nzuri zaidi.

Mwisho, naomba vikosi vya Zimamoto, viwahi kufika kwenye matukio. Kwa sasa zimamoto mara nyingi huchelewa sana kufika kwenye matukio ya moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, kwa hatuba aliyoiwasilisha Bungeni. Ni hotuba nzuri, inayotoa ufafanuzi juu ya masuala na majukumu ya Wizara yake. Nampongeza pia Naibu Waziri na wote waliomsaidia kuiandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ameeleza mengi kuhusu wakimbizi ukurasa wa 32 mpaka wa 36. Kama alivyoeleza, maeneo ambayo wakimbizi walifikia, yaliathirika sana kwa maana ya mazingira, vyanzo vya maji na kadhalika. Ambalo ni baya sana lakini halionekani na wala halisemwi ni namna wananchi wetu walivyoambukizwa tabia za ujambazi. Hii ni athari mbaya zaidi kuliko zote, kwa kuwa ni vigumu kuifanyia ukarabati tabia hiyo. Hivyo, Serikali izingatie ili katika mikutano ya Kimataifa, uwekwe utaratibu wa wakimbizi kubaki ndani ya nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaliwahi kujitokeza matukio kadhaa ya uchochezi wa Majeshi ya Burundi katika mipaka ya Burundi na Tanzania (Ngara) na raia kadhaa kuuawa, kwa madai kuwa, walikuwa wanafuatilia wakimbizi waliorudi kwao kufanya fujo.

Jambo hili lilizungumzwa katika hotuba mbalimbali na maswali hapa Bungeni na Serikali kuhojiwa juu ya fidia kwa hao waliokufa bila hatia, majibu ya Serikali yalikuwa ni kwamba, kwa wakati huo (1995 – 2000), isingewezekana kuidai fidia Serikali ya Burundi, kwa vile nchi hiyo ilikuwa haina amani. Sasa leo nchi hiyo ina amani, Serikali halali imeundwa na wakimbizi wanarejea kwao, Serikali inasemaje juu ya fidia kwa hao waliokufa bila hatia au Serikali imesahau? Naomba nipate majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENTIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi wanayoifanya kusaidia majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri mdogo kuhusiana na vitambulisho vinavyotarajia kutolewa. Ni kwamba, tusipokuwa waangalifu, tunaweza kuwapatia vitambulisho raia wa Kenya, kwa upande wa mpakani Sirari na Kigaja, Wilayani Tarime. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, makabila mawili ya Kikurya na Wajaluo, wanaoishi maeneo hayo, huwezi kuwatofautisha na wale walioko upande wa pili (Kenya). Kwa mfano, unakuta Mkurya wa Sirari ana udugu au anatoka ukoo mmoja na mwingine anayeishi Kenya na wanatembeleana kwa karibu, kiasi cha kutoweza kumhusianisha na upande wa pili.

Huu ndiyo wasiwasi wangu, maana lugha, majina mila na desturi, vyote ni sawa kwa Wajaluo wa Kenya na wa Tanzania. Nafikiri hii ni sawa hata kwa Wamasai wa Kenya na wale wa Tanzania. Ujue pia kuwa watu wetu hulindana, kwa hiyo, hata kiongozi wa kijiji, anaweza akasababisha mgeni akapewa kitambulisho, mradi ni ndugu yake, ili awe na uhuru wa kukitumia upande wa Tanzania. Hivyo, tuwe *very careful* kwa kujielimisha, kuhusu mahusiano haya ya jamaa hawa wa mpakani, hasa wanaoongea lugha moja na majina yanayofanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nawapongeza tena kwa yote, hasa utaratibu mzuri wa pasipoti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ya kutoa machache katika Wizara hii. Napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Waziri wa Wizara hii, pamoja na Naibu wake na Wataalam wote wa Wizara, kwa kuandaa bajeti hii na kuweza kusomwa ndani ya Bunge lako Tukufu. Kama ilivyokuwa kwenye bajeti zilizokwisha kusomwa ndani ya Bunge hili, zote ni nzuri, ikiwemo ya Wizara hii, ila tatizo huwa linajitokeza katika utekelezaji wa bajati hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujielekeza zaidi katika suala la msongamano katika magereza zetu, pamoja na sababu zilizotolewa na Kamati ya Bunge kuhusu suala hili. Bado kuna tatizo kwa Mahakimu wetu, ambao bado wanajihusisha na rushwa toka kwa watu ambao wana uwezo wa kifedha. Huwafungulia wenzao kesi na kwa kutumia uwezo wao wa kipesa huwaona Mahakimu hao na kuwapa rushwa ili waweke masharti magumu kwa mshtakiwa na wengi hushindwa kutimiza masharti hayo na wengi huishia magereza. Haya yote hufanya kwa kukomoana, hasa katika mambo binafsi. Napendekeza Wizara hii, pamoja na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, waone ni jinsi gani watafanya, kuokoa Watanzania wengi, ambao wanapata adhabu bila kufuata sheria. Wale mahakimu watakayogundulika kufanya hivyo, wachukuliwe hatua kali ili kukomesha kabisa mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magereza mengi yanatisha kutokana na uchakavu wa majengo, mengi yamejengwa wakati wa ukoloni na sasa yamechoka kabisa na yanaweza kubomoka wakati wowote. Naipongeza Wizara, imeonesha ujenzi wa magereza katika baadhi ya mikoa yetu, ila tunaomba ukarabati na ujenzi ufanyike haraka kabla ya madhara kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza Wizara, kwa kuwatoa wafungwa kwenye kaptura na kuwafikisha kwenye *suit.* Tunawapongeza sana ila huwezi kumvalisha mtu *suit* bila viatu, tunaomba hili litazamwe hili wafungwa wetu waweze kujikinga na maradhi na hata kuonekana nadhifu. Ufungwa wao, usiwanyime haki ya vitu muhimu wanavyohitaji katika maisha yao. Tuondoe tofauti zilizopo kati ya mnyapara, anayevaa viatu na yule mfungwa wa kawaida, ambaye hana cheo, naye ana haki ya kupata viatu hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magereza yetu mengi huduma ya chakula ni mbaya sana, hayatoi chakula bora, bali wanatoa chakula cha kujaza tumbo tu na hii husababisha wafungwa wengi kupata magonjwa mengi, kutokana na vyakula wanavyokula kutokuwa na virutubisho vinavyohitajika katika miili yao. Tunaomba Wizara, ilitazame hili ili kuokoa maisha ya ndugu zetu hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari Magereza hawana tofauti na wafungwa, kwa sababu muda mrefu huwa na wafungwa hao hivyo, wana kila sababu ya kuboreshewa maslahi yao ya mishahara na hata nyumba ambazo wanakaa, zitazamwe upya kwa sababu zimepitwa na wakati, zimechakzimechakaa, zina *rooms* mbili na nyingine moja. Ukizingatia askari hao wana familia, zenye watoto wakubwa ambao hawawezi kulala *room* moja na wazazi wao kutokana na mila zetu, hili nalo tunaomba litazamwe kwa hawa askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Ahsante.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jengo la Gereza la Biharamulo ni la zamani na dogo sana. Wakoloni walilijenga Gereza hilo kwa ajili ya wafungwa 64, sasa hivi kuna wafungwa zaidi ya mia mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za watumishi hazipo, kuna nyumba ya Mkuu wa gereza tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gereza letu halina gari hata moja, wafungwa hubeba kichwani kuni, maji na mazao. Baya zaidi, wafungwa wamekata miti yote ya Biharamulo na mji unaelekea kugeuka jangwa.

Vile vile hakuna jengo lolote kwa ajili ya Uhamiaji. Ofisi iliyopo ni chumba cha kupanga na watumishi wote wanapanga. Katika hotuba ya Waziri, hakuna kinachotajwa kuhusu maendeleo ya Wizara katika Wilaya yetu. Naomba maelezo kuhusu hayo mambo manne niliyoyaandika

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri na yenye ufafanuzi mzuri kuhusu Wizara.

Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, watumishi wa Idara ya Uhamiaji wafanya kazi nzuri, lakini wanakabiliwa na matatizo yafuatayo: Vitendea kazi ni vichache. Je Serikali ina mpango gani wa kuboresha vitendea kazi katika idara hiyo, hii itasaidia kuboresha utendaji wa kazi?

Je Serikali ina mpango gani kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na kuboresha maslahi yao?

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaendeleza watumishi wake kitaaluma hasa katika kipindi hiki cha Sayansi na Teknolojia?

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti wimbi la wahamiaji haramu hapa nchini na hasa wanaoingia/kupitia mipakani bila vibali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Jeshi la Zimamoto, linafanya kazi nzuri sana ya uokoaji yanapotokea majanga ya moto, lakini Jeshi hili linakabiliwa na upungufu mkubwa wa vifaa vya kisasa, yakiwemo magari ya kuzimia moto na vifaa vingine vya kuvaa, Serikali iboreshe vitendea kazi katika Jeshi hili na kuwapatia mafunzo ya kisasa. Serikali pia iboreshe maslahi ya watumishi wa Jeshi hili na kuangalia Muundo wa Utumishi *(Scheme of Service)* ya Jeshi hili ili ueleweke kama idara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Askari Magereza wanafanya kazi nzuri, lakini maslahi yao ni duni sana, Serikali iboreshe maslahi ya Askari Magereza na kuwapatia vitendea kazi vya kutosha ukiwemo usafiri, mawasiliano ya simu na matrekta kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mlundikano wa mahabusu magerezani, Wizara ya Mambo ya Ndani, ishirikiane na Wizara ya Usalama wa Raia ili kuhakikisha kwamba, kesi zinasikilizwa mapema na kutolewa hukumu. Hii itasaidia kupunguza mahabusu waliojaa magerezani na kesi zao huchukua muda mrefu bila kusikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Viongozi wa Polisi, wananyanyasa wananchi bila sababu za msingi kwa mfano, kuwaweka ndani kwa makosa ambayo sekta inaweza kuyapatia ufumbuzi. Ninao mfano hai uliotokea Arusha, kijana wangu, mfanyakazi wa *TTCL* kwa jina Shaame Mbaruk, aliswekwa ndani eti kwa kosa la kuhitilafiana na jirani yake kwa ujenzi wa ukuta katika nyumba yake. Suala hili lingeweza kutatuliwa na Manispaa, ni kwa nini aliwekwa ndani? Hatimaye ukuta wake ulivunjwa na alipokwenda Polisi kutaka kifungua kesi, akakataliwa. Hivi kuanzia lini, Polisi wana *sole right* ya kukataa mwananchi asifungue jalada?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuboreshe zaidi huduma za zimamoto mijini na ziwe *coordinated in such a way* panapotokezea *request* za dharura, waweze kuhudumiwa haraka. Hii itapunguza mzigo kwa zimamoto ya *airpot* na kusaidia *resources* chache zilizopo *airports*, zikidhi shida za dharura za *airpots* zitakapojitokeza.

Nazipongeza sana sana juhudi kubwa zinazofanywa na *Sector* ya Uhamiaji. Tunaelewa wapo wafanyakazi wachache tu ambao sio waaminifu. Naamini *on one to one basis,* hilo linaweza kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unyanyasaji unaofanywa kwa kisingizio cha *terrorism* na mataifa makubwa, lazima ulalamikiwe sio tu na *foreign affairs* bali pia na mambo ya ndani, kwani wananchi wanaharibiwa *passport* zao kwa hisia tu siku hizi. Inaudhi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri ule mpango wa kutoa *visa* wageni wanapofika tu *airport* uachwe, hata kama tunakaribisha watalii, hao ndio wanaogeuka wavamizi na kubaki nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wa Kichina waliojaa Kariakoo, wakiuza vibakuli na maua ya mapambo, sasa iwe basi. Hebu wapitieni, wapo madaktari feki wa Kichina na *Clinic* zisizo na mpango, wamejaa Dar es Salaam *as if* nchi hii haina utaratibu wa afya za wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wataalam wa kujitolea, *Peace Corp*, wengi hawana *knowledge* wala *skills* wanazosema wanazo, hatimaye kufanya mambo ya upelelezi na ukachero, kwa kutumia nafasi ya kujitolea. Hawa lazima wawe *censored* kabla ya kuwapokea.

**MHE. ANNA M. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, msongamano wa wafungwa magerezani ni ushahidi tosha wa mambo mawili muhimu yafuatayo:-

Kwanza, ni dalili tosha ya kuwa na jamii, isiyowajibika katika ujenzi wa Taifa letu mfano, wazazi kutowajibika katika ulezi wa watoto wao, watoto hutoka mikononi mwa wazazi wakiwa na umri mdogo, kuja mijini na kujikuta wakiangukia mikononi mwa jamii iliyopotoka.

Pili, Mahakama zinachelewesha sana usikilizaji wa kesi na ufinyu wa ushahidi ulio thabiti.

Tatu, rushwa iliyokithiri, inayofanywa na wahalifu na Mahakimu/*Police Procecutor,* hufanya kesi kuhukumiwa kwa upendeleo na kufanya wahalifu wakibaki huru na kuendeleza maovu na wanyonge kuishia magerezani. Yote haya ni kwa sababu wanyonge hawana uwezo wa kuweka mawakili, kwa hiyo, hujikuta wakisota magerezani bila ya kosa. Hii pia huchelewesha kesi kumalizika haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri wazazi wapatiwe elimu ya kuelezwa umuhimu wa kutoa malezi bora kwa watoto na mtoto anapotoweka nyumbani atafutwe. Kina baba wache tabia ya kuranda ovyo na kusababisha mimba zisizo za lazima na kumwacha mwanamke alee mtoto peke yake. Vile vile itungwe sheria kali kwa wazazi watakaopatikana na hatia ya kutupa watoto wao, bila jitihada ya kuwatafuta. Mtoto anapokutwa anaranda ovyo mitaani bila wazazi, akamatwe na kuulizwa anapotokea, wakipatikana wazazi wahukumiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kesi zichunguzwe kwa umakini, bila upendeleo na ziendeshwe kwa haraka ili hukumu itolewe bila kuchelewa. Mahakimu na wale wote wanaoshughulikia kesi, walipwe mishahara mizuri na marupurupu ili rushwa iangamizwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magereza yetu yanaongoza kwa uvunjwaji wa haki za binadamu kwa mfano mazingira machafu ya magereza yetu; vijana wetu kulawitiwa na kujikuta wana hali mbaya ya kijinsia au wafungwa sugu hupokezana kama mpira; magonjwa ya kuambukizwa; na wafungwa wanawake kutendewa vibaya, inasemekana askari magereza huwalazimisha kufanya nao mapenzi kwa kisingizio cha kupatiwa mahitaji bila shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ihakikishe kunakuwepo uangalizi wa karibu sana kwa wafungwa wa jamii zote. Usafi uwepo wa mara kwa mara, malazi bora na chakula kilichopikwa kwa usafi na uangalizi. Wafungwa sugu wasichanganywe na vijana au jamii ya wananchi walio hafifu kimaumbile. Kupigwa na mateso yasiyo na lazima Vituo vya Polisi, kwa visingizio vya usaili wa mkosa ni uonevu. Magereza kufanywa ndio ahera ya duniani ni vibaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wafungwa wapatiwe vipimo vya afya zao mara kwa mara na wawe karibu na waganga. Pia wafungwa wanawake wapatiwe heshima na askari magereza, watakapopatikana na hatia ya kumlazimisha mfungwa kufanya nae mapenzi hatua kali zichukuliwe. Nashauri askari magereza wanaume wasiruhusiwe kuingia katika gereza la wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Tanzania isipokee tena wakimbizi, kwani imekuwa tabu, ukarimu unatugharimu na silaha kubwa kubwa zinaingizwa nchini kwetu na wakimbizi na kufanya wimbi kubwa la ujambazi, ambao hufanywa na wageni hasa wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wageni ni wengi sana wanaoajiriwa hata kwa kazi ambazo Watanzania wanaweza kuzifanya, makampuni madogo yanayofunguliwa nchini

kama yanayonunua mazao na kuuza nje, yameajiri wageni hata makarani wadogo, mahotelini hata wapishi ni wageni, biashara ndogo ndogo hufanywa na wageni kwa kisingizio cha kusema eti waume zao au wake zao ni wawekezaji. Kama mume ni muwekezaji, inakuwaje mke auze fulana? Tuwe macho sana na wenzetu, wanajiita wawekezaji wanamaliza nchi hii na sisi tumebweteka tukisema ni utandawazi, tunaisha wageni wanamaliza nchi hii na mali zake zote.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani, kwa kuanza kusema kwamba, nampongeza Waziri, pamoja na Naibu Waziri wake, kwa hotuba yao nzuri.

Pili, napenda kutoa mapendekezo yangu kuhusu askari magereza. Askari hawa hawana tofauti na wafungwa hivyo, wanastahili kupewa mshahara unaokidhi haja, kwani baadhi yao wanafanya kazi ngumu ya kuwalinda wafungwa wanapokuwa katika kazi za nje. Wafungwa hao wengine huwa na makosa ya kuua na kufungwa katika magereza haya. Pia naiomba Wizara iweke mkakati kabambe wa kufuatilia makosa ya mahabusu, kwani mahabusu wengine hufikishwa gerezani kwa kukomoana na kazi hii hufanywa na baadhi ya askari wa usalama wa raia. Tunaomba Wizara ya Mambo ya Ndani na ile ya Usalama wa Raia, wafanye kazi pamoja ili kubaini askari hao, wanaopotosha maadili ya jeshi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba ongezeko la magari ya zimamoto katika Wilaya zenye majengo mengi na ongezeko la watu. Shughuli hizi za zimamoto zifanyike kwa usawa, pia wahudumu hawa wa zimamoto waishi katika maeneo ambayo magari hayo yanalala, ili isiwe tabu wakati wa maafa ya moto yanapotokea. Kuna baadhi ya magari ya zimamoto hukaa bila maji, huu ni uzembe. Tunaomba kusisitiza kwa kutoa sauti kwa hilo, ili magari yote ya zimamoto yakae na maji muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Uhamiaji bado haijawa makini sana hasa upande wa pasipoti, kwani Mmaafisa wa Uhamiaji mikoani, huwa hawatoi huduma ipasavyo. Pasipoti huchukua muda wa zaidi ya wiki tatu, fomu zinapomaliza kujazwa na kutumwa Makao Makuu ya Wizara na nyingine huchukua zaidi ya mwezi mmoja na nusu. Mfano, pasipoti ya binti mmoja aitwae Fatuma wa Mwanza, ambaye ilimaliza mwezi na zaidi na baada ya kufuatilia Dar es Salaam, tamko lilitoka kuwa ilitumwa Iringa. Ina maana wafanyakazi hao wa Uhamiaji, hawapitii mafaili ya kazi zao na kugundua makosa hayo na kuyatolea uamuzi wa kufuatilia. Kama mwananchi hana uwezo wa kuona pasipoti yake imechelewa na kuifuatilia, Wizara ingejuaje kama inatakiwa kutoka Iringa na kutumwa kunakohusika.

Je, Wizara ina utaratibu gani wa kutoa adhabu kwa wafanyakazi wanaofanya uzembe kama huo, kuchukua pasipoti ya mkoa fulani na kupeleka mkoa mwingine, bila kufuatilia zaidi ya mwezi mmoja na nusu na kusababisha mwombaji husika akibaki anapigizana kelele na Maafisa Uhamiaji wa Mkoa? Gharama za simu ya kuulizia pasipoti hiyo anayopewa mwombaji anatumia bila malipo. Tunaomba Wizara imulike maafisa wazembe kama hawa, ili wajue kazi zao na wanalipwa mashahara kwa kazi hizo, waache mzaha na uzembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nami nawapongeza Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Naibu Waziri, Mheshimiwa Bernard K. Membe, Katibu Mkuu, Ndugu Solomon Odunga na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri wanazofanya katika Wizara yao. Mikakati waliyoiweka ni mizuri sana ya kuboresha kazi za Wizara hii, nasema Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naunga mkono hoja iliyotolewa, mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuchangia katika maeneo yafuatayo; Magereza, Zimamoto na Uhamiaji.

Nikianzia kwanza na magereza. Suala la magereza zetu nchini kujaa ni tatizo sana. Magereza mengi yanajaa kutokana na kitengo cha mahakama kufanya kazi kwa kasi mpya hivyo, kesi nyingi kushughulikiwa, wengine hufungwa na kufanya idadi ya wafungwa kuongezeka. Kwa hiyo, kuna haja ya Serikali kuongeza majengo ya magereza. Isipokuwa wakati wa kuongeza magereza au kujenga magereza mapya, waanze kujenga katika Wilaya mpya, ambazo hazina magereza. Wilaya ya Ruangwa haina kabisa gereza, tangu wilaya hiyo ianze mwaka 1994. Wafungwa wa Wilaya hii hupelekwa Wilaya ya Nachingwea, kilomita 30 kwenda kufungwa na wale mahabusu huenda kuchukuliwa katika Wilaya ya Nachingwea kila siku kwa hukumu, kitu ambacho hupoteza mafuta na gharama kubwa.

Kutokana na kasi mpya ya utendaji na hivyo kuwa na wafungwa wengi, tunaomba Serikali ijenge magereza kwanza Wilayani Ruangwa Mkoa wa Lindi. Tafadhali hakuna magereza tangu mwaka 1994, ni wilaya ya zamani, ipewe umuhimu wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio ya moto sasa yamekuwa mengi na vyombo hakuna vya kuzimia moto. Nina mfano, mimi binafsi huko Lindi niliunguliwa moto mpaka nyumba ikaisha kuungua na mtoto wangu alikufa, hakukuwa na zimamoto iliyosaidia kwa vile kulikuwa na gari bovu ambalo halikufanya kazi. Kwa hiyo, tunaomba sasa kila Wilaya kuwe na zimamoto, hata kwa kuwaruhusu pia watu binafsi kutoa huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi matendo ya wahamiaji haramu yamezidi nchini kutoka mikoa na nchi ya jirani, wananchi wa kutoka nchi za jirani huja sana nchini kutoka Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Somalia, aidha huja kwa kukaa huku kwetu au kupita kuelekea Afrika ya Kusini. Kuna njia zao ambazo wakipita hawaonekani. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara, iimarishe Ofisi za Uhamiaji hasa Lindi. Huko Lindi kuna hoteli moja ya Kisomali, ambayo imeanza kufanya kazi mwaka 2006. Hoteli hii watu wanasema kuwa, ipo pale kwa ajili ya kuwahifadhi wahamiaji haramu, ambao wanatoka Somalia, Kenya na kwenda Afrika ya Kusini. Hupitia njia za panya kwa miguu wanapokuja kutoka Dar es Salaam na hufikia hapo. Tunaomba Serikali, ifuatilie suala hili, ikibidi hoteli hiyo ifutiwe leseni, endapo itabainika kuwa ipo pale kama kituo cha

kuwalisha chakula wahamiaji haramu. Maafisa Uhamiaji Lindi, bado hawana taarifa hii, ni taarifa mpya, tunawaomba walifuatilie kwa makini suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja tena kwa asilimia mia moja.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona mambo yanakwenda vizuri. Nampongeza Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua kama Wilaya yangu ya Sengerema imo miongoni mwa wilaya zitakazopata haya magari 64, kama ilivyoainishwa kwenye ukurasa wa 17 wa Hotuba. Kama hatumo mpango wa Serikali ni nini kuhusu Wilaya zilizobaki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, kama kuna namna ambayo Mheshimiwa Waziri ataweza kutusaidia kutupatia gari hilo mwaka huu, maana ni tatizo kubwa sana Sengerema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri na yenye mwelekeo. Aidha, ninaipongeza Wizara, kwa kazi nzuri inayofanya. Ninaiunga mkono hoja hii, lakini hata hivyo kuna mambo mawili:-

Kwanza, Gereza la Matongo, Wilayani Bariadi, lilianzishwa miaka ya themanini kama Gereza la Kilimo. Kusema kweli Gereza hilo lilitoa mchango wake miaka ya huko nyuma, sasa hivi Gereza hilo halistahili hadhi ya Gereza la Kilimo. Halina vitendea kazi kwa maana ya zana za kilimo. Gereza hilo sasa halitoi mchango wowote wa maana badala yake, ardhi waliyonayo inatumiwa na Askari Magereza kama sehemu ya MKUKUTA wao. Kibaya zaidi, hali ya Gereza hilo inatisha. Nyumba zote ni mbavu za mbwa, wafungwa waliopo hapo hawaishi kama binadamu. Je, Wizara bado ina nia ya kuendelea na Gereza hili? Je, haingekuwa busara kulifunga na kuwahamishia Askari Magereza wachache waliopo hapo katika vituo vingine kama vile Maswiwa?

Pili, kuhusu tafiti za nishati mbadala, nashauri Uongozi wa Magereza, utembelee Taasisi ya *CARMATEC*, Tengeru Arusha, ili ukajionee majiko ya kupia chakula yenye bei nafuu na ambayo pia ni rafiki wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uzima na kuweza kuhudhuria katika kikao hiki cha Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi za dhati kwako wewe, pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuliongoza Bunge letu bila ya ubaguzi wa aina yoyote. Pia nawapongeza Wenyeviti wa Bunge hili, kwa kuwasaidia vizuri kazi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, pamoja na Naibu wake, kwa bajeti yao iliyowasilishwa vizuri hapa Bungeni. Pia nawapongeza wananchi wa jimbo langu la Mtambwe, kwa kunichagua kwa kura nyingi. Nawashukuru sana na nitaendelea kushirikiana nao katika kuleta maendeleo ya jimbo letu pamoja na Taifa kwa jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya magereza katika nchi yetu hairidhishi. Ili magereza yaweze kuwa na hali nzuri, naiomba Serikali ijenge magereza mapya na kuyafanyia ukarabati yale yaliyopo ili kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani, watenganishwe mahabusu na wafungwa. Watuhumiwa wasiwekwe mahabusu kwa zaidi ya saa 24 na wasiadhibiwe kabla ya kuthibitishwa kwa makosa yao. Haki za binadamu zisivunjwe bali zithaminiwe au zilindwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utafutwe ufumbuzi unaofaa, kuhusu masharti magumu ya dhamana kwa mahabusu. Askari wanaowabambikizia makosa mahabusu, wachukuliwe hatua zinazostahili. Huduma mbalimbali kwa wafungwa kama vile chakula, malazi na mavazi, ziboreshwe ili kusaidia kuendeleza afya za wafungwa hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watuhumiwa huwekwa ndani kwa muda mrefu kwa madi kwamba, ushahidi haujakamilika, wakati hakuna juhudi yoyote inayochukuliwa kukamilisha ushahidi huo. Hii inapelekea kuadhibiwa kwa watuhumiwa kabla ya kuhukumiwa. Tunaziomba mahakama zetu, zitoe maamuzi yasiyochukua muda mrefu, kwa kesi zinazoonekana kuwa ni za kubabaisha na hazina ushahidi ili watuhumiwa waweze kutendewa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitambulisho vya uraia ni muhimu sana kwa Taifa letu. Vitambulisho hivi vinamhakikishia kila Mtanzania, uraia wake bila kujali rangi yake, dini yake, kabila lake au eneo analotoka. Vitambulisho vya uraia pia vinasaidia kuwatambua watu, yanapotokea matatizo kama vile ajali. Pia vinasaidia kuwajua wenyeji na wageni katika kutoa mambo ambayo ni haki za kiraia. Pia ni rahisi kuwatambua wahalifu katika matukio ya ujambazi au uvunjaji wa sheria wa aina yoyote

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uzima na kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hutuba nzuri, yenye matumaini kwa wa Tanzania na kwa wapenda amani wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia wananchi wa Jimbo la Fuoni, kwa imani waliyoitoa, kukichagua Chama cha Mapinduzi na kuniwezesha mimi kuwa Mbunge wa Jimbo hilo na kwa imani hiyo waliyoonesha kwangu na Chama cha Mapinduzi, ninaahidi kuwa sitowaangusha. Nitawatumikia kwa uwezo wangu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya jeshi hili ni kuhifadhi wahalifu wa aina zote ili kurekebisha tabia ili wanapomaliza adhabu zao wawe raia wema. Kazi hii ni kubwa sana hasa ukizingatia yule ni binadamu na hakuna kazi kubwa ila kumchunga binadamu mwezako hasa mkiwa mnalingana umri au kukushinda na hii ndiyo hali iliyokuwepo katika magereza yetu. Katika kufundisha watu wa namna hii, ni lazima utumie adhabu ili akufahamu na akuelewe. Mfungwa anapotaka kupigana na askari au anapoamua kutoroka, kuna adhabu gani inayostahili akiacha kumpiga kwa nia ya kumtia adabu, lakini askari akifanya hivyo na ikitokezea bahati mbaya mfungwa akaumia, askari anashtakiwa. Kwa kuwa kuna haki za wafungwa na askari nao wawe na haki zao, kwani kitendo cha kumshtaki askari au kumpa adhabu askari, nionavyo mimi ni kuupa nguvu wahalifu walioko magerezani na kuwavunja nguvu askari kufanya kazi zao ipasavyo. Kwa hiyo, naomba hali hii iangaliwe kwa makini, kama kweli tunawajali askari wetu na kama kweli tunataka kuwafundisha tabia nzuri wahalifu, ili wawe na tabia nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Uhamiaji ni sehemu muhimu sana katika ulinzi wa nchi yetu. Idara hii ina dhima kubwa ya nchi, hasa kutokana na amani na utulivu ulioko nchini mwetu, hasa ukilinganisha na nchi jirani ambazo amani imetoweka kutokana na hali hii. Kuna matarajio makubwa ya wageni wengi, ambao si rasmi wataingia nchini kwa kutumia njia haramu kuingia nchini mwetu na kwa kuwa wanapoingia nchini wageni hawa hujishughulisha na vitendo vya uhalifu, kuna haja ya kuongeza juhudi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi katika mipaka yetu, kuzidisha doria katika mahoteli kwa nchi nzima, pamoja na ukaguzi wa kina katika milango ya kuingilia na kutokea wageni. Pia ninaishauri Serikali kuwa na tabia ya kuhamisha hamisha katika vituo wafanyakazi wake na hasa katika milango ya kuingia na kutokea wageni, kwa sababu lazima tukiri, kuna wafanyakazi ambao si waaminifu hasa akiwa anafanya kazi sehemu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Zimamoto ina jukumu la kuokoa maisha na mali kwenye majanga ya moto na ajali mbalimbali za kuzima moto. Dhima ya kazi hii inakosekana wakati yanapotokezea majanga ya moto, vikosi vya uokozi huchukua muda mrefu sana kufika katika sehemu ya tukio na kusababisha hasara kubwa kwa waliopatwa na tatizo na wakati mwingine huona hakuna haja ya kikosi hiki. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali, iboreshe zaidi kikosi hiki, kwa kuvipatia vifaa vya kisasa, ambavyo vitawawezesha kutambua tukio na kuwawezesha kufika kwa haraka kwenye tukio.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameeleza kuwa programu ya kuwarekebisha wafungwa inaendelea. Iwe hivyo, lakini ipo haja Wizara inieleze, inakuwaje pamoja na mafunzo yote yanayotolewa bado inaonekana kuwa wafungwa wale wale mara nyingi huwa ndio wanaorejea tena kwenye magereza? Hapa inadhihirisha bado mafunzo yanayotolewa magerezani hayakidhi haja ya wafungwa hao kuwa raia wema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msongamano mkubwa wa wafungwa ndani ya magereza yetu, hali inayosababisha maambukizo ya maradhi kama kifua kikuu, inaonekana kuwa juhudi za kuikabili hali hiyo ni ndogo. Je, Serikali ina mkakati gani wa kulitatua tatizo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 27 Julai, 2006 wakati Mheshimiwa Waziri tarehe anakijibu swali nambari 249 la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Jimbo la Ziwani, kuhusu *passport,* pamoja na maelezo mengine, alisema mwananchi akikamilisha sifa za kupata *passport*, basi kwa aliyeko eneo la Makao Makuu, yaani Dar es Salaam inachukua wiki moja, nje ya hapo wiki mbili na kwa Zanzibar ni siku nne. Je, Mheshimiwa Waziri, ananieleza vipi juu ya ongezeko la siku za kupata *passport* kinyume na maelezo yake ambapo ni jambo la kawaida?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za zimamoto ni duni na hii inatokana na ukosefu wa vitendea kazi. Majanga ya moto yanasababisha gharama kubwa kwa mali na baadhi ya maisha ya wananchi. Serikali iweke mkakati wa kuikabili hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kuelekeza mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika malengo ya Jeshi la Magereza mwaka 2006/2007, Wizara inakusudia kujenga magereza mapya katika Wilaya tano za Karatu, Hanang, Nkasi, Ruangwa na Bukombe. Inasikitisha sana kuona Wilaya ya Muheza haipo katika mpango licha ya aliyekuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, ambaye sasa ndio Waziri wa Wizara hii, alipotembelea Gereza Dogo la Wilaya ya Muheza mwaka 2004, alijionea hali mbaya ilivyo katika Gereza hilo Dogo. Inaonekana amesahau hali hiyo inayosikitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana pia Wizara husika haijali hali mbaya sana ya nyumba za maofisa wake katika Gereza Dogo la Kilulu, Muheza, nyumba ni za tope fito, makuti na zinazovuja!

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuhudhuria semina ya haki za binadamu wiki iliyopita hapa Bungeni, naona iko haja kuikumbusha Wizara hii kwamba, ni kuvunja haki za binadamu kuendelea kuwaweka wafanyakazi wa Serikali na familia zao ndani ya nyumba kama zile za watumishi wa Gereza Dogo la Kilulu, Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuikumbusha tena Wizara husika juu ya hali mbaya sana ya Gereza na nyumba za watumishi wa Gereza la Kilulu, natarajia Mheshimiwa Waziri, atatoa mwelekeo thabiti wa mpango wa kuondoa tatizo hilo badala ya kujenga magereza mapya kabla ya kuboresha yale yaliyopo katika hali mbaya sana kama Gereza lile Dogo la Kilulu, Muheza. Hivi kwa nini Wilaya mpya zipate majengo mapya ya Magereza wakati Wilaya kongwe zinaendelea kubaki bila ya kuwa na gereza rasmi la wilaya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za kuboresha hali ya majengo ya magereza na wafungwa kwa ujumla ni za kupongezwa sana. Hata hivyo, msongamano katika magereza unaleta fedheha sana na kusababisha vitendo vichafu vya ngono za jinsia moja, hasa za kiume na ubebeshwaji wa mimba wanawake. La kusikitisha zaidi, viongozi wa magereza na hata Wizara, hawaoni aibu ya kuendelea kukua kwa vitendo hivyo na bila haya, kutojali kuwafichua wanaojishirikisha katika vitendo hivyo, wakiwemo baadhi ya viongozi katika magereza na Wizara husika. Lazima uwepo utaratibu wa Wizara kusimamia nidhamu, haki, afya na usalama wa wafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi kutoka nchi jirani hasa Msumbiji, Rwanda na Burundi, waliingia nchini zaidi ya miaka 60 iliyopita, kwa kufanya kazi maeneo ya mshamba ya mkonge hasa Mkoa wa Tanga. Wakati wanaingia, hawakuulizwa wala kusimamiwa, wala kushauriwa kuhusu sheria za uraia wao. Wamefanya kazi miaka yote bila kusaidiwa juu ya kurekebisha uraia wao. Wamezaa kwa kuchanganyika na raia wa Tanzania, wamepata vijukuu na vitukuu. Wengi wa wazazi hao ni wazee sana na hata hawana uwezo wa kurejea makwao. Serikali ina mpango gani wa haki za uraia wa wazee hao, watoto wao, wajukuu wao na vilembwe wao, ambao wamesomeshwa na Taifa hili, wanafanya kazi wamepewa ardhi na wengine wanamiliki ardhi au viwanja katika maeneo mbalimbali nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo sahihi na wa kudumu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naunga mkono hoja.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji, kwa kuandaa hotuba hii ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ni nzuri, pengine Mungu akijalia, itaenda kuboresha maeneo ya kazi na kupunguza adha kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi, naomba nichangie moja kwa moja katika bajeti hii Wilaya ya Bukombe iko jirani na nchi za Rwanda na Burundi, hali hii inasababisha msongamano wa wananchi ambao si raia. Kwa sababu upatikanaji wa *passport* mara nyingi umekuwa wa kununua, watu wengi wanaishi wakisema ni raia wa Tanzania. Hali ya usalama Wilayani Bukombe si nzuri na hii inasababishwa na wimbi la wakimbizi toka nchi jirani. Naomba Serikali, ifanye mkakati wa makusudi, kufuatilia

uraia wa watu wanaotiliwa mashaka hasa katika maeneo ya Uyone, Runzewe, Lugunga, Ushirombo, Masumbwe na sehemu nyingine. Hii ina maana ni pamoja na wafugaji wavamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri, kwa kunikumbuka kuniletea/kujenga gereza katika Wilaya ya Bukombe. Katika kitabu cha hotuba ukurasa wa.16, wameahidi, nami naomba iwe hivyo, kwani kukosa gereza, kumesababisha mlundikano katika Gereza la Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wafanyakazi wa Uhamiaji na Magereza, waandaliwe mahali pazuri pa kuishi, kwani kuwaacha hawa waishi nyumba za kupanga uraiani haipendezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *birth certificates,* wananchi wetu wanapata taabu sana. Naomba *birth certificates* zitolewe aidha Wilayani au Mkoani ili kuondoa urasimu wa utoaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono haja. Ahsante.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kimpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa hotuba yake nzuri. Aidha, nampongeza Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara. Kadhalika nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi ya Bunge na Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo matatizo mengi na ya jumla katika Wizara ya Mambo ya Ndani, ambayo tayari yameelezwa na Waziri pia Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Mwenyekiti wa Kamati. Napenda kukubaliana nao, hata hivyo, napenda kupata maelezo ya ziada katika maeneo yafuatayo:-

Nimepitia hotuba ya Waziri katika utekelezaji wa Wizara kwa mwaka uliopita na mipango ya Wizara kwa mwaka 2006/2007, hivi Wizara inatambua kwamba, yapo magereza huko Mpanda? Gereza la Mahabusu Mpanda na Gereza la Kilimo Kilalankulu, yapo katika hali mbaya, uchakavu wa majengo na nafasi kwa wafungwa, mlundikano wa wafungwa unatisha. Mlipuko wa mardhi na maradhi ya kuambukiza ni mambo ambayo yamezoeleka katika masikio yetu. Naomba Wizara itoe maelezo, kuna mpango gani wa kurekebisha hali hii katika Magereza ya Mahabusu Mpanda na Kilalankulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gereza la Kilimo Kalilankulukulu,lina eneo kubwa na zuri kwa shughuli za kilimo, eneo ambalo huwezi kulima kwa jembe la mkono eneo lote, haiwezekani vyombo vya kilimo ni chakavu na havitoshelezi. Hakuna magari kwa ajili ya usafiri wa kawaida kwa askari, wafungwa, wagonjwa na wananchi wengi wanaopata huduma katika gereza hilo. Wizara inasema nini katika kusaidia Gereza la Kalilankulukulu ili kweli liwe Gereza la Kilimo, vinginevyo Wizara itamke wazi kwamba sasa Gereza la Kilimo Kalilankulukulu si la Kilimo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wakimbizi limezungumzwa sana na naamini wachangiaji wengi, watagusia kuhusu wakimbizi, nami niwe miongoni mwao. Nataka kufahamu juu ya mradi wa kukabiliana na athari za wakimbizi, ambazo umepata fedha nyingi, kwa taarifa ya Msemaji wa Upinzani, awamu ya kwanza wamepata shilingi bilioni tisa, awamu ya pili watapata shilingi bilioni 10.9. Wizara inafahamu kwamba, Wilaya ya Mpanda tumekuwa tukipokea wakimbizi tangu mwaka 1963 na 1972 na Tabora kadhalika? Naomba maelezo ya kina juu ya mgao kwa makazi ya wakimbizi Katumba, Mishamo na Ulyankulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kutahadharisha juu ya vitambulisho vya uraia, hasa maeneo ambayo yana wakimbizi na hususan katika maeneo ambayo wakimbizi wamekaa zaidi ya miaka 30. Kama hatutakuwa waangalifu katika zoezi hili, vitambulisho vingi inawezekana wasiokuwa Watanzania watapata hivyo vitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MHE. OMAR YUSSUF MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwachanganya wafungwa wa muda mrefu na wale wa muda mfupi, inaonekana ni tatizo, hasa kwa kuzingatia matatizo ya kisaikolojia. Ni vyema yakawepo magereza tofauti kwa muda tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo tatizo kubwa kwa Maafisa wa Uhamiaji, kukaa muda mrefu bila ya kupandishwa vyeo. Je, kuna sababu gani za msingi na kama zipo kwa nini mhusika asiarifiwe sababu hizo?

Kuna Watanzania wengi walioko nchi za nje, wana uraia wa nchi mbili, wakati nchi yetu bado haijaanzisha utaratibu huo. Watanzania hao wanapokuja Tanzania, hutumia pasi za Tanzania na kuinyima nchi yetu fedha zinazotokana na *visa.* Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kuanzisha uraia wa nchi mbili *(Dual Citizenship)?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila ya kuhusisha cheti cha kuzaliwa, nina wasiwasi vitambulisho vya uraia watapewa hata wageni wanaofanya biashara katika mipaka yetu. Wakati huo huo sio Watanzania wote ambao wana vyeti vya kuzaliwa na ukishirikisha viongozi wa mitaa, baadhi yao sio waaminifu. Je, Serikali itafanya mipango gani kuhakikisha kuwa, watakaopewa vitambulisho vya uraia ni Watanzania na si vinginevyo?

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa hotuba nzuri waliyoiandaa na kwa kazi nzuri inayofanyika. Pamoja na shukrani, naomba kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gereza la Kongwa ni chakavu, tunaomba ukarabati mkubwa ufanyike, kuta zina nyufa, vyoo vya mtondoo, sina hakika kama *TV set* aliyoiagiza Mheshimiwa Waziri ilishanunuliwa. Nyumba za watumishi chache sana na ni ndogo mno kiramani. Ramani zile zipigwe marufuku, hazifai kwa askari mwenye

familia. Gereza linahitaji *tractors* angalau mbili kwa Gereza la Kongwa na Gereza Dogo la Mkoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shamba la Manyato lilikuwa la Magereza, inakuwaje sasa linalimwa na watu binafsi?

Gereza la Kongwa hawana kitalu cha miti, kwa matumizi ya kuni waliyonayo, wanapaswa kuotesha miti mingi. Maji wanayo, waanzishe vitalu na waanze kupanda kwenye eneo lao kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jiko la Gereza la Kongwa litumie *biogas*. Kinyesi cha ng'ombe waliopo na cha wafungwa wenyewe, kinatosha sana kwa matumizi ya jikoni. Mradi maalum upo hapa Dodoma utumike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa Gereza la Kongwa wanalalamikia haki zao, madai yao, malimbikizo yao, baadhi ni wastaafu na kupata haki zao ni taabu sana. Naomba lingaliwe suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wakimbizi kukaa muda mrefu kwenye makambi, linachangia kwa kiasi kikubwa, kuzowea mazingira na hatimaye kujiingiza kwenye vitendo vya ujambazi. Ni vyema wakati mwingine nchi inapoamua kuwa-*host* wakimbizi, basi ama kuwe na utaratibu wa kuwahamisha kwenye makazi ili kukwepa wasiyazowee mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yote ambayo wakimbizi wameishi, mazingira ya maeneo hayo yanaharibiwa kwa kiasi kikubwa. Makubaliano na utaratibu wa Mkataba wa *UN* na nchi zinazowapokea wakimbizi, ni kuwasaidia wananchi wa maeneo hayo, kwa faida ya nchi inayowahifadhi. Katika kipindi kifupi ambapo wananchi wangefurahia kuona kwamba, naeneo waliyoishi wakimbizi yanapata ufadhili toka *UN,* badala yake wakimbizi wanaandaliwa kuondoka bila kufidia maeneo ambayo yameathiriwa na ujio wao. Ni vyema Wizara inayohusika, iwabane *UN* kuhakikisha wanalipa fidia ama kuyakarabati maeneo hayo yaliyoharibiwa mfano barabara, msitu na mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu, Serikali imekuwa ikiwatangazia wananchi kuhusu kukamilika kwa vitambulisho vya uraia. Kitendo cha kutokutilia manani vitambulisho hivyo, kimeweza kuathiri kwa kiasi kikubwa, kuongeza kwa vitendo vya ujambazi vinavyofanywa na wageni toka nchi jirani. Kozi inayofanyika kwa sasa hivi ni kuwatambua wageni haramu na kuwakamata kwa kutumia misako inayoendeshwa na Wizara hiyo.

Hata hivyo, inaonesha dhahiri kwamba, uwezo mdogo wa Maafisa wa Uhamiaji wa kuwatambua wahamiaji haramu ni chachu katika Wizara hiyo. Kwa makusudi mazima ni vyema, mafunzo ya ziada na ya mara kwa mara, kwa maofisa hao yatolewe. Katika kuboresha zaidi, Wizara iwezeshwe kupata fedha za kuwasafirisha wageni haramu, wanaopatikana kutokana na misako badala ya kuwarundika watu wa aina hiyo kwenye magereza na kusababisha msongamano kwenye magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zimamoto ni Kikosi muhimu sana hapa nchini. Tatizo kubwa lililopo ni Kikosi hicho kutokupewa uhuru ama uwezo wa kujitegemea kwa kukifanya kiwe ni Jeshi kamili linalojitegmea. Kitendo cha kikosi hiki kufanya kazi kwa mtindo wa vipande vipande kama vile Zimamoto *Airport,* Zimamoto kwa kila Halmashauri, Zimamoto Bandari. Jeshi mahali popote linatakiwa kuwa na *Central Command.* Si kama ilivyo kwa Jeshi hilo hapa Tanzania, ambapo ni tofauti na jinsi Jeshi hilo lilivyo ama linavyokuwa kwa nchi nyingine. Napenda kupata maelezo ya kutosha ni kwa nini kikosi hiki kilicho muhimu, kisifanyiwe mabadiliko na kuwa Jeshi kamili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa makusudi mazima ni lazima Wizara iwe na Bajeti ya kuendesha mikutano ya mara kwa mara ili kukabiliana na uingiaji holela kutoka upande mmoja kwenda upande mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa, kwa watoto wanaozaliwa kwa visingizio tofauti. Aidha, zimekuwa zikitolewa sababu za maombi yote yanayohusu vyeti vya kuzaliwa kutolewa na Makao Makuu, ambayo ni Vizazi na Vifo na yapo Dar es Salaam. Hiki kimekuwa ni kichocheo kikubwa cha kupokea rushwa ili kupata cheti hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata maelezo ni kwa nini vyeti hivi visitolewe kwenye Hospitali za Wilaya na Mikoani ili kuweza kuhakiki upatikanaji wa vyeti hivi na uthibitisho ulio wazi kwamba, kinatolewa kwa mhusika?

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari Magereza ni miongoni mwa askari wanaofanya kazi zao katika mazingira magumu, kwani wao vile vile huonekana kama wafungwa, kwa sababu saa zote wanakuwa pamoja nao, wakati wa jua au mvua katika kutekeleza majukumu yao. Kutokana na uzito wa kazi hiyo, askari hao wanahitaji mazingira mazuri ya kazi, ikiwemo mishahara mizuri, nyumba za kuishi na vitendea kazi vilivyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mchele usiokokuwa na chuwa, baadhi ya askari hao wanawatesa wafungwa ambao tayari wamekuwa kiakili wameathirika kutokana na kufungwa kwao, kwa hiyo waache mtindo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafungwa ni binadamu, wanahitaji maisha bora kama watu wengine, kutenda kosa ni ubinadamu, unatenda aidha kwa bahati mbaya au kutokana na kutingwa na maisha. Mfungwa anahitaji mambo yote ya msingi ikiwemo chakula, malazi, afya, elimu, mavazi na kulindwa maisha yake, kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie hili kwani wafungwa ni binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafungwa wanaishi katika magereza ambayo hayana hadhi ya kuishi binadamu, kutokana na uchakavu wa majengo, vyumba vidogo ambavyo wanaishi kwa msongamano na hivyo kuwaletea magonjwa ya kuambukiza kama vile magonjwa ya ngozi na *TB.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Uhamiaji ni miongoni mwa Idara nyeti, lakini idara hii imekuwa na usumbufu kwa raia pale wanapokwenda kuomba pasi, urasimu umekuwa mkubwa hata kama vielelezo ulivyopeleka ni vya kweli. Ninaiomba Wizara iwaangalie wafanyakazi hawa walio na urasimu ili kupunguza malalamiko kutoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Zimamoto nayo inahitaji kupewa kipaumbele, ikiwemo vifaa vya kisasa vya kufanyia kazi hasa katika majanga makubwa aidha ya moto au milipuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hotuba ni nzuri na idara zote muhimu zimetajwa na malengo yake kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya Halmashauri ya Mji wa Babati, ambapo pia ni Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara, kwa ajili ya gari la zimamoto. Hili ni kati ya mambo muhimu sana na linasubiriwa kwa hamu sana na wakazi wa Mji wa Babati.

Naomba kwenye bajeti yetu ya Halmashauri ya Mji katika harakati za kuunda Kikosi cha Zimamoto, tumepangiwa *seargent of fire* na dreva mmoja. Kwa kuwa sasa tutapata gari, tunahitaji kupata watumishi zaidi na kuunda Kikosi cha Zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuanza kujenga ofisi ya Mkoa wa Manyara. Manyara ni mkoa mkubwa na unavutia watu wengi, kutoka sehemu mbalimbali hasa nje ya nchi, kwa ajili ya shughuli za utalii, uwindaji, uchimbaji wa madini na biashara nyingine. Hivyo, kuwa na ofisi nzuri na yenye vifaa vya kisasa ni muhimu zaidi, kuwa na usafiri unaoaminika ni muhimu sana. Hatuna gari la kuaminika kwa Ofisi ya Uhamiaji Wilaya ya Babati, ambayo ina Halmashauri mbili; Halmashauri ya Wilaya na ile ya Babati Mjini. Hivyo, natoa ombi maalum la gari kwa ajili ya Wilaya ya Babati. Ofisi ya mkoa ina gari moja tu kwa ajili ya Kamanda wa Mkoa wa Uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Babati ina gereza dogo lenye uwezo mdogo tu kulinganisha na mahitji makubwa. Kwa kuwa sasa Babati ni Makao Makuu ya Mkoa, ni muhimu kuwa na gereza kubwa la Mkoa ili kuondoa msongamano mkubwa uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwishom naunga mkono hoja na natoa mwaliko kwako na kwa Naibu Waziri wakom kutembelea Mkoa wa Manyara na hususan Babati.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mampongeza Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri ya kusimamia watendaji kuandaa bajeti ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia kama ifuatavyo: Kwanza, magereza kunyang'anya ardhi ya wananchi, Gereza la Utemini Ushora huko Ndago ndani ya jimbo langu la Uchaguzi la Iramba Magharigi. Eneo kubwa la kilimo sehemu za Mirangu limeporwa na Magereza. Naomba Waziri, atakapofanya majumuisho, anieleze sababu za Jeshi la Magereza kupora ardhi hiyo.

Pili, Vitendea kazi vya wafungwa vitolewe ikiwa ni pamoja na zana za kilimo na vifaa vingine vya ufundi na kadhalika.

Tatu, magereza zilizojengwa karibu na sehemu za raia, hasa vijijini, ziangaliwe kwa macho mawili, hasa kiuhalifu kwani mara nyingi wafungwa hupewa uhuru wa kujichanganya na raia hivyo, kupeleka tabia mbaya.

Nne, elimu ya UKIMWI itolewe magerezani. Jeshi la Magereza na hata Asasi zisizokuwa za Kiserikali, ziruhusiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri na ni jambo lisilopingika kwamba, magereza mengi humu nchini, yanaweka idadi kubwa ya wafungwa na mahabusu kuliko uwezo wake. Kwa kuwa wafungwa na mahabusu ni binadamu kama binadamu wengine, wana haki zao za msingi, miongoni mwa haki hizo ni pamoja na kupata chakula kizuri na kilicho bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na msongamano katika magereza ni wazi kwamba, huduma hii muhimu haiwezi kupatikana ipasavyo, hasa ukizingatia ufinyu wa bajeti ya Wizara. Wafungwa na mahabusu, kama ilivyo kwa binadamu wengine, wanastahili kuipata haki hiyo. Serikali itueleze ni magereza mangapi hapa nchini, yametengewa sehemu za ibada na kama sehemu hizi hazipo, Wizara ina mpango gani wa kuanzisha maeneo hayo ya kufanyia ibada ili wafungwa na mahabusu waweze kutekeleza shughuli zao za ibada?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ipo haja sasa kwa Serikali kuruhusu viongozi wa dini na madhehebu mbalimbali, kutembelea magereza yetu kwa madhumuni ya kuwapatia *Da'awa* na imani ya kiroho ili iwasadie wafungwa na mahabusu hao kubadili tabia zao mbaya kwa jamii na hatimaye kuwa wacha Mungu, wanaofuata maadili mema, hali itakayowawezesha kuishi maisha mazuri hapa duniani na kesho mbele ya Mungu. Je Serikali inatoa tamko gani kuhusu hali hii?

**MHE GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kuteuliwa kushika nyadhifa hizo. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa uwasilishaji mzuri wa hoja yake. Nawapongeza pia Watendaji wote wa Wizara, kwa jitihada zao za kuboresha huduma za Wizara hii katika ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara hususan Idara ya Magereza, kwa msukumo na msaada wa ujenzi wa majengo katika Gereza la Ileje. Kutokana na uwezo mdogo wa Halmashauri yetu ya Wilaya, tunaomba Wizara iendelee kutoa msaada kila inapowezekana katika miradi ya ujenzi inayoendelea, ikiwa ni pamoja na kufikisha umeme katika ofisi na majengo husika ya Gereza la Ileje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya yetu ipo mpakani na Malawi. Kumekuwa na tatizo la wahamiaji haramu au wakimbizi wanaopita Wilayani kwenda Malawi au Afrika Kusini. Kutokana na tatizo hilo, haja ipo ya kuimarisha ofisi na watendaji wa Uhamiaji Wilayani Ileje. Tunaomba Wizara ione umuhimu wa kujenga kituo cha kisasa pale mpakani Isongole (Darajani), kama ilivyo Kasumulu kule Kyela. Shughuli za biashara kati ya Tanzania na Malawi kwa Wilaya yetu, zinaongezeka na ni muhimu kuimarisha huduma za kudhibiti masuala ya uhamiaji kwa maslahi ya usalama wa nchi yetu. Tunawakaribisha kutembelea maeneo husika ili mjionee hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kazi njema, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kutoa pongezi zangu za dhati, kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa hotuba yake nzuri, yenye mwelekeo wa kupunguza matatizo mengi yanayoikabili Wizara yake. Napenda kumpongeza kipekee, Naibu Waziri, kwa umahiri wake kiutendaji, bila kumsahau Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vilivyoko mipaka ya Tanzania na nchi jirani ikiwa ni pamoja na Tunduma, Kasumulu, Kassesya, Horohoro na Holili, vina upungufu mkubwa wa watumishi wa Uhamiaji na vitendea kazi, hasa vile vinavyohitajika kwa upande wa doria na ukaguzi wa madawa ya kulevya na upitishaji wa magendo na magari yasiyo halali. Mipaka ya Tunduma, Kasumulu (Mkoani Mbeya) na Hororo (Mkoani Tanga), inavuja (iko *porous* kwa upitishaji wa vitu hivyo). Mpaka wa Kasesya Mkoani Rukwa umelala. Inadhaniwa kuwa, hakuna biashara muhimu inayofanyika na hivyo kuwa na wafanyakazi wasiozidi wanne. Mpaka huu ndiyo unaweza kuwa lango kuu la kupitishia vitu mbalimbali vikijumuisha madawa ya kulevya na silaha zinazomilikiwa isivyo halali, kwani ulinzi wake ni hafifu. Mipaka kati ya Tanzania na Zambia na Tanzania na Malawi ni mirefu na rahisi kupitika na watu wasiotaka kufuata taratibu za kisheria za kuvuka mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kimarisha shughuli za kuhakikisha kuwa taratibu zote ziafuatwa, kuna haja ya kuongeza idadi ya watumishi na kuwapatia zana za kazi ikiwa ni pamoja na pikipiki na magari kwa ajili ya doria, mafunzo ya kisasa kuhusu

utambuzi wa wabeba madawa ya kulevya na kuwapatia wataalam *kits* za kutambua aina za madawa ya kulevya yanapokamatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ingefaa watumishi wa mipakani wapewe nafasi za kuhudhuria semina na mafunzo rejea, badala ya kuwaacha bila ya kujiendeleza kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kusema kuwa, naunga mkono hoja. Hata hivyo, pamoja na kuunga mkono hoja, ninayo maoni ambayo ninayaona ni muhimu kwa ajili ya kuleta tija na maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo duniani kote, kazi kubwa ya magereza ni kuhifadhi wahalifu wa aina zote, pamoja na kurekebisha tabia zao wawe raia wema. Ninaipongeza Serikali kwa hatua ambazo imeanza kuchukua katika bajeti ya 2006/2007 za kutatua tatizo la msongamano katika Gereza la Kahama. Gereza la Kahama lenye uwezo wa kuhudumia wafungwa/mahabusu 70 tu, sasa lina watu zaidi ya 600. Hali hii ni mbaya sana, lakini ninaipongeza Serikali kwa kupanga kuongeza uwezo wa gereza hivyo, kupunguza tatizo la msongamano huu mkubwa. Ninaomba sambamba na kuongeza uwezo wa Gereza la Kahama, Serikali ione umuhimu wa kujenga nyumba za watumishi wa gereza hili, ili kupunguza adha wanayoipata watumishi wa magereza hapo Kahama, ambao wanaishi katika nyumba zisizostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuupatia Mji wa Kahama gari la Zimamoto kutokana na ukuaji wa haraka wa Mji huu, ambao unakua kwa kiwango cha asilimia saba kila mwaka. Kwa kushirikiana na Halmashauri, naiomba Serikali kuhakikisha kwamba, Watumishi wa kuendesha idara hii hapo Kahama, wanaajiriwa wenye elimu na uzoefu wa kazi, bila hivyo gari hilo litakuwa ni kiini macho.

**MHE. BRIG. JEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na hotuba iliyowasilishwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Kazi ya Wizara na Watendaji wake ni ya kuigwa na watumishi wote wa umma. Wote ni Wazalendo wa dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake wote, waendeleze moyo huo.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mheshimiwa Bernard K Membe, Naibu Waziri, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, kuongoza Wizara hii yenye jukumula kurekebisha tabia na kulea wananchi ili waweze kuwa raia wema na kuchangia uchumi wa Taifa letu. Kazi ya kuhakikisha kuwa nchi yetu haigeuzwi kuwa shamba/maficho ya wageni kutoka

nje kwa lengo la uhalifu, ndiyo kazi kubwa ambayo Wizara hii imesimamia kupitia Idara ya Uahmiaji. Hongera sana

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maombi maalum kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Rorya, Wilaya ya Tarime, kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake kama ifuatavyo:-

Kwanza, Jimbo la Rorya ni kati ya majimbo yaliyo katika Mkoa wa Mara, ambao upo Kaskazini Mashariki mwa Tanzania na sehemu kubwa unapakana na Jamhuri ya Kenya, lina eneo la ukubwa wa kilometa 9,472 za mraba. Eneo lote la Magharibi ni Ziwa Victoria, linalopakana na Kenya. Kutokana na jiografia ya Jimbo la Rorya, uimarishaji wa ulinzi wa mipaka na nchi jirani ni muhimu sana. Kwanza, wananchi wanaomba kituo cha Uhamiaji kilichopo Nyamagongo, umbali wa kilometa 20 kutoka mpakani na Kenya, kihamishwe kwenda Kijiji cha Kirongwe kilichopo mpakani na Kenya. Kutokana na shida wanayopata wanachi wanaoishi mbali kutoka kituo hicho hasa wale wanaoishi karibu na mpaka, kupekuliwa na kuwekwa chini ya ulinzi wakidhaniwa kuwa ni wananchi wa Kenya.

Sababu iliyofanya kituo hicho kihamishiwe karibu na mpakani ilitokana na ukosefu wa miundombinu barabara. Barabara ya Nyamagongo – Masongo – Bubombi - Kirongwe mpakani na Kenya, ilitengenezwa kuanzia mwaka 2002/2003 hivyo, wananchi wanaomba kituo hicho sasa kihamishwe kuwaondolea kero ya muda mrefu wananchi wa Vijiji vya Masonga, Bobombi, Bwisi, Thabacha, Nyambori, Nyahera, Nyamagongo na Kirongwe, kuhesabiwa kuwa ni raia wa Kenya kutokana na kituo cha uhamiaji cha kijiji cha Nyamagongo kuwa mbali na mpaka wa Kenya, kilomita 20 kutoka mpakani. Eneo la ujenzi wa kituo kipya lipo.

Upande wa mpaka katika Ziwa Victoria, Bandari ya *SOTA,* ambayo ndiyo kituo pekee, inayopakana na Jamhuri ya Kenya katika Mkoa wa Mara, ilifanyiwa ukarabati mwaka 2002 - 2004 na kuzinduliwa kwa ajili ya kuhudumia vyombo vya usafiri majini kati ya Kenya,Uganda na Tanzania tarehe 7 Januari, 2004. Tangu kuzinduliwa, meli ndogo na kubwa kutoka Kenya zinatumia Bandari ya *SOTA*. Wananchi wanaomba Kituo cha Uhamiaji kijengwe na kipatiwe watumishi wa kutosha, pamoja na vitendea kazi kwa lengo la kudhibiti wahamiaji haramu na wahalifu. Jimbo la Rorya limewekwa katika orodha ya majimbo nchini, ambayo yanafikiriwa kupandishwa hadhi ya kuwa wilaya kamili. Hivyo, kuna haja pia ya kuanza kufanya maandalizi ya ujenzi wa gereza katika Mji Mdogo wa Shirati. Ni matumaini yangu kuwa, maombi hayo mawili ya wananchi, yatapatiwa majibu ya kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Waziri kuwa, wananchi wa Jimbo la Rorya, wapo pamoja na Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. FATMA ABDALLA TAMIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuandika mchango huu. Pia nampongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wake wote, kwa kazi wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza mchango wangu huu mdogo kuhusu bajeti hii. Ukiangalia magereza yetu yana mahabusu wengi, wamekaliana bila ya kesi zao kusikilizwa kwa muda mrefu au kutopewa dahamana wakati pengine dhamana iko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika magereza kusema kweli kuna vitendo mbalimbali vichafu vinatendeka, ikiwemo kufanyiana vitendo vya ngono. Hii inachangiwa kwa sababu ya kuchanganya wafungwa wakubwa na wadogo. Ni bora zitengwe nafasi tofauti za walio wakubwa na walio wadogo ili kuondoa usumbufu huu wa wakubwa kuwaonea wadogo, kwa kuwabaka na pia kuchangia kuongezeka kwa gonjwa la UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari wetu wanajihusisha na vitendo viovu kama uuzaji wa madawa ya kulevya na kuchangia kuongezeka kwa veitendo viovu huko katika majela, badala ya kuondosha mambo mabaya na kuwatengeneza kuwa wazuri ili watakapotoka tupate kuwa na vijana wa Taifa la kesho, lililo bora, lakini sivyo, wanapotoka wanakuwa vijana walioharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli tunataka haki za binadamu zitendeke lakini tutazame hizo haki zitakapotendeka huyu mfungwa aliyefungwa kwa kosa la kutumia silaha kweli anastahili haki hizi azipate. Kwa kweli hizi haki za bianadamu zitendeke, lakini watazamwe wa kupewa haki hizi, sio mtu ameshaiba sana, ameshaua sana, halafu awekwe pamoja na mtu mwenye makosa madogo, pengine kaiba mkungu wa ndizi kwa shida za kimaisha. Pia mtu huyu atakapochanganywa na mtu niliyemtaja, atamharibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naanza kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ambayo imeandaliwa kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zangu zimfikie Waziri, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, kwa kupata na kuongoza Wizara hii nyeti, pia Naibu Waziri, Mheshimiwa Bernard K. Membe, kwa kuwa pamoja na kuweza kuiongoza Wizara hii, kwa msingi wa Utawala Bora, unaotoa maamuzi kwa kuzingatia ngazi zote kuhusishwa kwenye maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu niongelee kuhusu matatizo ya magereza yetu yaliyoko Wilayani Geita, ambako kuna magereza mawili, yaani la Geita Mjini, pamoja na Butundwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na jiografia ya Geita, ambayo Waziri wa Wizara hii anaifahamu fika, tunaomba yafuatayo:-

Kwanza, magereza yapanuliwe kutokana na mbanano uliopo. Majengo haya yalijengwa wakati Geita na Sengerema ilikuwa wilaya moja na ilikuwa na idadi ya watu laki mbili tu, lakini leo hii idadi ya wakazi wa Wilaya ya Geita pekee ni zadi ya laki nane.

Pili, Gereza la Butundwe liliahidiwa kupewa *tractor* hadi leo *tractor* hili halipo, katika kipindi hiki tunaomba ahadi ile itekelezwe.

Tatu, magereza yetu hayana maji safi. Katika Gereza la Geita katika kipindi kilichopita, walipanga kiasi cha shilingi10,000,000, lakini fedha hizo hazikufika na tatizo la maji bado liko palepale. Naomba juhudi zifanyike za makusudi, ule Mradi wa Lwenge ulioanzishwa na magereza, uboreshwe au wachimbe kisima kirefu pale gerezani.

Nne, magereza haya mawili hayana magari ya kufanyia kazi, wana KIA mtoto, ambalo limeharibika kabisa hivyo, kuzorotesha utendaji wa kazi. Wafungwa wanasindikizwa kwa miguu, ambapo ni hatari kwa askri wetu hasa ukizingatia kuwa, Geita ni Mji wa Kimataifa, sasa hivi mbinu zote za magaidi ziko pale. Ili kunusuru maisha ya askari hawa, wapewe gari la kubebea wafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. MASOUD ADBALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu, kutujalia uzima na afya njema. Ninawashukuru pia Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu Waziri na Wataalam wote, kwa jinsi walivyoiunda bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la wakimbizi na athari zake kwa Tanzania linaeleweka, katika mzigo huu mzito ambao wakati mwingine nchi yetu inalazimika kutumia fedha kuhami ulinzi na uchumi katika kuokoa maisha ya wakimbizi. Hata hivyo, ninaishauri Serikali iandae mpango kabambe wa kuwarejesha makwao wakimbizi wote walioko Tanzania. Kuwe na mashirikiano ya pamoja baina ya Uhamiaji, Polisi na JWTZ, yaani *Joint Military Operation* na si vibaya kukiwa na baraka japo ndogo za Shirika la Umoja wa Mataifa, linaloshughulikia Wakimbizi, yaani *UNHCR.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni yangu kuishauri Serikali kuandaa utaratibu kabambe, utakaowashirikisha kikamilifu, wakazi wa vijiji vilivyoko mipakani mwa Tanzania katika kupambana na wimbi la wahamiaji haramu kupitia njia za panya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nipate ufafanuzi wa utaratibu wa wafungwa wanaotakiwa kunyogwa, taratibu zinasemaje ikiwa wamekaa muda mrefu magerezani bila hukumu hiyo na kuna idadi gani ya wafungwa wanaotakiwa kunyongwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali iangalie namna ya kuiboresha hukumu hiyo iwapo wafungwa wanaonekana kujirekebisha kuliko kukaa muda mrefu bila hukumu kwa wafungwa hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafungwa walioathirika na ugonjwa wa UKIMWI, ni vyema kwa Serikali ikaangalia namna ya kuboresha sheria na taratibu kwa kuwasaidia, kwani kwa vyovyote vile, hatma ya waathirika hao ni kifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Kujamiiana ni vyema ikaangaliwa upya katika hali ya kukabiliana na msongamano mkubwa wa wafungwa magerezani, ambao idadi ya wafungwa kwa makosa haya, imekuwa ikiongezeka siku hadi siku.

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nikupongeze wewe binafsi, kwa kuliendesha bunge letu hili Tukufu kwa *Standards and Speed,* hali ambayo inaridhisha na kutufanya tuweze kufanya kazi zetu kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Uhamiaji inajitahidi kufanya kazi zake kwa uangalifu na ufuatiliaji wa hali ya juu sana, lakini bado tunaendelea kushauri juu ya jitihada zao. Bado ndani ya visiwa vyetu hasa Zanzibar, kuna uingiaji na utokaji wa Watanzania wenzetu, ambao wanashirikiana na vijana wa Zanzibar, kwa kufanya uhalifu na kuondoka bila ya kujulikana, kiasi ambacho inaleta ugumu wa kuwatambua wahalifu wanaofanya uhalifu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Zimamoto ni nyeti na yenye umuhimu mkubwa kwa jamii, kwani madhara ya moto ni matukio ya ghafla na utekelezaji wake unatakiwa uwe wa ghafla sana na wa dharura. Naipongeza Serikali kwa kuwapatia vifaa vya kutendea kazi idara hii, japokuwa ukuaji wa miji yetu ni mkubwa sana kiasi ambacho jitihada hizi kila zinapoongezeka, unaona hazitoshi lakini kwa kiasi kikubwa, inabidi tuzithamini jitihada hizo, ambazo matunda yake yanaonekana na Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kuendelea na ujenzi wa magereza mapya lakini ni vyema tukaangalia njia mbadala za kuwaelimisha wananchi, kuepuka kufanya makosa. Hiyo itatusaidia sana kupunguza msongamano ndani ya magereza, kwani naamini makosa mengine yanaweza kuepukika kama watu watakuwa na elimu ya kutosha kuhusu maisha yao. Najua binaadamu kufanya makosa ni kitu cha kawaida, lakini kujua haki yako na uhuru wako, kama binadamu ni muhimu piana kutokuelewa hayo, kunachangia kwa kiasi kikubwa kufanya makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri askari wetu wapewe huduma nzuri kutokana na majukumu tuliyowapa kama kuwapatia makazi mazuri, vitendea kazi kwa ujumla wake na mishahara mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kuchukua uamuzi thabiti wa kuwarejesha wakimbizi katika nchi zao, kwani ni mzigo mkubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu,Wakurugenzi na Makamishna wote, kwa kushirikiana pamoja kuleta hotuba ya bajeti ya mwaka 2006/2007, kwa ufasaha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi zangu kwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri sana ambazo wamekuwa wakizifanya

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa leo unahusu hali ya vitendo vya uhalifu vinavyofanywa na wakimbizi na wahamiaji haramu katika maeneo mbalimbali nchini, hasa mikoa yenye makambi ya wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, wakati wa kujibu michango mbalimbali iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, anipe majibu kuhusu hatua ya Serikali ya kufanya upembuzi na uchunguzi yakinifu, juu ya aina ya wakimbizi wanaokuja hapa nchini. Je, imejiaandaaje na imewahi kufanya uchunguzi mara ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imejitolea kuhifadhi wakimbizi, lakini hakuna hatua yoyote inayochukuliwa na Serikali kujua hawa wakimbizi wanaokuja ni watu wa aina gani au kama imeshafanya; nini matokeo yake? Hali hii inatia mashaka usalama wa nchi yetu, kwa sababu wapo wakimbizi waliothibitika kuwa walishiriki katika mauaji wakati wa vita katika nchi zao kama Rwanda,Burundi na Congo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kuwapokea wakimbizi hawa bila kuwajua na kufanya utafiti juu ya aina yao, kutafanya Taifa letu liwe na watu ambao watalifikisha Taifa katika adha kubwa, kwani wamekuwa wakiendeleza vitendo vya uhalifu. Mbaya zaidi watu hawa watakapojiamulia kuondoka/kutoroka katika makambi na kuamua kuakaa uraiani, tutakuwa katika Taifa ambalo halina usalama wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakimbizi hawa wamekuwa wakitoa visingizio vya kutotaka kurejea katika nchi zao, wakihofu kuchukuliwa hatua kwa makosa waliyoyafanya. Kutokana na hali hiyo, sambamba na Sheria ya Kimataifa ya kutowalazimisha wakimbizi hao kurejea kwa kwa nguvu, hata kama wamethibitika kufanya makosa, hili ni tatizo kubwa ambalo naiomba Serikali itoe au ieleze mkakati itakaofanya katika kuhakikisha wahalifu hawa wanachukuliwa hatua ili kuepusha vitendo vya uhalifu na usambaaji ovyo wa silaha nchini. Napenda kupata maelezo Serikali ina Mkakati gani wa kukuabiliana na tatizo hili la wakimbizi wahalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hotuba imeonysha ukomavu mkubwa na imetutia imani sisi sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ifanye tathmini ya haraka ili iweze kuwekeza mashamba makubwa katika Jimbo la Rufiji. Rufiji ina ardhi nzuri, maji mengi na mabwawa ya maji makubwa yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Katika tafiti zilizofanywa zimeonesha kuwa shughuli za kilimo cha mpunga, mahindi, pamba, mikorosho, michikichi, ufuta, mikunde na mifugo zinaweza kunyanyua uchumi wa Wizara na pia uchumi wa Jimbola Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. CELINA O. KOMBANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa hotuba nzuri, yenye mtiririko mzuri wa kueleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri wafungwa ndio wajenge nyumba za askari. Nashauri hivi kwa sababu wafungwa wanafanya kazi za kuzalisha mali kama vile kilimo na ujenzi wa nyumba za watu. Sasa kwa nini wafungwa wasijenge nyumba za askari? Kwa kweli ni fedheha kwa sasa nyumba wanazoishi askari magereza hazikarabatiwi tangu zijengwe. Naomba twende na wakati, askari magereza wawe askari kweli, wasiwe kama wafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi maalum ya gari kwa ajili ya Wilaya ya Ulanga. Wilaya hii ipo pembezoni mwa Mkoa wa Morogoro, inapakana na Wilaya ya Liwale. Kwa sasa wahalifu wote wanakimbilia wilaya zilizo pembezoni, kwa hiyo, mahabusu zinajaa kulingana na uhalifu unaoongezeka. Naomba wilaya hii ipewe gari kati ya magari 64 yatakayonunuliwa na Wizara. Wilaya hii haijawahi kupata gari kwa muda mrefu sana, naomba wasaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Magereza ya Kiberege na Idete ni kati ya magereza yanayozalisha mazao mbalimbali kama vile mpunga, mahindi, matunda, ndizi na kadhalika. Naomba wapatiwe matrekta ili waongeze uzalishaji zaidi kwa sababu magereza hayo yaliyoko Wilayani Kilombero, kuna rutuba nzuri inayoruhusu kuzalisha mazao yoyote.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia tena kwa mara nyingine hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani Nchi. Nampongeza Waziri na timu yake, kwa bajeti hii ambayo ina malengo ya kuboresha matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kuna msongamano mkubwa wa mahabusu, ambao kwa muda mrefu kesi zao hazikamiliki au kutopelekwa mahakamani. Serikali iangalie upya, utaratibu wa kusimamia suala hili. Kumekuwa na tabia mbaya ya baadhi ya Askari Polisi, kuwabambikia kesi wananchi. Naomba Waziri, anipe taarifa kama kuna wafungwa au mahabusu, ambao wameshawahi kulalamika kuhusu maelezo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri anipe ufafanuzi hadi leo ni wageni wangapi ambao Idara ya Uhamiaji imewapatia vibali vya kufanya kazi *(work permit),* kuanzia mwaka 2003 – 2006? Pia Idara ya Uhamiaji, hivi karibuni imetangaza inafuatilia kwa karibu, nyumba hadi nyumba, wahamiaji haramu ambao wapo nchini. Je, hadi leo ni wahamiaji wangapi wamepatikana hawana vibali vya uhamiaji?

Kumekuwa na wimbi kubwa la wakimbizi nchini, kwa kuwa baadhi yao wanajiingiza katika ujambazi. Je, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ina idadi ya matokeo haya kwa wakimbizi na wanatoka nchi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vitambulisho vya uraia, ni muhimu katika nchi yoyote duniani. Napenda kutoa maoni kuwa ni vizuri utaratibu huo uanze pale mtoto anapozaliwa, apewe namba yake ya uraia, ambayo ataitumia katika kitambulisho chake cha uraia na *passport.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kuwa na afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na timu yao yote ya Wizara hii, pamoja na Kamati yake na washiriki wote waliochangia hotuba hii na ikawa nzuri. Sasa naanza kuchangia hotuba. Mahabusu na magereza kwa kweli ni hali ya kusikitisha sana. Karibu miaka arobaini na tano sasa tangu tupate uhuru wetu, majengo ya majumba yao ni mabovu, chakavu na hayakidhi haja, kwani kuna msongamano wa wafungwa na mahabusu kupita kiasi. Hali hii inachangia kuambukizana maradhi na kuvunja haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahabusu huwekwa bila kufanyiwa upelelezi kuona kama wana makosa ya kuwekwa ndani au kesi za kubambikiwa tu na kupelekea kurundikana wafungwa na mahabusu. Askari wetu nao hupata kazi kubwa ya usimamizi huo na wafungwa nao huwekwa na njaa, chakula wanachopewa hakitoshelezi. Serikali iliangalie suala hili kwa kina, kwa kuwapa mahabusu kila kinachostahili kwa binadamu ili wawe wanatendewa haki na askari nao waongezwe mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitambulisho vya uraia vina umuhimu wa pekee kwa Taifa letu. Kitambulisho kitamuwezesha Mtanzania kujihakikishia uraia wake na kuwatambua wageni, wanaoingia nchini mwetu kiholela, kwani kuna wageni wengi nchini mwetu wanaoingia, wengi ni wafanyabiashara wengine ni wahalifu. Tuanze na

wafanyabiashara, hawa wanawabana wenyeji kwa ajira hiyo na wengine huajiriwa hata maofisini na kulipwa mshahara mkubwa kuliko wenyeji wa nchi hii. Kwa hiyo, Serikali iliangalie kwa undani suala hili, Watanzania wajivune na nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wakimbizi kwa kweli takrima yetu imetufikisha pabaya, nchi yetu ni nchi ya imani sana na kupenda wageni, hii ni mila yetu. Lakini wakimbizi hawa sasa wanaleta kero, mauaji, wizi, ubakaji na Serikali inafumbia macho kwa kuona ni suala la Kimataifa. Kwa hiyo, Serikali sasa iwe na ulinzi wa kutosha na wakikamtwa wapewe adhabu ya kutosha kama nchi nyingine.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kushika kalamu nami nikachangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani zangu hizo, sasa naomba nitoe mchango wangu. Kwa kuanzia niende kunako eneo la Magereza. Ni Idara muhimu katika Serikali yetu na kwa maendeleo ya jamii yetu. Malengo ya Wizara ni kumbadilisha raia aliyepatikana na hatia ya kuvunja sheria ya nchi, ili atokapo gerezani, awe raia mwema katika jamii. La kusikitisha, hali ya magereza yetu sio nzuri, kuanzia mazingira ya kuishi, majengo na kadhalika. Kuna mambo ya msingi kwa mwanadamu kama vile chakula, magereza mara nyingi humfanya mtu anayekuwa chini ya mamlaka ya Askari Magereza kuwa hana uhuru hata wa kulala kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chakula cha wafungwa na mahabusu katika magereza yetu ni maharagwe ama ugali, ni lazima chakula hiki. Hakuna utafiti kati ya mfungwa na mahabusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafirishaji wa mahabusu wetu inaonesha ama Idara haina magari au kutojali kuwa hawa ni watu kama walivyo wengine. Mahabusu hutiwa magarini kama wanyama na kusahau ajali za barabarani. Serikali itasema nini endapo gari la mahabusu likiwa limejaa watu ambao wamefungiwa wakapata ajali? Wizara ifahamu kufanya hivi ni kukiuka misingi ya haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipi tumtambue mahabusu na mfungwa, hivi hakuna utofauti. Kuhusu kilimo, wafungwa mara nyingi hufanya kazi ya kiliomo, Serikali itujulishe mazao yanayolimwa na wafungwa yanauzwa wapi na kiasi gani cha fedha zilizopatikana, kwani inaonesha mazao wanayolima hawayatumii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapaswa itofautishe umri katika magereza yetu, lakini wafungwa hawakai kutokana na umri wao. Inakuwaje mtoto mwenye umri wa miaka kumi na nane, umuweke na aliye chini ya umri huo; huu si udhalilishaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Uhamiaji. Mfumo wa Idara hadi leo ni mtindo wa kukupa fikra mteja ya kupita mlango wa nyuma. Hii inatokana na usumbufu. Mtanzania anayo haki yake ya kimsingi ya kwenda anakotaka, ili mradi anatembea kisheria. Kubwa katika hili ni *passports*. Wizara iondoe ugumu wa kutoa *passports*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijui ndani ya nchi yetu wapo wageni ambao wanaishi kama raia wa nchi yetu. Inaeleweka kuwa Watanzania wenzetu wapo ndani ya nchi nyigine, lakini bado ni Watanzania. Uhamiaji ndani ya nchi yetu imeshindwa kuwajua wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndoa inaweza kumwingiza raia wa nchi ile akawa raia wa nchi. Ni lini tatizo hili litatoweka katika nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitakia mema Wizara. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa na mimi naomba nimshukuru sana, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, maana kweli nilikuwa hapa Mezani, sikuweza kusemea kituo hicho cha Mukulu, lakini namshukuru sana na nadhani Mheshimiwa Waziri, atasema zaidi.

Ninaomba niwape taarifa ya kurudi kwa Mheshimiwa Spika. Namshukuru Mwenyezi Mungu, amemsafirisha salama safari yake na sasa hivi yuko tayari kuja kukalia Kiti na kuendelea na kikao chetu hiki cha leo jioni. Nampongeza Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, naona yeye bado ni Waziri Mkuu humu ndani. *(Makofi)*

*(Hapa Spika, Mheshimiwa Samuel J. Sitta Alikalia Kiti)*

**SPIKA:** Asante sana. Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyotangaziwa tumerudi salama kutoka Dar es Salaam. Naomba nimshukuru sana Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, ambaye mmekuwa naye tangu asubuhi. Kila siku tunasema kina mama wanaweza. Kwa hiyo, huko nilikokuwa sikuwa na wasiwasi wowote. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika na mimi naungana na wewe kukuhakikishia kwamba, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, amefanya kazi na nzuri sana na mimi nampongeza kwa kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nitamke rasmi kwamba, wakati Waziri mwenye dhamana alipokuwa anatoa hotuba yake asubuhi hii, alieleza shukrani zake na pongezi kwa viongozi wote wa Chama na Serikali. Napenda niungane naye bila kupoteza wakati, kuwapongeza viongozi wote waliochaguliwa ili niweze kwenda moja kwenye *agenda* zinazotuhusu.

Ni vyema nikawapongeza na kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mtama, walionichagua kuwa Mbunge wao na nikateuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ua Nchi. Huko wanakonisikia nawapongeza sana na ninawapenda wananchi wa Mtama, mnichague tena mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mnyimi wa fadhila, nikishindwa kumtambua Mrs. Membe, ambaye amenitunza wakati wote na kunipa nguvu ya kusimama hapa mbele leo, nampongeza sana mke wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengi yamesemwa na mengi yameandikwa na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana atawatambua wote waliohusika na mambo haya. Waheshimiwa Wabunge kadhaa pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama na Kambi ya Upinzani, wamezungumzia masuala mengi na nitayazungumzia matano. La kwanza, wamezungumzia matatizo na kero za wakimbizi nchini. Serikali inatambua tatizo hili kuanzia miaka yote baada ya uhuru na inatambua kwamba, tunalo jukumu la kufanya marekebisho na kutatua matatizo mbalimbali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imefanya jitihada ya kuondoa wakimbizi kwa utaratibu unaoeleweka na hadi kufikia Machi, 2006, wakimbizi 228,303 walirejeshwa kwao Burundi na *DRC* wakimbizi 17,948. Si haba na sasa hivi Serikali imebakia na mzigo wa wakimbizi 535,534, ni mzigo mkubwa, hasa kwa Mikoa ya Kagera, Kigoma na Rukwa, pamoja na sehemu nyingine ni mzigo mkubwa.

Waheshimiwa Wabunge wameomba kwamba, ni vyema kukawa na *operation* maalum ya kuwaondoa watu hawa, lakini taratibu za Serikali haziruhusu kuwa na *operation* ya Jeshi, Polisi, Uhamiaji, Magereza kuwatimua wakimbizi kwenda makwao, huo sio utaratibu unaokubalika na *Convention* ya *Geneva*. Utaratibu unaotumika kuwaondoa wakimbizi hawa ni utaratibu unaowahusisha Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi, pamoja na Idara ya Wakimbizi, kuwachuja na kuangalia hali ya usalama iliyoko katika nchi yao na pale tunaporidhika kwamba, nchini kwao kuna hali ya usalama na pale panapokuwa na *voluntary repatriation,* yaani wenyewe wanakubali kurudi, basi Serikali kwa kuunganisha na hilo Shirika la Umoja wa Mataifa linawaondoa wakimbizi hao. Kama nilivyosema, tumefanikiwa kuwaondoa 228,000, tumebakiwa na 500,000 na ni matumaini yetu kwamba, katika kipindi hiki, Serikali itaendelea na jitihada za kuwaondoa wakimbizi ambao wako nchini kwetu na wanaoleta mzigo mkubwa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mzigo huu, lipo suala la uharibifu wa mazingira. Tunakiri kwamba, mazingira katika nchi yetu yanaharibiwa sana na kufika kwa wakimbizi, ukataji wa misitu, uharibifu wa barabara, vyanzo vya maji, vyote hivi vinachangia katika uharibifu na ni mzigo mkubwa kwa Taifa letu. Lakini nafurahi kukufahamisha pamoja na Wabunge kwamba, Serikali inajitahidi kupata fedha hasa kutoka Denmark, ambao katika kipindi cha mwaka 2005/2006, kimeweza kutoa shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kutatua tatizo la uharibifu wa mazingira katika Mikoa ya Kagera na Kigoma. Lakini *UNHCR*, yaani Shirika la Umoja wa Mataifa nalo halipo nyuma na tunashukuru kwamba tatizo hili linashughulikiwa. Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mbunge wa Kibondo, amelizungumzia hili kwa ukali na akaomba turekebishe suala hili la mazingira au wakimbizi wote waondoke mara moja na napenda kumhakikishia kwamba, tutawaondoa kwa *phases* kutokana na hali ya usalama inavyojionesha kule. Ni matumaini yangu kwamba, wana-Kibondo watakuwa wavumilivu mpaka hali itakavyotengemaa. Lakini Serikali inatambua ugonjwa na vidonda wanavyovipata

wananchi wa Kibondo, Kasulu, Kagera na sehemu nyingine kutokana na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, suala la uraia, limeulizwa na Kambi ya Upinzani na Wabunge wengine wengi sana. Napenda kusema *point*s kama mbili au tatu kuhusu uraia. Suala la uraia ni muhimu kwa Tanzania inayozungukwa na nchi yenye wakimbizi wanaoingia nchini kwetu kila mara. Sisi sio kama nchi nyingine, nchi yetu wakati umefika sasa wa kulitatua suala uraia, kwa sababu ya wingi wa wakimbizi na watu haramu wanaotoka katika nchi jirani. Kwa hiyo, tumefika wakati mzuri na Serikali imetambua kwamba, huu ni wakati muafaka wa kujaribu kutatua tatizo hili la wakimbizi, kwa kutoa hati za uraia kwa wananchi wake ili tuweze kuwajua wageni ni nani, wakimbizi ni nani, nani wanastahili kuondolewa, nani wanastahili kushtakiwa na wahuni gain, ambao pengine wanaleta madhara ya ujambazi katika nchi yetu. Kwa hiyo, jibu moja la watu haramu wanaoingia nchini, kuwatambua wakimbizi wa kweli au raia wa kweli ni ku-*introduce* au kuleta kadi za uraia *(National IDs)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadi za uraia kama Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana alivyosema asubuhi, ipo kwenye mchakato na sasa karibu tutafikia ukingoni. Naomba nirudie kwamba, katika kipindi cha fedha cha mwaka 2007/2008, tunategemea kwamba, mradi huu wa vyeti vya uraia au hati za uraia, utakuwa umekamilika. Utakuwa umekamilika kwa sababu upembuzi yakinifu, kama tulivyambiwa umeshakamilisha na tayari washauri, wameshatoa hati maalum hati maalum, ambayo baadaye itapelekwa Serikalini kwa ajili ya kupata wazabuni na ni mchakato ulioanza. Serikali kama mlivyoambiwa, ilipata shilingi bilioni tatu, kwa ajili ya kuweka miundombinu ya kuanza utaratibu mpya wa kuwaorodhesha watu, pamoja na kuwasajili ili tuwapate raia na mchakato mzima ufanikiwe mwakani.

Kwa hiyo, nina imani mradi huu utakwenda. Napenda tu niwakumbushe Watanzania, Mradi wa *ID* au utengenezaji wa kadi hizi, haulingani na *business cards* au hizi kadi tunazozitumia. Ni kadi maalum, zina gharama kubwa, zina utafiti yakinifu na wa kisayansi na tunaomba wavute subira kwa sababu tuna-*introduce smart card system*. Kadi ambayo kwa vyovyote vile, ina uwezo wa kutunza taarifa zako za siri, Serikali inauwezo wa kuzitunza hizo taarifa za siri ili zisiangukie mikononi mwa maadui na pia ita-*protect privacy*, yaani siri za mtu binafsi, zitakuwa kwa kweli zinajikita katika kadi hiyo. Kwa hiyo, tuvute subira, italetwa kadi ya uraia nzuri, ya kisayansi na ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, nimezungumzia suala la wahamiaji haramu, lakini ningependa nilisisitize. Mheshimiwa Prof. Feethan F. Banyikwa, Mbunge wa Ngara na Mheshimiwa Mossy Suleiman Musa, Mbunge wa Mfenesini, wamelizungumza suala hili. Tunao wahamiaji haramu hasa kutoka Somalia na Ethiopia na wengine wanatoka nchi nyingine kama Pakistan. Ningependa kutoa wito tena, lakini kabla ya kutoa wito, nawapongeza Maafisa wa Uhamiaji, hasa Mkoa wa Ruvuma, Mbeya na sasa Mkoa wa Arusha, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwatambua na kuwakamata, wahamiaji haramu wanaoingia kwa mamia katika nchi yetu. Natoa pongezi pia kwa vyombo vyote vya ulinzi na usalama, likiwepo Jeshi la Polisi.

Ndugu Watanzania baadhi yetu wanashirikiana katika mradi huu wa kuleta wahamiaji haramu nchini na tunao Watanzania zaidi ya watano waliokamatwa, wanaoshirikiana katika mradi wa kuingiza na kuwapitisha wahamiaji haramu nchini. Ninawaomba Watanzania kwamba, tusifanye vitendo hivyo, ni vitendo vya kuvunja sheria. Tunawapongeza wananchi wa mpakani hasa Muhutwe, ambako wananchi wametoa taarifa nzuri Serikalini, zilizopelekea kukamatwa kwa wasomali ambao walilundikana pale kwa muda wa wiki mbili. Wasomali wapatao 57 na *Ethopians* 51. Tunawaomba wananchi waendelee kuwa macho, kwa sababu vipenyo vya watu hawa kuingilia katika nchi yetu ni vingi mno.

Serikali inajitahidi kujenga vituo vya uhamiaji, lakini macho ya wananchi na ukamilifu wa wananchi, utatusaidia kwa kweli katika kipindi cha sasa kukabiliana na tatizo la wahamiaji haramu. Tunawaonya wahamiaji haramu, wajiandikishe na wajitokeze tena, wale ambao hawatajitokeza na tukiwanasa, tutawafikisha kwenye vyombo vya Sheria na ndugu zetu walioingia kwenye njia za panya, warudi huko huko kwenye njia za panya. Nchi hii sio Jangwa la Sahara na tutapenda Sheria za Uhamiaji ziheshimiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msimamo wa Serikali ni kuwarudisha makwao na hili litatekelezwa kwa taratibu ambazo nimezieleza.

Wabunge Wengine wamezungumzia suala la zimamoto. Napenda nilimalizie hili kwa haraka kwamba, tatizo la zimamoto limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa George M. Malima, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Dr. Maua Abedi Daftari, Mheshimiwa Godfrey M. Zambi na Felix N. Kijiko.

Napenda kusema hivi; Jeshi la Magereza ni muhimu katika nchi, Serikali imenuia katika kipindi cha fedha cha 2006/2007, kutoa fedha za kutosha, ili kununua magari ya zimamoto, vifaa na vitendea kazi vya zimamoto, ili kukabiliana na majanga ya moto. Tutashirikiana na idara zote za zima moto na pia utaletwa Muswada Maalum katika Bunge hili, ili kuupa nguvu uongozi wa Kitaifa unaoeleweka. Jeshi letu la Zimamoto, nategemea katika kipindi hiki cha mwaka mmoja kwamba, matatizo yote yaliyoelezwa hapa na Waheshimiwa Wabunge yatatekelezwa na tutayafuatilia kwa sababu ni jeshi muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kengele kunigongea, napenda kuunga mkono hoja na namshukuru sana Waziri wa Mambo Mambo ya Ndani, kwa kunilea na kwa kunifundisha kazi. Nadhani naanza ku-*gain* na kupatapata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wote na ahsanteni sana kwa kunisikiliza. Naunga mkono hoja mia moja kwa mia moja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, bado nakushukuru sana, kwa kunipa nafasi hii ili nihitimishe hoja niliyoianzisha asubuhi ya leo. Nilipokuwa natoa hoja katika mlolongo wa shukrani, kwa sababu ya muda sikumaliza ule mlolongo, nataka nimalizie kutoa shukrani kwa wachache wafuatao:-

Kwanza, wananchi wa Jimbo langu la Manyoni Mashariki na baadhi yao wako pale Madiwani, kwa kunichagua kwa mara pili, kuwa mwakilishi wao na kwa Jimbo la Manyoni Mashariki, mimi ndio Mbunge wa kwanza kuchaguliwa kwa mara ya pili tangu uhuru. Wenzangu walikuwa wanapewa miaka mitano mitano tu, mimi ndio nilibahatika kupata kipindi cha pili, bila shaka wanayo madhumuni maalum na mimi nataka kuwaahidi kwamba, sijawaangusha. Vilevile napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais, pamoja na Waziri Mkuu, kwa kunipa wadhifa huu kuwa, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kama mnavyojua Wizara hii kwa kawaida Mawaziri huwa hawarudirudi, lakini safari hii nimetokea nashukuru sana, kwa imani hii niliyopewa, kuongoza kwa kurudia kipindi kingine tena baada ya kuwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, waliotoa michango ni wengi kweli na nitawatambua, nafikiri muda nitakaokuwa nasoma hautahesabiwa kwa sababu ni zaidi ya watu 80. Wametoa ushauri mzuri sana, siwezi kusema kwamba, tutamjibu kila Mbunge, kwa wale ambao hatutawajibu, mtatusamehe sana, muda hautoshi kuwajibu moja kwa moja hapa kwenye Bunge, lakini tutawajibu kwa maandishi na mtaletewa. Waliochangia hoja hii kwa kuzungumza hapa ndani ya Bunge kwanza alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa William Jonathan Kusila, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, waliofuata ni Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Hafidhi Ali Tahir, Mheshimiwa Paul P. Kimiti na mwisho sasa hivi Mheshimiwa Benard K. Membe. *(Makofi)*

Waliochangia wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu, lakini michango yao ilielekezwa kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani ni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, Mheshimiwa Mohamed S. Sinani, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Suzan A. Jerome, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Prof. Feethan F. Banyikwa na Mheshimiwa Bahati Ali Abeid. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi katika hoja hii ni Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Issa Kasim Issa, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Prof. Phillemon M. Sarungi, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimwia Bakari Shamis Faki, Mheshimwia Hafidhi Ali Tahir, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Mkiwa A.Kimwanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Anna M. Komu, Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Dr.Omari M. Nibuka, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Ernest G. Mabina, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mheshimwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mheshimiwa Celina O. Kombani, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Phares K. Kabuye, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Omar Yusufu Mzee, Mheshimiwa Fatma Abdalla Tamim, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Sophia M. Simba, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Gaudentia M. Kabaka, Mheshimwia Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mheshimiwa Haroub Said Masoud na Mheshimiwa Juma H. Killimbah. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa michango yao mizuri sana, ambayo itatusaidia katika utendaji wetu wa kazi katika kipindi hiki cha mwaka mmoja wa kazi. Hoja ni nyingi sana, lakini naanza na yale mambo ya jumla, moja la jumla limetajwa hapa ni dhana ya uraia wa nchi mbili. Sasa hivi sheria yetu inasema, Mtanzania utakuwa ni Mtanzania tu, huwezi ukawa na mtu mwenye uraia wa nchi mbili, ndio Sheria yetu inavyosema. Yako mawazo yametolewa na Wabunge wengi tu, akiwemo Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, akiwepo Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu na wengine wengi wamelisemea hili. Kwambas sasa wakati umefika tubadilishe sheria, iseme sasa Mtanzania awe na uraia zaidi ya mmoja. Ndio hoja ambayo imejengwa na baadhi ya wenzetu na wameuliza nini kauli ya Serikali? Kauli ya Serikali ni kwamba, jambo hili ni gumu lakini linazungumzika. Ni gumu kwa sababu Watanzania walio wengi, kule vijijini ukienda kule kwangu Manyoni, ukienda Karatu kule kwa rafiki yangu Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, popote utakakokwenda, mwulize Mtanzania, wewe bwana unataka uwe na uraia wan chi mbili, mwananchi atakushangaa kabisa, kwa sababu ni jambo ambalo halimhusu na kwanza haoni hata faida yake, Watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Ndio ugumu wenyewe, nadhani tutashawishi mpaka tukubaliane, waone nao kwamba, wanahitaji mabadiliko, ndio ugumu wa jambo lenyewe. Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, kasema kwamba, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa alipokuwa Marekani, alisema kabla hajaondoka madarakani, atahakikisha kwamba hii Sheria ya Uraia wa nchi moja, inafutwa tuingie katika uraia wa nchi nyingi. Kwa kweli unamsingizia tu, Mheshimiwa Rais hakusema hivyo, alisema kwamba jambo hili linazungumzika, tutakwenda kukusanya maoni ya wananchi, baadaye Serikali itaamua. Ndivyo alivyosema, Mheshimiwa Rais, hakusema kwamba, akirudi tu Tanzania atabadilisha sheria, ataleta uraia wa nchi mbili, hapana. Tangu wakati huo, jambo hili sisi tunakusanya maoni na ninyi mliotoa maoni yenu, Wizara yangu inakusanya. Yapo maoni ya upande wa pili kwamba, sasa dunia ya leo na huu utandawazi, kuna baadhi ya

Watanzania wenzetu wako huko nje, wamefanikiwa na kule nje wameshapata uraia, ukishapata uraia wa nje tu, huu wa kwetu Tanzania unafutika. Kwa hiyo, hoja ni kwamba, hao walio kule nje, ambao tumeshawafuta uraia, kwa nini tusiwaruhusu kule waendelee kuchuma, wanachochuma kule wakilete nchini kwetu? Ndio hoja ambayo inaletwa kutetea uraia wa zaidi ya Taifa moja.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tunakusanya maoni, kwa sababu linazungumzika. Katika dunia hii ziko nchi karibu 53, ambazo zina utaratibu wa *dual nationality* ya kuwa mtu anaruhusiwa kuwa raia wa nchi zaidi ya moja. Lakini kuna nchi zaidi ya 125, tukiwemo na sisi Tanzania, ambazo tuna mashaka na huu utaratibu, lakini unazungumzika na tunakusanya maoni kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais. Baada ya hapo tutaandika Waraka, utakwenda katika Baraza la Mawaziri na Serikali ndio baadaye itakuja kuamua kama tuendelee na sheria hii ama tubadilike. Huo ndio msimamo wa Serikali kwa sasa.

Jambo lingine la jumla ambalo limezungumzwa na Kambi ya Upinzani, ni hali ya mfumo wa mageuzi, jinsi tunavyoendesha magereza yetu. Yale maoni ya Upinzani, ukiyasoma vizuri, yana picha kama uendeshaji wa magereza hapa nchini ni wa kizamani, ni taratibu zile za kikoloni, ni za unyanyasaji, za uvujaji haki za binadamu, picha mbaya kweli kweli. Kusema kweli kuna mabadiliko makubwa sana, tangu wakati ule mfumo wa magereza wa mkoloni na leo, mabadiliko ni makubwa sana katika uendeshaji wa magereza yetu. Wakati wa mkoloni, magereza ilikuwa ni chombo cha mkoloni cha kumkomesha huyu mswahili, kumwogopesha, kulipiza kisasi, kumkomoa ili asifurukute. Chombo cha *oppression,* cha kumkandamiza huyu Mswahili. Magereza ilikuwa ni chombo au moja ya vyombo (*machinery)* za kumkandamiza huyu mtu. Lakini baada ya uhuru na mpaka leo, tumepiga hatua kubwa kweli kujiondoa huko, kwa hiyo, wakati wa mkoloni ilikuwa kwenda jela, asubuhi mpaka jioni ni adhabu tu, kazi za sulubu, wafungwa wanalala sakafuni, wanavaa vikaptura tu, wanajisaidia kwenye ndoo, kwenye debe, asubuhi abebe akamwage nje na kadhalika. Mlo ulikuwa maharagee yenye wadudu watupu, unga umeoza ili wakukomeshe, Mzungu anamkomesha huyu Mswahili.

Sasa hivi dhana ya magereza imebadilika kabisa, hatumpeleki mtu gerezani kwenda kumsulubu, sasa tunampeleka gerezani huyu mhalifu kwenda kumrekebisha tabia, sasa ndio mtazamo wetu sasa hivi. Kila tunapopata uwezo, tunaboresha mazingira magerezani ili huyu mhalifu tumwekee mazingira mazuri zaidi, aweze kubadilika kitabia. Kwa hiyo, sasa hivi magerezani kule hakuna kazi za sulubu, kule tunakufundisha stadi za kazi, ukikuta kuna mashamba ya magereza, wanafanya kazi ndani ya mashamba yale huku akifundishwa kilimo bora, akimaliza kifungo chake akatumie ujuzi alioupata aweze kulima kilimo bora. Tuna viwanda magerezani, wanajifunza stadi za viwandani, akimaliza aweze kujiajiri mwenyewe, mpaka tuna vyuo, mkoloni hakuacha chuo hata kimoja cha magereza hapa. Pale Mbeya kuna Chuo cha Magereza, ambapo wafungwa wanafundishwa stadi mbalimbali, ufundi mbalimbali na wanapata cheti cha *VETA,* anamaliza kifungo chake, ana cheti cha *VETA*, anaajiriwa au anajiajiri mwenyewe kwa sababu ufundi anao.

Sasa tunaposema, tumefanya yote hayo, Kambi ya Upinzani wanasema bado tuko kwa mkoloni, kwa kweli hatujitendei haki. Jamani tusijiseme mno kupita kiasi, pale ambapo tumepiga hatua, tuseme tupige hatua, sisemi kwamba, sasa tumeshaboresha mia kwa mia, hapana. Bado tuna matatizo, lakini ukweli ni kwamba, tumepiga hatua kubwa hata kwenye Hotuba ya Bajeti tumezungumza tunavyoboresha hali ya magereza kule ndani, hali ya wafungwa *uniform*, malazi, chakula mpaka elimu tunawapa. Sasa hivi kuna wafungwa wako *Open University*, wafungwa ndani ya magereza ni wanafunzi, wanasoma masomo ya Chuo Kikuu Huria, mkoloni hakumsomesha mtu katika magereza mpaka akafika Chuo Kikuu. Kwa hiyo, ndugu zangu tumepiga hatua kubwa sana, tusijiseme sana. Mazingira ya magereza kwa ujumla wake, hali ya askari ni ngumu, Mheshimiwa Paul P. Kimiti amesema. Nataka niseme kwamba, tumepita kipindi kigumu kati ya mwaka 1994 mpaka 2001. Jeshi la Magereza na kwa kweli majeshi yote, yalikuwa hayapati fedha za maendeleo, ile bajeti ya hela za maendeleo, majeshi yote, vyombo vyote vya ulinzi na usalama, vilikuwa havipati. Kwa hiyo, kuna miaka karibu kumi ambayo huduma za hawa askari hatukushiriki sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kuanzia mwaka 2001/2002 mpaka sasa Waheshimiwa Wabunge ninyi ni mashahidi, tumeanza sasa kutoa pesa za kutosha za *OC,* hazitoshi sana, lakini kuna mabadiliko makubwa sana na tumeanza kutoa hela za maendeleo. Kwa hiyo, tumeanza kubadilisha hali ya mazingira ya askari katika Jeshi la Magereza. Ujenzi wa nyumba ulisimama kabisa sasa tumeanza kujenga nyumba za askari, ukarabati wa nyumba zilizopo ulisimama kabisa tumeanza kukarabati nyumba, ununuzi wa magari hivi leo tumeomba karibu magari 82 katika bajeti hii yote hayo yanakwenda kuboresha vitendea kazi ili wakafanye kazi vizuri zaidi, tumeomba fedha za matrekta. Kuna miaka 10 kilimo kilikufa katika magereza kwa sababu hata yale matrekta yaliyokuwepo vipuri havinunuliwi yote yakafa, sasa hivi tunawapa hela za kununua matrekta.

Kwa hiyo, nataka kuwahakikishieni kwamba mazingira ya kazi katika Jeshi la Magereza, Mheshimiwa Paul Kimiti, tunaanza kuyabadilisha kwa sababu sasa tunawapa fedha, haziwatoshi sana lakini ni bora kuliko pale mwanzoni. Haya ni ya jumla ambayo nilitaka niyaseme kabla sijaingia kwenye kujibu hoja moja moja.

Mheshimiwa Spika, hoja ni nyingi sana sasa hapo kengele itakaponikutia ndiyo basi ndiyo hapo hapo msisikitike wale ambao sitawafikia.

Mheshimiwa Spika, nikianza na hoja za Idara ya Magereza, Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ilitushauri kwamba katika kupunguza msongamano kwamba tujenge magereza mapya hasa katika zile Wilaya ambazo hazina Magereza.

Mheshimiwa Spika, ni ushauri mzuri tunaendelea kujenga magereza mapya kila mwaka kutegemeana na fedha tunazopata. Mwaka huu hela ambazo tumepata tutaweza kuendelea kujenga gereza la Mbarali, Igunga na Mbinga, vile vile tutaanza ujenzi mpya kabisa katika Gereza la Karatu, Hanang, Nkasi, Ruangwa na Bukombe ndiyo uwezo umeishia hapo. Tungekuwa na uwezo mkubwa zaidi tungejenga magereza mengi zaidi lakini ushauri wa Kamati tumeupokea.

Mheshimiwa Spika,wafungwa wenye umri mkubwa watenganishwe na wenye umri mdogo kwa kweli ndiyo Sheria ya Magereza inavyosema na jitihada kubwa inafanywa kuwatenganisha watoto na watu wazima. Wakati najibu swali hapo juzi niliwaambia kabisa kwamba sasa tumeweka gereza la vijana peke yao kule Wami ni gereza la vijana watupu katika hilo hilo la kuwatenganisha wazee na vijana na kule vijana tunawapa elimu na tunawapa *training* ya Stadi za Kazi. Wameshauri kwamba Muswada wa kupanua wigo wa *PAROLE* uletwe, tumeshauandaa sasa hivi umebaki kwenda katika Baraza la Mawaziri ili uletwe hapa.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kujenga nyumba za askari uharakishwe na ziwe za ghorofa ndivyo tunavyofanya kutegemea na bajeti na mwaka huu tutaanza kujenga nyumba za ghorofa na tutaanzia kule Iringa na baadaye tutakwenda Mkoa kwa Mkoa.

Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, anasema kwamba Serikali ina mkakati gani kuona kwamba idadi ya wafungwa na mahabusu inaendana na uwezo wa magereza yetu. Mheshimwia Mwadini Abbas Jecha, sisi kule magerezani tunaletewa tu hatuwezi kusema gereza limejaa usilete, tunaletewa tu, ila tu tunafanya jitihada za kujenga magereza mapya, tunafanya jitihada za kutumia Sheria ya *PAROLE,* tunafanya jitihada ya kutumia Sheria ya *Community Service* na vile vile msamaha wa Rais. Hizi ndizo njia ambazo ndiyo madirisha ya sisi kuwaondoa wale ambao wanastahili kuondoka katika magereza zaidi ya hapo tunaletewa tu sisi hatuwezi tukakataa mtu.

Mheshimiwa Spika, wafungwa na mahabusu kupata chakula kizuri. Tunafanya jitihada kubwa sana kuboresha *diet* katika magereza. Kwa mwaka tunatumia karibu shilingi bilioni tisa kwa ajili ya chakula tu katika Magereza na wanapata lishe nzuri ikiwa ni pamoja na nyama, kuna kipindi ilifika mpaka walikuwa wanapata nyama mara nne kwa wiki sasa hivi kimepungua mpaka mara moja kwa wiki kwa sababu hapa katikati kila Wizara ilikatwa pesa zikaenda kununua chakula cha njaa. Tunawapa matunda karibu kila siku, wanakula wali mara moja au mara mbili kwa wiki, mboga inakuwa na viungo. Kwa hiyo, chakula magerezani ni kizuri na ninyi piteni Waheshimiwa Wabunge mpite katika magereza katika majimbo yenu mtashuhudia haya ninayoyasema.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja kwamba wanakula mara moja tu nadhani ilikuwa ni hija ya Mheshimiwa Diana Chilolo. Ni kweli asubuhi wanakunywa uji na mchana wanakula kwenye saa nane au tisa, ni kweli wanakula mara moja, lakini chakula wanachokula binadamu inakadiriwa kwamba mlo wake wa siku ni kama gramu 600 zaidi kidogo ya kilo moja kwa siku na ndivyo wanavyokula hawa mabwana, tatizo ni ratiba tu, lakini lishe na kiwango cha chakula ni kile kile kasoro ratiba.

Sasa ratiba ni mlo mmoja kwa siku kwa sababu ya mazonge tu mengi mara upikie kuni, mara sufuria, vikombe havitoshi hayo ndiyo mambo tunayarekebisha, kwanza gereza lenyewe limefurika watu 3,000 kula yaani wakianza kula saa saba mpaka mwisho wa wote ni saa 11 jioni, sasa ukitaka wale na chakula cha pili mwisho watakula mpaka usiku wa manane.

Kwa hiyo, tunafanya jitidaha kwanza kupunguza msongamano, kuondoa upikiaji wa kuni tuingie katika kupikia gesi, tuwe na vyombo vya kulia vya kutosha tukisha weka

mambo sawasawa na tumepeana muda na wenzangu ndani ya mwaka mmoja tutarudisha ratiba zile gram 600 badala ya kula mara moja wale mara mbili.

Mheshimiwa Guido Sigonda, alisema kwamba Serikali itoe gari kwa ajili ya Gereza la Ngwala anasema lori. Mheshimiwa Mbunge tumeshapeleka *pick up Land Rover STJ 9193* mwaka 2004/2005 na bado ni gari zima na linafanya kazi. Ameomba pia trekta, mwaka huu katika bajeti tumesema tunanunua matrekta matano nadhani wataalam watazingatia kipaumbele gereza lipi lipate kwa hiyo, kama ukikosa mwaka huu usikate tamaa, mwakani unaweza ukapata kwa sababu kila mwaka tunanunua matrekta.

Mheshimiwa Spika, kuanzisha kilimo cha kahawa, ushauri tumezingatia. Kujenga kambi ya kudumu Kambi ya Mkwajuni Mheshimiwa Mbunge ndiyo lengo letu lakini tunakwenda kwa awamu kwa sababu ya bajeti.

Mheshimiwa Stephen Galinoma, anasema chakula kwa ajili ya wahalifu wanaokamatwa vijijini na wanawekwa katika mahabusu za Mahakama za Mwanzo, wanakijiji wanaambiwa wapeleke chakula. Mahabusu za Mahakama za vijijini kwa kweli hawako moja kwa moja chini ya Wizara yangu kwa sasa, zamani ilikuwa ndiyo hivyo lakini sasa hivi jukumu hili tumelipeleka TAMISEMI nadhani watazingatia.

Mheshimiwa Gideon Cheyo, alisema juu ya kupeleka umeme kwenye Gereza la Ileje. Mheshimiwa Mbunge nisikudanganye kwamba kesho tu tutapeleka lakini tutazingatia katika bajeti ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lucas Selelii, anasema ujenzi wa Gereza la Igunga unakwenda pole pole mno, kwa hiyo, mahabusu wanajazana sana Gereza la Nzega. Mheshimiwa Lucas Selelii, ujenzi wa Gereza la Igunga unakwenda vizuri tu, tumeshamaliza bweni moja sasa kwa hiyo, wataanza kulala pale tumeshapeleka askari mwezi huu zaidi ya 30 pale na tumepeleka gari katika Kituo cha Igunga kwa hiyo, Mheshimiwa Lucas Selelii, uwe na uhakika kabisa kwamba mahabusu watakaa Igunga walio wengi badala ya kuja kujazana Nzega.

Mheshimiwa Spika, Serikali ijenge mabweni ya mahabusu huko huko Polisi na Mahakamani maana yake ndiko waliko mahabusu, ni ushauri mzuri tutatazama kama tunaweza kutekeleza badala ya mahabusu kwenda kujazana kwenye gereza wawekwe mahali pengine chini ya Mahakama ni wazo zuri tutalizungumza na wenzetu wa Idara ya Mahakama na Wizara ya Sheria lakini kwa sasa hivi huo utaratibu bado.

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya mzabuni Gereza la Nzega yapatiwe ufumbuzi. Mheshimiwa Lucas Selelii, Magereza walikuwa wanadaiwa sana na askari madeni ya zamani na wazabuni, bajeti hii niliyoisoma leo tunakwenda kumaliza kulipa madeni ya askari yote. Ndizo fedha tulizopewa ambazo ndizo tulizotengewa, fedha za wazabuni bado zinatafutwa nataka niwe mkweli tu maana nisikuahidi uongo.

Mheshimiwa Raynald Mrope, mgogoro kati ya Kijiji cha Ngalala na Gereza la Namajani. Ni kweli mgogoro huu upo lakini Mkuu wa Mkoa wa Mtwara ameunda Tume

ya kuchunguza mgogoro huu na kusuluhisha, kwa hiyo tusubiri matokeo ya Tume ya Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Wizara ya Mambo ya Ndani ishirikiane na vyombo husika ili kuhakikisha kwamba kesi za mahabusu waliopo magerezani zinasikilizwa mara moja. Tumepokea ushauri na wenzangu wa Wizara ya Katiba na Sheria wako hapa wanatusikiliza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lucy Owenya, alishauri kwamba wafungwa na mahabusu wawe wanapimwa kabla ya kuingia gerezani ili kuepuka kuambukizana magonjwa kama *TB*. Mheshimiwa Lucy Owenya, ndivyo inavyofanyika mahabusu wanapimwa afya zao na wale wanaogundulika kwamba wana *TB* wanawekwa katika selo tofauti na wazima ili wasiambukizane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malori ya kusafirisha mahabusu kwenda mahabusu yawe na viti. Ndivyo tunavyokusudia kufanya, asubuhi katika hotuba yangu nilisema kwamba sasa jukumu la kusafirisha mahabusu kutoka Gerezani kwenda Mahakamani na kurudisha sasa hivi linafanywa na Jeshi la Polisi sasa Jeshi la Polisi tumewarundikia mizigo mingi mno sasa moja ya mizigo ambayo sasa tunawapunguzia ili wapate muda wa kushughulika na majambazi ni huu wa kusafirisha mahabusu. Shughuli hii sasa itafanywa na Jeshi la Magereza sasa hivi tunawatafutia sasa magari ya kufanyia kazi hii na hayo magari ambayo tunawatafutia yatakuwa na viti na yatakuwa ni magari ya kisasa na ya karne ya 21 siyo tena karandinga bali yatakuwa ni mabasi yana viti, *radio call* na kadhalika safi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa George Lubaleje, anasema kuboresha maslahi ya askari magereza kwa kuwapatia vitendea kazi. Kama nilivyoeleza katika maelezo ya awali kwamba sasa hivi Serikali inafanya kazi ya kuboresha mazingira ya askari kwa maana ya kujenga nyumba, kwa maana ya vitendea kazi, magari pamoja na kuangalia maslahi yao. Nadhani Waziri wa Utumishi wakati nawasilisha bajeti hapa alisema kwamba katika bajeti ya mwaka huu katika makundi ambayo yameongenzwa kuliko wenzao ni vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na askari wa magereza.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Usalama wa Raia zishirikiane kupunguza msongamano. Tumeshaanza kushauriana, tuna vikao mbalimbali vya namna ya kufanya kwa pamoja kupunguza hili tatizo.

Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, anasema wafungwa kunyongwa wanaokaa muda mrefu magerezani taratibu zikoje? Wako wafungwa wangapi wa kunyongwa?

Sasa wafungwa wa kunyongwa wanapokuwa pale kwenye magereza yetu kwa kweli wako chini ya ridhaa ya Mheshimiwa Rais, akisema kesho huyu fulani anyongwe sisi tunanyonga tu, kama hajasema basi na sisi tuko naye tu mpaka Rais aseme. Kwa hiyo, hili kwa kweli haliko mikononi mwa Wizara ya Mambo ya Ndani, hili ni ridhaa ya

Rais mwenyewe akikaa kimya na sisi tunakaa kimya, akisema fanya na sisi tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, ameuliza pia kwamba sasa hivi idadi ya hao wanaosubiri kunyongwa wako wangapi? Khee, siku hizi wana luninga wanasikiliza wale kule tusiwatishe sana, lakini mara kwa mara Rais huwa anabadilisha ile hukumu kutoka kwenye kunyongwa kwenda kwenye kifungo cha maisha na hivi karibuni amewabadilishia watu kama hao wafungwa 112 kutoka adhabu ile ya kunyongwa kwenda kifungo cha maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie namna ya kuboresha sheria na taratibu za kuwasaidia wafungwa walioathirika na ugonjwa wa UKIMWI magerezani. Tunao utaratibu, kwanza wale ambao ni wagonjwa wako taabani na kama kosa alilolifanya sheria inaruhusu Rais kumsamehe hawa ni moja kati ya watu ambao tunawapeleka kwa Mheshimiwa Rais awape msamaha katika vigezo ambavyo huwa tunasamehe watu. Rais anasamehe watu, moja ni wale ambao ni wagonjwa walio taabani, walioathirika sana ambao hawana manufaa yoyote ya kukaa gereani na wale wengine ambao bado wana nguvu zao lakini imedhihirika kwamba wameambukizwa wanapatiwa matibabu haya ya dawa za kurefusha maisha.

Mheshhimiwa Spika, kufanya marekebisho ya sheria ya kujamiiana ili kupunguza msongamano mkubwa magerezani ni ushauri mzuri tutauzingatia kwa sababu ni kweli katika wale wafungwa tuliosema asubuhi katika wale karibu 25,000 robo yaani 25% ni wafungwa ambao kufungwa kwao kumetokana na makosa ya kujamiiana kwa hiyo, ni wengi sana. Tunalitazama hili na baadaye tutaleta mapendekezo ndani ya Bunge hili tuone jinsi ya kusaidiana kulitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, alisema Serikali iongeze majengo ya magereza ili kupunguza msongamano. Mheshimiwa Fatma Mikidadi, tutafanya kwa kadri uwezo utakavyoruhusu na Ruangwa imo katika ile orodha niliyoisoma asubuhi.

Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, amesema Magereza Bara na Chuo cha Mafunzo Zanzibar viunganishwe na kuwa ni vya Muungano. Hayo ni baadhi ya mambo ambayo yanazungumzwa kwenye ile Kamati ya Pamoja ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi kwa hiyo, tungoje na tusubiri muafaka utakavyotokea. *(Makofi)*

Vile vile alikuwa na maoni kwamba magodoro yaliyonunuliwa magerezani hayakuwafikia walengwa, yalikuwa kidogo sasa wafungwa wanalala kwenye majamvi. Mheshimiwa Mbunge magodoro yalinunuliwa kulingana na idadi ya watu walio magerezani kwa kweli yalifika magerezani mimi mwenyewe natembea sana magerezani nayakuta magorodo hayo magerezani kwa hiyo, kwamba hayakufika kwa walengwa kwamba yaliibwa mahali ni taarifa ambayo sina lakini kama una ushahidi Mheshimiwa basi uje uninong'oneze. Lakini mimi katika kutembea nimekuta magodoro yamefika na wote wanalala katika magodoro sioni kama watu wanalalia virago sasa.

Vile vile alikuwa na hoja kwamba Wizara ichukue hatua madhubuti kuhakikisha kuwa eneo la Magereza si eneo la kuzalisha UKIMWI. Aidha, wafungwa wababe wahasiwe, sasa Mheshimiwa Mbunge huu sasa utakuwa ni ubabe wa aina yake na tutapata taabu kweli na wenzetu wa haki za binadamu kwa hiyo, hawa tuendelee tu kuwashughulikia kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, yeye amezungumza habari za vitendea kazi na mishahara mizuri kwa askari. Kwa kweli ndizo jitihada za Serikali sasa hivi kuboresha mishara ya askari magereza na posho zao vile vile zinaboreshwa, vitendea kazi vinaboreshwa lakini vyote hivi tutafanya ndani ya uwezo ambao tunapata kupitia katika bajeti zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Janeth Massaburi, yeye alisema Serikali iboreshe Magereza ya Kilimo ili yaweze kuzalisha mahindi na maharage kwa ajili ya chakula cha wafungwa. Mheshimiwa Janeth Massaburi, ndivyo tunavyofanya kila mwaka sasa hivi katika miaka miwili kila mwaka tunanunua matrekta na kupeleka katika tumeshapeleka matrekta 18 na mwaka huu tumeomba katika bajeti matano yote haya lengo lake ni kuboresha kilimo katika magereza ya kilimo.

Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, anasema kwamba Serikali iboreshe maslahi ya askari hilo nimeshalijibu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa James Lembeli, yeye alisema kujenga nyumba za watumishi Gereza la Kahama ili kuondokana na adha wanazopata. Mheshimiwa James Lembeli, tumesikia hoja yako sasa hivi pale Kahama tuna ujenzi tumeanza kuongeza kwanza mabweni kwa sababu kuna msongamano wa ajabu sana katika lile gereza, nilitembelea mwezi uliopita na baada ya hapo tunaendeleza vile vile katika nyumba za askari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Juma Said Omar, alisema kujenga magereza mapya na kukarabati majengo yaliyopo ili kupunguza msongamano. Hilo nimekwisha jibu.

Mheshimiwa Grace Kiwelu, alisema Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Katiba na Sheria waone jinsi ya kuwaokoa Watanzania wanaopata adhabu ya kufungwa bila ya kufuata sheria. Sasa Mheshimiwa Grace Kiwelu, nafikiri wenzetu wa Wizara ya Katiba na Sheria wamesikia kwani sisi tunaletewa tu wameshafungwa tayari, sasa kama mtu kabambikiziwa au kafungwa sheria haikufuatwa sawa sawa nadhani wapo wenzetu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Usalama wa Raia, wapo hapa nadhani wameisikia na hii hoja hukuisema wewe tu wengi wameisema kupitia Wizarani kwetu, lakini kwa kweli nadhani kesho wenzetu wa Usalama wa Raia wataijibu vizuri zaidi hii hoja ya watu ambao wanabambikiziwa kesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, magereza mengi yanatisha kutokana na uchakavu. Ni kweli magereza yetu mengi ni machakavu lakini asubuhi wakati naomba fedha nilisema sehemu ya fedha hizo tunakwenda kukarabati magereza. Kwa hiyo, naomba muidhinishe fedha hizo tukafanye kazi hii ambayo mnatutuma sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafungwa wavalishwe viatu ikiwa ni kama kinga ya maradhi. Hili ndilo lengo letu maana tumeshawapa sasa suluari, shati, kaunda suti, lakini sasa kama wanapekua hata kaunda suti sasa inavunjiwa heshima. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa hili tutalifanyia kazi, hatuwezi kuwanunulia viatu kabisa vya kisasa vya ngozi, lakini viatu vya kawaida tu vya Mtanzania wa kawaida hivyo tunaviweza, nataka nitoe ahadi kwamba tutalifanya hilo. Hata Rais alipotembelea magereza vile vile alituagiza hili, alifurahi kwamba aliwakuta wako *smart* lakini chini aliwakuta baadhi wanapekua akasema kwa mavazi tumefanya vizuri lakini kwa viatu vipi Waziri? Nikamuahidi hivyo hivyo na nataka niliahidi Bunge lako Tukufu kwamba hivyo viatu, katambuga za Mtanzania wa kawaida hizi tunaziweza na tutawapa. *(Makofi)*

Kuhusu kuboresha chakula magerezani, hili nimeshalieleza, kuboresha maslahi ya askari nimeshaeleza, kuwepo utenganisho wa wafungwa wadogo na wafungwa wakubwa nimeshalieleza kwamba kwa kweli ndiyo utaratibu na ndivyo tunavyofanya.

Mheshimiwa Godfrey Zambi, amezungumzia kwamba kuwepo na utenganisho wa wafungwa magerezanii kwa kuzingatia umri pia Bodi ya *PAROLE* iendelee kuwatoa magerezani wafungwa wenye tabia nzuri. Wengi wamesema Bodi ya *PAROLE* pamoja na Mheshimiwa Paul Kimiti ni kweli Bodi ya *PAROLE* sheria ile jinsi ilivyo sasa bado inawaacha wafungwa wengi ambao wameshajirekebisha, hatuwezi kuwatoa katika sheria ile kwa sababu haina makosa hayamo katika ile orodha ya kupata msamaha. Kwa hiyo, kama lengo letu kwa kweli ni mtu ajirekebishe na ameshajirekebisha si vizuri tena kutafuta kilichomleta gerezani na hayo ndiyo marekebisho ambayo tunayaleta katika Bunge hili ili tusitazame fulani kafanya kosa gani tuone je, amejuta? Je amejirekebisha? Je, toba anayo?

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo sasa *sprint* ya sheria ambayo tunataka marekebisho, tunayaleta na tunaamini Waheshimiwa Wabunge mtatuunga mkono. Tukirekebisha hilo sheria hii inaweza ikatoa msaada mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Fatma Mikidadi, amesema kwamba Wilaya ya Ruangwa ijengewe gereza, tumeshatoa majibu kwamba wamo katika orodha.

Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, amesema kuhusu maslahi ya askari magereza hili tumeshalijibu.

Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, amesema Jeshi la Magereza lipewe vifaa vya kisasa vya kufanyia kazi ikiwa ni pamoja na usafiri, hili tumeshalijibu kwamba katika mwaka huu wa fedha tumeomba karibu magari 82 kwa ajili hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ernest Mabina, amesema Gereza la Geita na Butundwe yapanuliwe, Gereza la Butundwe lipewe trekta. Mwaka juzi tuliwapa trekta Butundwe sasa baadaye Mheshimiwa Ernest Mabina tukutane naye anieleze lile trekta limekuwaje maana

tuliwapa trekta mwaka juzi. Kupanuliwa kwa magereza ni kwamba magereza hayo yatapanuliwa kwa awamu kulingana na fedha.

Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, amesema mazingira ni machafu magerezani. Mheshimiwa Anna Komu nakushauri uende ukatembelee tena magereza, kwa hilo wamejitahidi sana kwa usafi, mwaka jana tuliwapeleka baadhi ya mabalozi wa nchi za nje, tuliwazungusha katika magereza baada ya kuzunguka wakasema sisi hatukutegemea kwamba magereza ya Tanzania yapo namna hii tulifikiri ni ya hovyo, machafu kupita kiasi na yananuka. Kwa hiyo, jitihada kwa kweli zinafanywa katika magereza hayo.

Mheshimiwa Spika, vijana wanalawitiwa. Sasa hili Mheshimiwa Anna Maulida Komu, kwa kweli ni hisia zaidi kuliko ukweli kwa sababu yale mazingira yenyewe ya wafungwa yaani mpaka wapate *privacy,* wapate nafasi ya peke yao wakafanye mambo hayo ni ngumu kweli maana yake mpaka usiku wanalala pale taa zinawaka, pale mahali pa kwenda kujisaidia hapafungwi yaani kupata *privacy* ya wawili mkafanye mambo hayo ni ngumu sana. Lakini hisia ni kwamba jambo hili kila siku linafanywa ndiyo utaratibu, kwa kweli ni hisia tu hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vipigo kwa wafungwa. Hili nioanishe na hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, ameleta hoja kwamba kuna vipigo vingi sana na mauaji ni mengi sana kutokana na vipigo.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba kwanza askari magereza kumpiga mfungwa ni kosa labda huyo mfungwa awe anafanya fujo yeye mwenyewe, anataka kukupiga kwa hiyo askari ni lazima ajitetee katika mazingira hayo ya *self defence* lakini katika mazingira mengine ni kosa kubwa sana. Kwa mara moja moja makosa kama yanatokea na anayefanya kosa hilo anachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, umetaja tukio la Kimbiji na ambalo hata kwenye vyombo vya habari sisi wenyewe Serikali tulitangaza. Katika tukio la Kimbiji ambalo askari alimpiga mfungwa na baadaye yule mfungwa akafariki, walikuwa ni askari sita na sisi wenyewe Serikali tulilaani kile kitendo tukawapeleka Mahakamani na mpaka sasa kesi iko Mahakamani kuonyesha kwamba ni kitendo ambacho hata sisi wenyewe Serikali tunakilaani na ili iwe ni fundisho kwa watu wengine kwa sababu kitendo kile hakiruhusiwi.

Pia umetoa mfano wa hapa Dodoma hivi karibuni ni kweli ilitokea tukio hilo la askari alimsukuma nadhani alikuwa mahabusu yule baadaye mahabusu yule akafariki, *post mortem* imefanywa kwanza yule askari jambo lenyewe liko polisi, polisi wamefanya *post mortem* na *post mortem* imeshatoka, daktari wanasema alikufa kwa kukosa hewa kwa sababu ya kifafa, wazazi wa yule Marehemu walithibitisha kwamba mtoto wao ni kweli ana matatizo ya kifafa pamoja na yote bado yule askari ana kesi ya kujibu, huo ni ushahidi wake utakwenda kumsaidia Mahakamani, ninapozungumza hapa ni kwamba amesimamishwa kazi. Kwa hiyo, yanapotokea matukio hayo si mengi lakini yanapotokea Serikali tunachukua hatua.

Mheshimiwa Diana Chilolo, amesema elimu ya kurekebisha wafungwa iboreshwe ili wakimaliza vifungo wajitegemee wenyewe. Ndivyo tunavyofanya na tumeanzisha

programu mbalimbali za kilimo, viwanda, ufugaji na vyuo kwa ajili hiihii kuwawezesha wakimaliza vifungo waweze wakajitegemea.

Mheshimiwa Said Amour Arfi, amesema kwamba Wizara itambue kuwepo kwa Gereza la Kalila kwani ni chakavu na lina msongamano mkubwa. Sawa tumesikia na tutatekeleza kwa mujibu wa uwezo mtakaotuwezesha katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Msemaji wa Upinzani alituuliza, je, hizi fedha ambazo mnaoomba zinakwenda kwenye uzalishaji mali huko Jeshi la Magereza zimeleta manufaa gani? Nataka kumjibu kwamba mwaka 1994 kwa sababu ya matatizo ya makusanyo ya fedha za Serikali Jeshi la Magereza lilikuwa halipati fedha za maendeleo, mwaka 2001 ndiyo wameanza kupata.

Mheshimiwa Spika, tulipoanza kuwapa fedha za maendeleo mwaka 2001/2002 wanazipeleka kufufua kilimo. Kwa hiyo, niseme hizi fedha zinaenda wapi, wanazipeleka katika kufufua kilimo katika kununua matrekta na pembejeo ili magereza waweze kuzalisha chakula cha kujitosheleza wenyewe na ziada waweze kuipeleka katika Akiba ya Taifa. Wanafufua viwanda, magereza wana viwanda vile vile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wananunua vipuri, wananunua *machine,* wanaboresha viwanda vya magereza, wanafufua mashamba ya mifugo, kununua mitamba na kadhalika. Huko ndiko fedha zinazokwenda kwa madhumuni mawili.

Kwanza, kuwezesha Jeshi la Magereza liweze kujitegemea kwa chakula na vifaa mbalimbali. Lakini la pili, ni katika kuwafundisha wafungwa stadi za kazi wakimaliza ziwasaidie katika kuendesha maisha.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kambi ya Upinzani walirudia swali la *over crowding,* ni kweli lipo, lakini jitihada kubwa sana zinafanywa kutumia sheria mbalimbali katika kupunguza wafungwa, tukishirikiana na wenzetu, walisema dhamana masharti ni magumu mno. Kwa hiyo, wanashindwa kubakia magerezani, tumesikia na wenzetu wa Katiba na Sheria wamesikia, nadhani siku ya bajeti yao watalitoa maelezo kuhusu hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uhamiaji, Kamati ya Ulinzi na Usalama imetupa ushauri kwamba pale tunapochapisha *Passport* ni pafinyu sana lile eneo na tunakubali.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika *speech* yangu mwaka huu tunajenga jengo kubwa kwa ajili ya Mkoa wa Dar es Salaam. Kwa hiyo, baadhi ya huduma za Makao Makuu zitahamishiwa katika hilo jengo kubwa watakuwa na nafasi ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *operatio*n dhidi ya wahamiaji haramu, Kamati inatushauri kwamba iongezwe kasi. Ndivyo tunavyofanya na sasa hivi tunaandaa *operation* kubwa katika baadhi ya Mikoa ambayo imeathiriwa vibaya sana na wahamiaji haramu. Tutashirikisha na vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Gideon Cheyo, alisema kituo cha kisasa Kisongole kijengwe, tumepokea hoja yako Mheshimiwa Mbunge, lakini kwa bajeti mwaka huu siwezi kukudanganya kwamba tutaanza ujenzi, lakini tutalizingatia katika bajeti ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, alizungumzia Idara ya Uhamiaji iwe Wizara kamili. Sasa hivi Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Idara ya Uhamiaji iko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani, lakini katika miaka ijayo inawezekana. Zipo nchi ambazo Uhamiaji peke yake ni Wizara kwa mahitaji yao na mazingira yao. Sisi tukifika huko basi tutafanya hivyo. Lakini kwa sasa hivi ni Idara inayojitegemea ina Mkurugenzi ambaye anateuliwa na Mheshimiwa Rais na ina *vote* yake.

Kwa hiyo, tukishaidhinisha fedha hapa ile *vote 93* wanajipangia wenyewe na wanafanya mambo wenyewe. Kwa hiyo, ile *autonomy* wanayo tu, lakini chini ya mwavuli wa Wizara ya Mambo ya Ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, suala la uraia wa nchi mbili nilishalitolea maelezo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitambulisho vya Taifa, nimesema katika hotuba yangu kwamba mchakato umeanza. Nataka kuwahakikishieni kwamba utakuwa ni wa wazi kabisa. Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, alikuwa anasema mbona mnafanya kificho ficho, mnaficha nini? Kila hatua itakuwa wazi na Bunge litaelezwa.

Mheshimiwa Spika, hatuna cha kuficha. Ameuliza je, mpaka sasa mchakato huu wa vitambulisho umeshatumia shilingi ngapi? Mpaka sasa pale Wizarani tumeshatumia shilingi 475, 697,880 katika ile hatua ya upembuzi yakinifu ambapo timu ilizunguka karibu nchi nzima. Ilikwenda mpaka Afrika Kusini, ilikwenda na Kenya na katika sehemu mbalimbali kutazama wenzetu wanafanyaje ili baadaye wanapotuletea ile ripoti, iwe imezingatia na wenzetu wanafanyaje. Wameshamaliza, wameshatupa ile ripoti na sasa hivi tunaitazama ili tuipeleke katika Baraza la Mawaziri, ule mchakato ukikubaliwa sasa na Baraza la Mawaziri tuanze huo utekelezaji na kila hatua tutaelezeni. Hatuna cha kuficha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, alisema kuwashirikisha wakazi wa vijiji vya mipakani kupambana wahamiaji haramu, Mheshimiwa Mbunge ndivyo tunavyofanya. Sasa hivi katika Mikoa ya mpakani tumepeleka madaftari ya kuorodhesha wageni. Sasa pale kijijini Mwenyekiti wa Kijiji, Wenyeviti wa Vitongoji na wazee ndiyo wanaowafahamu nani mwenyeji, nani mgeni na nani ni Mmtanzania na nani si Mtanzania, ndiyo wanaotusaidia. Kwa hiyo, tunawashirikisha. Kwa sababu Maafisa Uhamiaji hawatajua kila mgeni katika kila kijiji bila kuwashirikishi viongozi katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, amesema Idara ya Uhamiaji ipewe mafunzo maalum na kuongeza ajira kwa watumishi. Mheshimiwa Mbunge ndivyo tunavyofanya, tunayo *training* kabisa kila mwaka tuna-*train* vijana wa Uhamiaji na tumeeleza katika hotuba yetu ya bajeti na kama nilivyosema sasa tunajenga

Chuo kipya kabisa. Kwa miaka mingi sana tulikuwa sisi hatuna Chuo cha Uhamiaji. Sasa mwaka huu tutapata Chuo, majengo yapo tayari pale Moshi, tutakuwa na Chuo ili kusisitiza hili la mafunzo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, alizungumzia uimarishaji wa vituo vya mpakani kama Tunduma Kasumulu, Kasensa, Horohoro na Holili. Mheshimiwa Mbunge ndivyo tunavyofanya, lakini tunafanya kwa awamu kulingana na uwezo wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Godfrey Zambi, alisema Serikali iongeze mikakati ya kukabiliana na wahamiaji haramu, pia udhibiti wa njia za panya, ndivyo tunavyofanya Mheshimiwa Mbunge. Idara Uhamiaji tunawaongezea vitendea na tumeomba fedha hapa kwa ajili ya magari kwa kazi hiyo. Tumeomba fedha kwa ajili ya pikipiki karibu 30 kwa sababu hiyo. Tumeomba fedha kwa ajili ya boti za kufanya *patrol* kando kando ya Maziwa kwa ajili ya kupambana na watu wanaoingia nchini mwetu kinyemela.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, alizungumzia kudhibiti uingiaji na utokaji watu Visiwani uimarishwe ili kudhibiti Watanzania wanaoshirikiana na vijana wa Zanzibar kufanya uhalifu na kuondoka bila kujulikana. Mheshimiwa Mbunge, ushauri wako ni mzuri, tunao ushirikiano wa karibu sana kati ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa maana ya Uhamiaji na wenzetu wa Polisi. Vile vile kwa kushirikiana na wananchi. Kwa hiyo, tunaomba tu wananchi wa Zanzibar watoe ushirikiano kwa Uhamiaji na Polisi ili tuweze kukabiliana na watu wanaoingia kule Zanzibar na kufanya uhalifu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa George Lubeleje, amesema habari ya vitendea kazi ni vichache, Serikali ina mpango gani wa kuboresha vitendea kazi? Nilishasema kwamba mwaka wa fedha uliopita tulinunua magari 30, pikipiki 10 na boti tatu. Katika mwaka huu wa fedha tunaomba kununua magari 30, pikipiki 30 na boti nne, yote haya ni kuboresha vitendea kwa Idara ya Uhamiaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mariam Kasembe, alizungumzia ukaaji wa wageni haramu katika nchi yetu udhibitiwe, tutalizingatia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, amesema tuimarishe ulinzi wa mipaka yetu na nchi za jirani hasa Mkoa wa Mara katika Jimbo la Rorya. Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi tutalizingatia hilo. Mwezi Oktoba, 2006 Wakuu wa Uhamiaji wa Tanzania, Kenya na Uganda watapita katika maeneo ya mipakani pamoja na kule Rorya ili kuona maeneo ambayo tumeweka vituo vya Uhamiaji. Sasa tukiweka sisi na wenzetu wa Kenya lazima waweke, ukiweka wewe mwenzako asiweke kituo hakitafanya kazi sawa sawa. Kwa hiyo, hili litazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lucy Owenya, kuimarisha Idara ya Uhamiaji ngazi ya Wilaya na Kata tutakapoanza zoezi la vitambulisho tutaunda Kamati katika vijiji na Kata zitazowasaidia Uhamiaji kwamba huyu anayeomba apate kitambulisho je, ni

Mtanzania? Maana mtu yeyote anaweza akaomba tu pale. Kwa hiyo, hizo Kamati tutaziunda na ni moja ya mapendekezo ambayo katika ule upembuzi yakinifu wataalamu wametushauri kwamba tuunde Kamati hizi ili zitusaidie kutambua huyu mwombaji kama kweli ni Mtanzania ili vitambulisho hivi visiende kwa watu ambao sio Watanzania. Kwa hiyo, hili Mheshimiwa Lucy Owenya, tutalizingatia kwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Said Amour Arfi, tahadhari kuhusu kutoa vitambulisho kwa wageni ambao si raia, ndiyo hili ambalo nilikuwa namjibu Mheshimiwa Lucy Owenya kwamba tutachukua tahadhari kubwa ili tuwape vitambulisho kwa wale tu ambao wanahusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Sophia Simba, amesema Ubalozi wa Marekani unawanyanyasa sana Watanzania wanapokwenda kuomba *visa.* Ni kweli hayo malalamiko tumeyasikia, lakini tutashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa sababu kwa kweli hiyo Wizara ndiyo wanaotusemea kwa Mataifa mengine na ndiyo kiungo ili tuweze kulitatua.

Mheshimiwa Spika, hata sisi hatufurahi kuona Watanzania wananyanyaswa wanapokwenda kuomba *visa.* Wakati sisi hatuwanyanyasi raia wao wanapoomba *visa* hapa kwetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Phares Kabuye hakuna jengo la ofisi Biharamulo. Birahamulo kwanza tunayo Idara ya Uhamiaji iko pale. Ni kweli hatuna jengo letu sisi wenyewe tumepanga, lakini tukipata uwezo Mheshimiwa Phares Kabuye, tutajenga jengo letu sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Said Amour Arfi, aliulizia watumishi watano wa Uhamiaji ambao waliteremshwa vyeo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nilisema kengele itakaponikuta ni hapo hapo na imenikuta hapo. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 29 - Magereza**

Kifungu 1001 - *Prisons Headquaters ... ... 12,704,337,500/=*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nitayasoma majina yote ambaye hajatajwa basi labda Katibu amemruka.

Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Phares Kabuye, Mheshimiwa Raynald Mrope na Mheshimiwa Lucy Owenya. Basi tutaanza na Mheshimiwa Said Arfi.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi nazungumzia kwenye *programme 10, sub-vote 1001.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge hebu sogelea chombo husikiki.

**MHE. SAID A. ARFI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 250100 mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Sio mahali pake.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sera.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hakuna sera hapo ni Idara ya Magereza. Kama una jambo la kuongelea kuhusu Magereza vifungu viko hapo. Wizara bado. Naona huna hoja hapo kwenye Magereza. Namwita Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya. Tafadhali zima chombo. *(Makofi)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 29, programme 10, sub-vote 1001 Prisons Headquaters*. Idara ya Magereza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, taja kifungu.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo 250100.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hapo ni mshahara wa Kamishna wa Magereza na watu wake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, inaelekea kuna kitu mnataka kusema kuhusu Idara ya Magereza, tazameni vifungu hivyo vizuri. Nakupa dakika moja tu kutafuta hicho kifungu. Naona haukujiandaa. Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona na mimi nimeshindwa kujua ni kifungu gani. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *programme 10, sub-vote 1001,* kifungu 261100, *Other goods and services not classified above*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, endelee.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja yangu niliyomuuliza Mheshimiwa Waziri nilikuwa ni katika suala la haki za binadamu na inaonyesha hata hotuba yake ukurasa wa 10, alizungumzia namna Magereza inavyoboresha haki za binadamu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mhesimiwa Mohamed Mnyaa, hicho kifungu hakihusiki kabisa, mimi nitawasaidia. Kwa sababu hoja lazima zitoke. Subirini basi tunapokuwa kwenye *vot*e ya Waziri ndiyo mtauliza mambo ya sera. Ukichukua hapa itabidi uulize kuhusu shughuli fulani inayohusu kifungu hicho, kuhusu gereza fulani. Lakini kama unataka sera, haki za binadamu, mateso kwa wafungwa basi ni kwenye mshahara wa Waziri. *(Makofi)*

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *programme 10, sub-vote 1001, item 270300 Vehicle and Mobile Equipments*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, endelee.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia kwa maandishi nilikuwa nimesema kwamba Gereza la Biharamulo haLina gari. Wafungwa wanafyeka miti yote Mjini na nikasema kwamba Mji wa Biharamulo unakaribia kuwa jangwa. Sasa wakati Mheshimiwa Waziri anajibu hoja hakusema kwamba Biharamulo katika magari yatakayonunuliwa Biharamulo itapatiwa lori. Naomba maelezo.

**MWENYEKITI:** Hiyo ni halali kabisa kuuliza**.** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ufafanuzi kwa hoja ya Mheshimiwa Phares Kabuye, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, kwamba katika hotuba niliyoisoma asubuhi tumeomba fedha za kununua magari 82. Kwanza, hatujapata hizo fedha zenyewe ndiyo tunaziomba sasa hivi katika Bunge hili. Katika magari hayo 64 yatasambazwa katika magereza mbalimbali.

Sasa kwa sababu na fedha zenyewe hatujapata kusema kwamba sasa Gereza la Biharamulo litapata gari, mimi nashindwa kusema moja kwa moja, lakini naomba tu Mheshimiwa Mbunge tushirikiane, yeye atupitishie hicho kifungu magari yakishapatikana sasa Kamishna Mkuu wa Magereza atatazama mahitaji na shida iko wapi na kama mahitaji pale kwake Mheshimiwa Mbunge, yapo hayo magari 64. Naomba kwanza tuyapate tutampa ushirikiano. *(Makofi)*

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika, kwa sababu huwezi kuomba fedha bila kuwa na lengo. Nadhani wakati wa kuomba fedha mlikuwa na malengo kwamba mlikuwa na magereza ambayo hayana magari na kwa Miji mingine inayoanza kama Chato lazima mlilenga kwamba mnaagiza magari kufuatana na

mahitaji sio kuagiza agiza tu, mkishapata magari ndipo muanze ku-*locate* magari yaende wapi. Bado nahitaji kupata maelezo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kama nilivyosema kwamba sasa tukianza kukaa kwanza na kugawa magari hapa jamani kila mtu atataka gari liende kwake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hebu kaa chini kwanza. Mheshimiwa Mbunge anachosema na ni halali kabisa umefikiaje hesabu ya magari 82 au 64. Yeye anasema ana hakika Serikali inajua wapi kuna upungufu wa magari ndiyo *point* yake. Sasa mimi nilidhani ni rahisi tu kuijibu hiyo kuliko kusema kwamba tuko hapa ndiyo tugawe magari. Yeye hasemi hivyo, *in fact* yeye anachosema tayari mmekwishaamua kuhusu hayo magari na mnajua mnakoyapeleka. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shida ya magari inahusu magereza yote. Sisi tuliomba fedha za kununua magari kwa magereza yote. Yako magereza 122, lakini uwezo wa nchi umetupa fedha za kununua magari 64. Kwa hiyo, sasa tutatazama mahitaji ya kila gereza maana mazingira na mahitaji yanatofautiana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Phares Kabuye, nadhani hiyo inatosheleza. Kwa sababu Serikali kupitia Wizara hii walikuwa wanatafuta uwezekano wa kupata magari 122, bajeti yetu hii sasa kwa kupima vipaumbele yatapatikana magari 64. Haijaamuliwa kwamba Biharamulo itapata au itakosa. Kwa hiyo, tusubiri. Mtu akishajibu hivyo kazi ya Kamati sio kumlazimisha apeleke gari Biharamulo. Urambo hatuna gari lakini sina uwezo wa kuilazimisha Serikali ipeleke gari kwenye Jimbo langu. Kwa hiyo, nadhani turidhike hivyo na tungojee. Yatakapogawiwa hayo magari vigezo vitakavyotumika tutaona na tutauliza tu. Nadhani tusubiri. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 29, programme 10, sub-vote 1001,* kifungu kidogo 270300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali langu nimeuliza Waziri kwamba wafungwa wamekuwa wakisafirishwa kwa malori kama wanyama na katika jibu lake amesema kwamba magereza itachukua jukumu hilo na watasafirishwa wafungwa kwa mabasi yenye viti na *television* na kila kitu ndani ya mabasi hayo. Kitu kinachotaka kupata ufafanuzi ni kwamba ni mabasi mangapi yatayokuja na kifungu gani ambacho kitatumika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Owenya, hicho kifungu unachoulizia ni kifungu cha takrima yaani makamishna kuweza kuwapokea wageni na kadhalika *(Hospitality)*. Ungekuwa umeuliza kwenye hiyo 270300 au nikuruhusu kwenye hicho kifungu sasa.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hicho kifungu nimekitumia.

**MWENYEKITI:** Ulitamka 260300 bahati mbaya.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Hapana, nilisema kifungu 270300.

**MWENYEKITI:** Haya 270300 sasa. Hebu iweke hoja yako sasa ili Mheshimiwa Waziri aweze kukujibu.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alijibu kwamba magereza italeta magari ya kusafirishia wafungwa mazuri yenye viti na yenye vifaa vya mawasiliano, sasa nilichokuwa namuuliza ni kwamba ni mabasi mangapi yanakuja na kwenye bajeti hii ni kifungu gani kinachoonyesha kwamba kuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya mabasi hayo? Naomba kupata ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu chetu cha hotuba pale tumeonyesha kwamba shughuli ya kusafirisha mahabusu tumekasimia kununua magari kuanzia 11, kwa sababu hii kazi tunaifanya kwa awamu hayataanza kwa nchi nzima kwa mara moja. Kwa sababu walitaka karibu bilioni 3 ambazo wangeweza kuifanya kwa mara moja, haikuwezekana. Kwa hiyo, tunaanza na magari 11. Sasa akitaka kujua yapo katika kifungu gani basi aje ofisini tutafuta hicho kifungu. Lakini ni magari 11.

**MWENYEKITI:** *Infact* nadhani hapo kinachofuata ni 270300 katika *prisons rehabilitation.* Wa mwisho ni Mheshimiwa Raynald Mrope.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba mwongozo wa Mwenyekiti. Sijui naruhusiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, endelee.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mwongozo wa Mwenyekiti, ni kwa sababu kwa kweli nilikuwa nautaka mshahara wa Waziri. Nimekwenda hapa katika vifungu vyote sioni panapofanana na mshahara wa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeangalia huko mwanzoni ni *department* zilizopo katika Wizara hii ni *Prisons Headquaters, Parole Department, Prisons Welfare and Rehabilitation, Resettlement of Offenders. (Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hebu nikusaidie ni tatizo ndogo sana. Hiyo tutaifikia kwenye Fungu la 51. Fungu la 51 ndiyo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ndipo upo mshahara wa Waziri.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa mwongozo wako. Nitangoja hapo. *(Makofi/Kicheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya*

*Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 - *Parole Department ... ... ... ... ... ... .... 493,982,700/=*
Kifungu 2002 - *Prisons Welfare and Rehabilitation ...47,351,173,700/=*
Kifungu 2003 - *Resettlement of Offenders ... ... ... ... ... ...643,604,400/=*
Kifungu 3001 - *Prisons Staff College ... ... ... ... ... 1,058,831,900/=*
Kifungu 3002 - *Prisons Driving School ... ... ... ... ... ... 185,544,500/=*
Kifungu 3003 – *Prisons Trade School ... ... ... ... ... ... ...365, 290,900/=*
Kifungu 3004 - *Prisons College Kiwira ... ... ... ... ... ... ..828,905,200/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4001 - *Prison Building Brigade ... ... ... ... ... .. 996,160,600/=*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Sub-vote 4001 Prison Building Brigade*, hapa nashika mshahara wa huyo mhusika kwenye kitengo hiki. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge hakuna kitu cha namna hiyo. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hebu kaa chini kwanza nifafanue.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Sawa Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, narudia tena kama nilivyosema siku za nyuma, uwajibikaji wa Serikali katika chombo hiki chetu cha Bunge unapitia kwa Mawaziri. Huwezi kushika mshahara, tena huyu ndiyo mdogo kabisa, samahani kama ananisikia. Sijui kiongozi wa *Prison Building Brigade* ingekuwa hivyo ni hatari. Katiba inatulazimisha kwamba na ni vyema tu tunapotaka utendaji wa Serikali tuwaulize Waheshimiwa Mawaziri na ndiyo hao tunaweza kushika mishahara yao na hilo linafanywa hivyo kwa sababu kwanza wapo hapa hapa wanaweza kujibu. Lakini huyu mtu wa *Prison Brigade* kwanza haruhusiwi kuingia humu, anasikiliza tu. Kwa hiyo, hata ukisema haiwezi kusaidia. Lakini pia tunajishusha. *(Kicheko)*

Sisi sio kazi yetu kumwuliza Mkurugenzi sijui wa magari ya magereza ama sijui Koplo nani, hii haituhusu kabisa. Hapa ndani yupo Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, huyu ndiyo saizi yetu ni Mbunge mwenzetu. Huyu ndiyo tunamwuliza. *(Makofi/Kicheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4002 - *Prison Industries... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...692,330,400/=*

**Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kifungu 1001 - *Administration and General... ... ... ... ... 1,066,605,000/=*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina mambo mawili katika *Vote 51 program 10, sub-vote 1001,* Mshahara wa rafiki yangu Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza labda niliweke tu kwa sababu alieleza kwamba kengele itakapomkuta ndipo hapo hapo, inawezekana ilimkuta kwenye hoja yangu.

Sasa hilo nitaomba tu anipe kwa kirefu kwa sababu katika suala la vitambulisho nilikuwa nimeomba taarifa kamili ya fedha zilizopangwa kwa kutekeleza mradi na zilizokwisha kutumika. Hili nalisema kwa sababu mwaka juzi pia tulipata bajeti hapa hapa na kukawa na fedha kwa ajili ya kifungu hicho kwa kazi hiyo. Sasa leo naona kuna shilingi bilioni mbili kwenye kitabu cha Maendeleo, lakini zile za nyuma niliomba taarifa ili tujue mradi huu ni shilingi ngapi mpaka mwisho. Sasa kwa kuwa muda haukumtosha naomba nimwachie tu atupe kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ambalo nilitaka ufafanuzi ni suala la uraia wa nchi mbili. Mheshimiwa Waziri katika jibu lake alieleza kwamba Mheshimiwa Rais ninamsingizia.

Mimi nitakuwa tayari kumpelekea taarifa ya *video* ya *interview* ya Mheshimiwa Rais kule Canada, *CDC* na nitampelekea pia taarifa ya maandishi. Ameeleza yote hayo na akamalizia kama haitawezekana kumaliza hiyo kwa maana ya uraia basi tutafuata utaratibu ulioko Ethiopia. Wizara ina taarifa na mimi najua kwamba wanajua hilo. Waziri amependa kutumia neno kwamba tumepotosha, ningependa kuweka rekodi sahihi katika hilo. *(Makofi)*

Lakini Waziri mwenyewe nimemwuliza katika maswali yangu mambo matatu hivi. La kwanza, sheria hii tuliyonayo leo ni sheria ya ubaguzi, mwanamke wa Tanzania anapoolewa na mzungu au mwanamke wa Kitanzania anapoolewa kule anapata uraia *automatic* moja kwa moja. Lakini wa kule akiolewa hapa yule mwanaume hapati *automatic* vile vile. Sasa hii ni sheria ambayo inabagua. Mwaka juzi Waziri alinijibu hapa kwamba wanaleta hiyo sheria ili tuweze kuondoa hiki kipengele cha ubaguzi. Nilitaka kujua sasa kipengele hiki cha ubaguzi kinaondolewa vipi na lini? Waziri hakujibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, vile vile ni suala la maoni kwamba Waziri amesema tunatafuta maoni ya watu kuhusu uraia wa nchi mbili, akajibu tu kwamba wananchi hawapendi hili. Sasa mimi najua mambo mawili. La kwanza ilianzishwa *website* katika *Law Reform* na sijui kama iko chini yake au iko chini ya nani, lakini najua

Serikali ni moja. Sasa katika maoni yale wananchi walitoa maoni ghafla ile *website* imefutika. Nilitaka kujua sasa maoni haya yanakusanywa kwa njia gani na utaratibu upi wa wazi unaotumika kutafuta haya maoni ili hili swali sasa lifike mwisho wake. Kwa hiyo, nilimtaka Waziri anipe ufafanuzi huu na kazi hii itafanyika mpaka lini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa hayo mawili tu. La kwanza ameshasema mtajibu kwa maandishi, lakini hili la uraia wa nchi mbili na hili la ubaguzi wa waolewaji na waoaji.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kwa hoja ya Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Hili la uraia wa nchi mbili kama nilivyoeleza kwamba suala linazungumzika na sasa hivi limeanza kuzungumzwa kama jinsi yeye anavyozungumza sasa hivi na kwenye magazeti linaandikwa.

Napenda nichukue nafasi hii kwa sababu najua Watanzania wengi wanatusikiliza sasa hivi kwamba bado nafasi ipo ya kutoa maoni yao maana hili ni jambo kubwa sana si dogo hata kidogo, ni kubwa. Kwa hiyo, watu wanatoa maoni yao katika vyombo vya habari na iko ile Tume aliyoitaja ile ya *Law Reform Committee* inalifanyia kazi. Kwa hiyo, kwa kweli mimi sioni hata kwa nini linakuwa lina mgogoro wakati Serikali inasema jambo hili tunalifanyia kazi na sasa hivi wakati wowote tu Serikali inaweza ikatoa uamuzi baada ya kukusanya maoni ya kutosha. Kwa hiyo, ni jambo ambalo halitachukua muda mrefu, limeiva. Kwa hiyo, uwe na subira tu Mheshimiwa Dr, Wilbrod Slaa.

Kuhusu ubaguzi sheria ya sasa ni kweli nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sheria yetu ya sasa hivi Mtanzania mwanaume akioa mke kutoka nje yule mke akishakuja naye hapa Tanzania akiomba uraia, lakini lazima aombe, sio *automatic* ila ule mlolongo wa kupata uraia ni mwepesi. Kuomba si *automatic* lakini mlolongo ule wa kushughulikia hilo tatizo ni mfupi. Sasa lakini mwanamke Mtanzania akiolewa na mgeni yule mumewe akija naye hapa inabidi afuate ule utaratibu mrefu kidogo wa kuomba na kuchunguzwa ndiyo baadaye tukiridhika tunampa uraia. Watu wengi hasa akinamama wamekuwa wanalalamika na sasa hivi ile sheria tunaifanyia *review* ya uraia ili kipengele hiki tukirekebishe tuwe na mfumo mmoja tu wa mwanamke wenye umoja. Kwa hiyo hili litarekebishwa.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, sijaridhika. Hili la uraia nashukuru kwamba linafanyiwa kazi na kwamba ubaguzi unafanyiwa kazi. Nitasubiri tena mpaka nione ni lini. Lakini hili la uraia ningependa Waziri sasa atuambie ukisema tu maoni tunayakusanya, hujawaambia watu wapeleke wapi sidhani kama umelisaidia Bunge hili. Nimeeleza kwamba ile *website* iliyokuwepo kwenye *Law Reform* ilishaondoka zaidi ya mwaka mmoja sasa kwa wale wanaofuatilia mambo wanajua. Sasa nataka kujua ni wapi wananchi wapeleke maoni yao, ni chombo gani kinayaratibu na tutakuja kuyajumlisha kwa utaratibu upi ili tuje tufikie muafaka wa Kitaifa. Hili ndilo suala ambalo Waziri ningependa tu alijibu. Nadhani ni rahisi kwamba atuambie kama ni yeye tumpelekee basi wananchi wote tutamwandikia barua.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kujibu vizuri suala la *dual citizenship* au uraia wa nchi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba *Law Reform Commission* niliifanyia kazi juu ya *dual citizenship* na kwamba ripoti wameshaifikisha muda si mrefu. Pande zote mbili zimekuwa na maoni kwa wale ambao wanaona ni vyema kuwa na *dual citizenship* lakini vile vile kuna upande mwingine. Sasa *process* inaendelea baada ya Waziri wa Katiba na Sheria kupokea ripoti kutoka *Law Reform Commission* itakayofuata sasa ni kuangalia pande zote mbili na kupeleka kwenye Baraza la Mawaziri.

Kwa hiyo, *process* inaendelea na iko kwenye hatua nzuri. Sasa kama kuna wenye maoni zaidi bado wanaweza wakawasilisha lakini *Law Reform Commission* imekusanya ripoti zote na zimewasilishwa Wizara ya Katiba na Sheria na kazi inaendelea, kwa hiyo, tuvute subira muda si mrefu tutakamilisha kazi hiyo.

**MWENYEKITI:** Ni Tume ya Kurekebisha Sheria inapokea maoni. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa na wananchi wengine wapeleke maoni huko.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 51 program 10 sub-vote 1001,* kifungu kidogo 250100 Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipotoa mchango wangu nilizungumzia masuala ya Haki za Binadamu na unyanyaswaji wa wafungwa na mahabusu. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ukurasa wa 10 ameeleza uboreshwaji wa Haki za Binadamu katika Magereza na akatoa mfano hata hawavai kaptura siku hizi wanavaa kaunda suti. Lakini moja katika misingi mikubwa ambayo inavunjwa unyanyaswaji wa Haki za Binadamu katika Magereza ni kutoruhusiwa kupiga kura wafungwa na ni haki yao ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Mheshimiwa Waziri atufafanulie sasa hivi kwa kipindi kijacho moja katika litakaloboreshwa na watakuwa na *right,* wafungwa wa Tanzania kupiga kura ambayo ni haki yao ya msingi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nadhani Waziri atoe tu maelezo. Sio lazima atoe ahadi kwamba uchaguzi ujao ama hivi. Suala hapa ni kwenye Kamati ni kupata ufafanuzi tu wa hali ilivyo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ufafanuzi wa suala la Mheshimiwa Mohamaed Mnyaa, kuhusu haki ya wafungwa kupiga kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upigaji kura unatawaliwa na ile Sheria ya Uchaguzi ndiyo inayotawala na inasema nani ana haki na nani hana haki vile vile Katiba ya nchi inafafanua. Kwa hiyo, si suala ambalo si la moja kwa moja la Mambo ya Ndani, ni suala letu sote tungeweza kubadilisha. Tukitaka wapige kura lazima tubadilishe kile kipengele cha Katiba na ile Sheria ya Uchaguzi na mtu wa kufanya mambo hayo ni sisi wenyewe

sisi Waheshimiwa Wabunge hapa. Kwa hiyo, mkibadilisha, maboksi mtaleta kule, watapiga kura lakini kama hamjabadilisha wataendelea kuwa hawapigi kura. Kwa hiyo, ni suala ambalo tulifanyie kazi kwa pamoja.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru niko kwenye *vote 51 programu 10 sub vote 1001* kifungu kidogo 250100 Mshahara wa Waziri *(Basic Salary).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nimetoa maoni yangu kwa maandishi na pia Wabunge wengi wamechangia kuhusu suala zima la sheria ya kunyongwa. Wakati Waziri anatoa majumuisho yake ameelezea kwamba watu hunyongwa kutokana na amri au *discretion* ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wote tunaelewa athari za kisaikolojia wanazopata wafungwa wale ambao wameshaambiwa kwamba watanyongwa tarehe fulani lakini hawanyongwi. Sasa basi nilikuwa naomba Waziri atuambie hii sheria ikifutwa italeta madhara gani hasa ikizingatiwa kwamba haitekelezeki?

Lakini la pili, nilikuwa naomba kumwuliza Waziri toka tumepata Uhuru ni wafungwa wangapi walikuwa wamehukumiwa kunyongwa, wamenyongwa na mara ya mwisho mfungwa kunyongwa ilikuwa lini? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Hili la pili nadhani Mheshimiwa unaweza kuliuliza kipekee ili kupata takwimu kwa sababu ni refu sana. Ukitaka kujua wafungwa toka mwaka 1961 tarehe 9 Desemba. Lakini lile la kwanza kuhusu kama kweli watu wanahukumiwa kunyongwa na hawanyongwi na sheria inabaki hivyo hivyo Waziri anaweza kufafanua.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi wa swali la Mheshimiwa Susan Lyimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sheria ya kunyongwa tunayo muda mrefu na maoni ni wananchi pale watakapotuambia kwamba sasa hawataki itumike. Kwa sababu sheria ni yetu wote si kwamba sheria imewekwa na Waziri wa Mambo ya Ndani. Sheria ipo lakini mimi nina hakika Mheshimiwa Susan Lyimo, tukienda tu mitaani pale tukasema ebu sasa tunataka sheria hii ya kunyongwa ifutwe. Watanzania wengi bado wanaona kwamba sheria hii bado iwepo ili wale wanaokusudia kuua wenzao wajue kwamba na wenyewe watauawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndizo fikra za sasa za Watanzania walio wengi lakini pale fikra zikibadilika na ziko nchi duniani tu ambazo wameshafuta hii sheria. Lakini kwa Tanzania bado Watanzania wengi wanadhani sheria hii iko pale kama tishio kwa yule ambaye anataka kumwua mwenzake akijua kwamba na yeye atauawa. Kwa hiyo, kwa sasa bado nadhani wananchi wengi wanaitaka

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kabla sijaomba ufafanuzi naomba kwanza nitoe *clarification* naona Mheshimiwa Waziri alini-*quote* vibaya. *Vote 51, program 10, sub-vote 1001,* kifungu kidogo 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu asubuhi nilielezea hali halisi ya mazingira na nikasema bado majengo ni ya kizamani, ya kikoloni, mazingira na chakula bado yaani hakiko kizuri. Lakini yeye amesema mimi nimesema kwamba wanateswa wananyanyaswa hayo sikuyasema.

Kwa kweli nilikuwa naomba nitoe *clarification* na haitofautiani sana na yeye katika ukurasa wa tatu ameeleza hali halisi ya mazingira kwamba yale makubwa bado ni machakavu, ni ya zamani na ya kikoloni. Kwa hiyo, ndicho nilichosema, sikusema wananyanyaswa, wanateswa pale ni mahali watu wanakwenda kuwa *touch up*.

Kwa kuomba ufafanuzi kifungu hicho hicho. Katika hotuba yangu nilielezea fedha zilizoombwa bajeti ya mwaka jana katika kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo nikaelezea kuhusu viwanda. Mwaka wa fedha uliopita waliomba shilingi milioni 500 ili kuboresha viwango, mwaka huu imeombwa kiasi hicho hicho. Halafu mwaka uliopita pia waliomba shilingi milioni 400 kwa ajili ya kuboresha mashamba lakini mwaka huu wameomba shilingi milioni 500. Sasa nilichokuwa naomba kujua miradi yote ya Magereza iliyokuwa inahusisha hao wafungwa imeingiza kiasi gani na zinatumikaje? Ndicho nilichotaka kujua. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Sasa Waheshimiwa Wabunge Magereza ama uje uulize kwenye kitabu cha nne, kwa sababu kifungu cha Magereza chote tumekwishapita, kwa sasa hivi kama unaulizia miradi. Kwa hiyo, ama ni kitabu cha nne, kifungu cha Magereza kwa Matumizi ya Kawaida tayari. Sasa sina hakika tutakikuta kwenye kitabu nne.

Katibu ananiambia kipo, kwa hiyo, usubiri mpaka wakati huo.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 51, program 10, sub-vote 1001* kifungu kidogo 250100 - Mshahara wa Waziri.

Kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameiwasilisha hapa Bungeni na mchango wangu wa maandishi kwa Wizara nimeona kwamba kuna mradi wa kukabiliana na athari za Wakimbizi katika mikoa ya Kigoma na Kagera.

Mradi wa kwanza na sasa hivi wana mpango wa kupata mradi wa pili kwa ajili ya kupambana na athari za wakimbizi katika mikoa hiyo. Sasa nilikuwa nataka tu Waziri aniambie kwamba wanatazama vipi mikoa ambayo ilianza kubeba wakimbizi kama miaka 30 ya nyuma, Tabora na Rukwa hasa makazi ya Mishamo, Ulyankulu na Katumba. Kwa nini? Anaifikiria vipi anaweza kuisaidia na hayo maeneo ili na yenyewe yakaweza kunufaika katika mipango ya baadaye. Nilikuwa naomba maelezo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kwa hoja ya Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati,

ni kweli kwamba fedha zinazotolewa kusaidia maeneo yaliyoathirika na wakimbizi zinatolewa kwa mikoa ya Kigoma na Kagera kwa maana ya Wilaya ya Ngara na sio kwa mikoa ya Rukwa na Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti tu yenyewe ni kwamba wale wahisani wanatoa hizi fedha kwa wakimbizi wanaotunzwa kwenye makambi. Sasa hivi makambi yako Kigoma na Ngara na fedha zinakwenda kule. Tabora hatuna kambi ya wakimbizi, lakini hawakai katika kambi, wanakaa katika sehemu inaitwa makazi. Ni kijiji tu wanalima mashamba yao, wanajenga nyumba zao, wanaishi tu kama Mtanzania kasoro tu hatujawapa Utanzania ndiyo tofauti. Lakini ukiwakuta pale Mishamo au Katumba wanaishi tu kama Mtanzania tu amejenga nyumba zake, wana maduka na shughuli zao kama kawaida. Sasa katika mazingira hayo wale wahisani hawatoi hii misaada. Misaada inakwenda kwa yale maeneo ambapo wakimbizi wanakaa kwenye makambi kwa maisha yao, wako *confined* kwenye makambi. Hiyo ndiyo sababu fedha zinakwenda Kigoma lakini haziendi Rukwa. *(Makofi)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri bado sijaridhika. Ni kweli Katumba, Mishamo na Ulyankulu ni makazi. lakini ni ya muda mrefu. Lakini yameathiriwa na hao hao wakimbizi kama jinsi wanavyoathiri kambi za sasa hivi za Ngara na Kigoma. Nataka Waziri anipe maelezo ya kuniridhisha kwamba atafikiria kutusaidia na sisi katika kurekebisha zile dosari za athari ya mazingira katika makazi ya Ulyankulu, Katumba na Mishamo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Lakini Mheshimiwa Said Arfi, Waziri ameshatoa sababu kwa nini makambi kama hayo ambayo sasa yamekwisha hata kutoka wengine wamekuwa raia na kadhalika hayawekwi katika hali kama ile ya Kagera ambayo wakimbizi wameingia siku za karibuni. Ndiyo tofauti hiyo kwamba yale ya zamani yalikwishahudumiwa na watu wakapewa nafasi ya kuchagua na uraia sasa hali ni ya kawaida kabisa. Mimi nafahamu kule kwangu Urambo baadhi ya wakimbizi hao unaowasema ni matajiri kuliko wenyeji kwa hivi sasa, ndiyo ukweli wenyewe. Hawana shida kama vile walivyoingia mwaka 1972. Sasa Serikali nayo kuendelea tu kufanya huruma kwa watu kama hao tumewalea kwa miaka kadhaa sasa wako tayari na mpaka wanawaajiri wenyeji. Sasa sijui unataka msaada upi tena wapewe tena na Serikali ama sikukuelewa wapewe nini sasa?

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kurekebisha athari za mazingira. Kuwepo kwao kumetuathiri sana. Mfano vyanzo vya maji vimeharibika, maeneo mengi misitu imekatwa na hao hao wakimbizi pamoja na utajiri wao hawawezi kurudisha hali waliyoikuta mwaka 1972, Serikali inasemaje?

**MWENYEKITI:** Sasa kama hiyo ni mipango ya nchi yenyewe ambayo tumeipitia kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii upandaji miti na kadhalika.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 51, program 10, Administration, sub-vote 1001,* kifungu kidogo 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 21 Mheshimiwa Waziri amesema naomba ninukuu kidogo tu kwamba: “Halmashauri ambazo zimepata magari ya

Zimamoto zinashauriwa zianze kuunda vikosi vya Zimamoto na kuajiri askari wa Zimamoto ili kujenga uwezo wa kupambana na majanga ya moto."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la utawala tu la ufafanuzi kidogo kwamba Halmashauri ya Mji wa Babati ni mpya, nashukuru kwanza imepata gari kwenye bajeti hii, kwa hiyo, tunampongeza na tunashukuru sana. Lakini kwenye bajeti pale Halmashauri ya Mji nimeona nafasi mbili tu ambazo zipo kwa ajili ya kuunda kikosi cha Zimamoto. Kuna mtu anaitwa *Serjeant of Fire* pamoja na dereva. Sasa huu uundaji wa vikosi vya Zimamoto Mheshimiwa Waziri ebu atufafanulie kidogo tu kwamba tunawapata wapi hawa askari, ni Wizara yake itatupa au ni Halmashauri itawapeleka kwenye *training* au watatoka kwenye Vyuo vya Polisi au namna gani? Ufafanuzi wa kwanza huo.

La pili, ni jambo la utawala nalo dogo tu. Niliulizwa swali moja kwenye mikutano ya hadhara na kijana mmoja baada ya Halmashauri ya Mji kuanzishwa. Akaniambia kwa nini hamfanyi utaratibu wa kununua magari ya Zimamoto manne, matano kwenye mji ili kukabiliana na hayo majanga? Sasa mimi nilimjibu tu kwamba kwa kweli magari haya ni ghali. Pengine gari moja inaweza hata ikafikia au ikazidi gharama ya kilometa moja ya barabara ya lami kwa maana kwamba ni ghali sana.

Sasa nataka tu Mheshimwa Waziri ebu afafanue hili, haya magari gharama yake ni kiasi gani ili walau na wananchi waweze kufahamu kwamba magari ni ghali sana. Walau gari moja gharama yake ni kiasi gani ili tuweze kujua kama anaweza kufafanua hivyo. Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:**Mheshimiwa Waziri, ingawa nafahamu Mheshimiwa Omar Kwaangw', anafahamu bei ya gari la Zimamoto. Lakini nadhani yeye anataka kusikia ili yule kijana kule Babati naye asikie.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge wa Babati kama ifuatavyo:-

Kwanza Vikosi vya Zimamoto wanasema vinaundwaje, askari wanapatikanaje na je, Wizara yangu ndiyo inatoa hawa askari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi ni kwamba vinaundwa na Halmashauri yenyewe, watawasiliana na Kamishna wa Zimamoto, watawapa sifa askari wa Zimamoto awe na sifa zipi halafu baadaye watakwenda kuchukua kozi. Kuna Chuo za Zimamoto pale Dar es Salaam kwa gharama za Halmashauri zenyewe kwa sababu ndiyo inaowaajiri. Huyu Kamishna wa Zimamoto yeye anasaidia kutoa ushauri tu wa kitaalam. Lakini mwenye shughuli ni Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu magari, ni kweli haya magari ni ya ghali sana. Gari la lita 5,000 litakwenda mpaka shilingi milioni 400. Sasa Halmashauri nyingi za Mji kama Babati ziwe na hela za kununua gari la Zimamoto ni ngumu sana na hili ni gari dogo tu. Mwaka jana tulipewa fedha za kununua gari kubwa pale Dar es Salaam

linalobeba maji mengi na linalozima moto mpaka ghorofa ya 18 iligharimu shilingi bilioni moja na nusu lile gari na vikorombwezo vyake. Ni ghali kweli. Ndiyo maana Serikali Kuu sasa inatenga fedha kwa ajili ya kusaidia hizi Halmashauri. Msaada wa Serikali Kuu kuziwezesha hizi Halmashauri kama ile ya Babati kununua haya magari. Ni ghali sana lakini nafikiri Mheshimiwa Mbunge likishafika mtalitunza vizuri. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nipo katika *sub-vote 1001,* kifungu kidogo 250100 Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka ni ufafanuzi tu na maelezo kidogo kutoka kwa Waziri kutokana na tatizo tulilolonalo katika jimbo letu kati ya Gereza la Namajani na wanakijiji wa Ngalole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale sasa hivi kuna hali ya hatari kweli kweli. Uhusiano kati ya *instutions* tu hizi mbili ni mbaya. Nashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri amesema wamemtuma Mkuu wa Mkoa aunde Tume ili waende wakachunguze na kuona hasa matatizo ya pale. *(Makofi)*

Sasa ninachomwomba Mheshimiwa Waziri sasa wananchi wale wanaozunguka gereza hawana maeneo ya kulima magereza yamejitandaza mpaka kwenye upande wao, ninachoomba wakati Tume hii inafanya kazi Waziri si awaruhusu hawa wananchi wafyeke, watayarishe mashamba yao ili waweze kulima? Hilo la kwanza.

La pili ni kwamba katika migogoro hiyo hiyo mwaka 2003 kulikuwa na ugomvi kati ya magereza na wanakijiji uliopelekea wanakijiji 87 kupelekwa mahakamani na kule walishitakiwa na kosa hasa la kufyeka mpaka wao na wao walifyeka mpaka huu kwa sababu magereza nao walifyeka mpaka wao. Sasa hawa kwa sababu hawana nguvu, wala kitu chochote wakasombwa wote wakapelekwa Mahakamani wakatozwa faini ya shilingi 5,000/= jumla ya kiasi cha shilingi 425,000/=. Sasa naomba kwa Waziri kwamba kwa ajili ya *good neighbourness* (uhusiano mzuri). Je, haoni kwamba fedha hizi magereza ingezitoa kijijini ili kuleta uhusiano mzuri kati ya magereza na wanakijiji wa Ngalole?

**MWENYEKITI:** Hiyo faini ilipiga nani, Magereza?

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mahakama.

**MWENYEKITI:** Sasa magereza watarudishaje Mheshimiwa Raynald Mrope? Haziendi magereza, hebu jibu la kwanza Mheshimiwa Waziri la mahusiano hilo nadhani hilo ndiyo kubwa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa hoja aliyoitoa, rafiki yangu Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi. Huu mgogoro kati ya hili gereza na majani na kile kijiji ni wa siku nyingi. Ilifika mahali kama walielewana kwa sababu baadaye mpaka lile eneo likapimwa na *beacon*s zikawekwa mipaka ya gereza. Mimi mwenyewe nimeshatembelea hilo eneo nimekuta ile mipaka imeshawekwa na kwa kipindi kile niliona kama hali imetulia kwa

sababu watu walishajua mpaka sasa ni huu, kama analima analima mpaka hapa basi na hao waliotozwa faini ni wale waliovamia na mahakama ikathibitisha kwamba wamevamia eneo la gereza ndiyo wakakuta wanahatia ndiyo wakatozwa faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka ipo, lakini kwa sababu kuna baadhi ya wananchi bado wananung'unika pamoja na hatua zote hizi za kisheria kukamilika, bado watu wananung'unika na Mheshimiwa Raynald Mrope, akaja akasema lile tatizo pamoja na wewe kwenda kule lakini bado lipo, bado manung'uniko yapo, ndipo Wizara yangu tukazungumza na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara kwamba bado manung'uniko yapo hebu unda Tume iende ikatazame tatizo ni nini tupate suluhu. Gereza na wananchi tunataka washirikiane vizuri, hiyo Tume imeshaundwa sasa hivi inafanya kazi. *(Makofi)*

Sasa akisema kwamba wakati Tume ipo kazini halafu tuwaruhusu wananchi kutumia ardhi hiyo maana yake sasa tena waingie tena katika lile aneo ambalo ule ugomvi ulishafika mpaka mahakamani. Ushauri wangu na naomba rafiki yangu, yeye tunaelewana vizuri tu hebu tusubiri hii Tume iliyoundwa na Mkuu wa Mkoa imalize kazi halafu tutakaa tuone jinsi ya kuleta uhusiano mwema. Hilo ndilo lengo letu

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, *sub-vote 1001*, *Item 250100,* mshahara wa Waziri.

Mimi nataka jambo dogo tu anisaidie, je, Wizara yake imefikiriaje kuwasaidia kitengo hiki cha ujenzi cha magereza ambacho wanajenga vizuri kwa uaminifu bila ya rushwa. Azungumze na Serikali kwa ujumla hasa Wizara ya TAMISEMI wawe wanapewa *tender* ya ujenzi kwa sababu hawa wanajenga kwa urahisi na kwa uaminifu, je, ameshawahi kufikiria suala hilo?

Lakini la pili, je, ameshawahi kuandaa miradi ya kitengo hiki ili wakopeshwe hela, wapewe maeneo wajenge nyumba ili wauze kwa wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana muda umefika wa kupitisha vifungu kwa *guillotine.*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kitengo hiki cha ufundi cha jeshi la magereza ni kweli kinafanya kazi vizuri na *tender* kinapata, mwaka jana na juzi kilipata *tender* ya kukarabati jengo la Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, kilifanya vizuri tu.

Tuliwapa kujenga jengo la Wizara ya Mambo ya Ndani pale Ofisi yangu ilipo, ghorofa nne, ni kikosi hiki hiki. Nyumba za kisasa hapa hapa Dodoma katika mradi ule wa nyumba 300, zaidi ya nyumba 50, kikosi hiki kilijenga. Kwa hiyo, *tender* kinapata na sitaki kuwapigia debe lakini watu wowote wanaotaka kujenga majengo yao basi wajue kwamba kikosi kipo na wakiomba *tender* wapewe kwa sababu ni waaminifu wanafanya kazi vizuri, *working ship* yao ni nzuri kabisa.

Sasa kuhusu kupewa hela ili waweze kujenga wakauza hilo linazungumzika, ni ushauri mzuri.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu sasa nasikitika inabidi tuyapitishe mafungu jumla jumla hivyo hivyo. Nashauri, Waheshimiwa Wabunge tuvitazame hivi vitabu, tutakwenda vizuri zaidi.

Lakini tunaposimama wote kwenye mshahara wa Waziri sasa inakuwa vigumu hatufikii hata kitabu cha maendeleo ambapo baadhi ya mnaotaka kujua yangeweza kuulizwa mahsusi kwenye kifungu kinachohusika. Sasa ni bahati mbaya lakini tutaendelea kuzoea nadhani. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts ... ... .... ... ... ... 357,057,000/=*
Kifungu 1003 - *Policy and Planning ... ... ... ... ... ... ...330,014,000/=*
Kifungu 1004 - *Community Service Secretariat ... ... ... ..557,433,000/=*
Kifungu 1005 -*Information,Education and Community..2,375,793,000/=*
Kifungu 3001-*Fire and Rescue Services ... ... ... ... ... 1,113,221,000/=*
Kifungu 3002-*Fire and Rescure Services Training Inst. ... 451,423,000/=*
Kifungu 4001 - *Refugees Unit ... ... ... ... ... ... ... ... ... .. 510,888,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 93 – Uhamiaji**

Kifungu 2001-*Immigration Zanzibar ... ... ... ... ... ... ... 527,944,300/=*
Kifungu 2002-*Immigration Mainland ... ... ... ... ... ... 12,699,476,700/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 29 - Magereza**

Kifungu 1001-*Prisons Headquarters ... ... ... .... ... ... ... 200,000,000/=*
Kifungu 2002-*Prisons Welfare and Rehabilitation ... ... 2,200,000,000/=*
Kifungu 4001-*Prison Building Brigade ... ... ... ... ... ... 2,060,001,000/=*
Kifungu 4002 -*Prison Industries ... ... ... ... ... ... .... ... ...500,000,000/=*
Kifungu 4003 -*Prison Farms ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 500,000,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kifungu 1003-*Policy and Planning ... ... ... ... ... ... ... 1,093,000,000/=*
Kifungu 4001-*Refugees Unit ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 1,173,000,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 93 - Uhamiaji**

Kifungu 2002-*Immigration Mainland ... ... ... ... ... ... 5,362,998,000/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi atoe taarifa kuhusu kazi ya Kamati ya Matumizi.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia kifungu kwa kifungu Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa mwaka 2006/2007 kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba makadirio haya sasa yakubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa mwaka 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja sasa iliyo mbele yetu ni kuyakubali na kuyapitisha Makadirio ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2006/2007 na ili kuipitisha hoja hiyo, nitawahoji.

Kwa hiyo, natangaza kuwa Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2006/2007 yamepitishwa rasmi na Bunge hili. *(Makofi)*

Naomba sasa nitoe tangazo, nadhani ni moja hili. Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ikishirikiana na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Chama cha Madaktari Bingwa, Chama cha Ugonjwa wa Kisukari na Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania watatoa huduma ya kupima afya za Waheshimiwa Wabunge kuanzia kesho tarehe 26 hadi 28 Julai, 2006 kwa siku hizo tatu mfululizo. Huduma hiyo itatolewa katika Ukumbi wa zamani wa Bunge. Vipimo vitakavyofanyika katika zoezi hili ni kama ifuatavyo:-

Kisukari, Mafuta ndani ya damu *(Cholesterol), Blood Urea* na kitu kinaitwa *Serium Chreatin* ambayo sielewi nini. Lakini nadhani ni muhimu na kupima urefu na uzito.

Aidha, damu itachukuliwa asubuhi kati ya saa moja na saa tatu asubuhi yaani kwa vipimo hivi inabidi damu ichukuliwe ili ikapimwe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimethibitishiwa na Mheshimiwa Waziri wa Afya kwamba hawapimi kitu kingine chochote ila hivi tu nilivyovitaja. *(Kicheko)*

Sasa masharti, anayetoa damu asubuhi ahakikishe kwamba kwa kipindi cha saa nane kabla ya kuchukuliwa damu asiwe amekula kitu chochote.

Kwa hiyo, ni dhahiri kifungua kinywa huwezi kutumia kwa sababu utaharibu upimaji, inaweza kuonekana mafuta kumbe ni mafuta ya mayai ya siku hiyo hiyo. Ili kuwe na huduma nzuri isiyo na msongamano, Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kujiandikisha pale mapokezi kwenye ukumbi wa zamani kati ya tarehe hizo ili tuweze kuwatangazia.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mfano ikiwa Mheshimiwa Mbunge unataka kupima tarehe 27 au 28 basi itajulikana na orodha ile tutaiweka kwa hiyo, hakutakuwa na msongamano. Sasa itabidi niongee na Wizara ya Afya kwa sababu kwa kesho nadhani tumechelewa namna ya watu kujipanga. Labda wajaribu kwenda tu hapo kabla ya saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Afya ameniomba niseme tu kwamba jambo hili si la mzaha, inakumbukwa siku za nyuma kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walipimwa na pale pale walipelekwa *Regional Hospital,* Dodoma. Kwa sababu ilionekana hata ile *blood pressure* iko juu mno.

Kwa hiyo, jamani naomba sana tuitikie wito, huduma yote hii ni bure hakuna chochote unachotakiwa kulipa na vipimo vyote ni siri, inahusisha Daktari ambaye anakiapo pamoja na Mheshimiwa Mbunge ni vizuri kwa afya zetu kwenda kupima. *(Makofi)*

Pia kuna Mheshimiwa Mbunge amedondosha ufunguo nadhani hii ni *Toyota* anaweza kuupata pale.

Baada ya kusema hayo naliahirisha Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 01.44 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano, Tarehe 26 Julai, 2006 saa tatu asubuhi)*